

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 22 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, Kikao cha leo ni cha Kumi na Nne. Waheshimiwa Wabunge msishangae kumuona Spika naye leo amekuja kivingine, majibu yake ni rahisi tu ukishamshaona Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi naye amepiga barakoa maana yake ni kwamba lazima tufuate utaratibu. Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu hatutakuwa naye badala yake tunaye Dkt. Hussein Mwinyi yeye ambaye ana kaimu nafasi hiyo ya kuongoza shughuli Bunge. Kwa hiyo, wenyewe yoyote ya kiserikali tuwasiliane naye.

Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA - K.n.y. MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA
MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. DEVOTA M. MINJA - NAIBU MSEMADI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI,
UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO):**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na.123

Mradi wa Maji Kutoka Pongwe Kwenda Muheza

MHE. YOSEPHER F. KOMBA aliuliza:-

Kwa muda mrefu mradi wa maji unaotoka Pongwe kwenda Muheza Mjini umekuwa ukisusua na upelekaji fedha za mradi usioridhisha:-

(a) Je, mradi huo una gharama kiasi gani mpaka ukamilike, na Je, mpaka sasa ni kiasi gani cha fedha kimepelekwa kwa ajili ya mradi huo?

(b) Je, ni lini wananchi wa Wilaya ya Muheza wategemee kukamilika kwa mradi huo ili waondokane na kero ya maji inayowakabili kwa sasa?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya Maji katika Mji wa Muheza, mwaka 2017 Serikali ilianza kujenga mradi huo kwa kupanua mtandao wa maji kutokea katika mtandao wa maji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga. Mradi huo umebuniwa kutekelezwa kwa awamu mbili kwa jumla ya shilingi bilioni 6.11. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Serikali imeshafanya malipo ya jumla ya Shilingi Bilioni 3.6 kwa Wakandarasi waliokuwa wakidai kutokana na kazi walizotekeleza.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa laki saba (700,000), ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 16.9, ujenzi wa nyumba mitamba na ufungaji wa pampu mbili za maji, utekelezaji wake umefikia asilimia 95 na utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020. Awamu ya pili ya mradi huo inahusisha ujenzi wa bomba la majisafi lenye kipenyo cha milimita 300 na urefu wa kilomieta 8.2 kutoka Mowe hadi Pongwe. Utekelezaji wa awamu hii unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2020.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwalipa Wakandarasi kwa wakati ili kuwzesha mradi huo kukamilika kama ilivyokusudiwa na kuwapatia wananchi wa Muheza huduma ya Majisafi na salama.

Tatizo la Mabomba Kutoa Maji Machafu – Manispaa ya Mtwara Mikindani

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la kutoka maji machafu ya bomba katika Manispaa ya Mtwara Mikindani

Je, tatizo hilo linasababishwa na nini na litaisha lini?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya maji vinavyotumika kuwashudumia wananchi katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ni visima vilivyoko kwenye mabonde ya Mtawanya, Mchuchu na Rwelu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli maji yanayopatikana kwenye visima vinavyotumika katika Manispaa ya Mtwara yana changamoto ya kuwa na rangi ya tope kutohana na chujio lilipo lina uwezo mdogo hivyo linazidiwa na kiasi cha maji kinachozalishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa chujio hasa uondoshaji wa tope linalosalia kwenye maji (*rapid sand filter*) kwenye eneo la Mangamba.

Aidha, pamoja na jitihada nzuri za Serikali zinazoendelea kufanyika, tatizo hili litakwenda kukoma kabisa kuititia utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Mtu Ruvuma – Magamba.

Na. 125

Kuanzisha Shule Maalum za Vipaji vya Michezo na Sanaa

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Shule Maalum za Vipaji vya Michezo na Sanaa.?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi (Mbunge), Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule maalum katika kuibua na kukuza vipaji na vipawa mbalimbali hapa nchini. Kwa msingi huo, Serikali inaandaa Mwongozo wa Usajili wa Shule utakaowezesha wadau wa elimu hapa nchini kuanzisha na kusajili shule za kuibua na kukuza vipawa na vipaji katika tasnia mbalimbali ikiwemo Michezo na Sanaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na wataalam wa Sanaa na Michezo watakaofundisha katika shule zetu, Serikali inaendelea kuandaa walimu kupitia Chuo cha Ualimu Butimba ambacho hutoa Astashahada na Stashahada za Ualimu katika michezo. Aidha, Serikali inaandaa walimu wa Michezo na Sanaa katika ngazi ya Shahada kupitia Vyuo Vikuu. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutoa Shahada za Elimu ya Michezo (*Physical Education*), Sanaa za Ufundi (*Fine Arts*), Muziki (*Music*) na Sanaa za Maonesho (*Performing Arts*). Aidha, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa Bagamoyo vilivyo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo vinatoa fursa nyingine ya kuendeleza vipaji vya Sanaa na Michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali imekuwa ikitoa elimu ya Michezo na Sanaa shulenii kupitia vipindi vya masomo darasani, shughuli za nje ya darasa na mashindano

mbalimbali ya Michezo na Sanaa kama vile mashindano ya michezo kwa shule za Msingi (UMITASHUMTA) shule za Sekondari (UMISETA) na kwa Vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA).

Na. 126

Uzalishaji wa Madini ya Niobium Wilaya ya Mbeya

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je, ni lini uzalishaji wa madini ya Niobium utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya?

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oran Manase Njeza (Mbeya Vijijiini), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa uchimbaji madini ya Niobium unamilikiwa na Kampuni ya *Panda Hill*. Kampuni hii ina ubia na kampuni ya *Cradle Resources Limited* asilimia 50 na *Tremont Investments* asilimia 50. Kampuni hiyo inamiliki Leseni tatu za Uchimbaji wa Kati wa madini ML 237/2006, ML 238/2006 na ML 239/2006 zilizotolewa tarehe 16 Novemba, 2006 zikiwa na kilomita za eneo la mraba 22.1.

Mheshimiwa Spika, mradi utahusisha uchimbaji wa madini ya *Niobium* ambayo yataongezewa thamani kwa kuchanganywa na madini ya Chuma na kuwa *Ferro-Niobium* zao ambalo litauzwa kwa wanunuzi mbalimbali waliopo Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji ameshafanya Upembizi Yakinifu (*Feasibility Study*) uliokamilika mwaka 2016 na kujiridhisha uwepo wa mashapo ya kutosha utakaowezesha uhai wa mgodi kuwa takribani miaka 30. Hata hivyo, kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017, Mwekezaji alilazimika kupitia upya na kurekebisha taarifa ya upembizi yakinifu ili kuzingatia

viwango vipya nya mrabaha, kodi na hisa za Serikali. Hivyo, mwekezaji amewasilisha andiko la mradi la kuomba ufanuzi wa vipengele mbalimbali nya Sheria na kutoa mapendekezo yake juu ya utekelezaji wa mradi huo, pamoja na suala la fidia ya ardhi kwa Gereza la Mbeya ambalo linatakiwa kuhamishwa ili kupisha Mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea andiko hilo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwemo majadiliano na mwekezaji ambapo, Wizara inatarajia kutoa mapendekezo yatayowezesha kuanza kwa utekelezaji wa Mradi huo.

Na. 127

Ushirikiano Kati ya TFF na ZFF

MHE. SAADA MKUYA SALUM aliuliza;

Je, ni kwa kiasi gani Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*) limeweza kushirikiana na Shirikisho la Soka la Zanzibar (*ZFF*) katika kukuza Soka la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, Mbunge wa Welezo kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirikisho la mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*) na Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFF*) yamekuwa yakishirikiana kwa karibu katika kuratibu na kukuza mchezo wa mpira wa miguu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushirikiano wa mashirikisho haya umejikita katika maeneo mbalimbali muhimu ya maendeleo ya soka hapa nchini ikiwemo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuendesha Soka la vijana, *TFF* kwa kushirikiana na *ZFF* mashindano yote ya Kitaifa ya Vijana (U15 na U17) hushirikisha mikoa yote ya Tanzania bara

na Zanzibar kuanzia hatua za awali hadi fainali ya mashindano husika. Mashindano haya ndio yanayowezesha vipaji vya vijana wetu kuonekeana na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Timu za Taifa katika mashindano ya CAF na FIFA (Taifa Stars, Twiga Stars, na Serengeti Boys) hushirikisha wachezaji kutoka katika pande zote mbili za Muungano kulingana na vigezo vya mwalimu katika uteuzi wa wachezaji husika. Hivi sasa *TFF & ZFF* wamo katika mazungumzo ya namna bora zaidi ya uteuzi wa viongozi wa kiutawala (*none technical staff*) kwenye timu zetu za Taifa.

Mheshimiwa Spika, *TFF* na *ZFF* wamekuwa wakishirikiana vema katika kuendesha mafunzo ya waamuzi pamoja na walimu wa soka (*coaches*) kwa kozi zote za CAF na FIFA zinazoendeshwa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo. Aidha mitihani ya kufuzu uteuzi wa waamuzi wa daraja la FIFA inafanyika kila mwaka waamuzi wenye sifa kutoka pande zote mbili za muungano wanashiriki.

Mheshimiwa Spika, katika mashindano ya CECAFA ya wanawake yaliyofanyika mwaka 2019 *TFF* na *ZFF* walikubaliana kuwa *TFF* walipie gharama zote za ushiriki wa timu ya wanawake ya Zanzibar baada ya *ZFF* kuwasilisha bajeti husika, jambo ambalo liliyanyika kama liliyopangwa. Aidha hivi sasa katika eneo la utawala, sekretarieti ya *TFF* na ile ya *ZFF* zipo kwenye mchakato wa kuandaa utaratibu (*road map*) wa kuboresha ushirikiano baina yao na kuimarishe utendaji kwa pande zote mbili.

Na. 128

**Wananchi Waliobuni au Kutunga Nyimbo
Zinazoitambulisha Nchi yetu**

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatambua na kuwaenzi wananchi wazalendo ambao walitumia vipaji vyao kubuni vitu au kutunga nyimbo ambazo zinatambulisha Taifa

letu na kuhamasisha uzalendo kama Nembo ya Taifa, Jina la Nchi yetu Tanzania, Wimbo wa Taifa na nyimbo nyingine za Kizalendo?

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la kuwatambua na kuwaenzi wananchi wazalendo ambao walitumia vipaji vyao kubuni na kutunga nyimbo ambazo zinatambulisha Taifa letu na kuhamasisha Uzalendo sio tu la kiungwana bali ni la kisera kadiri ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997; ambapo inahilmizwa uanzishwaji wa utaratibu wa kuwatambua na kuwaenzi wasanii maarufu wa Kitaifa; kwa kuwatambua na kuwapa tuzo wale wanaoonesha mafanikio makubwa katika Ubunifu, Utunzi na utendaji kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi zake za BASATA, TaSUBa, BAKITA, BODI YA FILAMU wameweka mikakati mbali mbali yenye lengo la kutambua na kuwatunza wananchi wote walitunga na kubuni vitu viliyoyolitambulisha Taifa letu. Moja ya mikakati hiyo ni kuanzisha tuzo mbalimbali kama vile, Tuzo za Muziki za Tanzania (*Tanzania Music Awards*), Tuzo za Filamu Tanzania (*Tanzania Film Awards*) na kwa sasa Serikali inapitia mikataba mbali mbali hasa ile ambayo wasanii wetu waliingia bila kufuata taratibu za Kisheria. Vilevile Serikali, imeongeza zaidi nguvu katika kufuatilia haki za wabunifu kwa kushirikiana na Chama cha Hakimiliki Tanzania (*COSOTA*) ili kuboresha mifumo pia kupitia Kamati ya Kutetea Haki za wasanii ambapo wabunifu hao au warithi wao watanufaika zaidi na ubunifu huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inao mkakati wa kuanzisha Tamasha kubwa kila mwaka likiwa na lengo la kuwaenzi wasanii nguli na wote waliobuni kazi za Sanaa zilizotukuka. Aidha Mkakati mwingine ni kuendelea kuzitumia

kazi zao za ubunifu na kuhifadhi kumbukumbu zao ili kujenga Taifa lenye Uzalendo na kurithisha kizazi cha sasa na kijacho, kama yalivyo matakwa kwenye sehemu ya 4.1.4 ya Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997.

Na.129

Hitaji la Vituo vya Polisi Kata za Lugubi, Itumba na Igunga

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Kata za Lugubi, Itumba na Igunga ni kata zenyе idadi kubwa ya watu na kuna matukio mengi ya uhalifu.

Je,ni kwa nini Serikali isijenge vituo vya Polisi katika Kata hizo ili kukabiliana na matukio ya uhalifu yanayoendelea siku hadi siku na kutishla maisha ya watu na mali zao?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la miundombinu katika kituo cha Polisi Igunga na kukosekana kwa vituo vya Polisi katika Kata za Itumba na Lugubi. Kituo hiki cha Polisi Igunga ndicho kinachohudumia wananchi wa Kata za Itumba na Lugubi zilizopo takribani umbali wa kilometra 40.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao,Jeshi la Polisi linaendesha operesheni za kiusalama ikiwa ni pamoja na doria za mara kwa mara kwa kushirikisha wananchi katika Mpango wa Ulinzi shirikishi ili kudumisha amani na usalama katika kata hizo. Aidha, kwa kuwa mahitaji ya ujenzi wa vituo vya Polisi nchini ni makubwa na yanahitaji rasilimali fedha nyingi, Jeshi la Polisi litatekeleza ujenzi wa vituo hivi kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo Wananchi na Taasisi nyinginezo.

Na. 130

**Askari wa Usalama Barabarani Kupiga Picha
Gari kwa Kificho**

MHE. ALI HASSAN OMAR KING aliuliza:-

Je, ni sahihi kwa askari wa Usalama barabarani kupiga picha magari yenye mwendokasi eneo moja kwa kificho na Askari mwingine kukamata magari haya eneo tofauti na tukio?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ali Hassan King-Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi pamoja na wajibu wake wa kulinda maisha na Mali ya wananchi pia linao wajibu wa kusimamia sheria na kuhakikisha kila mtu anatii sheria bila shuruti.

Katika utendaji kazi na kuhakikisha kuwa dhana ya utii wa sheria bila shuruti inatekelezwa. Jeshi la Polisi hutumia mbinu mbali mbali ili kubaini tabia za madereva wawapo barabarani na uhiari wa kutii sheria za barabarani.

Mheshimiwa Spika, kupiga picha gari iliyozidisha mwendo katika eneo moja tena ambalo askari huwa amejificha ni mojawapo ya mbinu za kuhakikisha madereva wanatii sheria bila shuruti na hivyo madereva wanao zidisha mwendo hupigwa picha na kisha kuituma kwa askari walio mbele ili kuweza kumkamata kwani askari mwenye speed camera huwa ni vigumu kupiga picha na kisha kulikamata gari hilo kwa wakati huo huo.

Na. 131

Hitaji la Chuo Cha Mafunzo ya Gesi- Mikoa ya Kusini

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA aliuliza:-

Mikoa ya Kusini ndiyo inayotoa gesi kwa wingi kwa sasa:-

Je, ni lini serikali itajenga Chuo cha kutoa mafunzo juu ya rasilimali hiyo na mafuta ili wananchi wa Mtwara na Lindi wapate fursa zaidi ya elimu ya gesi na mafuta?

WAZIRI WA NISHATI, alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 gesi iliyogunduliwa nchi kavu na baharini ni futi za ujazo trillioni 57.54. Ugunduzi wa gesi asilia umefanyika kuanzia mwaka 2010 katika vitalu Na. 1, 2, 3 na 4 vilivyopo katika maeneo ya kina kirefu cha bahari (*deep sea*) ambapo kuna futi za ujazo 47.27 TCF. Matumizi ya gesi asilia iliyogunduliwa Songo Songo na Mnazi Bay yalianza mwaka 2004 na mwaka 2006 sawia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (*TPDC*), Kampuni za Kimataifa za Mafuta na Gesi (*IOC's*) na Vyuo vya Ufundishadi (*VETA*) hutoa mafunzo kwa Watanzania wenye sifa, Wanafunzi na Wakufunzi ili kujenga uwezo wa kitaalamu kwa watanzania na kukidhi mahitaji ya Wataalam katika soko la ndani. Hadi sasa vyuo vya VETA katika Mikoa ya Lindi na Mtwara hutoa mafunzo ya kiufundi yanayohusu masuala ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa zaidi ya wahitimu 350 wa VETA wamepatiwa vyeti vinavyotambuliwa kimataifa (*International Accreditation*) ili kuwawezesha kupata ajira

katika Kampuni za Kimataifa za mafuta na gesi asilia nchini na nje ya nchi. Jitihada hizi zimegharimu takribani dola za Marekani milioni nne (\$4m).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufundisha Vijana kupitia VETA, *TPDC* kwa kushirikiana na Makampuni ya Gesi na Mafuta ya Kimataifa (*IOC's*) hutoa mafunzo kwa wajasiriamali ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma katika shughuli na Miradi ya Mafuta na Gesi Asilia. Hadi sasa wajasiriamali 195 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara wameshapatiwa mafunzo hayo. Serikali kupitia *TPDC* imefungua klabu 32 za mafuta na gesi katika shule za sekondari za Lindi na Mtwara kwa lengo la kutoa elimu inayohusu tasnia ya mafuta na gesi asilia pamoja na namna inavyoweza kuwanufaisha kupitia fursa zinazotengenezwa na tasnia hii katika maeneo yao.

Na. 132

Umeme Kufika Kwenye Mitaa yote ya Kibiti

MHE. ALLY S. UNGANDO aliuliza:-

Katika Jimbo la Kibiti umeme umefikia kwenye maeneo ya barabarani tu lakini sehemu kubwa ya mitaa ya Jaribu, Mpakani, Bungu, Pagae, Mtamanya, Kimbunga, Kibiti na maeneo mengine hakuna umeme.

(a) Je, ni sababu zipyi zilizosababisha umeme kufika kwenye barabara kuu tu na siyo kwenye mitaa yote ya Kijiji husika?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme kwenye mitaa yote ya Kibiti?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia taasisi zake za Wakala wa Nishati Vijiji (REA) na Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) inatekeleza miradi mbalimbali ya usambazaji umeme katika Wilaya ya Kibiti. Baada ya kazi ya kuunganishwa Wilaya ya Kibiti katika gridi ya Taifa kukamilika, TANESCO kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ilitenga fedha za kupeleka umeme katika vijiji 10 vya Wilaya ya Kibiti.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme unaoendelea umefanyika katika maeneo yote yenye mahitaji ya umeme ikiwemo maeneo ya mitaa, vijiji, vitongoji, taasisi na maeneo ya karibu na barabara. Hivyo siyo kwa maeneo ya barabarani tu. Hadi kufikia tarehe 15 Aprili, 2020, vijiji sita vya Tomoni, Kinyanya Jeshini, Mchonjogoro, Mchukwi A, Njiapanda Mchukwi na Lumyozi (Ikulu Ndogo) vilipatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa TANESCO inaendelea na kazi ya kupeleka umeme katika Viji 4 vya Makaoni, Nyatanga, Mbebetti B na Lukanga ambapo kazi hiyo itakamilika kabla ya mwezi Juni, 2020. Gharama za kupeleka umeme katika vijiji hivyo 10 ni Shilingi 495,776,011/=.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali kupitia REA inaendelea kupeleka umeme katika Wilaya ya Kibiti ambapo maeneo mbalimbali yalinufaika vikiwemo vijiji vya Kitembo na Mkupuka.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia REA pamoja na TANESCO itaendelea kusambaza umeme kupitia mradi wa ujazilizi Awamu ya II utakaoteklezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. TANESCO pia itaendelea na jukumu lake la kusambaza umeme katika mitaa na maeneo yenye mahitaji ya umeme.

SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

SPIKA: Moja kwa moja nimkaribishe Waziri wa Habari, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Tafadhali wasilisha hoja yako, una nusu saa, karibu. (*Makofii*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwasilishwa, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa kuwa ninachowasilisha hapa ni sehemu tu ya hotuba yangu, naomba hotuba yangu yote ya maandishi iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii mwanzoni kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutukutanisha tena hapa Bungeni tukiwa wenyewe afya na uzima na kuendelea kuijalia nchi yetu hali ya amani, utulivu na upendo. Hata hivyo, natambua Taifa letu na dunia kwa ujumla tunapitia katika kipindi kigumu cha janga la ugonjwa wa kutisha wa Homa Kali ya Mapafu unaosababishwa na virusi vya *Corona*. Natumia fursa hii kuendelea kuwakumbusha wananchi hususan wadau wa Wizara yangu kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sina budi kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna mnavyoendesha Bunge hili na ushirikiano mzuri mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu yangu katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee na kwa dhati kabisa, naomba kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunipa adhama kubwa ya kusimamia sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo zinazowagusa moja kwa moja vijana ambao ni takribani theluthi tatu ya Watanzania wote. Wizara yangu pia inawagusa Watanzania wa rika zote kwa namna tofauti. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi hiki cha kwanza cha Awamu ya Tano kama inavyoshuhudiwa kupitia hotuba mbalimbali za bajeti zinazoendelea kuwasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapatano Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/2021 kupitia Kikao cha tarehe 27 Machi, 2020. Wizara yangu itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, fauka ya hayo, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri mliyofanya katika miaka hii mitano ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nimpongeze pia Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu (Mbunge wa Singida Mashariki - CCM), kwa kuchaguliwa kujunga na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa na kuwezesha changamoto nyingi ambazo miaka ya nyuma zilionekana za kudumu, leo ni aridhio ya jana. Kwa mfano, mawasiliano kukatika kati ya Tarafa za Ntebelia na Unyakyusa kwa zaidi ya miezi 6 kila mwaka kutokana na maji mengi ya mvua na mafuriko kutokana na mito inayofurika na kukatiza Wilaya kuelekea Ziwa Nyasa na kuharibu barabara sasa ni historia baada ya

kukamilika kwa ujenzi wa barabara bora kiusanifu na kiujenzi ya Kikusya-Matema (km 39.5) yenye madaraja makubwa matatu na njia za ziada 277 za kuitisha maji mengi ya mvua na mafuriko; kukamilika kwa barabara hii, kunafungua fursa mpya kwa wana-Kyela kupata barabara ya uhakika kati ya Matema na Ikombe; ujenzi wa daraja la Ngorwa ili kuwapa wananchi barabara fupi ya moja kwa moja toka daraja jipya la Kagera, Lusungo hadi Matema; ujenzi wa gati la Matema kuegeshea meli za mizigo na abiria; na uanzishwaji wa hifadhi raski ya samaki wa mapambo eneo la Lyulilo, ndani ya Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa shukrani nisipompa kongole kwa niaba ya wana-Kyela wote, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio haya na mengine mengi ukiwemo mradi wa barabara ya Mbambo - Ipinda kuunganisha na barabara ya Kikusya - Matema ahadi ya Mheshimiwa Rais mwenyewe na miradi ya pamoja na Jamhuri ya Malawi. Pia ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha unaofanyika Kasumulu - Kyela na miradi mikubwa ya umeme na kilimo cha umwagiliaji ya Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia wanangu wapendwa George, Mosses na Peter kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kibunge na kifamilia.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Naibu Waziri wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Wana-Songwe hakika, wamepata jembe la kutumainiwa kwa kipindi kirefu kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, niwapongeze na kuwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara walioleuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais ambao ni Dkt. Hassan Abbas - Katibu Mkuu na Dkt. Ally Possi - Naibu Katibu Mkuu wameanza kazi kwa kasi na ubunifu mkubwa Wizarani. Niwashukuru pia

Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake walioko Makao Makuu hapa Dodoma na kote nchini kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, kwa tija na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, Bunge lako Tukufu limewapoteza Wawakilishi wenzetu wawili, Mheshimiwa Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijiji na Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge Viti Maalum. Nitumie fursa hii kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na wapiga kura wao.

Aidha, nitumie fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wasanii, wanamichezo n a wanahabari waliopoteza maisha katika kipindi hiki wakiwemo Wanahabari galacha, Marin Hassan Marin na Lutengano Haonga wa *TBC* na mwenzao Joseph Kambanga Meneja wa TEHAMA *TBC*. Mungu azilaze roho zao pamoja na za Wadau wengine wa sekta ninazosimamia mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/2020 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa niangalie kwa kifupi Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020. Nianze na Makusanyo ya Maduhuli. Mwaka 2019/2020, Wizara ilikadiria kukusanya Sh.959,905,000 ambapo Sh.918,176,330 zimekusanya hadi Machi, 2020 sawa na asilimia 96 ya lengo. Kwa upande wa Taasisi saba zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanya ni jumla ya Sh.37,324,804,000 ambapo hadi Machi, 2020 Sh.15,196,407,535 zilikusanya sawa na asilimia 41 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha ni kama ifuatavyo: Mwaka 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa Sh. 30,879,483,000 ambapo Sh.24,879,483,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Sh.6,000,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2020, Wizara ilipokea Sh.18,749,949,178 ambayo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh.18,249,949,178 ambayo ni sawa na asilimia 73 ya bajeti ya Matumizi ya kawaida, na Sh.500,000,000 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Hili limeelezwa kwa kina sehemu ya 3.2 ukurasa wa 12 - 84 wa hotuba yangu. Kwa muhtasari utekelezaji kupitia sekta na taasisi zilizo chini ya Wizara ullkuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Habari. Sekta hii inahusisha Idara ya Habari Maelezo ambaoo pia ndiyo Ofisi ya Msemajji Mkuu wa Serikali, Shirika la Utangazi Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (*TSN*) na Kamati ya Maudhui iliyopo chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Kwanza, Msemajji Mkuu wa Serikali, mbali na kufanya mikutano tisa (9) na wana habari alishiriki katika vipindi 31 vya redio na televisheni kwa lengo la kuelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kushirikiana kati ya Idara ya Habari na *TBC* jumla ya vipindi 51 vya TUNATEKELEZA viliratibiwa na kurushwa hewani kupitia *TBC* ambavyo viliwawezesha Wakuu wa Mikoa 15 na Wakuu wa Taasisi za Umma 36 kuelezea kwa umma kuhusu sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali na fursa zilizopo za kuwaletea wananchi maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu, katika kutekeleza azma ya kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika kuwekeza kwenye uchapishaji wa magazeti/majarida ili kupanua wigo

wa upatikanaji wa habari kwa wananchi, jumla ya magazeti/majarida 233 yalisajiliwa hadi Machi, 2020 ambapo ya sekta binafsi ni 181 ambayo ni asilimia 78 na Serikali na Taasisi zake ni 52 ambayo ni asilimia 22. Katika kipindi hiki (2019/2020), leseni mpya 18 zilitolewa kwa ajili ya magazeti/majarida ambapo 14 zilitolewa kwa wamiliki binafsi na nne (4) kwa Taasisi za umma. Aidha, leseni 43 za magazeti/majarida zimehuishwa hadi Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, nne, Wizara imeratibu jumla ya Mikutano ya Waandishi wa Habati (*Press Conference*) 38 ikihusisha Wizara na Taasisi nyingine za Serikali kwa ajili ya kutoa taarifa mbalimbali kwa wananchi pamoja na kuratibu ushiriki wa Vyombo vya Habari katika Matukio mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ikiwa ni lengo la kuongeza weledi wa kitaaluma kufanya tasnia ya habari kuwa taaluma kamili na iheshimike kama taaluma nyingine, Kifungu cha 67(b) cha Sheria ya Huduma za Habari Namba 12 ya mwaka 2016 kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 17(20)(a) ya Kanuni za Sheria ya Huduma za Habari 2017 kwa pamoja kinawataka wanahabari wote kuijendeleza na kuwa na sifa ya kitaaluma ya angalau stashahada (*diploma*) ndani ya kipindi cha miaka mitano baada ya kuanza kwa sheria hiyo iliyoanza kutumika rasmi tarehe 31 Desemba 2016. Kwa kuwa kipindi hiki cha miaka mitano kinakwisha mwezi Desemba, 2021, natumia nafasi hii kutoa wito kwa waandishi wote wa habari nchini ambao bado hawajajiendeleza kielimu ili kukidhi matakwa ya sheria wafanye hivyo kwa muda uliosalia ili wawze kuendelea na kazi ya uandishi wa habari baada ya muda huu wa mpito kuisha. Kipekee nawapongeza wengi walioitikia wito na kwa sasa wanajiendeleza au wameshamaliza masomo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TBC*, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha usikivu wa redio za *TBC* (Taifa na FM) ambapo mwaka 2017 tulizifikia Wilaya 87 asilimia 54 tu na mwaka 2019 tukafika Wilaya 102 (asilimia 63). Tatizo la nchi yetu ni hali ya milima/miinuko inayofanya

mawimbi ya *FM* tunayotumia sasa yasifike kila sehemu sawia hivyo kuilazimu *TBC* ihakiki maeneo yote mara kwa mara na kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, pamoja na kufunga mitambo ya kurushia matangazo Wilaya za mipakani za Nyasa, Rombo, Kibondo, Tarime na Longido mwaka juzi na kuweka mtambo mkubwa wa Watt 1000 Geita ambao umewezesha matangazo kufika maeneo ya Bukombe, Chato, Geita Mjini, Geita Vijiji, Kahama, Nyang'wale na baadhi ya maeneo ya Biharamulo, bado *TBC* italazimika kufanya tathmini katika maeneo yote hayo ili kubaini changamoto na kuchukua hatua zaidi za kiufundi pale ambapo mawimbi yanashindwa kufika kwa sababu moja au nyingine. Ndiyo maana pamoja na kwamba ukarabati unaendelea wa mitambo yetu mikubwa ya kurushia matangazo Mnyuzi (Tanga), Lushoto, Mabungo (Moshi), Manyara, na kadhalika bado Bumbuli, Mlalo, Rombo, maeneo mbalimbali ya Longido, Manyara na kadhalika yatahitaji mitambo ya ziada kuongezea nguvu kutokana na tatizo hilo la kijiografia.

Mheshimiwa Spika, tayari, katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Njombe, pamoja na Zanzibar (Unguja na Pemba) yamefanyika maainisho ya kiufundi (*technical specifications*) yatakayofuatiwa na ununuzi wa mitambo na vifaa kwa lengo la kuongeza usikivu katika maeneo hayo. Miradi mingine itakayoteklezwa na *TBC* kwa fedha kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ni Upanuzi wa Usikivu katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero, Ludewa na Morogoro Vijiji. Kukamilika kwa kazi hii kutawezesha kuongezeka usikivu wa *TBC* (Taifa na FM) hadi Wilaya 125 ambayo ni asilimia 78 mwaka huu 2020.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Machi, 2020 *TBC* ilizindua rasmi mfumo mpya wa utoaji habari uitwao ARIDHIO. Mfumo huu umetimiza ahadi niliyoitoa hapa Bungeni kuwa *TBC* itafanya maboresho na mageuzi makubwa katika kupeleka ujumbe kwa watazamaji. Nitumie fursa hii, kuwapongeza *TBC* kwa ubunifu na mapinduzi makubwa katika upashanaji habari kuitia mfumo

huo mpya wa uandaaji na urushaji wa taarifa ya habari ya dakika 120 iliyosheheni uchambuzi wa kina, matukio mubashara na kwenye studio zilizoboreshwa zenye muonekano wa kisasa. Hakika ARIDHIO imekuwa mrindimo katika nyoyo za Watanzania kwa sasa, hiyo ndio *TBC*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Chaneli ya Safari inayojikita katika maudhui ya utalii, utamaduni na historia ya nchi yetu, iliendelea kuimarishwa kwa kuajiri watumishi wapya 28 na kununua vifaa mbalimbali yakiwemo magari kwa ajili ya kupiga picha kwenye vivutio mbalimbali, kamera 12, droni mbili (2) na transiva. Chaneli hii tayari kwa sasa inaonekana katika visumbuzi vyote vilivyopo nchini pamoja na mitando ya kijamii. Kupitia *DSTV* inaonekana katika nchi za Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Somalia, Malawi, Congo, Zambia na Uganda.

Aidha, kupitia *ZUKU* inaonekana katika nchi za Zambia, Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kupitia *AZAM TV*, inaonekana katika nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, licha ya hayo *TBC* imeanzisha program Tumizi *App* ili kuwezesha maudhui ya chaneli hii kuwafikia watu wengi zaidi duniani ambapo hadi kufikia Juni mwaka huu maudhui yatarushwa kupitia program hii katika lugha mbalimbali za kimataifa zikiwemo Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kijeumanzi na Kiitaliano. Hiyo ndio *TBC*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa jengo la *Studio* Televisheni za *TBC* katika eneo la Mikocheni Jijini Dar es Salaam kwa ufadhili wa Serikali ya Korea Kusini pia umeanza kutekelezwa na mitambo inayofaaa kwa ajili ya mradi huu imeshawasili nchini. Mradi huu ambao utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2020 na kugharimu shilingi bilioni 2.38, utaiwezesha *TBC* kuwa na *Studio* zenye ubora na za kisasa kwa shughuli za utangazaji. Ni faraja kubwa kwa Serikali kufanikisha masuala makubwa wa matatu kwa upande wa Televisheni ya *TBC*.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni upatikanaji wa Televisheni ya *TBC* nchini kote ili mradi mwananchi ana kisumbuzi cha aina yoyote ile, kishikwambi au simu janja. Pili muonekano wa *TBC* umeboreshwa vizuri sana na tatu mwananchi anapata matangazo yenye maudhui ya Kitaifa bila kulipia ili kulinda matakwa ya kikatiba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 77, chini ya Ibara ya 18(d) inayompa kila mtu haki ya kupata taarifa wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti *TSN* iliendelea kuboresha maudhui na mwonekano wa magazeti yake ili kumudu ushindani katika soko la bidhaa na ukamilisha wa ufungaji wa mtambo mpya na wa kisasa ambao umeanza kuchapisha vitabu, kalenda na machapisho mengine ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TCRA* zimesajiliwa radio nane binafsi na ya jamii moja na televisheni binafsi 15; 14 za maudhui ya kulipa *content by subscription* na moja ya maudhuhi yanayotazamwa bila kulipia yaani *free to air*.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Tanzania na jumla ya televisheni zilizosajiliwa 44 ambapo za umma ni tatu tu, sawa na asilimia 7%; binafsi ni 38, sawa na asilimia 86; na za halmashauri ni tatu, sawa na 7%. Upande wa redio tuna jumla ya vituo vya redio 186 nchini ambapo vya umma ni viwili tu, sawa na asilimia moja; vya halmashauri ni tisa, ambayo ni 5%, vya kijamii ni 11, sawa na 6% na binafsi ni 164, sawa na asilimia 88. Mbali ya hayo nchi yetu ina televisheni za mitandaoni *online TV* 264, redio mtandaoni 22, *blogs* 85, siongezi neno hapo mambo yanajieleza yenyewe Wanasheria wana msemo *res ipsa loquitur*.

Mheshimiwa spika, kuhusu maendeleo ya utamaduni; nimesikia kengele, naomba sasa nieleze kwa kifupi, kuhusu utamaduni, tulikuwa na mgogoro wa muda mrefu wa takribani miaka 49, Chuo cha Ufundji Arusha na

Wazee wa kimila wa Kimasai. Napenda kukueleza kwamba tumeumaliza mgogoro huo. Vilevile kwenye maendeleo ya sanaa, tulikuwa na mgogoro wa umiliki wa eneo la Mwenge kati ya wachonga vinyago na wafanyabiashara. Uamuzi wa Serikali ni kulikabidhi eneo hilo kwa Baraza la Sanaa (BASATA) ili litumike kwa faida ya makundi yote yaliyokuwa yanagombana kwa miaka yote 33, kinachosubiliwa na Mamlaka husika kukabidhi hati ya eneo hilo kwa BASATA.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa suala la michezo kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi nydingine inakamilisha andiko la ujenzi la uwanja wa ndani ambao ni *Sports and Arts Arena*. Mradi utatekelezwa kwa kushirikisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema michezo ni kiwanda kikubwa sana kinachobeba ajira lukuki hususan kwa vijana wetu na hivyo basi ni kiwanda chenye mamilioni ya wadau ambacho hakina budi kuchangia katika maendeleo ya uchumi ya nchi. Katika muktadha huo, Serikali imehakikisha michezo inapewa fursa kwenye mitaala ya shule, lakini vilevile kila mwaka lazima tufanye mashindano ya shule za msingi na sekondari; UMITASHUMITA na UMISETA. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunaibua vipaji vingali vichanga kwa lengo kwa kuviendeleza, viweze kuonekana na kutumika Kimataifa na vilevile kupeperusha bendera ya Tanzania katika michezo mbalimbali.

Kwa kuwa michezo ya kulipwa inazidi kuongezeka nchini, tunao wajibu kama Taifa kuwa na utaratibu unaofanana kimaudhui kwa michezo yote na kuruhusu wachezaji wa kigeni kuchzeza vilabu vyetu, lakini kuendana na misingi ya kulinda na kuendeleza fursa za ajira kwa Watanzania kama ilivyo katika uwekezaji wowote hapa nchini. Tutaua vipaji vya ndani kuachia milango wazi kwa wachezaji wa nje bila ukomo wenye tija na tunaufanya mchango wa Serikali kuititia UMITASHUMTA na UMISETA ukose maana yoyote na msisitizo wa vilabu kuona timu za vijana nao ukose mashiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeiagiza BMT iliangalie suala hili lakini iwe shirikishi na kufikia tarehe 15 mwezi ujao tuwe tumeshapata majibu ya mwelekeo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda nimesikia kengele ikigonga, naomba tu nieleze tu kwamba, kwa mwaka 2020/2021 Wizara imetengewa bajeti ya Sh.40,140,641,000 na kati ya fedha hizo mishahara ni Sh.20,979,231,000. Matumizi mengine ni Sh.11,446,410,000 na miradi ya maendeleo ni Sh.7, 715,000,000. Kiambatisho namba tisa ni mgawanyo wa bajeti ya Wizara na Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kuteleleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2021 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liliidhie na kuidhinisha bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/2021 yenye jumla ya Sh. 40,140,641,000. Kati ya fedha hizo mishahara ni Sh.20,979,231,0000; matumizi mengine ni Sh.11,446,400,0000 na miradi ya maendeleo ni Sh. 7,715,000,000.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kueleza kwamba, Wizara imepata mafanikio makubwa katika miaka mitano, ni matokeo ya maono na juhudhi kwa kweli binafsi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Kiongozi nguli na ngalacha mwenye maono ya mbele na mbali.

Katika hii miaka mitano kwa kweli ametusaidia sana kutoa fedha nyingi kusaidia michezo na wasanii, amekutana na wanahabari, amewaita wasanii lkulu, ameungana na wanautamaduni. Niseme lipi zaidi ya hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wasaidizi wake vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunawapa kongole maalum kwa kuwa nasi kila tunapowahitaji. Nimalizie kwa kuzishukuru sana Taasisi za Kimataifa zote zilizotusaidia na niishie hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena natoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ambazo mnazijua.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyezekiti wa Kamati, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena kwenye Bunge lako Tukufu tukiwa wenge afya na uzima, na kuendelea kuijalia nchi yetu hali ya amani, utulivu na upendo. Hata hivyo, ninatambua Taifa letu na dunia kwa ujumla tunapitia katika kipindi kigumu cha janga la ugonjwa wa kutisha wa Homa Kali ya Mapafu (Covid-19) unaosababishwa na virusi vya Corona. Natumia fursa hii kuendelea kuwakumbusha wananchi wote na hususan wadau wa Wizara yangu kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huu kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa Afya.

3. *Mheshimiwa Spika*, Sina budi kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge

wote kwa ushirikiano mzuri mnaonipa, unaoniwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu yangu katika Bunge hili Tukufu.

4. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee na kwa dhati kabisa, naomba kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunipa adhama kubwa ya kusimamia sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zinazowagusa moja kwa moja vijana ambaao ni takribani theluthi tatu ya Watanzania wote. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata katika kipindi hiki cha kwanza cha Awamu ya Tano kama inavyoshuhudiwa kupitia hotuba mbalimbali za Bajeti zinazoendelea kuwasilishwa hapa Bungeni.

5. *Mheshimiwa Spika*, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/21 kupitia Kikao cha tarehe 27 Machi, 2020. Wizara yangu itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2020/21.

6. *Mheshimiwa Spika*, fauka ya hayo, nitumie fursa hii kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyosimamia vyema Bunge hili ambalo ni mhimili muhimu kwa maendeleo ya watu na Taifa letu kwa ujumla. Aidha, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wake kwa kazi nzuri waliyoifanya katika miaka hii mitano ya kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili. Nimpongeze pia Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu (Mbunge wa Singida Mashariki, CCM), kwa kuchaguliwa kuijunga na Bunge lako Tukufu.

7. *Mheshimiwa Spika*, nitumie pia fursa hii kuvishukuru na kuvipongeza Vyombo vyaa Habari vyaa redio, televisheni, magazeti, majarida na mitandao ya kijamii kwa kuendelea

kuhabarisha, kuburudisha na kuuelimisha umma kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini hususan mageuzi makubwa ya kuchumi yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwaleta wananchi maendeleo na masuala ya kimataifa bila kusahau wajibu tulionao kama Taifa wa kulinda utamaduni wetu.

Pamoja na vyombo vya habari, nawapongeza pia wasanii, vikundi vya sanaa, wanautamaduni na wanamichezo kwa kuitangaza na kuiweka nchi yetu katika tawira nzuri na kwa ushirikiano wa karibu na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake.

8. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii adhimu niwashukuru wananchi wa Jimbo la Kyela kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa na kuvezesha changamoto nydingi ambazo miaka ya nyuma zillionekana za kudumu, leo ni aridhio ya jana: mawasiliano kukatika kati ya Tarafa za Ntebelia na Unyakyusa kwa zaidi ya miezi 6 kila mwaka kutohakana na maji mengi ya mvua na mafuriko ya mito kadhaa inayokatiza Wilaya kuelekea Ziwa Nyasa na kuharibu barabara, sasa ni historia baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara bora kiusanifu na kiujenzi ya Kikusya-Matema (km 39.5) yenye madaraja makubwa matatu (3) na njia za ziada 277 za kupitisha maji mengi ya mvua na mafuriko.

Kukamilika kwa barabara hii, kunafungua fursa mpya kwa wana-Kyela kupata barabara ya uhakika kati ya Matema na Ikombe; ujenzi wa daraja la Ngorwa ili kuwapa wananchi barabara fupi ya moja kwa moja toka daraja jipya la Kagera, Lusungo hadi Matema; ujenzi wa gati la Matema kuegeshea meli za mizigo na abiria; na uanzishwaji wa hifadhi rasmi ya samaki wa mapambo eneo la Lyulilo, ndani ya Ziwa Nyasa.

Nitakuwa mtovu wa shukrani nisipompa kongole kwa niaba ya wana-Kyela wote, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio haya na mengine mengi ukiwemo mradi wa barabara ya Mbambo-Ipinda kuunganisha na barabara ya Kikusya-Matema (ahadi ya Mheshimiwa Rais mwenyewe) na miradi ya pamoja na

Jamhuri ya Malawi: ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha unaofanyika Kasumulu, Kyela na miradi mikubwa ya umeme na kilimo cha umwagiliaji ya Bonde la Mto Songwe.

Niwashukuru pia wanangu wapendwa George, Mosses na Peter kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kibunge.

9. *Mheshimiwa Spika*, sina budi kumshukuru kwa dhati Mhe. Juliana Daniel Shonza (Mb.), Naibu Waziri wa Wizara yangu kwa msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Wana-Songwe hakika, wamepata jembe la kutumainiwa kwa kipindi kirefu kijacho. Aidha, niwapongeze na kuwashukuru watendaji wakuu wa Wizara walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais ambao ni Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu na Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu ambapo wameanza kazi kwa kasi na ubunifu mkubwa ambao pamoja na mambo mengine, umesaidia kukamilika mapema kwa maandalizi ya hotuba tunayoiwasilisha Bungeni leo. Niwashukuru pia Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake walioko Makao Makao hapa Dodoma na kote nchini kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi.

10. *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2019/20 Bunge lako Tukufu liliimpoteza mwakilishi mwenzetu, Mheshimiwa Rashid Akbar, Mbunge wa Newala Vijiji (CCM). Nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Newala Vijiji. Aidha, nitumie fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wasanii, wanamichezo na wanahabari waliopoteza maisha katika kipindi hiki ikiwemo Mwanahabari galacha, Marin Hassan Marin wa TBC. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, AMINA.

11. *Mheshimiwa Spika*, Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2019/20 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2020/21.

12. *Mheshimiwa Spika*, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu nane (8): Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2019/20 na Sehemu ya Nne inaeleza changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2020/21; Sehemu ya Sita ni Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21; Sehemu ya Saba ni Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Mwaka 2020/21 na Sehemu ya Nane ni Shukrani kwa Wadau mbalimbali wa Wizara.

2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

13. *Mheshimiwa Spika*, Dira ya Wizara ni kuwa na Taifa linalohabarishwa vizuri, liliohamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za Sanaa na lenye umahiri mkubwa katika michezo ifikapo Mwaka 2025.

14. *Mheshimiwa Spika*, Dhima ya Wizara ni kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa Habari, kukuza Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya Jamii kiuchumi.

Majukumu ya Wizara

15. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango mbalimbali ya Serikali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Wizara inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbalimbali zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Aidha, Wizara inasimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Programu ya Urihi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na pia Kamati ya Maudhui ambayo kimuundo ipo chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Vilevile, Wizara ina jukumu la kuimarisha rasilimaliwatu ili kuwezesha majukumu na malengo ya Wizara kufikiwa kwa ufanisi na tija.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2019/20

3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

16. *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2019/20, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tisa Hamsini na Tisa, Mia Tisa na Tano Elfu (Sh.959,905,000) kutokana na vyanzo mbalimbali vinavyotoka kwenye Idara ya Maendeleo ya Michezo na Idara ya Habari-MAELEZO. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa Kumi na Nane, Mia Moja Sabini na Sita Elfu, Mia Tatu Thelathini (Sh. 918,176,330) sawa na asilimia 96 ya lengo.

17. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni jumla ya Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tatu Ishirini na Nne, Mia Nane na Nne Elfu (Sh.37,324,804,000) ambapo hadi mwezi Machi, 2020 Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Moja Tisini na Sita, Mia Nne na Saba Elfu, Mia Tano Thelathini na Tano (Sh.15,196,407,535) zilikusanywa sawa na asilimia 41 ya lengo la mwaka. Kuongezeka kwa ushindani katika biashara za huduma za utangazaji ikiwemo magazeti (*print media*) kutokana na kasi ya ukuaaji wa teknolojia katika Sekta ya habari hususan matumizi ya mitandao ya kijamii katika utoaji wa matangazo ni baadhi ya sababu zilizoathiri ukusanyaji wa mapato.

3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

18. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2019/20, Wizara iliidhinishiwa Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Mia

Nne Themanini na Tatu Elfu (Sh.30,879,483,000) ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Mia Nane Sabini na Tisa, Mia Nne Themanini na Tatu Elfu (Sh.24,879,483,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ikijumuisha Mishahara Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Nne Themanini na Tatu, na Sabini na Tatu Elfu (Sh.15,483,073,000) na Matumizi Mengineyo Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Mia Nne Kumi Elfu (Sh.9,396,410,000). Miradi ya Maendeleo iliodhinishiwa Shilingi Bilioni Sita (Sh. 6,000,000,000). Miradi hiyo ni:

- a) Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) uliodhinishiwa Shilingi Bilioni Tano (5,000,000,000); na
- b) Habari kwa Umma, uliodhinishiwa Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000)

19. *Mheshimiwa Spika*, hadi mwezi Machi, 2020 Wizara ilipokea Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Saba Arobaini na Tisa, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu, Mia Moja Sabini na Nane (Sh.18,749,949,178) ambayo ni sawa na asilimia 61 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Mbili Arobaini na Tisa, Mia Tisa Arobaini na Tisa Elfu, Mia Moja Sabini na Nane (Sh.18,249,949,178) ambayo ni sawa na asilimia 73 ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Saba Themanini na Nane, Mia Nne Themanini na Tisa Elfu, Mia Tisa (Sh.10,788,489,900) ni Mishahara sawa na asilimia 70 ya bajeti ya Mishahara na Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nne Sitini na Moja, Mia Nne Hamsini na Tisa Elfu, Mia Mbili Sabini na Nane (Sh.7,461,459,278) ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 79 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo.

20. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Wizara tayari imepokea Shilingi Milioni Mia Tano (Sh.500,000,000) kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Habari kwa Umma sawa na asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa mradi huo. Aidha, kuhusu Shilingi Bilioni Tano kwa ajili ya kuboresha Usikivu wa TBC, Wizara ya Fedha na Mipango

imeshatoa kibali kwa TBC kuanza mchakato wa ununuzi wa vifaa mbalimbali ili fedha zilizotengwa zitolewe katika robo hii ya nne ya mwaka huu wa fedha.

3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20

3.2.1 SEKTA YA HABARI

21. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Sekta ya Habari ni pamoja na kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya mwaka 2016 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miradi mbalimbali inayotekelizwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo.

22. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni hatua ya kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali na kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali, Msemaji Mkuu wa Serikali alifanya mikutano tisa (9) na waandishi wa habari na alishiriki katika vipindi 31 vya Redio na Televisheni.


23. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha upatikanaji wa habari kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Wizara kwa kushirikiana na TBC iliendelea kuratibu kipindi cha "TUNATEKELEZA" kinachorushwa hewani kupitia TBC, ambapo jumla ya vipindi 51 vilitangazwa. Kupitia kipindi hiki, jumla ya Wakuu wa Mikoa 15 na Wakuu wa Taasisi za Umma 36 walipata fursa ya kuelezea Umma kuhusu hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, Wizara iliratibu jumla ya mikutano ya Waandishi wa Habari (*press conferences*) 38 zikihusisha Wizara na Taasisi nyingine za Serikali ambapo taarifa mbalimbali zilitolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari. Fauka ya hayo, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Maofisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano Serikalini (TAGCO) ilichapisha nakala 5,000 za Jarida Maalumu la *NCHI YETU* liliilosheheni mafanikio ya Miaka

Minne ya Serikali ya Awamu ya Tano na kuzisambaza nakala hizo kwa wadau mbalimbali.

24. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza azma ya kuhakikisha Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika kuwekeza kwenye uchapishaji wa magazeti/majarida ili kupanua wigo wa upatikanaji wa habari kwa wananchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Tanzania ilikuwa na jumla ya magazeti/majarida 233 yaliyosajiliwa, ambapo yanayomilikiwa na Sekta Binafsi ni 181 (78%) na Serikali na Taasisi zake ni 52 (22%). Katika kipindi hiki (2019/20), leseni mpya 18 zilitolewa kwa ajili ya magazeti/majarida ambapo 14 zilitolewa kwa wamiliki binafsi na nne (4) kwa Taasisi za umma. Aidha, leseni 43 zilihuishwa. Vilevile, ili kuwapa waandishi wa habari fursa ya kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, jumla ya vitambulisho (*Press Cards*) 494 vilitolewa kwa waandishi wa habari ambapo katika hao 487 ni wa ndani ya nchi na 7 ni kutoka nje ya nchi.

Kielelezo Na. 1: Magazeti na Majarida Yaliyosajiliwa hadi Machi, 2020.



25. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 67(b) cha Sheria ya Huduma za Habari Namba 12 ya Mwaka 2016 kinawataka wanahabari wote kuijendeleza na kuwa na sifa ya kitaaluma

ya angalau Stashahada (*Diploma*) ndani ya kipindi cha miaka mitano baada ya kuanza kwa Sheria hiyo. Kwa kuwa kipindi hiki cha miaka mitano kinakwisha mwezi Desemba 2021, natoa wito kwa waandishi wa habari ambao bado hawajajiendeleza kielimu ili kukidhi matakwa ya sheria wafanye, hivyo ili waweze kuendelea na kazi ya uandishi wa habari baada ya muda huu wa mpito kuisha.

Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji wa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria hii. Chombo kingine kinachopaswa kuundwa ni Baraza Huru la Habari ambalo litaundwa na wanahabari wenyewe baada ya kuanzishwa kwa Bodi ya Ithibati. Majukumu ya Baraza hili ni pamoja na kuandaa Kanuni za maadili ya taaluma ya wanahabari kwa kushirikiana na Bodi ya Ithibati na kushughulikia malalamiko mbalimbali ya maudhui chini ya Kamati ya Malalamiko illyoundwa ndani ya Baraza.

26. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo Maofisa Habari Serikalini ikiwa ni hatua ya kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na wananchi katika ngazi zote. Katika kutekeleza azma hii, jumla ya Maofisa Habari 244 kutoka Serikali Kuu, TAMISEMI na Taasisi nyngine za Serikali walipatiwa mafunzo mkoani Dodoma mwezi Septemba na Desemba, 2019. Mafunzo yalijikita katika masuala ya mbinu za upigaji picha za mnato na jongeju; ubunifu katika uandishi wa taarifa kwa umma na habari za Serikali; namna ya uwekaji taarifa katika tovuti za Halmashauri pamoja na matumizi ya mitandao ya kijamii katika kutangaza shughuli za Serikali.

27. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu ushiriki wa vyombo vyta ya habari katika matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya SADC; Mikutano ya Mawaziri wa Kisikta wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa Sekta za Viwanda, Mawasiliano, Afya, Utalii, Kazi, Ajira na Mazingira na Tamasha la Nne la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) liliofanyika Dar es Salaam mwezi Septemba, 2019.

3.2.1.1 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

28. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni pamoja na kutoa huduma ya utangazaji kwa kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha. Shirika hili linamiliki vituo vitatu vya televisheni vya TBC₁, TBC₂ na TBC₃ (*Tanzania Safari Channel*) na kwa upande wa redio linamiliki idhaa tatu za TBC_{Taifa}, TBC_{FM}, na TBC_{International}. Shirika linamiliki pia studio za redio za Kanda zilizopo Arusha, Dodoma, Kigoma, Lindi na Songea na lina mifumo ya utangazaji ya kielektroniki kama vile tovuti na programu tumizi (App) zinazowezesha redio na televisheni za TBC kupatikana duniani kote kuititia mtandao wa intaneti.

29. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha usikivu wa redio za TBC (Taifa na FM) ambapo mwaka 2017 tuliweza kuzifikia Wilaya 87 (asilimia 54) na mwaka 2019 Wilaya 102 (asilimia 63). Tatizo la nchi yetu ni hali ya milima/miinuko inayofanya mawimbi ya FM tunayotumia sasa yasifike upande wa pili wa milima hivyo kuilazimu TBC ihakiki maeneo yote kwa uangalifu mkubwa. Hivyo, pamoja na kufunga mitambo ya kurushia matangazo Wilaya za mipakani za Nyasa, Rombo, Kibondo, Tarime na Longido mwaka juzi na kuweka mtambo mkubwa wa Watt 1000 Geita ambao umewezesha matangazo kufika Bukombe, Chato, Geita Mjini, Geita Vijiji, Kahama, Nyang'wale na baadhi ya maeneo ya Biharamulo, bado TBC italazimika kufanya tathmini katika maeneo yote ili kubaini changamoto na kuchukua hatua pale ambapo mawimbi yanashindwa kufika kwa sababu moja au nyininge ya kiufundi. Ndio maana Mhesimiwa Spika pamoja na kwamba ukarabati unaendelea wa mitambo yetu mikubwa ya kurushia matangazo Mnyuzi (Tanga), Lushoto, Mabungo (Moshi), Manyara, n.k, bado Bumbuli, Mlalo, Rombo, maeneo mbalimbali ya Longido, Manyara, n.k yatahitaji mitambo ya ziada ya kuongezea nguvu kutohana na tatizo hilo la kijiografia.

Tayari, katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Njombe, pamoja na Zanzibar (Unguja na Pemba) yamefanyika maainisho ya kiufundi (*technical specifications*) yatakayofuatiwa na

ununuzi wa mitambo na vifaa kwa maeneo hayo tu. Miradi mingine inayotekelawa na TBC kwa fedha kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ni Upanuzi wa Usikivu katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero, Ludewa na Morogoro Vijijini. Kukamilika kwa kazi hii kutawezesha kuongeza usikivu wa TBC hadi Wilaya 125 (78%) mwaka 2020.

30. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 30 Machi, 2020 TBC ilizindua rasmi mfumo mpya wa upashanaji habari nchini uitwao ARIDHIO. Mfumo huu umetimiza ahadi nilioitoa hapa Bungeni kuwa TBC itafanya maboresho na mageuzi makubwa katika kupeleka ujumbe kwa watazamaji. Nitumie fursa hii, kuwapongeza TBC kwa ubunifu na mapinduzi makubwa katika upashanaji habari kupitia mfumo huo mpya wa uandaaji na urushaji wa taarifa ya habari ya dakika 120 iliyosheheni uchambuzi wa kina, matukio mubashara na kwenye studio iliyoboreshwa na kuwa ya kisasa. Hakika ARIDHIO imekuwa mrindimo katika nyoyo za Watanzania kwa sasa.

31. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha TBC inakuwa na studio zenyé ubora kwa ajili ya shughuli za utangazaji, Shirika hilo linaendelea na ujenzi wa jengo la studio za televisheni katika eneo la Mikocheni, Jijini Dar es Salaam. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea Kusini. Aidha, jiwe la msingi la ujenzi wa mradi liliwekwa na Mhe. Harrison G. Mwakyembe (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tarehe 30 Machi, 2020 na ujenzi ulianza mwezi Februari, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2020. Mitambo na vifaa kwa ajili ya mradi huu vimeshawasili nchini. Kukamilika kwa mradi huu kunatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 2.38 na hivyo kuwezesha TBC kumiliki studio za televisheni za kisasa kwa ajili ya shughuli za utangazaji.

32. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha Chaneli ya Safari inayojikita katika maudhui ya utalii, utamaduni na historia ya nchi yetu, TBC imefanya yafuatayo:

a) Kuajiri watumishi wapya 28;

- b) Kununua vifaa mbalimbali, yakiwemo magari mawili (2) maalumu kwa ajili ya kupiga picha kwenye vivutio mbalimbali, kamera 12, droni mbili (2) na transiva; na
- c) Kukamilisha mchakato wa kuingia mkataba na watozi binafsi watakaoanda vipindi ili kupanua wigo na uanuwai wa maudhui ya utalii.

33. *Mheshimiwa Spika*, Chaneli hii inayotangaza vivutio vyetu vya utalii na utamaduni wetu nje ya nchi, tayari kwa sasa inaonekana katika visimbuzi vyote vilivyopo nchini pamoja na mitandao ya kijamii. Aidha, chaneli inaonekana kupitia DSTV katika nchi za Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Somalia, Malawi, Congo, Zambia na Uganda na kupitia ZUKU katika nchi za Zambia, Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, kupitia AZAM TV, chaneli hii inaonekana katika nchi zote za Afrika Mashariki na kwa sasa TBC inakamilisha makubaliano na kampuni ya "Etisalat" ili chaneli ioneokane katika nchi za Asia ifikapo Juni, 2020.

34. *Mheshimiwa Spika*, ili chaneli hii iwafikie watu wengi zaidi duniani, TBC imeanzisha programu tumizi (*App*) ili kurusha maudhui yake mtandaoni. Aidha, kufikia Juni, 2020 maudhui katika programu tumizi yatarushwa katika lugha mbalimbali za kimataifa zikiwemo Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kijerumanji na Kiitaliano.

35. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mkataba baina ya TBC na Star Times Techonologies ya China wa uendeshaji wa Kampuni ya Ubia ya Star Media Tanzania Limited. Kufuatia hatua zilizochukuliwa, tarehe 8 Januari, 2020 Kampuni hii ya Ubia ilitoa gawio kwa Serikali kwa mara ya kwanza kiasi cha Shilingi Milioni 500 na imeanza kuilipa TBC Shilingi Milioni 500 kati ya fidia ya Shilingi Bilioni 3 iliyotokana na kutozingatia baadhi ya vipengele vya Mkataba wa Ubia. Mwelekeo wa Kampuni kwa sasa ni kuimarisha utendaji ili kutengeneza faida na ushirikiano katika Ubia.

Ni faraja kubwa kwa Serikali kufanikisha masuala makubwa matatu upande wa televisheni ya TBC: kwanza ni upatikanaji wa TBC nchini kote alimradi mwananchi ana kisimbuzi cha aina yoyote ile, kishikwambi au simu janja; pili muonekano wa TBC umeboreshwa vizuri sana na tatu mwananchi anapata matangazo yenyewe maudhui ya kitaifa bila kulipia ili kulinda matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, chini ya Ibara ya 18(d) inayompa kila mtu haki ya kupata taarifa wakati wowote.

36. *Mheshimiwa Spika*, TBC imepatiwa eneo mkoani Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu yake kwenye eneo liliopo katika Kata ya Mtumba, Mtaa wa Vikonde B lenye jumla ya ekari 60. Kazi inayoendelea kwa sasa ni kuboresha michoro ya majengo yatakayojengwa katika eneo hilo inayofanywa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi ambayo inatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Aprili, 2020.

3.2.1.2 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)

37. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya TSN ni pamoja na kuchapisha na kusambaza magazeti ya Serikali ambayo ni *Daily News*, *Sunday News*, *HabariLeo* na *SpotiLeo*. Aidha, TSN inamiliki tovuti ambazo huzitumia kutoa habari kwa njia za kielektroniki kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na pia hutumia mitandao ya kijamii ikiwemo *Twitter*, *Facebook*, na *Youtube* katika kuhabarisha.

38. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni hatua ya kuimarisha soko la bidhaa za TSN, Kampuni hiyo iliendelea kuboresha maudhui na mwonekano wa magazeti yake kwa kuongeza ubunifu katika uandishi wa habari na usanifu wa kurasa za magazeti yake. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kujikita katika uandishi wa habari za kijamii na kimaendeleo, kuendelea kuchapisha makala maalumu za kila wiki kwenye majarida mbalimbali katika gazeti la *HabariLeo* na *Daily News*, kuongeza matumizi ya vielelezo mbalimbali katika habari zinazochapwa ili kuboresha mwonekano wa kurasa za magazeti na kutoa machapisho maalumu (*Special Supplements*).

39. Mheshimiwa Spika, Kampuni imewekeza katika Mtambo wa Kidijiti wa Uchapaji Kibiashara ambao umeshafungwa Makao Makuu ya TSN Jijini Dar es Salaam na tayari kazi za uchapaji kibiashara zimeanza kufanyika. Mtambo huu unatoa huduma za uchapaji kibiashara, ikiwemo uchapaji wa vitabu, majarida, taarifa mbalimbali, vipeperushi, shajara, kalenda na utengenezaji wa mabango.

40. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Kampuni ilitoa huduma ya uchapishaji kwa taasisi mbalimbali ikiwemo maadhimisho ya Siku ya Baba wa Taifa, Uhuru, Mapinduzi na Muungano; mukutano wa SADC, Tamasha la JAMAFEST, pamoja na Siku ya Wafanyakazi Duniani. Matoleo haya pamoja na kuongeza maudhui, pia yaliwezesha kuimarisha mapato ya Kampuni.

Aidha, Kampuni illendelea kutumia fursa ya soko la Afrika Mashariki kwa kuchapa matoleo maalumu ya Afrika Mashariki kuititia magazeti ya HabariLeo na Daily News ambayo huchapwa kila Jumanne. Matoleo haya yanalenga kuitangaza Tanzania ndani ya Jumuiya na vilevile kueneza na kubidhaisha lugha ya Kiswahili kuititia gazeti la HabariLeo.

41. Mheshimiwa Spika, TSN imeendelea kuboresha habari kwa njia ya mtandao kwa kuchapisha habari za kijamii na matangazo mubashara kwa matukio mbalimbali. Kampuni imewafikia wafuatiliaji takriban milioni 11.8 katika mitandao yote. Jitihada hizi zimeweza pia Kampuni kupata wasomaji wapya 1,211 wa magazeti kwa njia ya mtandao na hivyo kuongeza idadi ya wanunuzi wa magazeti haya wanaolipa kuititia mitandao kufikia 6,530 kutoka wasomaji 5,319 mwezi Machi, 2019.

42. Mheshimiwa Spika, TSN iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato yake ikiwemo uendeshaji wa Majukwaa ya Fursa za Biashara na Uwekezaji na utoaji wa huduma za habari na machapisho ambayo yaliingizia Kampuni mapato ghafi ya zaidi ya Shilingi Milioni 270. Katika kipindi hiki, Kampuni iliandaa kongamano na maonesho ya biashara na fursa za uwekezaji Mkoani Pwani na kutoa


machapisho maalumu ya tukio hilo lililohudhuriwa na washiriki zaidi ya 600. Makongamano haya yamekwishafanyika katika Mikoa ya Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Tanga, Arusha, Tabora, Lindi na Geita. Aidha, kongamano maalumu lilifanyika Zanzibar. Katika makongamano haya, TSN hutumia magazeti yake kuhabarisha na kuhamasisha wananchi na wawekezaji kutumia fursa za biashara na uwekezaji zilizopo katika Mikoa husika na vilevile kupanua biashara ya Kampuni.

3.2.1.3 MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)

43. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuititia Kamati ya Maudhui ina jukumu la kumshauri Waziri mwenye dhamana ya Habari kuhusu utekelezaji wa Sera ya Utangazaji, kusimamia na kufuatilia maudhui ya vituo vya utangazaji, kushughulikia malalamiko kutoka kwa watangazaji na watumilajili wa huduma za utangazaji pamoja na kuhakikisha kuwa Kanuni za Utangazaji zinafuatwa.

44. *Mheshimiwa Spika*, katika kupanua wigo wa vyombo vya utangazaji nchini na hivyo kuwezesha wananchi kupata habari kwa urahisi na uhakika, TCRA iliendelea kusajili Redio na Televisheni ambapo katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 redio nane (binafsi 7 na jamii moja) na televisheni binafsi 15 (14 za maudhui ya kulipia-*content by subscription* na moja ya maudhui yanayotazamwa bila kulipia-*Free to Air*) zilisajiliwa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Tanzania ina jumla ya Televisheni zilizosajiliwa 44 ambapo za umma ni tatu (7%), binafsi 38 (86%) na Halmashauri 3 (7%); na vituo vya Redio 186 ambapo vya umma ni viwili (1%), Halmashauri tisa (5%), vya kijamii 11 (6%) na binafsi 164 (88%). Aidha, nchi yetu ina vyombo vya habari vya mitandaoni vilivyosajiliwa ambavyo ni Televisheni za Mtandaoni (*Online TV*) 264, Redio Mtandaoni 22 na blogu 85.

Kielelezo Na. 2: Vituo vya Televisheni Vilivyosajiliwa Hadi Machi, 2020



Kielelezo Na. 3: Vituo vya Redio Vilivyosajiliwa Hadi Machi, 2020

45. Mheshimiwa Spika, Kiambatisho Na. I kinabainisha Vyombo vya Habari vilivyosajiliwa katika kipindi cha mwaka 2010-2019.

46. Mheshimiwa Spika, TCRA iliendelea kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji wa maudhui ya ndani yanayozingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania kwa

kutoa mafunzo kwa waandaaji wa maudhui 263. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Wahariri, Waandishi wa Habari, Watangazaji na Wasimamizi wa vipindi kutoka Mikoa 12 ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Mtwara, Lindi, Katavi, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe na Rukwa. Aidha, TCRA itaendelea kutoa mafunzo kama hayo kwenye Mikoa mingine iliyobaki.

Mafunzo haya pamoja na mambo mengine, yaliyikita katika kuwajengea uwezo kuhusu Kanuni za Mawasiliano ya Posta na Kielektroniki (Maudhui ya Redio na Televisheni) za mwaka 2018. Aidha, mafunzo kama haya yaliyendeshwa na TCRA mwezi Desemba, 2019 kwa Wasimamizi wa Vituo, Wahariri, Waandishi wa Habari, Watangazaji, Wasimamizi wa vipindi na Waandaaji wa vipindi katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe.

47. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kujengenea uwezo vituo vya utangazaji kuhusu namna bora ya kuripoti matukio ya uchaguzi ambapo mafunzo yametolewa kwa washiriki 248. Katika Kanda ya Kaskazini (Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga) mafunzo yalifanyika tarehe 10-20 Julai, 2019 na kuhusisha wadau 91 ambapo katika Kanda ya Mashariki (Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Morogoro) mafunzo yalifanyika tarehe 01-12 Oktoba, 2019 na kuhudhuriwa na wadau 72. Aidha, katika Kanda ya Kati (Mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida na Kigoma) mafunzo yalifanyika katika Mikoa ya Tabora na Dodoma tarehe 6 na 11 Februari, 2020 mtawalia. Mafunzo yaliyofanyika katika Mikoa ya Tabora na Dodoma yalijumuisha washiriki kutoka katika Mikoa ya Kigoma na Singida ambapo jumla ya washiriki 85 walihudhuria.

48. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha shughuli za utangazaji zinaendeshwa kwa kuzingatia masharti ya leseni, Kamati ya Maudhui ya TCRA ilitembelea jumla ya Vituo vya Utangazaji 68 katika Kanda ya Kati (vituo 17), Kanda ya Mashariki (vituo 30) na katika Kanda ya Kaskazini (vituo 21). Kamati ilibaini kuwepo kwa watendaji katika ngazi ya cheti ambao bado wanafanya kazi katika vituo vingi na iliwatahadharisha

wamiliki kuhusu sharti la kisheria la wanahabari kuwa na angalau elimu ya Stashahada (Diploma) ifikapo Desemba, 2021. Aidha, tarehe 20 Novemba, 2019 TCRA ilitoa taarifa kwa vyombo vyote vya habari kuhusu watangazaji wasiokuwa na taaluma ya uandishi wa habari kuanza kufanya maandalizi ya kufikia kiwango cha Stashahada au Shahada katika masuala ya habari.

49. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na hatua mbalimbali kuchukuliwa dhidi ya ukiukwaji wa maadili, malalamiko ya ukiukwaji wa maadili yanazidi kuongezeka, hivyo kuilazimu Serikali kuititia Kamati ya Maudhui ya TCRA kuchukua hatua za ziada ikiwemo kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatilaji.

Aidha, Kamati ya Maudhui ilitoa uamuzi wa kupewa onyo pamoja na kulipa faini kwa vituo vitano (5) vinavyotoa huduma za maudhui mtandaoni ambavyo ni Global TV, Lemutuz Online TV, Kwanza Online TV, Millard Ayo Online TV na Watetezi Online TV. Vilevile, TCRA imeendelea kufuatilia watoa huduma za maudhui ya mitandaoni ambao hawajajisajili na kupewa leseni. Jumla ya watoa huduma za maudhui mtandaoni 23 wasio na leseni walifikishwa kwenye vyombo vya Sheria.

3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

50. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni nchini imekuwa kichocheo cha amani, umoja na utulivu katika kuhimiza uzalendo na utaifa kwa jamii ya Watanzania kuititia Maktaba Hai ambao ni wazee wa jadi na kimila. Kila mwanajamii wa Taifa hili ameonesha dhahiri na kuuishi utamaduni wa nchi yetu. Hili ni jambo la kujivunia kwa kizazi cha sasa na kijacho.

51. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni inahusisha Idara ya Maendeleo ya Utamaduni na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA).

52. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Idara ya Maendeleo ya Utamaduni ni pamoja na kuratibu, kuenzi, kuendeleza,

kulinda na kuweka kumbukumbu za urithi wa utamaduni ikiwa ni pamoja na historia, mila, desturi, sanaa, lugha, maadili na uzalendo. Katika kipindi hiki, ililandaliwa Rasimu ya Kitabu cha Maadili ya Taifa kitakachotumika kuelimisha jamii kuhusu uzingatiaji wa maadili ya Kitaifa. Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau ili kuhakikisha kitabu hicho kinakuwa na uwakilishi mpana na stahiki kuhusu maadili, mila na desturi za Taifa letu.

53. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuhifadhi na kudumisha Utamaduni wa Mtanzania, Wizara imefanya utafiti wa awali wa maktabani wa lugha ambazo zipo katika hatari ya kupotea. Lugha hizo ni Kizaramo, Kisegeju, Kividunda na Kiburunge kutokana na kupungua kwa idadi ya wazungumzaji wa lugha hizo. Hatua kubwa zinazofuata ni kufanya utafiti wa uwandani wa lugha hizo na utafiti katika makabila mengine.

Aidha, kwa kushirikiana na Maofisa Utamaduni wa Mikoa na Wilaya, taarifa kuhusu Himaya za Kichifu kumi na nne zenye maeneo ya kuapisha machifu, ibada za kimila, matambiko, makaburi walipozikwa machifu zilipatikana katika Mikoa ya Geita, Mwanza na Shinyanga. Elimu ya kuyahifadhi maeneo hayo ya kihistoria ilitolewa kuititia viongozi wa maeneo hayo.

54. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia Wizara kukamilisha utafiti katika Himaya ya Chifu Kingalu wa Kinole Morogoro na kubaini utajiri wa urithi wa utamaduni uliopo katika eneo hilo, Wizara imepanga kuendelea na mkakati wa kuyatambua maeneo mengine yote yaliyokuwa chini ya himaya za Viongozi wa jadi (Machifu) kwa lengo la kubaini amali za urithi wa kiutamaduni zilizopo katika maeneo hayo zinazofaa kuendelezwa na kudumishwa ikiwemo historia, mila, desturi, miiko na maadili kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye. Aidha, Wizara imepanga kuandaa historia ya kila eneo la kichifu litakalobainika kwa kulitangaza na kuliwekea mazingira rafiki ili litumike kama eneo la utalii wa kiutamaduni.

Fauka ya hayo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii inaangalia uwezekano wa kuanzisha au

kuwahamasisha wadau kujenga makumbusho ndogondogo katika maeneo yote ya himaya ya machifu ili kuimarisha jitihada za uhifadhi za urithi wa klutamaduni unaopatikana katika himaya hizo, ikiwemo kuweka bayana vifaa vyta kijadi vya kila eneo la machifu kwa kuvitolea ufanuzi wa matumizi yake kwa jamii na kutoa elimu ya uhifadhi wake kwa vizazi vijavyo.

55. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha historia ya ukombozi wa Taifa letu inafahamika vizuri kwa Watanzania wote hususan Vijana, Wizara imeamua kufanya utafiti wa kina katika maeneo yote nchini ambayo yalitoa mchango mkubwa katika harakati za kulikomboa Taifa letu kutoka katika minyororo ya utumwa wa kikoloni. Hii inatokana na ukweli kwamba taarifa nydingi za historia ya ukombozi kwa nchi yetu zimeandikwa na wageni tena kwa kupotoshwa. Nitumie nafasi hili kuwapongeza viongozi, watafiti wa historia na wadau wa historia wa Mkoa wa Singida kwa kuchukua hatua kuthibitisha historia ya mpigania uhuru wa kike wa Mkoa wa Singida Bibi. Letri Kidanka maarufu kama Liti, aliyetumia ncha ya mkuki kama kitit chake na sayansi ya nyuki kupambana na wakoloni wa Kijerumani.

Aidha, taarifa nydingine za kihistoria na michango iliyotolewa katika kupigania uhuru hazijaandikwa mahali popote licha ya kuwa na umuhimu mkubwa katika Urithi wa Historia ya Ukombozi wa Taifa letu mfano michango ya baadhi ya machifu walioshiriki bega kwa bega kuikomboa nchi umesahaulika au kutotambuliwa kabisa.

Wizara inaendelea kuandaa orodha ya maeneo yote yaliyotumika katika harakati za kupigania uhuru yale ambayo hayakuandikwa na yale yaliyoandikwa. Aidha, mbali na fuvu la kichwa cha Chifu Mkwawa ambalo lilisharudishwa nchini mwaka 1954, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kufuatilia urejeshwaji wa mafuvu ya machifu wengine katika nchi mbalimbali za Ulaya kwa lengo la kuhifadhi historia ya nchi yetu kwa faida ya vizazi vijavyo.

- 56. *Mheshimiwa Spika*,** Tathmini ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 iliyokuwa ikifanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilikamilika na hatua inayofuata ni kufanya mapitio ya Sera kwa kuzingatia masuala yaliyoibuliwa katika tathmini ikiwemo changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha takriban miaka 23 ya utekelezaji wake na masuala mapya ya kuzingatiwa hasa ukuaji wa kasi wa Sekta za Sanaa na Filamu katika uchumi wa nchi.
- 57. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimwa Waziri Mkuu, zoezi la kuhuisha Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa liliendelea kufanyika ambapo fedha za kuanzisha Mfuko huo zimetengwa katika Bajeti ya Mwaka 2020/21. Mfuko huu ambao unatokana na maoni ya wadau, utaimarisha juhudzi za Serikali za kuendeleza Sekta za Utamaduni na Sanaa nchini.
- 58. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kushirikiana na UNESCO na Tume ya UNESCO Tanzania, Wizara imeandaa taarifa ya kitaifa ya utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 2005 unaohusu Kulindwa na Kuendelezwa kwa Uanuwai wa Kujielezea Kiutamaduni (*Convention on Protection and Promotion of the Diversity of Cultural Expression, 2005*). Aidha, taarifa hiyo, imewasilishwa UNESCO Makao Makuu mwezi Machi, 2020 kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye taarifa ya Kimataifa ya Uchumi ambayo huandaliwa na shirika hili. Taarifa ya Kimataifa ya Uchumi hutolewa kila baada ya miaka minne (4), hivyo taarifa hiyo inatarajiwa kutolewa tena mwaka 2023. Aidha, Wizara imeandaa na kusaini hati ya makubaliano ya ushirikiano wa masuala ya utamaduni na sanaa kwa nchi za Namibia na Malawi mwaka 2019 na mikakati ya utekelezaji inaandaliwa.
- 59. *Mheshimiwa Spika*,** ili kubidhaisha Kiswahili nje ya nchi, kulifanyika vikao mbalimbali baina ya Wizara yangu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuandaa miongozo ya ufundishaji Kiswahili kwa Wageni na kubainisha mahitaji ya uandaaji wa mitaala ya kufundishia Kiswahili katika nchi za kigeni. Aidha, Andiko la kujenga hoja kwa nchi

Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya kuridhia lugha ya Kiswahili kuwa mionganoni mwa lugha rasmi za SADC liliandaliwa na lugha hiyo iliridhiwa kuwa mionganoni mwa lugha rasmi za SADC katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya hiyo uliofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti, 2019.

60. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, jukumu ambalo nchi yetu ilipewa mwaka 2011 kutohana na kuwa kiongozi, ngome na kinara wa kuongoza mapambano ya harakati za kulikomboa Bara la Afrika hususan katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika. Hati Miliki ya eneo la kujenga Kituo cha Kikanda cha Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika liliopo Bunju 'B' Manispaa ya Kinondoni imepatikana. Majukumu mengine yaliyotekelawa ni kukamilika kwa Makala Bainifu kuhusu utungwaji wa Sheria ya Kuhifadhi na Kulinda Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika uliopo Tanzania, kuendelea na ukarabati wa majengo yaliyokuwa yaktumika na iliyokuwa Kamati ya Ukombozi ya OAU na kushiriki katika maandalizi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kufanya maonesho yenyeye maudhui ya "*Mchango wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere katika Kuongoza Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika*".

61. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliongoza mchakato mzima wa kutafuta muwafaka wa mgogoro kati ya Chuo cha Ufundii Arusha na Wazee wa Kimila wa Kabilia la Maasai kuhusu eneo lilitokuwa na mgogoro la Oretiti Longaik mkoani Arusha. Mgogoro huu ambaao umedumu tangu mwaka 1970, (takriban miaka 49 iliyopita) umetatuliwa kwa chuo kupunguza sehemu ya ardhi yake ili kuongeza nafasi kwa viongozi wa kimila wa Kimaasai ili wawezekuendesha shughuli mbalimbali za kimila katika eneo hilo.

Eneo hili limekuwa likitumiwa na Jamii ya Kimaasai ya Afrika Mashariki kama kitovu cha shughuli mbalimbali za kijadi kuanzia karne ya kumi na nane yamkini kuanzia mwaka 1887 kwa maelezo ya kihistoria kwa masuala mbalimbali ya kimila

na kijadi. Baadhi ya shughuli za kijadi ambazo zimekuwa zikifanyika katika eneo hili ni mikutano, vikao na matamasha mbalimbali ya kijadi ya mila na desturi. Lengo la shughuli hizo ni kutoa elimu kuhusu maadili na miiko ya kijamii; kutatua migogoro ya ndoa na ardhi; kuvunja vyungu ikiwa ni ishara ya kulaani wanaodhulumu wengine; kujenga moyo wa upendo, umoja na ushirikiano; kufanya tohara kwa vijana wa kiume na kufanya ibada za matambiko kwa ajili ya majanga yanayoikabili jamii kama vile ukame, njaa na magonjwa.

3.2.2.1 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

62. *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967 iliyorekebishwa mwaka 1983, pamoja na marekebisho madogo ya mwaka 2016. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Baraza ndilo mratibu na msimamizi wa matumizi na maendeleo ya Lugha ya Kiswahili nchini na kufuatilia maendeleo yake nje ya nchi.

63. *Mheshimiwa Spika*, BAKITA iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza na kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo:

a) Kutambua na kuwaingiza wataalamu 1,327 katika Kanzidata ya Kitaifa ya wataalamu wa Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu waliotambuliwa, 1,185 wana shahada ya kwanza sawa na asilimia 89%, shahada ya umahiri ni 118 sawa na asilimia 8.89, stashahada ya uzamili (PGD) ni 14 sawa na asilimia 1.05 na shahada ya uzamivu ni 10 sawa na asilimia 0.75. Aidha, kati ya wataalamu waliotambuliwa na kukamilisha mahitaji yote ya utambuzi wanaume ni 564 sawa na asilimia 48.5 na wanawake ni 599 sawa na asilimia 51.5;

b) Kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 678 kupitia redio na televisheni mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Vipindi hivi vilivyorushwa hewani kupitia TBC₁, TBC_{Taifa}, Radio One, Clouds FM, Kiss FM, Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa na Dar 24 vilihuisha mada mbalimbali za sarufi

na fasihi ya Kiswahili ikiwemo Matumizi ya Kiswahili katika Nchi mbalimbali za Afrika na Nje ya Afrika, Ufundishaji wa Lugha Kupitia Mitandao ya Kijamii, Matumizi ya Lugha ya Kiswahili kwa Waandishi wa Habari, Matumizi ya Kiswahili katika Maonesho ya Biashara, Dhima ya Misemo katika Kukuza Lugha, na Mchango wa Lugha za Mitaani katika Kukuza Msamiati wa Lugha ya Kiswahili;

c) Kusajili vituo 10 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Vituo vilivyoasajiliwa ni Swahili Dar Language School - (Dar es Salaam), Training Centre for Development Cooperation Usa River Arusha Tanzania (TCDC) – (Arusha), South Africa Fellowship of Churches – (Afrika Kusini), Peace Corps Tanzania - (Morogoro), Learn Swahili – (Dar es Salaam), Insiders Language Centre – (Dar es Salaam), Kiswahili na Utamaduni (KIU) – (Dar es Salaam), Lilinga Kiswahili Centre – (Iringa), Kiswahili Hub – (Dar es Salaam), na Kituo cha Kiswahili Italia. Vilevile, Baraza lilitambua na kusajili Chama cha Wanafunzi na Wahitimu wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu na vya Kati Tanzania (CHAWAKITA).

d) Kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wataalamu 226. Mafunzo yalitolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam (wataalamu 122 kwa awamu tano), Mwanza (wataalamu 45 kwa awamu moja), Arusha (watalamu 27 kwa awamu moja) na Dodoma (watalamu 22 kwa awamu moja):

e) Kuendesha semina saba (7) za matumizi bora ya Kiswahili kwa waandishi na watangazaji wa TBC1 (38), TBC_{Taifa} (30) na ITV (45) katika jiji la Dar es Salaam pamoja na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya-MUST (6). Aidha, semina ilitolewa kwa waandishi wa Uhuru Media Group (14), Dodoma FM Radio (12) na A-FM Dodoma (13);

f) Kukamilisha uandaaji wa Kamusi Kibindo mbili ambazo ni Kiswahili –Kiingereza – Kiarabu na Kiswahili –Kiingereza – Luganda. Aidha, Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza-Kireno na Kiswahili – Kiingereza – Kifaransa ziko katika hatua za mwisho za uhariri;

- g) Ili kuendana na kasi ya kuhitajika kwa Kiswahili katika nchi za SADC na kwingineko duniani, BAKITA imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kufundisha Kiswahili kwa Wageni. Hatua inayofuata ni kushirikisha wadau ili kuboresha mwongozo huo; na
- h) Kukamilisha maandalizi ya awali ya Kituo cha Kufundisha Kiswahili kwa Wageni kilichopo kwenye Makao Makuu ya Baraza jijini Dar es Salaam. Kituo hiki kitatoa mafunzo ya ngazi ya awali na kati kwa wageni.

64. *Mheshimiwa Spika*, Baraza liliendelea kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka mbalimbali ambapo nyaraka kubwa 24 na kazi ndogondogo 530 zilifanyiwa tafsiri. Aidha, Baraza lilitibitisha tafsiri 2,762 zilizofanywa na mawakala wake na kutoa ithibati kwa miswada 34 ya vitabu. Miiongoni mwa vitabu hivyo vya kiada ni viwili ambavyo ni Kiswahili - Kitabu cha Mwanafunzi – Darasa la 3 na Kiswahili - Kitabu cha Mwanafunzi – Darasa la 4.

Aidha, vitabu 29 vya marejeo vilipewa ithibati. Vitabu hivyo ni Mjue Dkt. John Pombe Magufuli, Mnyama Mzuri kupita Wote, Reba Atamani Aiskrimu Dawa, Kofia, Kuku Watoto, Siku ya Kuzaliwa, Simba na Ngiri, Uwanja wa Langutani, Tunakwenda Wapi, Kuhesabu Wanyama, Diwani ya Gambiwa, Mpelelezi Kinyago, Jamila wa Kamali, Hapo Zamani, Ndoto ya Upendo na Soso. Pia, vitabu vingine vilivyopewa ithibati ni Supu ya Elimu, Saketi ya Kirekebu, Shahada Yangu, Ni Chakula Gani Leo?, Hazina ya Kiswahili, Busara Haikinai, Nyota Yako, Mbwa Mwitu Kwenye Ngozi ya Kondoo, Mwanambuzi Mwekundu, Ufahamu Mkoa wa Kagera, Kilimo, Kamusi ya Kiswahili –Kichina, Jeneza Bandia na Mtutu. Vilevile, Baraza lilikusanya matini za maneno 500,000 kwa ajili ya kongoo la Kiswahili.

3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

65. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Sekta hii ni pamoja na kusimamia maendeleo ya shughuli za sanaa, filamu na ubunifu nchini. Aidha, Sekta hii inahusisha Idara ya


Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa).

66. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2017 Tanzania ilipewa dhamana ya kuwa mwenyeji wa Tamasha la Nne la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) kwa mwaka 2019. Malengo ya Tamasha hili ni kutoa jukwaa la kuonesha Utamaduni kama msukumo madhubuti wa utangamano na maendeleo ya kikanda; kuwaleta pamoja wataalamu na wasimamizi wa sekta za Sanaa na Utamaduni ili kuenzi na kuendeleza utajiri wa urithi anuwai wa utamaduni wa Afrika Mashariki; kutoa fursa ya majadiliano ya kitaaluma baina ya wananchi wa Afrika Mashariki; kuchochea ukuaji wa uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia ukuzaji wa sekta za ubunifu na utamaduni; na kutumia Utamaduni na ubunifu kama nyenzo ya kuenzi na kukuza utambulisho wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.


67. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu Tamasha hilo liliofanyika nchini tarehe 21 - 28 Septemba, 2019 katika Uwanja vya Taifa, Jijini Dar es Salaam. Tamasha lilitengeneza na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na liliongozwa na kauli mbiu "*Uanuai wa Kiutamaduni: Msingi wa Utangamano wa Kikanda, Maendeleo ya Kiuchumi na Kushamiri kwa Utalii*". Tamasha hilo ambalo lilihirikisha watendaji wa sanaa na utamaduni 3,117 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (isipokuwa Sudani Kusini) pamoja na Kisiwa cha Mayote (baada ya kuwasilisha maombi), lilihudhuriwa na watu 102,019. Idadi hii ya washiriki na mahudhurio ni kubwa ikilinganishwa na katika nchi nyingine wanachama, hivyo kutoa fursa kubwa kwa nchi yetu kuonesha na kutangaza utamaduni wake na wadau wa kazi za Sanaa kutangaza na kuuza bidhaa zao na kujenga mitandao ya kibashara.

**Kielelezo Na. 4: Idadi ya Washiriki Tangu Tamasha la Jamafest
Lilipoanza Mwaka 2013**

Kielelezo Na. 5: Mahudhurio katika Tamasha Tangu



Kielelezo Na. 6: Idadi ya Maonesho ya Jukwaani Tangu Kuanza kwa Tamasha Mwaka 2013




68. *Mheshimiwa Spika*, Tamasha hili lilihusisha shughuli mbalimbali za Sanaa na Utamaduni ambazo ni matembezi ya kiutamaduni, maonesho ya kiutamaduni, maonesho ya bidhaa za sanaa, masoko ya bidhaa za kitamaduni na ugunduzi, midahalo na warsha, michezo ya watoto, uoneshaji wa Filamu, michezo ya jadi, maonesho ya vyakula vya asili, ziara, tuzo na utalii pamoja na maonesho ya mavazi na ulimbwende. Tamasha lilitoa pia fursa ya majadiliano ya kitaaluma ambapo mada sita (6) ziliwasilishwa na waendesha mijadala sita (6) kutoka kila nchi mwanachama.

69. *Mheshimiwa Spika*, Tamasha pia lilitoa tuzo kwa washindi wa sanaa za maonesho, sanaa za ufundi, muziki, mwandishi bora wa habari za utamaduni na sanaa, insha, filamu na makala za filamu zilizowasilishwa na nchi wanachama. Tuzo zilizoandaliwa ni zenye taswira ya *Zinjanthropus* ili kuendelea kutangaza vivutio mbalimbali vya nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na duniani. Aidha, kwa kuwa maudhui na shughuli za Tamasha hili yalishabihiana na Tamasha la Urithi (*Urithi Festival*) iliamuliwa wiki ya kwanza ya Tamasha la JAMAFEST iunganishwe na Tamasha la Urithi linaloratibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. JAMAFEST ilifungwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Idd.

70. Mheshimiwa Spika, tayari tathmini ya Tamasha la JAMAFEST imefanyika kwa kushirikisha nchi wanachama ambapo Tamasha la Tanzania limepata asilimia 96.2 kwa ufanisi ikilinganishwa na Matamasha yaliyotangulia. Wizara inaishukuru Serikali kwa kuwezesha Tamasha hili na kutimiza wajibu wake katika Jumuiya. Aidha, Wizara inawashukuru wadau mbalimbali waliojitekeza kufadhilli/kudhamini Tamasha hili ikiwemo Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Kampuni ya Multichoice Tanzania na Kampuni ya Cocacola Kwanza.

Kwa kuwa Serikali itakuwa ikiendesha Tamasha la Kitaifa lenye mfanano wa JAMAFEST, na pia nchi yetu kushiriki katika matamasha yajayo ya JAMAFEST ikiwemo la mwaka 2021 nchini Burundi, natoa wito kwa wadau kushirikiana kikamilifu na Wizara yangu ili kutumia fursa hii na kuendelea kubakia kileleni.

71. Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kuenzi sanaa zetu, Wizara ilishirikiana na wadau katika kuendesha Matamasha



72. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa Serikali katika kutambua thamani ya kazi za sanaa, iliweka mazingira wezeshi na endelevu kwa wasanii wa Tanzania kuzalisha kazi zao na kutoa fursa endelevu kwa vijana na makundi maalumu wakiwemo watu wenye ulemavu kwa kutoa maeneo mahususi ya kufanya shughuli zao za Sanaa tangu miaka ya 1972. Aidha, itakumbukwa Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere

alitoa eneo katikati ya jiji la Dar es salaam mtaa wa Ohio kiwanja Na. 2366/49 chenyehati Na. 186056/34 ya umiliki wa miaka 99 kwa Wasanii waliokuwa wakifanya kazi zao katika Nyumba ya Sanaa katika mtaa wa Mansfield tangu mwaka 1972 na kuhamishiwa katika kiwanja hicho kipywa baada ya ujenzi wa jengo la Nyumba ya Sanaa kukamilika. Jengo hilo ambalo eneo lake lilitolewa na Serikali lilizinduliwa na Mwl. Julius Nyerere mwenyewe tarehe 17/10/1983.

73. *Mheshimiwa Spika*, katika uendeshaji wa Nyumba ya Sanaa kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu takriban miaka 20 ambao umechangiwa na sababu mbalimbali. Wizara inakamilisha uchunguzi wa awali kuhusu suala hili ili kuhakikisha haki inatendeka.

74. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ushiriki wa vikundi vyaherudani na hamasa katika Maadhilisho ya Sherehe za Miaka 58 ya Uhuru na Miaka 57 ya Jamhuri kwa Mwaka 2019 yaliyoahimishwa Jijini Mwanza, tarehe 09 Desemba, 2019. Kikundi cha ngoma za asili cha Mang'ombega kutoka Wilaya ya Magu na Kwigwa, vikundi vyaherudani na ngoma vyaherudani na Nyakitali kutoka Tarime Mkoani Mara, Buyegu na Mwanalyeko kutoka Wilaya ya Magu na vikundi vyaherudani na Bujora na Chapa Kazi kutoka Mwanza vilishiriki katika maadhilisho hayo. Wadau wengine wa sanaa na burudani walioratibiwa katika maadhilisho hayo ni Bendi ya Muziki ya TOT kutoka Dar es Salaam, kwaya ya AICT - Makongoro kutoka Mwanza, Kikundi cha Kakau Band kutoka Kagera na Msanii wa kizazi kipywa Harmonize.

75. *Mheshimiwa Spika*, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara iliratibu na kuendesha Tamasha la Urithi (*Urithi Festival*) katika Mikoa 12 ya Tanzania Bara na Zanzibar ambapo kilele cha Tamasha hilo kilikuwa tarehe 31 Oktoba – 02 Novemba, 2019. Tamasha lilishirikisha mashindano, ziara za kiutalii na kiutamaduni na shughuli mbalimbali kwa Mikoa husika ikiwemo maonesho na mashindano ya mitumbwi, mbio za baiskeli, kwaya, kazi za mikono za ubunifu, ngoma na vyakula vyaherudani na zawadi mbalimbali zilitolewa kwa washindi zikiwemo fedha taslimu, ngao, vifaa vyaherudani na muziki, pipipiki na gari aina ya Suzuki Carry (Kirikuu). Aidha,

liliandaliwa tamasha la kumbukizi la wasanii na wanamichezo nyota ambapo nishani na vyeti vilitolewa kwa nyota hao wa zamani kutokana na mchango wao katika jamii.

76. *Mheshimiwa Spika*, itakumbukwa kuwa mwaka 2015, wakati wa Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za SADC uliofanyika Jijini Harare, Zimbabwe lilitolewa wazo na Rais wa zamani wa nchi hiyo Hayati Robert Mugabe, la ujenzi wa Sanamu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kutumia malighafi ya shaba nyeusi (*bronze statue*) katika viwanja vya jengo la Amani na Ulinzi la Julius Nyerere liliopo Makao Makuu ya Umoja wa Afrika Jijini Addis Ababa, Ethiopia. Wazo hili lilitenga kutambua na kuenzi mchango wa waanzilishi wa SADC katika kulikomboa Bara la Afrika, hususan mchango wa Mwalimu Nyerere katika kuyakomboa Mataifa yaliyo kusini mwa Bara hili. Jukumu la kusimamia mradi huu, kutoa msanii atakayetengeneza Sanamu hiyo, vigezo vya Sanamu na upatikanaji wa Meneja Mradi atayesimamia Mradi huo yalikabidhiwa kwa Tanzania. Tayari majukumu hayo yametekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Hata hivyo, kulingana na uhalisia wa kazi yenewe, Tanzania haikuweza kupata msanii kutokana na kutokuwepo kwa nyenzo za utengenezaji wa Sanamu za aina hiyo kwa kutumia shaba nyeusi. Hivyo, ililazimu zabuni ya kumpata msanii/kampuni ya kutengeneza sanamu hiyo kutangazwa kwa tenda ya wazi ya kimataifa kuititia tovuti ya SADC kwa nchi wanachama. Hatua za utoaji wa zabuni zinaendelea na ujenzi wa Sanamu unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka 2019/2020.

77. *Mheshimiwa Spika*, katika kutatua migogoro iliyogubika Sekta ya Sanaa kwa muda mrefu na kuwanyima wasanii haki ya kuyatumia maeneo yao kujipatia kipato, Wizara yangu imeshautafutia ufumbuzi mgogoro wa umiliki wa eneo la Mwenge kati ya wachonga vinyago na wafanyabiashara wa vinyago uliodumu kwa zaidi ya miaka 33. Uamuzi wa Serikali ni kulikabidhi eneo hilo kwa Baraza la Sanaa la Taifa

(BASATA) ili litumike kwa faida ya makundi yote mawili. Kinachosubiriwa ni mamlaka husika kukabidhi hati ya eneo hilo kwa BASATA.

78. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha vyombo vinavyohusu haki, maslahi na upatikanaji wa huduma kwa wasanii vinawekwa chini ya Wizara yenye dhamana ya moja kwa moja na wadau husika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imelifanya kazi suala la kuhamisha Chama cha Hakimilikki (COSOTA) kuja Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hatua iliyofikiwa ni kukamilisha andiko la pamoja kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mamlaka za uamuzi.

79. *Mheshimiwa Spika*, halikadhalika, zoezi la kuhakikisha vyombo vinavyohusu haki, maslahi na upatikanaji wa huduma kwa wasanii vinakuwa chini ya mwamvuli mmoja ili kuwaondolea usumbufo, gharama na hata upotevu wa stahili zao, limefikia hatua nzuri ambapo Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha rasimu ya Andiko. Hatua inayofuata ni kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri.

80. *Mheshimiwa Spika*, katika ukusanyaji wa taarifa za wasanii mashuhuri wa Tanzania ambao walifanya maonesho mbalimbali nje ya nchi yakiwemo maonesho yajulikanayo kama Expo70 nchini Japan, Wizara yangu imeiomba Serikali ya Japan kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupatiwa nakala za picha jongevu za maonesho ya wasanii wetu wakiwemo wanamuziki Mbarak Mwishehe na Morris Nyunyusa nchini humo kwa ajili ya kuzihifadhi na kuzitumia kwa ajili ya faida ya wasanii hao na vizazi vyao. Dhamira ya Wizara yangu ni kuhakikisha kazi zote zilizoshirikisha wasanii nguli akiwemo Mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa ambaye kazi zake zipo Afrika Kusini na Uingereza zinapatikana na kuhifadhiwa. Aidha, Wizara inafuatilia kazi za Bendi ya Cuban Marimba nchini Cuba chini

ya uongozi wa msanii galacha Juma Kilaza aliyepeperusha vizuri bendera ya nchi yetu.

3.2.3.1 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

81. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya BASATA ni pamoja na kuendeleza kazi za sanaa nchini, kutoa ushauri na utaalamu wa kiufundi kwa wasanii na wadau wa sanaa, kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu maendeleo ya sanaa nchini na kuratibu na kusimamia maonesho, mashindano, matamasha, makongamano na warsha mbalimbali zinazohusu kazi za sanaa.

82. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha kunakuwa na kazi bora za muziki zinazokidhi mahitaji ya soko, Baraza husajili na kuhakiki maudhui ya kazi zote za muziki nchini ambapo hadi Machi, 2020 jumla ya kazi za muziki 2,625 zilihakikiwa. Aidha, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, BASATA ilihakiki maudhui ya kazi za muziki 173 na kutoa ithibati ili zitumike.

Vilevile, katika kutekeleza jukumu la kutoa ushauri kwa wadau wa sanaa, jumla ya wadau 102,080 walipewa ushauri hadi Machi, 2020 ambapo kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020 Baraza limetoa ushauri kwa wasanii na wadau 2,958 kutoka maeneo mbalimbali nchini. Ushauri hutolewa katika maeneo ya upatikanaji wa masoko ya kazi za sanaa, uendeshaji wa matukio, utafutaji fedha kwa vikundi na taasisi pamoja na masuala ya sheria, maadili, usajili na vibali.

83. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha Sanaa ya Tanzania inatangazwa nje ya nchi na pia kuwawezesha wasanii wetu kupata uzoefu na kuimarisha kazi zao, Baraza limetoa jumla ya vibali 1,620 kwa wasanii wa Tanzania kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa hadi Machi, 2020. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 vibali viliviyotolewa na Baraza kwa muktadha huo ni 135. Vilevile, Baraza limetoa jumla ya vibali 527 kwa wadau kuingiza wasanii kufanya shughuli za sanaa nchini ili kujifunza sanaa ya Tanzania ambapo vibali 25 vimetolewa katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020. Pia, Baraza kwa kushirikiana na ubalozi wa India nchini, liliipeleka kikundi cha sanaa cha Lumumba Theatre Group kushiriki katika Tamasha la 34 la Kimataifa la

kazi za Sanaa liliolofanyika Surajkund nchini India. Takribani watazamaji zaidi ya 1,000,000 walilifuatilia tamasha hili.

84. Mheshimiwa Spika, ili kupata uzoefu katika usimamizi na uratibu wa shughuli za sanaa, Baraza liliifanya ziara katika Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) Zanzibar kupata uelewa juu ya masuala mbalimbali ya usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Sanaa kwa upande wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na masuala ya usajili, utoaji wa vibali kwa wadau, uratibu wa matukio na maonyesho ya Sanaa.

Aidha, ziara hii ililenga kupata uzoefu kuhusiana na kuunganishwa kwa Baraza la Sanaa la Zanzibar (BASAZA) na Bodi ya Ukaguzi ya Filamu ya Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudzi za Serikali katika uunganishaji wa Mamlaka zote zinazosimamia Sekta ya Sanaa nchini kwa lengo la kutoa huduma bora na zenyeharama nafuu kwa wadau.

85. Mheshimiwa Spika, Baraza liliendelea kuchukua hatua za kuhamasisha sanaa mashulenii kwa kutoa Tuzo kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari waliofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza masomo ya Sanaa ya Muziki, Sanaa za Ufundji (*Fine Arts*) na Maonesho kwa mwaka wa masomo wa 2017 na 2018. Jumla ya wanafunzi 18 wamepeewa Tuzo katika shule za Sekondari zifuatazo; Edmund Rice Sinon (Arusha); Alpha James na Mvuha (Morogoro); Bukoba Sekondari, Piece, na Murugwanza (Kagera); na Shule ya Sekondari ya Mbeya (Mbeya). Aidha, Baraza lilitoa vyeti kwa shule na walimu wa masomo ya Sanaa kutoka katika shule hizi.

Vilevile, kwa kuzingatia ubunifu uliotukuka, wasanii wa Tanzania wameweza kuipeperusha vyema bendera ya nchi yetu nje ya nchi na hivyo kulitangaza vyema Taifa letu. Baadhi ya wasanii hao ni Nasibu Abdul (Diamond Platnumz), Alli Salehe Kiba (Ali Kiba), Rajabu Abdul Kahal (Harmonize), Vanessa Mdee, Ommary Nyembo (Ommy Dimpoz), Ali Darasa Mahamati (Darasa) Raymond Shaban Mwakyusa (Rayvanny) na wasanii wanoshiriki Tamthilia za Sarafu, HUBA kapuni na vichekesho vyaa Kitim.

Wengine ni kikundi cha ngoma za asili cha Lumumba Theatre, Wabunifu Asia Idarus, Mustafa Hassanali, Martin Kadinda, Miriam Odemba, Flaviana Matata, Herieth Paul, Ally Rehmntula, Happiness Magesa na Miss Tanzania 2019, Bi. Sylvia Sebastian Bebwa.

86. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana wasanii hawa na kuwaasa wasanii wengine kuongeza kasi na ubunifu katika kazi zao ili zivutie masoko ya ndani na nje ya nchi.

3.2.3.2 BODI YA FILAMU TANZANIA

87. *Mheshimiwa Spika*, Majukumu ya Bodi ya Filamu ni pamoja na kusimamia utayarishaji wa picha jongevu na michezo ya kuigiza; kuhakiki na kupanga madaraja katika picha jongevu na michezo ya kuigiza na kusimamia usambazaji na uoneshaji wa kazi hizo. Aidha, Bodi hiyo ina majukumu ya kutoa ithibati kwa miundombinu, kampuni na wadau wa filamu na michezo ya kuigiza pamoja na kusimamia maendeleo ya Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini.

88. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Filamu iliendelea kusimamia utayarishaji wa filamu, kuhakiki, kupanga katika madaraja, kutoa vibali na leseni kwa kazi na miundombinu mbalimbali ya filamu. Katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi Machi, 2020 jumla ya vibali 615 vilitolewa ambapo kwa watengenezaji wa ndani ni 138 na wa nje ni 477. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 vibali 108 vilitolewa ikiwa ni asilimia 60 ya vibali vilivyopangwa kutolewa katika mwaka 2019/20 ambavyo ni 180. Kati ya vibali hivyo, 84 vilitolewa kwa watengenezaji kutoka nje ya nchi na vibali 24 kwa watengenezaji Watanzania.

89. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya filamu 3,503 zilihakikiwa, kupangwa katika madaraja na kupewa vibali katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2019/20 ambapo filamu 2,986 ni za Kitanzania na filamu 517 kutoka nje ya nchi. Aidha, katika mwaka 2019/20 filamu 805 ikiwa ni asilimia 81 ya lengo la

mwaka la filamu 1,000 zilihakikiwa, kupangwa katika madaraja na kupewa vibali. Kati ya filamu hizo, Filamu 686 ni kutoka ndani ya nchi na filamu 119 kutoka nje ya nchi zikijumuisha filamu zilizohakikiwa katika majumba ya cinema. Vilevile, zilitolewa leseni 23 na vitambulisho 49 kwa wadau wanaojihusisha na masuala ya filamu.

Kiambatisho Na. II kinabainisha vibali vya utayarishaji wa filamu na picha jongevu vilivyotolewa mwaka 2013/14 - 2019/20 na *Kiambatisho Na. III* ni filamu za ndani na nje ya nchi zilizohakikiwa na kupewa vibali katika kipindi hicho. Aidha, *Kiambatisho Na. IV* ni Tuzo mbalimbali zilizotolewa kwa wanatasnia wa kazi za filamu mwaka 2013/14 - 2019/20.

Kielelezo Na. 7: Vibali Vilivyotolewa kwa Watayarishaji wa Filamu kutoka Ndani na Nje ya Nchi Mwaka 2016/17-2019/20

Kielelezo Na.8: Filamu za Kitanzania na Kutoka Nje ya Nchi Zilizohakikiwa na Kupewa Vibali Mwaka 2019/20

90. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha shughuli za filamu zinaendeshwa kwa kuzingatia Sheria na Taratibu stahiki, zilibanyika operesheni 24 kwenye maduka ya kuza filamu, vyombo vya usafiri na vyombo vya habari, ambapo jumla ya filamu 23 zilibainika kutokuzingatia sheria. Wahusika wa filamu hizo walipewa maelekezo ya kuziondoa mitandaoni na madukani, kupewa elimu na ushauri wa kitaalamu pamoja na kutozwa faini.

Vilevile, ili kudhibiti uoneshwaji na urushwaji wa Filamu bila kufuata Sheria, Bodi ya Filamu ilifanya vikao na Vyombo vya Habari ikiwemo Vituo vya Televisheni vya *ITV, East Africa Television (EATV)*, Azam, Kampuni ya Wasafi (WCB), Kampuni ya Zuku na Kampuni ya *Multichoice* Tanzania kwa lengo la kuvitaka vyombo hivyo kuzingatia matakwa ya Kisheria. Vyombo hivyo vyote sasa vimeanza kuzingatia Sheria na kuhakikisha filamu katika vituo vyao hazionyeshwi kabla ya kuwasilishwa Bodi ya Filamu kwa ajili ya uhakiki. Bodi ya Filamu imeendelea kuchukua hatua kwa filamu zilizoingia sokoni bila kuhakikiwa na kupangiwa madaraja.

91. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kunakuwepo na mazingira rafiki na yenye gharama nafuu ya uendeshaji wa kazi za filamu, Serikali ilifanya marekebisho ya Kanuni za Sheria ya Filamu za mwaka 2011 ambapo rasimu ya Kanuni hizo imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Marekebisho hayo pamoja na mambo mengine, yanalenga kuweka tozo rafiki na nafuu kwa wadau wa Filamu. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ya usambazaji na utayarishaji wa filamu ambapo jumla ya miundombinu ya filamu 4,188 ikijumuisha vibanda vya kuoneshea filamu, maeneo ya utayarishaji (*studios*) ilibainishwa na kutambuliwa.

Kwa upande wa maeneo rasmi ya kuoneshea kazi za filamu, jumla ya majumba ya cinema kumi na moja (11) yaliyopo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Mwanza na Dodoma yaliratibiwa.

92. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Filamu Tanzania imeendelea na juhudhi za kuitangaza Tanzania kama eneo mahususi la upigaji picha kwa kutoa elimu kwa umma kupitia maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Kwa upande wa Kitaifa, Bodi ilishiriki maonesho ya Sanaa na Utamaduni kama vile Tamasha la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST), Tamasha la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, Wiki ya Viwanda ya SADC na Kongamano la Warushaji Maudhui na Watangazaji (BDF) ambapo katika matukio hayo Bodi ya Filamu ilipata fursa ya kukutana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wanaojihusisha na masuala ya filamu na hivyo kutangaza fursa mbalimbali zilizopo kwenye Tasnia ya Filamu nchini hasa maeneo, mandhari na maudhui mbalimbali yanayoweza kutumika katika utayarishaji wa picha jongevu.

Kwa upande wa Kimataifa, Bodi ya Filamu Tanzania ilishiriki na kutoa mada kwenye Tamasha la Filamu la Kimataifa la Afrika (*Africa International Film Festival - AFRIFF*) liliofanyika Jijini Lagos, Nigeria mwezi Novemba, 2019 pamoja na Kongamano la FOCUS2019 liliofanyika mwezi Desemba, 2019 jijini London, Uingereza, ambapo Bodi ilitumia nafasi hiyo, pamoja na mambo mengine, kuitangaza Tanzania kama eneo mahususi la upigaji picha na uwekezaji katika masuala ya filamu.

93. *Mheshimiwa Spika*, ili kuhakikisha kuwa wasanii wanapata haki na stahili zao, Bodi iliunda na kuratibu Kamati ya Kutetea Haki za Wasanii kwa maelekezo ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo. Kamati hiyo ilipokea jumla ya malalamiko 12 na kuyashughulikia ambapo baadhi yamekamilika na mengine yapo kwenye hatua mbalimbali za usuluhishwaji. Kati ya malalamiko hayo, saba (7) yalishughulikiwa ambapo manne (4) wahusika walifikiana na matatu (3) yalimalizika bila kufikia suluhu, na hivyo wahusika kushauriwa kufikisha masuala yao mahakamani. Aidha, malalamiko matano (5) yanaendelea kushughulikiwa na Kamati;

Miongoni mwa malalamiko yaliyofikishwa kwenye Kamati hiyo ni shauri la Mama mzazi wa Marehemu Steven Kanumba Bi. Florence Mutegoha dhidi ya kampuni ya Star Times ambapo kampuni hiyo imemlipa shilingi milioni 5 na Asteria Mvungi na wenzake (jumla yao ni 10) dhidi ya mزالشاجي wa filamu Ernest Rwandala ambapo walalamikaji hao wamelipwa takriban Shilingi milioni 2 kila mmoja.

Aidha, mbali na malalamiko hayo 12 yaliyofikishwa kwenye Kamati, Bodi ilishughulikia malalamiko mawili ambayo yalimalizika kabla ya kufikishwa kwenye Kamati. Malalamiko hayo ni shauri la Liro Promotions na Twins Media dhidi ya kampuni ya Star Times ambapo zaidi ya Shilingi milioni 80 zimelipwa kwa walalamikaji, pamoja na mزالشاجي wa filamu John Lister dhidi ya msambazaji Swahiliflix, ambapo msambazaji huyo alimlipa mlalamikaji John Lister kiasi cha Shilingi milioni 5.

Katika kuimarisha ushirikiano utakaoboresha utendaji na maendeleo ya Tasnia ya Filamu, Bodi ya Filamu ilikutana na Bodi ya Filamu na Machapisho ya Afrika Kusini na Bodi ya Filamu ya Kenya kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji wa masuala ya filamu pamoja na kuanzisha ushirikiano na Taasisi hizi. Bodii imeshaanza taratibu za kuanzisha uhusiano wa kikazi na Taasisi hizo.

3.2.3.3 TAASISI YA SANA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

94. *Mheshimiwa Spika*, Jukumu kubwa la TaSUBa ni kutoa mafunzo ya Sanaa na Utamaduni katika ngazi ya Cheti na Astashahada. Aidha, Taasisi hii hutoa mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wasanii wa sanaa na utamaduni kadiri ya mahitaji.

95. *Mheshimiwa Spika*, TaSUBa imeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 235 mwaka wa masomo 2018/19 hadi kufikia 411 mwaka wa masomo 2019/20 (ongezeko la 75%). Mafunzo yanayotolewa na Taasisi ni Astashahada NTA 4, Stashahada NTA 5 na Stashahada NTA 6 kwa programu tatu

ambazo ni Sanaa za Maonyesho na Ufundzi (*Performing & Visual Art*), Uzalishaji wa Vipindi vyta Televisheni na Filamu (*TV & Film Production*) na Uzalishaji wa Muziki na Teknolojia ya Sauti (*Music & Sound Production*). Aidha, wanachuo wa kozi fupi waliosajiliwa katika kipindi hiki ni 80. *Kiambatisho Na.* V kinaonyesha Wanafunzi waliohitimu mafunzo katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni mwaka wa masomo 2010/11-2018/19.

Aidha, katika mwaka wa masomo 2019/20 Taasisi imetoa ufadhili kwa Watanzania wa kike wapatao kumi (10). Ufadhili huu ni wa awamu tatu, ambapo awamu ya mwisho ni mwaka wa masomo 2020/21, ambapo Taasisi itafanya tathmini ya endapo malengo ya kuanzishwa kwa utaratibu huu yamefikiwa. Malengo hayo ni kuhamasisha wanawake zaidi kujunga na Chuo na kuongeza idadi yao katika tasnia ya Sanaa.


Kielelezo Na.9: Wanafunzi Waliodahiliwa katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), 2014/2015-2019/2020

96. Mheshimiwa Spika, TaSUBa iliendelea na zoezi la kuanzisha mitaala mipya ya sanaa na utamaduni kwa mujibu wa mahitaji ya soko na tasnia. Hadi sasa mitaala ya programu mbili (2) za Astashahada na Stashahada ambazo ni Uongozi na Masoko "*Art Management and Marketing*", na "*Cultural Heritage and Tourism*" imekwisha chakatwa na taratibu za kuiwasilisha kwenye Baraza la Elimu ya Ufundzi (NACTE) kwa

ajili ya kupatiwa ithibati zinakamilishwa. Mitaala hii itawawezesha wadau hususan vijana kupata taaluma muhimu katika mawanda ya sanaa, urithi wa utamaduni, utalii wa kitamaduni, masoko na uongozi katika tasnia ya sanaa na utamaduni. Aidha, mchakato wa utayarishaji wa mtaala wa *Lugha ya Kiswahili* kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada umeanza.

97. Mheshimiwa Spika, Ushirikiano baina ya TaSUBa na wadau wa Sanaa ndani na nje ya nchi uliendelea kuimariswa kwa maendeleo ya Taasisi hii. Wasanii kutoka Ujerumani kwa jina la *Musicians for Better Life*, wasanii kutoka *nchini Sweden* kwa jina la *Music Hands On*, mtaalamu wa studio kutoka nchini Denmark pamoja na ujumbe kutoka China na Korea Kusini walishirikiana na Taasisi katika masuala mbalimbali ikiwemo kuendesha warsha na kubadilishana utaalamu. Jumla ya Wanachuo na Wakufunzi 56 wameshiriki ambapo kati ya hao, Wanafunzi ni 49 na Wakufunzi ni 7.

98. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na *Clouds Plus*



ilikuwa ni vifaa. Tamasha la 39 linatarajiwa kufanyika tarehe 19 – 26 Septemba, 2020 kwa kushirikiana na wadau wa sanaa hasa *Clouds Plus Production* ambao wameonyesha utayari wa ushirikiano.

3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

99. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Maendeleo ya Michezo inahusisha Idara ya Maendeleo ya Michezo na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Jukumu kubwa la Sekta hii ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa miundombinu na wataalamu wa michezo kwa kushirikiana na wadau, kuhamasisha umma kushiriki katika michezo na kuhakikisha Timu za Taifa na wachezaji wanafanya vyema katika mashindano ya Kimataifa kwa kushirikiana na wadau.

100. *Mheshimiwa Spika*, ili kuimarisha Sekta ya Michezo, Wizara iliandaa Rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Michezo. Mkakati huo unalenga kuimarisha na kupatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Michezo. Pamoja na Mkakati kuzingatia maoni ya wadau yaliyowasilishwa, pia umezingatia changamoto zilizoibuliwa katika tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995. Kwa sasa Wizara inaendelea kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu ya Mkakati kabla haujakamilishwa na kuzinduliu rasmi.

101. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Baraza la Michezo la Taifa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) iliandaa programu ya kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu shulenii utakaofadhiliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu la Bara la Ulaya (UEFA) kwa kushirikiana na TFF. Pamoja na mambo mengine ya kiu fundi katika hatua za utekelezaji wa programu hiyo, imekubalika itatekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa watoto wa jinsi zote katika shule mbili kwa kila Mkoa (1 ya Msingi na 1 ya Sekondari). Programu inatarajia kuanza mwezi Julai, 2020 kwa TFF kutoa mafunzo kwa walimu wa mpira wa miguu watakaofundisha katika shule za Msingi na Sekondari zitakazoteuliwa. Kamati ya Wataalam kutoka katika Wizara na Taasisi hizo inaendelea kuratibu upatikanaji wa shule mbili kutoka katika Mikoa yote kwa kutumia vigezo viliviyowekwa.

102. *Mheshimiwa Spika*, katika kuboresha usimamizi wa michezo na kuweka mikakati ya kuhakikisha nchi yetu

inafanya vizuri katika medani mbalimbali za michezo, Wizara iliendesha Kikao Kazi cha Maofisa Michezo kilichohusisha mikoa 26 ya Tanzania Bara. Kikao Kazi hicho ambacho kilifanyika tarehe 12 – 13 Desemba, 2019 Jijini Dodoma na kuhusisha Maofisa na wadau wa michezo 265 kilijadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya michezo katika maeneo yao ya kazi na nchi kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati/maazimio mbalimbali ya kuzipatia ufumbuzi.

103. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuratibu ujenzi wa uwanja wa michezo wa Dodoma kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyoahidi kuwajengea wananchi uwanja wa michezo wa kisasa katika Jiji la Dodoma. Tayari hatua za awali za ujenzi zimekwishafanyika ikiwemo uandaaji wa mchoro wa usanifu majengo na mchoro ya miundo (*architectural drawings* na *structural drawings*), ukadiriaji wa ghamama za ujenzi (BOQ), *geotechnical survey* na *tathmini* ya mchanga wa eneo (*soil investigation*), *tathmini* ya eneo kuhusu tetemeko la ardhi (*earthquake analysis*) na *topographic survey*. Hatua nyingine ni kufanyika kwa tathmini ya athari za mradi katika mazingira na jamii (*environmental and social impact analysis*), *feasibility study* na kuandaa Mpango wa Biashara (*Bussines Plan*). Jumla ya ekari 328.6 zimetengwa katika eneo la Nanenane Jijini Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huu.

104. *Mheshimiwa Spika*, Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 inaelekeza kuwa ujenzi wa viwanja vya michezo utafanyika kwa ushirikiano baina ya Serikali, watu binafsi, Mashirika, kampuni na Taasisi mbalimbali. Pamoja na Wizara yangu kuendelea na utunzaji na uendeshaji wa Viwanja vya Taifa na Uhuru, kampuni na Taasisi mbalimbali zimeonyesha mfano kwa kujenga miundombinu bora na ya kisasa ya michezo. Ninaomba nitaje kwa uchache Taasisi hizo kuwa ni pamoja na Uwanja wa Azam Complex uliopo Mbagala Dar es Salaam, uwanja wa Klabu ya Simba-Dar es Salaaam, General Waitara Golf Court, Kili Golf, Boko Veteran-Dar es

Salaam, Gwambina Stadium-Misungwi, Filbert Bayi Indoor Court, Uwanja wa Majaliwa-Lindi, Ngarenaro Sports Complex kinachomilikiwa na Jiji la Arusha na St. Patrick Sports Academy, Arusha.

Nitumie fursa hii kuwahamasisha wadau wengine wa michezo ikiwa ni pamoja na kampuni, taasisi, watu binafsi, Halmashauri na Majiji yote nchini kuiga mfano wa kujenga miundombinu ya michezo ili kuharakisha maendeleo ya michezo nchini.

105. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni hatua ya kuimarisha miundombinu ya michezo nchini, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi nydingine wadau, imeanza maandalizi ya Andiko la ujenzi wa Uwanja wa Ndani utakaotumika kwa ajili ya michezo ya ndani na sanaa mbalimbali kwa wakati mmoja (*Sports and Arts Arena*). Andiko hilo linalotarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha litatoa fursa ya utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Tayari wadau mbalimbali wa maendeleo ya michezo na sanaa wameonyesha nia ya kutaka kushirikiana na Serikali katika mradi huu wa aina yake utakaotekeliza ndani ya eneo changamani la Michezo, Jijini Dar es Salaam.

106. *Mheshimiwa Spika*, michezo ni kiwanda kikubwa kinachobeba ajira lukuki hususan kwa vijana wetu ndani na nje ya nchi, kiwanda chenye mfumo mahsus wa elimu kwa ngazi mbalimbali na mtandao mkubwa wa miundombinu (iliyopo na inayoendelea kujengwa kuendana na mahitaji). Hivyo basi, ni kiwanda chenye mamillioni ya wadau ambacho hakina budi kuchangia katika maendeleo ya uchumi ya nchi.

Ni katika muktadha huo, Serikali imehakikisha michezo inapewa fursa kwenye mitaala ya shule zetu na kila mwaka mashindano ya michezo kwa watoto wa shule za msingi (UMITASHUMTA) na shule za sekondari (UMISETA), yanafanyaika yakikusanya maelfu ya watoto kutoka kila kona ya Tanzania. Tunalazimika kuingia gharama hizo kila mwaka ili kuibua vipaji vingali vichanga kwa lengo la kuvienda viweze kuonekana na kutumika kimataifa na vilevile kupeperusha bendera ya Tanzania katika michezo mbalimbali.

107. *Mheshimika Spika*, kwa kuwa michezo ya kulipwa inazidi kuongezeka nchini (iklwemo soka, mpira wa pete, mpira wa kikapu, cricket na ngumi), tunao wajibu kama Taifa kuwa na utaratibu (unaofanana kimaudhui kwa michezo yote) wa kuruhusu wachezaji wa kigeni kuchezea vilabu vyetu lakini kuendana na misingi ya kulinda na kuendeleza fursa za ajira kwa Watanzania kama ilivyo katika uwekezaji wowote hapa nchini. Tunaua vipaji vya ndani kwa kuachia milango wazi kwa wachezaji wa nje bila ukomo wenyе tija na tunaufanya mchango wa Serikali kuititia UMITASHUMTA na UMISETA ukose maana yoyote na msisitizo kwa vilabu vyetu kuwa na timu za vijana nao ukose mashiko.

108. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuzingatia kwamba vilabu vyetu vikubwa vya Simba na Yanga vinajivunia historia ndefu ya soka iliyotukuka bila wachezaji wa nje kuwa mhimili wa timu; kwamba timu ya Taifa ya soka ya vijana (Serengeti Boys), ya wanawake ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens) na ya wanawake ya Taifa (Twiga Stars) ambazo zinafanya vizuri sana kimataifa na zinaundwa na vijana wanaotoka kwenye shule au vilabu visivyo na wachezaji wa nje; nchi zote zenye mafanikio makubwa katika soka duniani hazina sera ya "mlango wazi" kama tuliyonayo Tanzania ambapo kila mcheza soka (awe wa timu ya daraja la 3 au bila daraja) alimradi anatoka nje ya mipaka, anaweza chezea Ligi Kuu ya Tanzania; Wizara imeliagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuhakikisha kwamba tuna ukomo wenyе tija wa wachezaji wa nje nchini kwa michezo yote ili wadau wa michezo wawe na umakini zaidi kuingiza nchini wachezaji bora tu wenyе sifa stahili (quality players) mfano wa akina Morrison, Kagere, Shikalo, Wawa, Niyonzima na Louis (kwa vipimo vyangu). Aidha, waelekeze pia macho yao kwenye timu zao za vijana na mashindano mbalimbali ya kuibua vipaji ndani ya nchi yakiwemo ya UMITASHUMTA na UMISETA, na walimu tunaowapata kutoka nje ya nchi walazimike kuwa na walimu wasaidizi wa Kitanzania. BMT imeagizwa kuhakikisha zoezi hilo linakamilika ifikapo tarehe 15 Mei, 2020 kwa hatua za utekelezaji.

109. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa ajili ya kuwapatia wadau mbalimbali wa michezo ujuzi wa kufundisha michezo. Aidha, chuo kimechimba kisima cha maji safi na kukarabati viwanja vya michezo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki takribani 203 kwenye mikoa ifuatayo; Njombe (wilaya ya Wangingombe washiriki 83), Rukwa (wilaya ya Kalambo washiriki 48) na Mwanza (Wilaya ya Kwimba washiriki 72). Aidha, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 jumla ya wanafunzi 110 walidahiliwa katika Chuo hicho kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu (Stashahada).

Mwenendo wa usajili katika Chuo hiki kwa mwaka 2010-2019 ni kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na. VI*. Vilevile, Wizara ilikamilisha Andiko la kukihiusha Chuo hiki ili kiwe Wakala anayejitegemea katika kutoa mafunzo ya michezo pamoja na kufanya tafiti na kutoa ushauri katika nyanja za michezo.

110. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kinaboresha mitaala na masomo yake ili kutoa watalaan watakaokuwa na tija kwa maendeleo ya michezo, Chuo hicho kimeanza ushirikiano na Mashirikisho mbalimbali ya michezo ndani na nje ya Nchi. Kwa sasa chuo kimeanzisha ushirikiano na Chama cha Mchezo wa Mpira wa Mikono (TAHA) ambapo chama hicho, kupitia watalaan wake wa ndani na wa kimataifa hutoa mafunzo ya michezo huo chuoni. Aidha, Chuo na TFF wapo katika hatua za mwisho za kuingia makubaliano ya kuwezesha wakufunzi wa michezo wa mpira wa miguu wa ndani na nje kutoka katika Mashirikisho ya Kimataifa ya CAF na FIFA kutoa mafunzo katika Chuo hicho. Hatua hii itawezesha kupata watalaan wenye uwezo kulingana na matakwa yanayokubalika na Mashirikisho hayo na pia kuwezesha wahitimu wa Chuo hicho kuwa na sifa za kutosha za kitalaan ili kuendelea na kozi nytingine za ubobezi katika michezo.

Nia ya Chuo ni kuendelea kuanzisha na kuimarisha ushirikiano na Taasisi nyingine ili kuhakikisha wanafunzi wanaohitimu wanakuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza michezo nchini.

111. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kutoa huduma za Kinga na tiba kwa Wanamichezo kupitia Kitengo cha Tiba na Kinga kwa wanamichezo kilichopo katika Uwanja wa Taifa. Jumla ya wanamichezo na wadau 1,952 walipata huduma hiyo katika kipindi hiki.

3.2.4.1 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

112. *Mheshimiwa Spika*, Baraza la Michezo la Taifa lina jukumu la kusimamia na kuendeleza aina zote za michezo kwa kushirikiana na vyama vya michezo, kutoa mafunzo mbalimbali ya michezo pamoja na kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho/Vyama vya Michezo.

113. *Mheshimiwa Spika*, Baraza iliendelea kusajili na kusimamia Vyama, Vilabu na Wakuzaji wa Michezo ambapo hadi sasa jumla ya Vyama na Vilabu 9,189 vimesajiliwa. Aidha, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Vyama vya Michezo 18, Vilabu 231, Vituo vya Michezo 21 na Wakuzaji/ Mawakala wa michezo 19 vilisajiliwa. *Kiambatisho Na. VII* kinabainisha mwenendo wa usajili wa Vyama, Vilabu, Vituo vya Michezo na Mawakala wa Michezo katika kipindi cha 2010 – 2019. Aidha, kulifanyika uhakiki wa Vyama vya Michezo 70 vya Kitaifa kwa kuzingatia Mwongozo uliotolewa kwa vyama hivyo wa kuwa na Ofisi na Anuani ya Makazi, kumiliki Akaunti za Benki pamoja na kuandaa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Majukumu. Uhakiki huo umebaini kuwa Vyama 18 vimekidhi vigezo vyote vitatu, vyama 37 vimetekeleza kigezo kimoja au viwili kati ya vigezo vitatu vilivyoainishwa na Vyama 15 havijakidhi kigezo hata kimoja cha mwongozo huo na wala havifanyi shughuli zozote za Michezo na hivyo kuamuliwa vifutiwe usajili wake.

Aidha, Baraza lilikamilisha uandaaji wa taarifa za usajili wa Vyama na Vilabu vya Michezo 9,189 kutoka kwenye vitabu vya rejista ili kuiweka orodha kwenye mfumo wa kielekroniki kwa ajili ya kutengeneza mfumo mpya wa usajili. Hatua hii itaimarisha utunzaji wa takwimu na taarifa za Vyama na Vilabu hivyo.

114. *Mheshimiwa Spika*, BMT lilitratibu ushiriki wa Timu za Tanzania katika Michezo ya 12 ya Mataifa ya Afrika (*All African Games*) yaliyofanyika nchini Moroko tarehe 16 – 31 Agosti, 2019. Wachezaji wa Timu ya Riadha katika mbio za Kilometa 21 (Nusu Marathon) walishika nafasi ya Tano (5) na Saba (7). Aidha, Timu za Taifa za Kuogelea, *Paralympic*, Ngumi za Wazi, *Amputee Football*, *Wheelchair Basketball*, Mpira wa Meza zilitratibiwa na kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

115. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, kuliwepo na mafanikio katika michezo mbalimbali kimataifa kama ifuatavyo:

- a) Kufuzu kwa Timu ya Wale mavu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kushiriki katika mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika London, Uingereza kati ya mwezi Januari na Februari, 2021;
- b) Timu ya Riadha ya Wanawake kushinda Medali za dhahabu saba (7) na fedha moja (1) katika michezo ya riadha iliyofanyika katika Jiji la Nagai nchini Japan;
- c) Timu ya Wanawake ya Mpira wa Miguu kutwaa Kombe la COSAFA kwa Timu za Wanawake za Mpira wa Miguu chini ya umri wa miaka 20 mwezi Agosti, 2019, nchini Afrika Kusini;
- d) Timu ya Taifa ya wanaume chini ya umri wa miaka 20 kutwaa Kombe la Afrika Mashariki la Mpira wa Miguu;
- e) Kufuzu kwa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kushiriki Mashindano ya wachezaji wanaocheza ligi za ndani ya nchi "*Championnat D'Afrique Des Nations*" (CHAN);

- f) Timu ya Wanawake ya Mpira wa Meza ilishinda nafasi ya pili katika mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Uganda mwezi Januari, 2020;
- g) Tanzania kuwa mwenyeji katika mashindano ya kufuzu *Basketball Africa League* (BAL) kundi D, yaliyofanyika Dar es Salaam mwezi Oktoba, 2019. Timu ya Tanzania ilifuzu kwenda hatua ya pili katika mashindano yaliyofanyika nchini Rwanda mwezi, 2019. Katika mashindano hayo Mtanzania Baraka Sadik alitwaa Tuzo ya Mfungaji Bora wa Afrika na Stephano Mshana alipata Tuzo ya mtoa pasi za mwisho bora wa Afrika. Hii ni mara ya kwanza katika historia ya mchezo wa Mpira wa Kikapu hapa nchini;
- h) Timu ya Wanawake ya Mpira wa Wavu wa Ufukweni – U21 (Zone V Championship) ilishinda nafasi ya kwanza katika mashindano hayo yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam;
- i) Bondia Hassan Mwakinyo alimshinda Amel Tinampay, raia wa Ufilipino kwa *point* katika mchezo uliofanyika Dar es Salaam mwezi Novemba, 2019;
- j) Bondia Abdallah Paziwapazi alimchapa Zulipikaer Maimaitiali, raia wa China kwa *KO* katika pambano la *WBO Asia Pacific Super Middle Title* liliofanyika nchini China mwezi Agosti, 2019;
- k) Bondia Hamis Maya alimtwanga Piergiulia Ruhe, raia wa Ujerumani kwa *KO* katika pambano la *Global Boxing Council Intercontinental Welter* liliofanyika nchini Ujerumani mwezi Novemba, 2019;
- l) Bondia Bruno Melkiory Tarimo (Vifua Viwili) alimpiga Nathaniel May, raia wa Australia kwa *point* katika pambano la *Boxing Federation International Super Feather Title* liliofanyika nchini Australia mwezi Desemba, 2019; na
- m) Bondia Salimu Jengo alimchapa Suriya Tatakhun, raia wa Thailand kwa *KO* katika pambano la *Universal Boxing*

Organization World Light Title liliofanyika Jijini Tanga mwezi Januari, 2020.

116. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni hatua ya kuwezesha vijana wa Kitanzania kufanya vizuri katika michezo ya kulipwa, BMT ilifanya maboresho ya Sheria ya BMT ya mwaka 2018 na kuitambua michezo ya kulipwa. Kwa sasa Baraza linaandaa Mwongozo utakaoweka mazingira wezeshi ya kuwasaidia wachezaji wa Kitanzania kufanikiwa katika michezo ya kulipwa bila kupata kikwazo chochote. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 vibali 45 vimetolewa kwa Timu za Taifa, Vilabu, Vituo vyta michezo, mabondia na wataalam kwenda nje ya nchi kushiriki mashindano mbalimbali.

117. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kwa namna ya pekee kabisa inatoa pongezi kubwa kwa wachezaji wa Kitanzania wanaozidi kuongezeka kila uchao kufuzu vigezo vyta kimataifa na kucheza michezo ya kulipwa katika nchi mbalimbali na kupeperusha vyema bendera ya Tanzania. Jumla ya wachezaji 48 wanacheza michezo ya kulipwa nje ya nchi katika michezo ifuatayo: mpira wa miguu 28, mpira wa kikapu 16, mpira wa wavu watatu na ngumi za kulipwa mmoja.

118. *Mheshimiwa Spika*, Napenda kutumia fursa hii kumpongeza mchezaji wetu nyota na nahodha wa Timu ya Taifa ya Soka, Taifa Stars, Mbwana Ally Samatta ambaye siyo tu amekuwa mchezaji wa kwanza Mtanzania kusajiliwa na kuichezea Klabu ya Aston Villa ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Uingereza, ambayo ni moja ya ligi bora duniani na inayotazamwa na mashabiki wengi zaidi, lakini pia Samatta amekuwa Mtanzania wa kwanza kufunga goli katika ligi hiyo. Serikali itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ili tuzidi kupata wachezaji wengi wa kulipwa kama nilivyobainisha awali kwani vipaji vingi bado viro hapa nchini na tunaviendeleza.

119. *Mheshimiwa Spika*, uchaguzi wa Mashirikisho na vyama vyta michezo vitatu (3) uliratibwa na kusimamiwa kwa lengo la kuimarisha utawala bora katika Vyama vyta Michezo.

Mashirikisho hayo ni Shirikisho la Mchezo wa Taekwondo Tanzania (TTA), Shirikisho la Michezo ya Vyuo Vikuu Tanzania (SHIMIVUTA) na Chama Cha Kriketi Tanzania (TCA).

Vilevile, utatuzi wa Migogoro ya Vyama iliyohusu ukiukwaji wa utawala bora, ikiwemo kutokutoa taarifa za mapato na matumizi katika Vyama vya Mchezo wa Kuogelea Tanzania, Shirikisho la Mieleka Tanzania na Chama cha Riadha Tanzania umefanyika. Pia, marekebisho ya Katiba za Vyama vya Michezo vitatu (3) ambavyo ni Tanzania Ladies Golf Union (TLGU), Chama cha Kriketi Tanzania, Chama cha Mpira wa Miguu Wilaya ya Serengeti, Klabu moja (1) ya Mpira wa Miguu ya Fountain Gate yameidhinishwa.

120. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kufanya Mapitio ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya mwaka 1976 ambapo rasimu ya Sheria mpya imeandaliwa. Marekebisho ya Sheria yamezingatia mabadiliko makubwa ya kisayansi, kijamii, kiuchumi na uendeshaji wa Sekta ya Michezo. Aidha, Mkakati wa Kufanya Vizuri katika Michezo (*High Sports Performance*) umeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wa michezo ambao ni Kamati za Michezo za Mikoa na Wilaya, Viongozi wa Vyama na Mashirikisho, Kampuni zinazodhamini michezo na Kamati ya Olimpiki Tanzania.

121. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza Mpango wa Michezo kwa Jamii, yalitolewa mafunzo ya uongozi na utawala katika michezo (*sports administration*), mafunzo ya ukocha katika mpira wa mikono, mpira wa miguu na mpira wa netiboli. Vilevile, elimu ya huduma ya kwanza katika michezo na elimu ya mazoezi ya viungo imetolewa kwa walimu 31 katika Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufundisha somo la michezo, kuratibu shughuli za michezo, kuhamasisha ushiriki wa jamii katika shughuli za michezo na kuibua vipaji vya michezo. Pia, mafunzo ya uelewa wa Sheria na majukumu ya Baraza kwa Maofisa michezo wa Mikoa na Wilaya ilitolewa katika mkutano ulioandaliwa na Wizara yenye dhamana ya Michezo tarehe 12 – 13 Desemba, 2019.

122. *Mheshimiwa Spika*, ikiwa ni hatua ya kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo, BMT iliratibu mashindano ya Kitaifa ya riadha ya wanawake yajulikanayo kama "Ladies First" kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Chama cha Mchezo wa Riadha Tanzania, mashindano yalifanyika tarehe 7 - 8 Desemba, 2019 katika Uwanja wa Taifa, Jijini Dar es Salaam. Lengo la mashindano hayo lilikuwa ni kuibua vipaji vya wanawake katika mchezo wa riadha, ambapo jumla ya wanawake 186 walishiriki kutoka katika Mikoa 24 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALI DATU

123. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha utendaji na kutoa huduma bora kwa wateja na wadau wake wa ndani na nje. Jumla ya watumishi saba (7) waliruhusiwa kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na 20 mafunzo ya muda mfupi ikiwa ni hatua ya kuimarisha uwezo wao wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi na tija. Aidha, watumishi 10 walithibishwa kazini na mmoja (1) alibadilishwa kada baada ya kukidhi vigezo stahiki. Vilevile, watumishi 198 walijengewa uelewa kuhusu Mfuko Mpya wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF). Ili kuhakikisha watumishi wanashirikishwa na kutoa mawazo yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kulifanyika Mikutano miwili ya Baraza la wafanyakazi mwezi Januari na Machi, 2020.

Fauka ya hayo, Wizara iliratibu Vikao vya Ushirikiano kati ya Wizara zenyeye dhamana ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vilivyo fanyika mwezi Julai, 2019 na Machi, 2020 Mkoani Dodoma na Zanzibar mtawalia. Vikao hivi ambavyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, vinalenga kuimarisha ushirikiano, kujadili changamoto na kuweka Mikakati inayolenga kuimarisha utendaji wa Wizara na Taasisi zenyeye majukumu yanayoshabihiana katika pande mbili za Muungano. Katika Vikao hivi, maazimio mbalimbali yaliafikiwa na utekelezaji wake unaendelea.

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

124. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2019/20, pia kulijitokeza changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Wizara ni kama ifuatavyo:

- a) Kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na utandawazi inayosababisha upotoshwaji wa mila, desturi na maadili hususan kwa vijana na wasanii. Katika kukabiliana na changamoto hii Wizara imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kwa njia mbalimbali ikiwemo makongamano, semina na warsha kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili, mila na desturi za Mtanzania na umuhimu wa kutengeneza kazi za sanaa na utamaduni zenyenye staha kwa jamii. Vilevile, kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazosimamia masuala ya habari, filamu, sanaa, muziki, ulimbwende na kazi zote za ubunifu. Aidha, kwa kuwa suala la maadili ni mtambuko, wazazi wanaaswa kuwalea watoto na vijana kwa kuzingatia dhana ya malezi na makuzi ya asili ya Kitanzania na kuepuka mila na desturi zisizoendana na utamaduni wetu.
- b) Kuwepo kwa baadhi ya Vyombo vya Habari vinavyotekeleza majukumu yao bila ya kuzingatia Sheria ya Huduma za Habari Na.12 ya mwaka 2016 na Sheria nyingine. Vilevile, kumekuwepo na matumizi ya mitandao ya kijamii bila kuzingatia matakwa ya Sheria pamoja na maadili. Wizara imeendelea kutoa elimu na miongozo juu ya kuzingatia Sheria na taratibu katika utoaji wa taarifa na matumizi ya mitandao ya kijamii.
- c) Uchakavu na upungufu wa miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa). Ili kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imetenga fedha za maendeleo katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Taasisi hizi kama inavyofafanuliwa katika Kiambatisho Na. IX katika Hotuba hii.

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

125. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Taasisi zake ambapo majukumu mbalimbali yamepangwa kutekelezwa kama inavyobainishwa hapa chini.

5.1 SEKTA YA HABARI

126. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO itatekeleza majukumu yafuatayo:- kuendelea kkusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza taarifa kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelawa na Serikali; kuisemea Serikali katika masuala mbalimbali; kuchapa na kutoa leseni za magazeti na majorida pamoja na vitambulisho vya waandishi wa habari; kununua vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na usambazaji wa taarifa kwa wananchi; na kuandaa na kutoa picha za viongozi wa kitaifa. Vilevile, itawezesha utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kwa kutoa ruzuku.

5.1.1 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

127. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni: kuhabarisha umma wa Watanzania kupitia vyombo vyake vya utangazaji kuhusiana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ili kutimiza jukumu hilo, kutanunuliwa vifaa vya kisasa, kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa vipindi mahususi vinavyohusiana na maandalizi ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi. Majukumu mengine ni kuendelea kuboresha maudhui ya Chaneli ya Tanzania Safari ili iweze kuwafikia watazamaji wengi nje ya Tanzania na kuimarisha mifumo ya utangazaji kwa kuboresha studio za redio na televisheni.

128. *Mheshimiwa Spika*, TBC itaendelea kuboresha studio za Redio na Televisheni zilizopo jijini Dodoma pamoja na ununuuzi wa mitambo na vifaa vya urushaji wa matangazo

mubashara. Aidha, itaendelea na ujenzi wa mitambo ya kurushia matangazo kwa ajili ya upanuzi wa usikivu katika Wilaya za Same, Sikonge, Kahama, Bunda, Nkasi, Kasulu na Karagwe kwa kutumia Fedha za Maendeleo. TBC pia itajenga mitambo ya FM katika Wilaya za Tanganyika, Makete, Uvinza, Mbinga, na Ngorongoro kwa Fedha za ufadhili kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Kukamilika kwa miradi hii kutawezesha TBC kufikia usikivu wa Wilaya 137 sawa na asilimia 85.1. TBC itaendelea na ukarabati wa studio za redio (TBC_{Taifa}, TBC_{FM} na TBC_{International}) kwa kufunga mitambo na vifaa vyta kisasa vya kidijiti vitakavyoboresha pia urushaji wa matangazo kuititia mitandao ya kijamii.

5.1.2 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)

129. *Mheshimiwa Spika*, TSN itaendelea kuimarisha ubora wa bidhaa na huduma za Kampuni; kuboresha uwezo wa Taasisi katika utendaji na shughuli za kibashara; kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa kuititia Mpango wa Utekelezaji wa Kampuni; kuimarisha hali ya fedha ya Kampuni; na kuimarisha ufanisi wa rasilimali watu na kuongeza na kuboresha vitendea kazi.

5.1.3 MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)

130. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka itaendelea kutoa leseni za redio, televisheni na mitandao ya kijamii; kufuatilia maudhui yanayotolewa na Vituo vya Utangazaji na Watoa Huduma za Maudhui Mtandaoni na kushughulikia ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya kiseka ikiwa ni pamoa na kusikiliza malalamiko na kuyatolea uamuzi. Majukumu mengine ni kuhamasisha utengenezaji na uzalishaji maudhui ya ndani yenye ubora (Quality local Content); kutoa elimu juu ya kuandaa vipindi na taarifa zinazohusu masuala ya uchaguzi; na kuhamasisha uanzishwaji wa redio za kijamii katika miji na Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Aidha, TCRA itakutana na wadau wa utangazaji ili kutatua changamoto za sekta ya utangazaji kuititia Mkutano Mkuu wa Mwaka wa wadau wa Utangazaji (*Annual Broadcasters Conference*).

5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

131. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yafuatayo yatakelezwa:- kukamilisha zoezi la uhuishaji wa Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997; kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa; kuratibu mikutano ya Kitaifa na Kimataifa kuhusu utamaduni; kuratibu na kuendesha mukutano wa mwaka wa Maofisa Utamaduni na kuratibu Tamasha la Urithi (Urithi Festival) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na wadau wengine. Majukumu mengine ni kuratibu na kuendesha program za Kiutamaduni kwa Shule za Msingi katika Mikoa ya Mwanza na Dodoma; kuratibu maadhimisho ya Siku ya Utamaduni Duniani; kuratibu uanzishwaji wa kituo cha kuhifadhi taarifa za kiutamaduni; na kukuza matumizi ya Kiswahili kama lugha ya Kimataifa.

Fauka ya hayo, Wizara kwa kushirikiana na BAKITA itanunua seti mbili za vifaa vya kukalimani, kuandaa machapisho mbalimbali ya kufundisha Kiswahili kwa wageni na kutoa mafunzo kwa wakalimani wa Kiswahili; kutambua na kuandaa Orodha ya Kitaifa ya Vipengele vya Urithi wa Utamaduni Usioshikika; kuratibu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na kutoa ruzuku kwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA).

5.2.1 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

132. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yatakayotekerezwa ni: kuchapisha kamusi ndogo za Kiswahili - Kiingereza- Kifaransa na Kiswahili- Kiingereza – Kireno zitakazosaidia ubidhaishaji wa Kiswahili katika nchi za SADC; kuandaa mafunzo maalumu ya kuwawezesha wakalimani 50 waliotambuliwa kuboresha uwezo wao wa kiutendaji; kupitia na kuboresha kitabu cha Furahia Kiswahili ambacho kitatumika kama kitabu cha msingi katika kufundisha Kiswahili kwa wageni ndani na nje ya nchi; kuandaa na kurusha hewani vipindi 620 vya redio na televisheni na kuandaa makala 20 zitakazochapishwa katika gazeti la HabariLeo ambavyo kwa ujumla wake vitalenga kuelimisha umma kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya

Kiswahili; kusanifu istilahi za uga wa bandari; kutambua vituo vitano (5) vya kufundisha Kiswahili kwa wageni; na kuendesha semina kwa waandishi na watangazaji wa vituo kumi (10) vya redio na televisheni. Majukumu mengine ni kutoa mafunzo ya kuimarishta stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa wataalamu 400; kuchapisha Kamusi ya Kiswahili kwa shule za Msingi; kukusanya matini za maneno 1,000,000 kwa ajili ya kongoo la Kiswahili; na kutoa ithibati ya lugha kwa vitabu 40 vinavyokusudiwa kutumika shuleni. Halikadhalika, Baraza litatoa huduma ya tafsiri katika nyaraka 4000 za mashirika, taasisi na kampuni za Serikali na watu binafsi pamoja na kutoa huduma ya ukalimani katika mikutano ya kitaifa na kimataifa.

5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

133. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaratibu Kampeni ya Uzalendo na Utaifa (Nchi Yangu Kwanza); kuratibu uanzishwaji wa Ukumbi wa Sanaa (*Sports and Arts Arena*) kwa kushirikiana na Wadau wengine; kuratibu ujenzi wa Sanamu la Mwalimu Nyerere katika Jiji la Addis Ababa nchini Ethiopia; kuratibu upatikanaji wa Kanzi data ya Wasanii mashuhuri na kuhifadhi kazi zao katika maandishi; na kuratibu uanzishwaji wa Mamlaka ya Tasnia za Ubunifu na Hakimiliki.

Majukumu mengine ni kuratibu Tamasha la Kitaifa la Sanaa na Utamaduni Tanzania, ambalo litafanana na Tamasha la JAMAFEST ili kuandaa Washiriki wa JAMAFEST 2021; kuendesha Kongamano la Sanaa la Kimataifa; na kuendelea na kuratibu Tamasha la Urithi (Urithi Festival) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Pia, itaratibu ushiriki wa vikundi vya sanaa katika Maadhimisho ya Uhuru na Muungano na matukio mengine ya Kitaifa na Kimataifa; kuratibu urasimishaji wa matamasha yote ya Sanaa nchini; na kuimarishta Utendaji wa Taasisi zenyeye dhamana ya masuala ya Sanaa (BASATA, TaSUBa na Bodi ya Filamu) kwa kuzipatia ruzuku na kukamilisha mchakato na maelekezo ya kukihamisha Chama cha Hakimiliki (COSOTA) ambacho kiko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuja Wizara ya Habari kwa lengo la

kusimamia haki za wasanii na wanatasnia wengine kwa ufanisi zaidi.

5.3.1 BODI YA FILAMU TANZANIA

134. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yatakayoteklezwa ni:- kupitia na kuchambua Miswada 500 ya kutengeneza picha jongevu, makala za filamu, matangazo ya biashara na michezo ya kuigiza; kuhakiki, kupanga katika madaraja na kutoa vibali kwa kazi za picha jongevu 1,000; kubaini, kuimarisha, kuendeleza na kutoa ithibati za uendeshaji wa shughuli na biashara za picha jongevu; na kuendesha operesheni 38 dhidi ya kazi za filamu zinazoingia sokoni kinyume cha taratibu.

Majukumu mengine ni kuratibu uendeshaji wa matamasha mbalimbali; kuwajengea uwezo wadau kupitia mafunzo, matukio/makongamano na vikao ndani na nje ya nchi; kuanzisha mchakato wa kutunga Sheria mpya ya Filamu na Michezo ya Kuigiza; kuendelea na urasimishaji wa maeneo yasiyokuwa rasmi ili kuimarisha taarifa za kisekta pamoja na kupanua wigo wa soko la kazi za filamu; na kuitangaza Tanzania kama eneo lenye mandhari za kipekee kwa upigaji picha za filamu, utengenezaji wa makala za filamu na matangazo pamoja na kutangaza huduma zinazotolewa na Bodi ya Filamu.

Vilevile, kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi na kuzindua matumizi ya mfumo wa utambuzi na usajili wa watendaji/wadau katika sekta ya filamu na michezo ya kuigiza nchini.

Majukumu mengine ni kufufua utamaduni wa Watanzania kuangalia filamu kwenye kumbi za cinema ili kuinua sekta ya filamu Tanzania kwa kuhamasisha uzalishaji wa filamu bora za Kitanzania zenye vigezo vya kuonyeshwa kwenye kumbi za cinema, na kuamsha ari ya Watanzania kuangalia filamu hizo kwenye kumbi tajwa, ikiwa pia ni njia ya kuzipandisha hadhi filamu hizo.

5.3.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

135. *Mheshimiwa Spika*, Baraza litaendelea na ukamilishaji wa Mradi wa Ukumbi wa Maonyesho ya Sanaa na kuanza matumizi ya ukumbi huo kwa shughuli mbalimbali za maonyesho ya Sanaa. Aidha, BASATA litaendelea kukuza weledi na kujenga uwezo kwa wasanii ikiwa ni pamoja na masuala ya maadili; kukuza Sanaa kwa wanafunzi wa shule na watoto; kuimarisha uhusiano wa Baraza na wasanii/ wadau wake; kulitangaza Baraza na majukumu yake kwa wadau wake na kuongeza mapato ya Baraza kwa kuyafikia maeneo mengi na wadau wengi zaidi. Majukumu mengine ni kujenga uwezo kwa watumishi; kuimarisha uendeshaji wa ofisi na kuwekeza katika ulipaji wa madeni ya taasisi.

5.3.3 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TASUBa)

136. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yatakayotekelezwa na TaSUBa ni kuendelea na udahili wa Wanachuo 450 kwa mwaka wa masomo 2020/21 na kuimarisha ubora katika kujifunza na kufundisha; kutoa mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa ngazi ya astashahada, stashahada na kozi fupi; kuimarisha ushirikiano na wadau wa sanaa ndani na nje ya nchi kwa kuendesha warsha na kubadilishana utaalamu kwa wanachuo na wakufunzi; kuandika maandiko ya miradi ya maendeleo hasa kuimarisha miundombinu; kukamilisha maandalizi ya Mitaala mipya na kuanza kuitumia katika Mwaka wa Masomo 2020/21- (udahili wa mwezi wa Machi, 2021), baada ya kuidhinishwa na kupewa ithibati na NACTE. Majukumu mengine ni kuitangaza Taasisi na huduma zake ili zижilikane kwa wadau wengi kuititia vyombo vya habari; kuandaa na kuendesha Tamasha la 39 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kukarabati madarasa, maktaba na studio ya kufundishia kwa vitendo na kununua vifaa vya kufundisha na kujifunzia.

5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

137. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuratibu ushiriki wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa kwa kushirikiana na wadau; kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Michezo; kuratibu uanzishwaji wa Kituo cha Kitaifa cha Kudhibiti Matumizi na Mbinu Haramu Michezoni (National Anti-Doping Organization-NADO) kwa kushirikiana na Kamati ya Olympic Tanzania (TOC) na kuratibu usimamizi na utunzaji wa Viwanja vya Taifa na Uhuru pamoja na miundombinu mingine ya michezo.

Majukumu mengine ni kufanya tathmini ya hali ya miundombinu ya michezo katika Mikoa na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu ujenzi na uendelezaji wa miundombinu hiyo; kutoa mafunzo kwa wataalamu wa michezo ikiwemo walimu, makocha na wasimamizi wa michezo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; kutoa huduma za kinga na tiba kwa wanamichezo kupitia Sehemu ya Tiba na Kinga iliyopo katika Uwanja wa Taifa; Kuratibu michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI; kuratibu ushiriki wa Timu za Taifa katika mashindano ya Kimataifa ikiwemo Michezo ya Olimpiki ya Tokyo na Jumuiya ya Afrika Mashariki; kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa kuhusu michezo; na kutoa ruzuku kwa Baraza la Michezo la Taifa.

Vilevile, kuimarisha makusanyo ya mapato yatokanayo na shughuli zinazofanyika katika viwanja vya Taifa na Uhuru ambavyo vinamilikiwa na Serikali ikiwemo kuboresha mfumo wa ukusanyaji mapato katika viwanja hivyo; kuratibu uanzishwaji wa Mpango wa Ukuzaji wa Vipaji vya Mpira wa Miguu kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, WEST, BMT, TFF na Shirikisho la Mpira wa Miguu Bara la Ulaya (UEFA); kuendelea na maandalizi ya Mradi wa Ujenzi wa Sports and Arts Arena, ambaao unatarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Pia, kufanya ukarabati katika maeneo mbalimbali ya Uwanja wa Taifa; kujenga madarasa matatu, bwalo pamoja na kuweka miundombinu yake na samani katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

5.4.1 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

138. *Mheshimiwa Spika*, BMT itaendelea kusajili Vyama/Mashirikisho, Vilabu, Vituo vya Michezo na Wakuzaji/Mawakala wa Michezo; kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wa michezo ili kuwajenyea uwezo; kufanya mikutano yenye tija na viongozi wa Vyama/Mashirikisho ya Michezo katika kuhamasisha dhana ya uongozi na utawala bora katika michezo; kuendelea kuratibu ushiriki wa Timu za Taifa katika Mashindano ya Ndani na Nje ya Nchi; na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika michezo kama ajira na kuimarishe afya.

5.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA

139. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuimarishe nguvukazi yake kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuajiri, kupandisha vyeo na kubadilisha kada watumishi watakaokidhi vigezo na kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa mujibu wa Mpango wa Mafunzo. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya kazi na utoaji wa huduma kwa kununua vitendea kazi muhimu na kulipa kwa wakati stahili mbalimbali za watumishi pamoja na kufanya vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Halikadhalika, watumishi watahamasishwa kujikinga na magonjwa ya VVU na UKIMWI na magonjwa mengine ya kuambukiza na yasiyoambukiza ikiwemo shnikizo la damu na kisukari na pia watapewa mafunzo ya kujiepusha na rushwa mahala pa kazi.

6.0 MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

6.1 MAPATO

140. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2020/21 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini (Sh. 960,000,000) kuititia Idara ya Habari-MAELEZO na Maendeleo ya Michezo. Aidha, kwa upande wa Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara kiasi kinachokadiriwa kukusanya ni jumla ya Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja Sabini na Moja, Mia Mbili Sitini na Nne Elfu (Sh.40,171,264,000). *Kiambatisho Na.*

V/// ni mchanganuo wa maduhuli yanayotarajiwa kukusanywa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2020/21.

6.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO

141. *Mheshimiwa Spika*, Mwaka 2020/21 Wizara imetengewa bajeti ya Shilingi **Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja Arobaini, Mia Sita Arobaini na Moja Elfu (Sh. 40,140,641,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Sabini na Tisa, **Mia Mbili Thelathini na Moja Elfu** (Sh. 20,979,231,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Arobaini na Sita, **Mia Nne Kumi Elfu** (Sh. 11,446,410,000) na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Kumi na Tano** (Sh. 7,715,000,000). *Kiambatisho Na IX* kinaonyesha mgawanyo wa Bajeti ya Wizara kwa Idara na Vitengo, Taasisi zilizo chini ya Wizara na Miradi ya Maendeleo.**

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MPANGO WA MWAKA 2020/21

142. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2020/21 naomba sasa niliombe Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2020/21 ya jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja Arobaini, Mia Sita Arobaini na Moja Elfu (Sh. 40,140,641,000). Kati ya fedha hizo Mishahara ni **Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Sabini na Tisa, Mia Mbili Thelathini na Moja Elfu** (Sh. 20,979,231,000), Matumizi Mengineyo ni Shilingi Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nne Arobaini na Sita, **Mia Nne na Kumi Elfu** (Sh. 11,446,410,000) na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Kumi na Tano** (Sh. 7,715,000,000).**

8.0 MWISHO NA SHUKRANI

143. *Mheshimiwa Spika*, mwisho kabisa niruhusu nitoe tanbihi na kufanya dhukuru kidogo: mafanikio yaliyopatikana katika Wizara yangu katika kipindi cha miaka hii Mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano ni makubwa, ya kujivunia na yanayojuzu

kuendelezwa. Hii ni Wizara inayolipa Taifa heshima kubwa duniani, na hii ni Wizara ambayo kupitia sekta zake zote inalipa nguvu na uhai Taifa letu kufanya vyema zaidi katika nyanja nyingine; kwani bila sekta imara na inayowajibika kitaaluma ya habari, Taifa litakosa taarifa na maarifa; na Taifa lisilo na taarifa ni sawa na ndege asiyé na mbawa;

Sekta za utamaduni, sanaa na michezo nazo pia ndizo msingi mkubwa wa afya na furaha kwa Watanzania. Muziki uliozalishwa na wasanii wetu katika kipindi chote hiki umekuwa chakula muhimu cha roho na kuitafakarisha pamoja na kuiliwaza jamii. Filamu zilizozalishwa zimeonesha mazuri na maendeleo ya nchi yetu na ushiriki wetu katika michezo umeimarisha afya na kulitambulisha Taifa letu kuwa nchi yenye watu wenye siha na mwenendo faavu.

144. *Mheshimiwa Spika*, lakini mafanikio haya, pamoja na kazi za kila siku za sisi wa Wizarani na wadau mmoja mmoja au kwa makundi yao, lazima tukiri, ni matokeo ya maono na juhudhi binafsi za Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli; kiongozi, nguli na galacha mwenye maono ya mbele na mbali. Katika hii miaka mitano ametoa fedha kusaidia michezo na wasanii, amekutana na wanahabari, wasanii na wanamichezo, ameonekana akishiriki kujichanganya na wasanii kwa kupiga ngoma, ameungana na wanautamaduni kuonesha urithi wa nchi yetu, amekwenda viwanjani kushuhudia michezo, amewasaidia wasanii, wanahabari na wanamichezo kila walipokuwa na shida au hata kutoa salamu walipofikwa na misiba au majanga. Amekuwa karibu na kila sekta bila kubagua. Rais Magufuli ni aina ya kiongozi ambaye Watanzania na sisi wadau wa sekta zangu tunapaswa kumlipa wema kwa wema kwa kuendelea kumpa nafasi ya kutoa maono yake na uongozi zaidi katika nchi yetu.

145. *Mheshimiwa Spika*, mwisho lakini si kwa umuhimu, mafanikio haya yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Serikali na Wizara iliupata kutoka kwa Wadau mbalimbali: vyombo vyá habari na wanahabari, wasanii, wanautamaduni na wanamichezo. Wadau wengine wa

ndani ni pamoja na: Chama cha Maofisa Habari na Mawasiliano Serikali (TAGCO), TFF, SportPesa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, NSSF, TTCL, Kampuni ya Coca-Cola, Multichoice Tanzania LTD, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), StarTimes, na UCSAF.

Kwa upande wa wadau wa nje ni pamoja na UNDP, UNESCO, EU, JICA, Balozi za Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Korea Kusini, Moroko na Ujerumani. Kwa niaba ya Wizara, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana wadau hawa na kuwaomba kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuziendeze Sekta zake za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

146. Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara kwa anuani za: www.habari.go.tz na www.maelezo.go.tz.

147. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe. Hoja imetolewa na imeungwa mkono na tunakushukuru sana kwa uwasilishaji mzuri kabisa, wenye ufasaha na umeweza kuwasilisha kwa wakati tuliojipangia.

Sasa naomba tuelekee kule Msekwa ambako atakuwepo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba, ambaye atasoma hotuba hiyo kutokea kule Msekwa. Mheshimiwa Peter Serukamba, tafadhalii.

MHE. PETER J. SERUKAMBA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nianze kwa kuomba ripoti yetu yote kama ilivyo iingie kwenye *hansard*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuchukua nafasi hii

kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2019/2020, pamoja maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kutoa pole kwako wewe binafsi, familia, Wabunge, Chama cha Mapinduzi, Wananchi wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Watanzania wote kufuatia kifo cha Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude P. Rwakatare Mbunge. Hakika tumepokeza mtu muhimu na atakumbukwa kwa mchango wake kwa Bunge lako, Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Chama cha Mapinduzi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; katika Taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilitoa jumla ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo nane kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa na Wizara na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yetu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa masuala yanayohusu upatikanaji wa fedha bado hayajatekelezwa kikamilifu kama vile Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*) kuwezeshwa kifedha kwa ajili ya kupunguza changamoto inazokabiliana nazo kama za usikivu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 38.28. Kufikia Februari, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 14.46 sawa na asilimia 37.7 tu ya lengo kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja. Kamati inatoa rai Wizara iongeze bidii ili kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 30.87. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 15.48 sawa na asilimia 50.1 na matumizi mengine shilingi bilioni 9.39 sawa na asilimia 30.4. Aidha, bilioni sita sawa na asilimia 19.4 ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati ilielezwa kuwa kufikia Februari, 2020, Wizara ilipokea shilingi bilioni 15.84 sawa na asilimia 51.3 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge hata hivyo hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba mbili.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 27 Machi 2020 Waziri alieleza mipango ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 yenye kujumuisha namna itakavyokusanya maduhuli na namna itakavyotekeleza majukumu yake kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kukusanya makusanyo ya maduhuli ya shilingi bilioni 41.1. Kati ya makadirio hayo shilingi milioni 709.99 sawa na asilimia 1.73 zinakadirwa kukusanywa kutoka katika Idara ya Maendeleo ya Michezo; Shilingi milioni 250 sawa na asilimia 0.61, kutoka Idara ya Habari Maelezo; shilingi milioni 40.1 sawa na asilimia 67 yakusanywe katika Taasisi saba zilizo chini ya Wizara kama ilivyoonekana kwenye kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 96 inakadirwa kutumia shilingi bilioni 40.14. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 20.97 sawa na asilimia 52.3 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 11.44 sawa na asilimia 28.5 kwa ajili ya matumizi mengine; na shilingi bilioni 7.71 sawa na asilimia 19.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba nne.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa bajeti ya Wizara ya mwaka 2020/2021, kwa ujumla imeongezeka kwa asilimia 9.26, sawa na ongezeko la asilimia 29.99 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni, Ushauri na Mapendeleko ya Kamati; baada ya uchambuzi huo wa Kamati, naomba kutoa maoni, ushauri na mapendeleko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ilivyobainishwa kwenye uchambuzi wa Kamati bajeti kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara 2019/2020, ilikuwa hajitatoka hadi Kamati inakutana na taarifa hii. Fedha hizo ambazo ni asilimia 83.3 ni fedha za mradi za usikivu wa *TBC*, ni muhimu sana ikizingatiwa changamoto ambazo *TBC* inakumbana nazo. Kamati inashauri fedha hizo zitoke kabla ya mwaka 2019/2020 kuisha ili kusaidia *TBC* kutekeleza malengo ambayo wamejiwekea.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji *TBC*; changamoto kubwa ya *TBC* ni usikivu katika maeneo mengi. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na *TBC* bado maeneo mengi hayapati mawasiliano ya *TBC*. Kamati inatambua kuwa haki ya kupata habari ni haki ya kila mwananchi, hivyo kukosa habari sio sawa, kama mfanyakishara ambaye pia aliwahi kuwa Mtendaji Mkuu wa 21st *Century Fox*, James Murdoch alivyowahi kusema:

"Information is the most valuable commodity in the world today and this business is about giving people access to information that is relevant to their lives".

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa topografia ya nchi milima na mabonde imekuwa ni kikwazo kwa mitambo ya *TBC* kuweza kuwafikia wananchi wa maeneo mengi. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri *TBC* kununua

mitambo ya kisasa ambayo itakuwa ina uwezo wa kuwafikia wananchi wengi bila ya kujali topografia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Kamati inarudia ushauri ililoutoa mwaka 2019/2020, kuhusu kupungua kwa mapato ya *TSN*/kunakotokana na mauzo duni ya magazeti yake kama vile *Daily News*. Pamoja na hilo, Kamati imebaini kuwa Serikali na Taasisi zake pia zinadaiwa fedha nyingi na *TSN*. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali na Taasisi zake kuhakikisha zinalipa madeni yake kwa wakati; na

(b) *TSN* iwezeshwe kifedha ili kuweza kununua mtambo wa kisasa na kuuweka Mkoani Dodoma ili kuongeza nguvu ya usambazaji wa magazeti nchini ili kusaidia pia kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (*TaSuBa*); Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga Shilingi Milioni 250 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Taasisi. Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti ya *TaSuBa* ili isaidie kufanya yafuatayo:-

(a) Kukarabati miundombinu yake ambayo ipo kwenye hatari ya kuharibika zaidi kutokana na Mawimbi ya Bahari na hivyo eneo la Taasisi kuendelea kuliwa na maji siku hadi siku; na

(b) Kununua Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Michezo; msingi bora wa michezo pamoja na mambo mengine unategemea pia uwepo wa viwanja bora vya michezo. Bado hali ya viwanja vyetu nchini siyo ya kuridhisha kutokana na vingi ya viwanja hivyo kuwa chini ya kiwango. Kamati inatambua kuwa ujenzi wa viwanja hivi ni gharama sana na hivyo inaona kuna haja ya kushirikisha Sekta Binafsi ili isaidie ujenzi wa viwanja hivyo vyenye hadhi ya Kimataifa katika kila mkoa kama ilivyofanya kiwanja cha Kidongo Chekundu pale *JK Park* Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA); Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya BAKITA ili iweze kujiardaa katika kutoa huduma mbalimbali kama ukalimani, tafsiri mbalimbali, ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za *SADC* pamoja na uandaaji wa mitaala ya kufundisha na kujifunza, baada ya kuamuliwa Kiswahili kutumika katika nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kwa mara nyingine napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa hii ya Kamati pamoja nawe napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu. Ni ukweli ulio wazi kuwa mmefanya kazi nzuri ya kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kushiriki vyema katika shughuli zote za Kamati ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii ambayo orodha yao inaonekana kwenye taarifa mliyopewa.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe; Naibu Waziri, Mheshimiwa Juliana D. Sonza; Katibu Mkuu. Dkt. Hassan Abbasi; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ally Possi; pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu, Ndugu Gerald Magili na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho ila siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Nyamwanja C. Chilemeji kwa kuratibu shughuli zote za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Fungu Na. 96 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja jumla ya shilingi 40,140,641,000.00

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza.

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kutoa pole kwako wewe Binafsi Mhe. Spika, Familia, Wabunge, Chama cha Mapinduzi, Wananchi wa Mkoa wa Morogoro pamoja na Watanzania wote kufuatia kifo cha Mhe. Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare (Mb). Hakika tumepoteza Mtu muhimu na atakumbukwa kwa mchango wake kwa Bunge Iako, Kamati yetu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Chama cha Mapinduzi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Bajeti ya Wizara hii. (Kanuni ya 6(5) (b) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016).

1.1 MUUNDO WA TAARIFA

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Kamati imejikita katika kueleza mambo yafuatayo:-

- i) Hali ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- iv) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- v) Hitimisho

SEHEMU YA PILI

**2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO
WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA
MWAKA WA FEDHA 2019/2010**

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 27 Machi 2020, Kamati ilifanya uchambuzi wa namna Wizara ilivyotekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 (Ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na za kutekeleza Miradi ya Maendeleo) kama ifuatavyo:-

2.1 *Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati*

Mheshimiwa Spika, Katika Taarifa yake kuhusu Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilitoa jumla ya Maoni, Ushauri na Mapendekezo **8** kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Wizara. Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa na Wizara na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa masuala yanayohusu upatikanaji wa fedha bado hayajatekelezwa kikamilifu kama vile Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kuwezeshwa kifedha kwa ajili ya kupunguza changamoto inazokabiliana nazo kama za usikivu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, TBC iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi Bilioni 5** kwa lengo la kuboresha Usikivu. Kamati ilijulishwa kuwa hadi wakati wa kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 27 Machi 2020 fedha hiyo ilikuwa haijaenda. Kamati itaendelea kusisitiza kwenye Taarifa hii umuhimu wa Serikali kuhakikisha inapelekea fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utendaji bora wa Wizara na Taasisi zake.

2.2 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 38,284,709,000.00**. Kati ya makadirio hayo ya makusanyo, **Shilingi 709,902,000.00** sawa na **asilimia 1.85** zilikadiriwa kukusanya kutoka kwenye Idara ya Maendeleo ya Michezo, **Shilingi 250,003,000.00** sawa na **asilimia 0.65** kutoka Idara ya Habari – MAELEZO na **Shilingi 37,324,804,000.00** sawa na **asilimia 97.49** kilikadiriwa kukusanya kutoka katika Taasisi saba za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kufikia Februari 2020, Wizara ilikuwa hajafikia hata nusu ya lengo kwani ilikuwa imekusanya **Shilingi 14,460,255,840.00** sawa na **asilimia 37.7 tu** ya lengo. Katika Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa ukusanyaji wa Tasisi siyo wa kuridisha kwani zimekusanya Shilingi **14,460,255,840.00** sawa na asilimia **36.7** ya lengo. (**Kielelezo Na. 1**).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwa makusanyo madogo ya Taasisi yanachangiwa pia na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kwani imekusanya **Shilingi 6,264,219,563.00** sawa na **asilimia 25** ya Makadirio ya kukusanya **Shilingi 24,996,514,000.00**. Kamati illezwa sababu kubwa ya makusanyo madogo ya Kampuni hii ni kutokana na kushuka kwa biashara ya matangazao na mauzo ya nakala za magazeti na kuchelewa kuanza kwa mradi wa uchapaji kibiashara ambao ndiyo ulitegemewa kuwa chanzo kingine cha mapato ya Kampuni. **Kamati inaona kuna haja ya kuboresha Utendaji wa TSN kwani ni miaka mingi sasa ukusanyaji wake wa maduhuli umekuwa siyo wa kuridhisha.**

Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Fungu 96 kwa Mwaka 2019/2020


Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2020 na Usanifu wa Kamati

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara kupitia **Fungu 96** iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **30,879,483,000.00** ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo Mishahara iliidhinishiwa **Shilingi 15,483,073,000.00** sawa na **asilimia 50.1** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 9,396,410,000.00** sawa na **asilimia 30.4**. Aidha, **Shilingi 6,000,000,000.00** sawa na **asilimia 19.4** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa, kufikia Februari 2020, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 15,844,522,823.00** sawa na **asilimia 51.3** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi ya Wizara. Kwa ajili ya Mishahara zimepokelewa **Shilingi 9,490,239,527.00** sawa na **asilimia 61.29** ya fedha iliyoidhinishwa, **Shilingi 6,354,283,296.00** sawa na **asilimia 67.62** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.2**.

Kielelezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020



Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2020 na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali/Wizara ya Fedha, kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii hususan Shilingi Bilioni 5 za TBC ambazo zimetengewa mahsuswi kwa jili ya uboreshaji wa USIKIVU. Changamoto ya usikivu wa TBC ni kubwa nchini na ikumbukwe kuwa TBC ndiyo Shirika la Utangazaji la Taifa. Serikali haina budi kuliwezesha kifedha ili liendane na Majukumu yake.

2.4 MAELEZO KUHUSU MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilipaswa kufanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka 2019/2020/. Katika Mwaka wa Fedha 2019/

2020, Wizara ilitengewa **Shilingi Bilioni 6** kwa ajili ya Miradi miwili ambayo ni pamoja na Mradi wa Upanuzi wa TBC ambao ilitengewa Shilingi **Bilioni 5** na Mradi wa Habari kwa Umma **Shilingi Bilioni 1**.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuweza kufanya ukaguzi wa Miradi hiyo ya Maendeleo kwani hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepokelewa. **Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kutoa fedha za Miradi hii kabla ya mwisho wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili Wizara iweze kutekeleza Miradi hiyo.**

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 27 Machi, 2020. Waziri alieleza Mipango ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 yenye kujumuisha namna itakavyokusanya maduhuli na namna itakavyotekeleza majukumu yake kulingana na Bajeti itakayoidhinsihwa na Bunge kama ifuatavyo:-


3.1 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara inakadiria kufanya makusanyo ya maduhuli ya **Shilingi 41,107,964,000.00**. Kati ya makadirio hayo, **Shilingi 709,997,000.00** sawa na **asilimia 1.73** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika Idara ya Maendeleo ya Michezo, **Shilingi 250,003.000.00** sawa na **asilimia 0.61** kutoka Idara ya Habari Maelezo na **Shilingi 40,147,964,000.00** sawa na **asilimia 97.66** zinakadiriwa kukusanywa kutoka katika Taasisi saba zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Makadirio ya Makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka 2020/2021 yameongezeka kwa **Shilingi 2,823,255,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 7.37** ya Makadirio ya Makusanyo kwa

mwaka 2019/2020. (**Kielelezo Na. 3**). Ogezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa Makadirio ya Taasisi na hususan TBC, BAKITA, BASATA na BMT.

Kielelezo Na.3: Ulinganisho wa Maduhuli kwa Mwaka 2019/2020 na 2020/2021



Chanzo: Randama ya Wizara ya Machi 2020 na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Wizara kwa kuendelea kuongeza Makadirio ya Makusanyo mwaka hadi Mwak. Ni imani ya Kamati kuwa lengo la makusanyo litafikiwa ifikapo mwisho wa Mwaka.

3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021


Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 96 inakadiria kutumia **Shilingi 40,140,641,000.00** kwaajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 20,979,231,000.00** sawa na **asilimia 52.3** ni kwaajili ya Mishahara, **Shilingi 11,446,410,000.0** sawa na **asilimia 28.5** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 7,715,000,000.00** sawa na **asilimia 19.2** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021 kwa ujumla imeongezeka kwa **Shilingi 9,261,158,000.00** sawa na ngezeko la **asilimia 29.99** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2019/2020 ya **Shilingi 30,879,483,000.00**. Ongezeko zaidi (**asilimia 35.5**) linaonekana kwenye Mishahara ikifuatiwa na Miradi ya Maendeleo kwa **asilimia 28.58**. (**Kielelezo Na. 4**). Kamati iliuliza sababu ya kupanda kwa fedha za mishahara na ilielezwa kuwa Wizara inatarajia kuajiri Watumishi wapya 20 lakini pia kuna watumishi 125 watakaopandishwa vyeo na watumishi 4 watabadilishwa kada baada ya kukidhi sifa za Muundo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa Miradi mipyä ikiwemo Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (**Milioni 515**), Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (**Milioni 250**), Ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya (**Milioni 300**) na Ujenzi wa Eneo la Changamani la Michezo Dar es Salaam na Dodoma (**Milioni 650**).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi hiyo mipyä. Kamati ina amini kabisa kuwa fedha hizi zitatoka kwa wakati ili kusaidia kutekeleza Miradi hiyo kama ilivyopangwa.

Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti Mwaka 2019/2020 na 2020/2021



Chanzo: Randama ya Wizaraya Machi 2020 na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi huo wa Kamati, naomba kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

4.1 *Kutopatikana kwa Fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo*

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyobainishwa kwenye uchambuzi wa Kamati, Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa Mwaka 2019/2020 ilikuwa haijatoka hadi Kamati inaandika Taarifa hili. Fedha hizo ambazo **asilimia 83.3** ni fedha za Mradi wa Usikuwa wa TBC ni muhimu sana hasa ikizingatiwa changamoto ambazo TBC inakumbana nazo. **Kamati inashauri Fedha hizo zitokea kabla ya mwaka huu wa Fedha 2019/2020** kuisha ili kusaidia TBC kutekeleza malengo ambayo imejiwekea.

4.2 *Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)*

Mheshimiwa Spika, Changamoto kubwa ya TBC ni usikivu katika Maeneo mengi. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na TBC bado maeneo mengi hayapati mawasiliano ya TBC. Kamati inatambua kuwa Haki ya kupata habari ni haki ya kila mwananchi hivyo kukosa habari siyo sawa kama Mfanyabiashara ambaye pia aliwahi kuwa Mtendaji Mkuu wa 21st Century Fox James Murdoch alivyowahi kusema "***Information is the most valuable commodity in the world today and this business is about giving people access to information that is relevant to their lives***".

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa topografia ya nchi (Milima na Mabonde) imekuwa ni kikwazo kwa Mitambo ya TBC kuweza kuwafikia wananchi wa maeneo mengi. Kutokana na hali hiyo, **Kamati inashauri TBC kununua**

mitambo ya kisasa ambayo itakuwa inauwezo wa kuwafikia wananchi wengi bila ya kujali topografia ya nchi.

4.3 *Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inarudia ushauri ilioutoa mwaka 2019/2020 kuhusu kupungua kwa mapato ya TSN kunakotokana na mauzo duni ya magazeti yake kama vile *Daily News*. Pamoja na hilo, Kamati imebaini kuwa Serikali na Taasisi zake pia zinadaiwa fedha nyingi na TSN. Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Serikali na Taasisi zake kuhakikisha zinalipa madeni yake kwa wakati; na
- b) TSN iwezeshwe kifedha ili kuweza kununua Mtambo wa kisasa na kuuweka Mkoani Dodoma ili kuongeza nguvu ya usambazaji wa magazeti nchini ili kusaidia pia kuongeza mapato.

4.4 *Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TaSuBa)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga **Shilingi Milioni 250** kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Taasisi. Pamoja na pongezi hizo Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti ya TaSuBa ili isaidie kufanya yafuatayo:-

- a) Kukarabati miundombinu yake ambayo ipo kwenye hatari ya kuharibika zaidi kutokana na Mawimbi ya Bahari na hivyo eneo la Taasisi kuendelea kuliwa na maji siku hadi siku; na
- b) Kununua Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.

4.5 *Viwanja vya Michezo*

Mheshimiwa Spika, msingi bora wa michezo pamoja na mambo mengine unategemea pia uwepo wa viwanja bora vya vya michezo. Bado hali ya viwanja vyetu nchini siyo ya kuridhisha kutokana na vingi ya viwanja hivyo kuwa chini ya

kiwango. Kamati inatambua kuwa ujenzi wa viwanja hivi ni gharama sana na hivyo inaona kuna haja ya kushirikisha Sekta Binasi ili isaidie ujenzi wa viwanja hivyo vyenye hadhi ya Kimataifa katika kila Mkoa kama ilivyofanya kwa Kiwanja cha Kidongo Chekundu cha JK PARK – Dar es Salaam.

4.6 Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza bajeti ta BAKITA ili iweze kuijandaa katika kutoa huduma mbalimbali kama ukalimani na tafsiri mbalimbali, Ufundishaji wa Kiswahili katika nchi za SADC, pamoja na uandaaji wa mitaala ya kufundishia na kujifunza baada ya Kiswahili kuamuliwa kuanza kutumika katika nchi za SADC.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa hii ya Kamati. Pamoja nawe napenda kuwashukuru na kuwapongeza Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu. Ni ukweli ulio wazi kuwa mnafanya kazi nzuri ya kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kushiriki vyema katika shughuli zote za Kamati ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:

- | | |
|---|--------|
| 1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb | Mjumbe |
| 2. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | Mjumbe |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Peter Ambroce Lijualikali, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Bernadeta K. Mushashu, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Vicky Paschal Kamata, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Deogratius Francis Ngalaawa, Mb | Mjumbe |

10. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
13. Mhe. John Peter Kadutu, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mgeni Jadi Kadika, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Joseph Leonard Haule, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Maulid Ally Mtulia, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Hawa Abdulrahmani Ghasia, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Namshukuru sana Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb), Naibu Waziri Mhe. Juliana D. Shonza (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Hassan Abbas, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ally Possi pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndgg. Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri bila vikwazo. Napenda pia kumshukuru Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndgg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndgg. Gerald Magili na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuisaidia Kamati wakati wote. Mwisho ila siyo kwa umuhimu nawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndgg. Pamela Pallangyo na Ndgg. Nyamwanja C. Chilemeji kwa kuratibu vyema shughuli zote za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja jumla ya Shilingi **Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja na Arobaini, Laki Sita na Elfu Arobaini na Moja (40,140,641,000.00).**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Peter Joseph Serukamba (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA
NA MAENDELEO YA JAMII**
22 APRILI 2020

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Peter Serukamba. Tunakushukuru sana kwa usomaji wa umakini na utulivu kuhusiana na *reportya* Kamati yenu na tunawapongeza sana Wanakamati wote kwa kuja na taarifa nzuri inayoisaidia Wizara kuweza kufanya kazi vizuri zaidi.

Sasa twende kwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi lakini kabla hujanza nikuongoze tu kidogo. Nitakuomba fungu 16, 17 na 18 hayo tu uyaache, mengine yote unaweza ukaendelea nayo. Tafadhali unaweza ukaendelea, una dakika 20.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, japokuwa hayo uliyoyatao ndiyo mawe lakini naamini nitachangia, kwa hiyo, nitayapiga kwa *style* ya kupitia kule.

Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa nafasi. Pia naomba sasa nisome hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Nami pia sitasoma hotuba yote, kwa hiyo, naomba baadhi ya yatakayobaki yote yaende kwenye Kumbukumbu za *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba nitumie fursa hii kutoa salamu za

rambirambi kwa Shirika la Utangazaji la Taifa – *TBC* kwa kuwapoteza watumishi wake watatu ndani ya kipindi kifupi cha takriban wiki mbili. Taifa litawakumbuka sana Marehemu Marin Hassan Marin, Mtangazaji na mwasisi wa kipindi cha *TBC Aridhio*; Marehemu Joseph Kambanga, Meneja wa TEHAMA wa *TBC*; na Marehemu Lutengano Haonga, Mwandishi Mwandumizi wa *TBC*.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu hao na inamwomba Mwenyezi Mungu aliye chanzo na ukomo wa uhai wa binadamu kuziweka roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni Mkutano wa Mwisho katika Kalenda ya Mikutano ya Bunge ya Miaka Mitano (2015 – 2020), hili itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho vile vile kwa Bunge hili la Kumi na Moja nikiwa kama Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hata hivyo, nina matumaini makubwa ya kurejea tena katika ukumbi huu wa Bunge nikiwa Waziri Kamili mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda kwa miaka yote mitano ya Bunge hili na kunipa nguvu na ujasiri wa kukabiliana na dhoruba nyingi za kisiasa na kijamii zilizonikumba hasa katika kipindi hiki cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, ni katika muktadha wa kumbukumbu hiyo mbaya na katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano ambapo Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na viongozi wengine waandamizi wa CHADEMA walipita njia ile ile niliyopita mimi ya kushtakiwa kwa makosa ya kutumia uhuru wao wa mawazo na kueleza fikra zao; uhuru ambaa ni wa Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapa hongera viongozi wangu wa CHADEMA waliokumbwa na mkasa huo kwa kuvumilia misukosuko na mikiki mningi ya Vyombo vya Dola tangu mwezi Februari, 2018 waliposhitakiwa mpaka walipohukumiwa Gerezani na adhabu ya kulipa faini ya shilingi milioni 320, hukumu iliyotolewa tarehe 10 Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hila ya kuwafunga viongozi wetu kwa kuweka faini kubwa ili washindwe kulipa na hivyo kufungwa Gerezani, wananchi wa Tanzania walipinga na kuishinda hila hiyo. Watanzania walihamua kujinyima na kutoa fedha zao za kujikimu ili wawatoe viongozi wetu Gerezani na *Inshallah*, ndani ya siku tatu fedha taslimu, shilingi milioni 320 zilipatikana na leo viongozi wetu wako huru. Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kwa niaba ya chama changu (CHADEMA), nasema ahsanteni sana Watanzania. Daima kumbukeni kuwa umoja wetu ndio nguvu yetu na huo ndiyo msingi wa falsafa yetu ya nguvu ya Umma (*people's power*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu janga la *Corona* na hatima ya tasnia ya michezo na sanaa; Dunia nzima iko kwenye taharuki kutokana na janga la *Corona*. Athari za moja kwa moja katika afya ya binadamu ziko wazi kutokana na idadi ya vifo inavyoendelea kuongezeka. Katika uchumi hali ni mbaya zaidi kutokana na kufungwa kwa mipaka baina ya nchi mbalimbali, viwanda vingi kusitisha uzalishaji na biashara mbalimbali kusimama.

Mheshimiwa Spika, tasnia ya michezo na sanaa hapa kwetu Tanzania imekuwa mhanga wa kwanza wa athari za kiuchumi kutokana na maambukizi ya *Corona*. Toka kisa cha kwanza na mgonjwa wa *Corona* kiripotiwe hapa nchini, Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu ambavyo ndiyo kitaku cha ukuzaji vya vipaji vya sanaa na michezo vimefungwa. Aidha, michezo na sanaa mbalimbali inayovuta mikusanyiko mikubwa imesitishwa kufuatia tishio la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, athari za kusitishwa kwa shughuli hizi za michezo na sanaa ni kubwa. Mosi, fedha ambazo

zilikuwa zikusanywe kutoka kwenye matamasha mbalimbali ya michezo hazitakusanywa. Hii ina maana kwamba *clubs* zinazohusika na matamasha hayo na michezo zitapoteza mapato makubwa na hivyo kushindwa kujidoresha. Aidha, Serikali itapoteza mapato ya kodi itokanayo na michezo hiyo. Hizi ni athari za sasa hivi, lakini hatujui janga hili litadumu kwa muda gani hapa nchini. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, imejiandaa viperi kibajeti kukabiliana na mtikisiko wa uchumi katika tasnia ya michezo na sanaa ili kuzuia tasnia hizo kuanguka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia janga la *Corona*, Serikali ya Kenya imetoa jumla ya shilingi milioni 100 za Kenya kwa Wasanii wa Filamu na Muziki ili waendelee kuwatumbuiza Wakenya kwenye Televisheni na Redio kwa kipindi hiki ambacho mikusanyiko imekatazwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huu ungekuwa mfano mzuri wa kuigwa na Serikali yetu ili kuwanusuru wasanii na wanamichezo wetu na mkwamo wa uchumi hasa katika kipindi hiki cha *Corona*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya utendaji na ufanisi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita; kama inavyofahamika, Serikali hii ya Awamu ya Tano, inatarajiwa kuondoka madarakani mwezi Oktoba, 2020 baada ya kumaliza muhula wake wa miaka mitano. Pamoja na ukweli huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni vema kufanya tathmini ya utendaji wa Serikali hususani katika Wizara hii ninayoismamia ili Bunge na wananchi kwa ujumla wajue Serikali kuititia Wizara hii imewafanya nini Watanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyokaa madarakani?

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi na tafakuri ya kina, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba miaka mitano ya utendaji wa Serikali kuititia Wizara hii, imeacha *record* mbaya ya uvunjaji wa Katiba, Demokrasia na Haki za Binadamu kuwahi kutokea katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, miaka mitano ya utawala wa Serikali hii ya CCM ya Awamu ya Tano itakumbukwa kama

miaka ya giza nene kwa Watanzania. Hii ni kwa sababu ni katika kipindi hicho Serikali kupitia Wizara hii iliamua kuzima urushwaji wa moja kwa moja wa mijadala ya Bunge (*Bunge Live*) kupitia Televisheni ya Taifa (*TBC1*) na hivyo kuwanyima Watanzania haki yao ya msingi ya kupata habari kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Bungeni ndiko masuala nyeti ya nchi yanakojadiliwa na Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi; hivyo kuwanyima haki ya kujua kinachojadiliwa katika Bunge kwa ukamilifu wake ni sawa sawa kabisa na kuwapoka wananchi hao bila ridhaa yao. Huo ni uhaini dhidi ya mamlaka ya wananchi kwa Serikali, mamlaka ambayo yameainishwa katika Ibara ya 8(1)(a) ya Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni katika kipindi cha utawala wa Serikali hii ambapo Taifa limeshuhudia magazeti yanayoandika habari za kiuchunguzi yakifutiwa usajili na mengine kufungiwa kwa muda usiojulikana kama adhabu ya kuandika ukweli kuhusu makosa yanayofanywa na watendaji wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile ni kipindi cha awamu hii ambapo matumizi ya sheria kandamizi za Makosa ya Kimtandao (*Cyber Crimes Act*.) Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (*Media Services Act*), Sheria ya Takwimu (*Statistics Act*), ambazo kwa pamoja zililenga kuminya uhuru wa kupata na kusambaza habari. Sheria hizi ziliweka masharti magumu na adhabu kali ikiwa ni pamoja na kuafilisi wamiliki binafsi wa vyombo vya habari ikiwa wangepatikana na hatia ya kutoa habari zilizokatazwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba sheria hizi zilipingwa sana nje na ndani ya Tanzania na matumizi yake yalisababisha nchi kama Marekani kuondoa misaada yake kupitia Mradi wa *Millenium Challenge* na misaada mingi ya kibajeti imesitishwa mpaka hapo sheria hizo zitakapofanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, para ya 16, 17 na 18 umezi-*ommit*.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii siyo wa kuridhisha. Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikitumia Wizara hii kama fimbo ya kuudhibiti upinzani hapa nchini kwa kuhakikisha kwamba hakuna uhuru wa mawazo wala wa kupata na kusambaza habari lakini Serikali hiyo hiyo imeshindwa kuipatia Wizara hii fedha za maendeleo ili iweze kutekeleza matakwa yake dhidi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, tukichukulia mwaka wa fedha 2018/2019 mathalani, Wizara hii ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini hadi kufikia Februari, 2019 kiasi kilichopelekwa kilikuwa ni shillingi bilioni 5.2 sawa na asilimia 59 ya fedha illyoidhinishwa. Hii maana yake ni kwamba bajeti hiyo haikutekelezwa kwa asilimia 41 na kwamba asilimia 41 ya miradi au shughuli za kimaendeleo katika Wizara hazikutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huo huo wa fedha, ukirejea randama ya Wizara kwa mwaka huo ukurasa wa 42 utaona kwamba kiasi cha shilingi milioni 150 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Michezo, Malya lakini fedha hizo hazikutumika kufanya ujenzi huo na mpaka leo hakuna majibu fedha hizo zilitumika kufanya nini na kwa idhini ya nani. Matokeo ya matumizi hayo mabaya ya fedha ni kuendelea kusinyaa kwa tasnia ya michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, tofauti na mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ilitekelezwa angalau kwa asilimia 59; hali ni mbaya zaidi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Fedha kwenye Kamati ya Bajeti ya tarehe 30 Machi, 2020, fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa TBC kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni shilingi bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi kufika mwezi Machi, 2020 hakuna fedha yoyote iliyokuwa imetolewa kwa

fungu hili. Majibu ya Serikali kwenye hoja hii ni mepesi na dhaifu sana. Eti Serikali inasema utoaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo uwepo wa bajeti, upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa shughuli zilizopokea fedha za awali na kukamilisha taratibu za manunuzi. Aidha, Serikali inaendelea kusema kuwa kwa upande wa miradi ya ujenzi, ukarabati, mafungu yanapaswa kuwasilisha mikataba ya kazi kwa miradi mipya, hati za madai kwa miradi inayoendelea na vielelezo vya utayari wa kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, majibu hayo yanaashiria kwamba hakuna uongozi (*leadership*) wala uwajibkaji kwenye Wizara hii. Haiwezekani tuko kwenye robo ya tatu ya mzunguko wa bajeti eti Wizara haijatekeleza kigezo hata kimoja katika hivyo wanavyosema ili fedha itoke halafu Katibu Mkuu wa Wizara bado yuko Ofisini. Anafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua kwamba hakuna *seriousness* yoyote katika Wizara hii, maelezo ya Wizara kwenye Kamati ya Bajeti ni kwamba inatarajia kuwa fedha hizo shilingi bilioni tano zitatolewa katika kipindi kilichobaki cha utekelezaji wa bajeti ya 2019/2020 kwa kuzingatia vigezo vilivyoelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikumbuke kwamba imebaki takribani miezi miwili mwaka wa fedha 2019/2020 umalizike. Ni mambo gani yenye thamani ya shilingi bilioni tano itakayoyafanya ndani ya kipindi cha miezi miwili? Kama kwa kipindi cha miezi 10 tangu bajeti iidhinishwe na Bunge, Wizara imeshindwa kutekeleza vile vigezo ilivyosema ni lazima vitekelezwe ndipo fedha itoke: Je, wanawezaje kutekeleza ndani ya miezi miwili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwatendea haki walipakodi wa Tanzania. Kutotekeleza miradi ya maendeleo inayolipiwa na kodi za wananchi kwa maelezo dhaifu kama hayo ni dhihaka kwa walipa kodi. Haiwezekani fedha itengwe, ipitishwe na Bunge halafu Wizara ishindwe kutekeleza halafu inaanza kujitetea

kwamba vigezo havikutimizwa. Kwa nini iliomba fedha hiyo kama ilijua haina uwezo wa kuitumia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa wananchi watambue kuwa hakuna mtu duniani anayependa kuteswa, kunyanyaswa, kudhalilishwa. Njia ngumu na chungu tunayoipitia sisi Wabunge wa Upinzani hatuitamani na pengine tungeweza kumwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na kikombe hicho cha mateso; lakini kufanya hivyo ni kukimbia jukumu alilotukabidhi Mwenyezi Mungu la kuwaongoza watu wake kuelekea kwenye uhuru wa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, hatuna budi kukinywea kikombe hicho cha mateso kwa ajili ya ukombozi wa Watanzania wallotoka katika vifungo mbalimbali vikiwemo uchumi, elimu, ajira, haki za binadamu, uhuru wa mawazo, uhuru wa habari, uhuru wa kukusanyika na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa wananchi kuchangua viongozi ambaao kwa kauli na matendo yao, kwa sera na falsafa zao wanaonekana dhahiri kukerwa na uvunjaji wa wazi wazi wa Katiba na ukandamizaji wa demokrasia na haki za msingi za binadamu uliofanywa na Serikali inayoondoka madarakani ili isirudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHESHIMIWA JOSEPH OSMUND MBILINYI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021- KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge

A. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba nitumie fursa hii, kutoa salamu za rambirambi kwa Shirika la Utangazaji la Taifa – TBC kwa kuwapoteza watumishi wake watatu ndani ya kipindi kifupi cha takriban wiki mbili. Taifa litawakumbuka sana Marehemu Marin Hassan Marin – Mtangazaji na mwasi wa kipindi cha TBC Aridhio; Marehemu Joseph Kambanga – Meneja wa TEHAMA wa TBC na Marehemu Lutengano Haonga Mwandishi Mwandamizi wa TBC. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawapo pole ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu hao na inamwaomba Mwenyezi Mungu aliye chanzo na ukomo wa uhai wa binadamu kuziweka roho za marehemu hao mahali pema peponi, Amina.
- 2. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa huu ni Mkutano wa Mwisho katika Kalenda ya Mikutano ya Bunge ya miaka mitano (2015 – 2020); hii itakuwa ni hotuba yangu ya mwisho vilevile kwa Bunge hili la 11 nikiwa kama Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hata hivyo, nina matumaini makubwa ya kurejea tena katika ukumbi huu wa Bunge nikiwa Waziri Kamili mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2020.
- 3. Mheshimiwa Spika**, Kwa sababu hiyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda kwa miaka yote mitano ya Bunge hili na kunipa nguvu na ujasiri wa kukabiliana na dhoruba nyingi za kisiasa na za kijamii zilizonikumba hasa kipindi hiki cha utawala wa Serikali ya awamu ya tano.
- 4. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa mimi nilikuwa mfungwa katika kipindi hiki; na sababu ya kufungwa eti ni kwa kuwa nilitumia uhuru wangu wa mawazo na kueleza fikra zangu kwenye Mkutano wangu na wananchi – uhuru ambaao ni haki yangu ya msingi kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Nchi yetu.

5. Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa uchungu kwa kuwa kufungwa kwangu kulipelekea kifo cha mama yangu mzazi, ambaye alipata mshtuko baada ya kupata taarifa kuwa mwanaye mpendwa, aliyekuwa chanzo cha furaha yake amefungwa gerezani. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi! Amina.

6. Mheshimiwa Spika, ni katika muktadha wa kumbukumbu hiyo mbaya, na katika kipindi hiki hiki cha Serikali ya awamu ya tano ambapo Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na viongozi wengine waandamizi wa CHADEMA walipita njia ile ile niliyopita mimi ya kushtakiwa kwa makosa ya kutumia uhuru wao wa mawazo na kueleza fikra zao – uhuru ambao upo kikatiba. Napenda kutumia fursa hii kuwapa hongera viongozi wangu wa CHADEMA waliokumbwa na mkasa huo, kwa kuvumilla misukosuko na mikiki mingi ya vyombo vya dola tangu mwezi Februari, 2018 waliposhtakiwa mpaka walipohukumiwa kifungo gerezani au adhabu ya kulipa faini ya shilingi milioni 320 - hukumu iliyotolewa tarehe 10 Machi, 2020.

7. Mheshimiwa Spika, pamoja na hila ya kuwafunga viongozi wetu kwa kuweka faini kubwa ili washindwe kulipa na hivyo kufungwa gerezani, wananchi wa Tanzania waliipinga na kuishinda hila hiyo. Watanzania waliamua kujinyima na kutoa fedha zao za kujikimu ili wawatoe viongozi wetu gerezani na Inshallah, ndani ya siku tatu fedha taslimu, shilingi milioni 320 zilipatikana na leo viongozi wetu wako huru! Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Kwa niaba ya chama changu - CHADEMA; nasema asanteni sana Watanzania! Daima kumbukeni kuwa, "*Umoja Wetu ndio Nguvu Yetu*"na huo ndio msingi wa Falsafa yetu ya '*Nguvu ya Umma*'.

B. JANGA LA CORONA NA HATIMA YA TASNIA ZA MICHEZO NA SANAA

8. Mheshimiwa Spika, dunia nzima iko kwenye tararuki kutokana na janga la Corona. Athari za moja kwa moja katika afya ya binadamu ziko wazi kutokana na idadi ya vifo inavyoendelea kuongezeka. Katika uchumi hali ni mbaya

zaidi kutokana na kufungwa kwa mipaka baina ya nchi mbalimbali, viwanda vingi kusitisha uzalishaji na biashara mbalimbali kusimama.

9. Mheshimiwa Spika, tasnia ya michezo na sanaa hapa kwetu Tanzania imekuwa mhanga wa kwanza wa athari za kiuchumi zitokanazo na maambukizi ya Corona. Toka kisa cha kwanza na mgonjwa wa Corona kiripotiwe hapa nchini shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ambavyo ndio kitalu cha ukuzaji vya vipaji vya sanaa na michezo vimefungwa! Aidha, michezo na sanaa mbalimbali inayovuta mikusanyiko mikubwa imesitishwa kufuatia tishio la Corona.

10. Mheshimiwa Spika, athari za kusitishwa kwa shughuli hizi za michezo na sanaa ni kubwa! Mosi, fedha ambazo zilikuwa zikusanywe kutoka kwenye matamasha mbalimbali ya michezo hazitakusanya. Hii ina maana kwamba klubu zinazohusika na matamasha hayo ya michezo zitapoteza mapato makubwa na hivyo kushindwa kuijendesha. Aidha, Serikali itapoteza mapato ya kodi itokanayo na michezo hiyo. Hizi ni athari za sasa hivil; lakini hatujui janga hili litadumu kwa muda gani hapa nchini. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, imejiandaa vipi Kibajeti kukabiliana na mtikisiko wa uchumi katika tasnia ya michezo na sanaa ili kuzuia tasnia hizo kuanguka?

11. Mheshimiwa Spika, kufuatia janga la Corona, Serikali ya Kenya imetoa jumla ya shilingi milioni 100 za Kenya kwa Wasanii wa Filamu na Muziki ili waendelee kuwatumbuiza Wakenya kwenye Televisheni na Redio kwa kipindi hiki ambacho mikusanyiko imekatazwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huu ungekuwa mfano mzuri wa kuigwa na Serikali yetu ili kuwanusuru wasanii na wanamichezo wetu na mkwamo wa uchumi hasa katika kipindi hiki cha Corona.

C. TATHMINI YA UTENDAJI NA UFANISI WA WIZARA YA HABARI, MICHEZO, UTAMADUNI NA SANAА KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO ILIYOPITA

12. Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, Serikali hii ya awamu ya tano, inatarajiwa kuondoka madarakani mapema mwezi Oktoba 2020, baada ya kumaliza mhula wake wa miaka mitano. Pamoja na ukweli huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni vema kufanya tathmini ya utendaji wa Serikali na hususani katika Wizara hii ninayoismamia, ili Bunge na wananchi kwa ujumla wajue Serikali kuititia Wizara hii imewafanya nini Watanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyokaa madarakani.

13. Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi na tafakuri ya kina, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kwamba miaka mitano ya utendaji wa Serikali kuititia Wizara hii, imeacha rekodi mbaya ya uvunjaji wa Katiba, demokrasia na haki za binadamu kuwahi kutokea katika historia ya nchi yetu.

14. Mheshimiwa Spika, miaka mitano ya utawala wa Serikali hii ya CCM ya awamu ya tano itakumbukwa kama miaka ya giza nene kwa Watanzania! Hii ni kwa sababu ni katika kipindi hicho, Serikali kuititia Wizara hii iliamua kuzima rasmi urushwaji wa moja kwa moja wa mijadala ya Bunge (Bunge Live) kuititia Televisheni ya Taifa (TBC1) na hivyo kuwanyima Watanzania haki yao ya msingi ya kupata habari kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba yetu. Ikumbukwe kwamba Bungeni ndiko masuala nyeti ya nchi yanakojadiliwa na Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi; hivyo kuwanyima haki ya kujua kinachojadiliwa katika Bunge lao kwa ukamilifu wake, ni sawasawa kabisa na kuwapoka nchi yao bila ridhaa yao na huo ni uhaini dhidi ya mamlaka ya wananchi kwa Serikali mamlaka ambayo yameainishwa katika ibara ya 8(1)(a) ya Katiba ya nchi yetu. Aidha, ni katika kipindi cha utawala wa Serikali hii ambapo Taifa limeshuhudia magazeti yanayoandika habari za kiuchunguzi yakifutiwa usajali na mengine kufungiwa kwa muda usiojulikana kama adhabu ya kuandika ukweli kuhusu makosa yanayofanywa na watendaji wa Serikali.

15. Mheshimiwa Spika, vilevile ni kipindi cha awamu hii ambapo matumizi ya sheria kandamizi za Makosa ya Kimtandao (Cyber Crimes Act); Sheria ya Huduma za Vyombo

vya Habari (Media Services Act); Sheria ya Takwimu (Statistics Act) ambazo kwa pamoja zililenga kuminya uhuru wa kupata na kusambaza habari. Sheria hizi ziliweka masharti magumu na adhabu kali ikiwa ni pamoja na kuwafilisi wamiliki binafsi wa vyombo vya habari ikiwa wangepatikana na hatia ya kutoa habari zilizokatazwa. Itakumbukwa kwamba sheria hizi zilipingwa sana nje na ndani ya nchi, na matumizi yake yalisababisha nchi kama Marekani kuondoa misaada yake kuititia Mradi wa Millenium Challenge na misaada mingi ya kibajeti imesitishwa mpaka hapo sheria hizo zitakapofanyiwa marekebisho!

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

19. Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali uminyaji wa uhuru wa habari kwa kiwango cha hali ya juu ambacho hakijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu yapo mambo mengine ambayo Serikali hii imeshindwa kuyatekeleza katika kipindi chote cha miaka mitano iliyokaa madarakani. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kushindwa kutoa Ruzuku kwa Vyama vya Michezo na Wasanii

20. Mheshimiwa Spika, Ni Serikali hii hii ya awamu ya tano ilikataa kuvipatia ruzuku vyama vya michezo ili viweze kujidesha, na hivyo kuweza kuwasaidia wanamichezo wa nchi hii kutimiza ndoto zao katika tasnia ya michezo. Ikumbukwe kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa pendekezo la kuvipatia ruzuku vyama vya michezo na wasanii tangu Mkutano wa Kwanza wa Bajeti wa Bunge la 11 katika mwaka wa fedha 2016/2017.

21. Mheshimiwa Spika, msingi wa pendekezo hilo ultokana na uhalisia kuwa vyama vya michezo vilikosa fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wanamichezo kiasi ambacho ilifikia hatua ya kushindwa kulipa nauli kwa timu zake kwenda kwenye mashindano nje ya nchi na badala yake kulazimika kupeleka watu wawili au watatu ambao ushiriki wao katika mashindano hayo ni kama vile haukuwepo. Lakini mpaka

Serikali hii inamaliza mhula wake, imegoma kutoa ruzuku hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali yetu kujifunza kutoka kwa nchi jirani ya Kenya ambapo Serikali ya Kenya inatoa ruzuku ya hadi shilingi milioni 200 za Kenya kila mwezi kwa vyama nya michezo na wasanii.

22. Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kugoma kutoa ruzuku kwa vyama nya michezo na wasanii ili kuiendeleza tasnia nzima ya michezo na sanaa, Serikali imekuwa na desturi mbaya ya kuwarubuni baadhi ya wasanii hasa wa muziki katika vipindi nya kampeni za uchaguzi; ilhali imegoma kuwasaidia kwa ujumla wao kukuza na kuboresha vipaji vyao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kutoa wito kwa wasanii kukataa kurubuniwa kwa namna hiyo; na badala yake kama chama cha siasa kinataka huduma ya usanii katika kampeni zake; basi kiingie mkataba na vyama nya wasanii na slo msanii mmoja mmoja.

ii. Kushindwa Kurejesha Viwanja nya Michezo nya CCM vilivyopatikana wakati wa Mfumo wa Chama Kimoja kwenye Umiliki wa Umma

23. Mheshimiwa Spika, Serikali hii imekataa kurejesha katika umiliki wa umma viwanja nya michezo nya CCM vilivyopatiakana wakati wa mfumo wa chama kimoja cha siasa. Itakumbukwa kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza viwanja vyote nya michezo vilivyopatikana na kumilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kabla ya mwaka 1992, (siasa ya vyama vingi ilipoanza) virejeshwe Serikalini ili viweze kuendelezwa kwa ajili ya kukuza sekta ya michezo nchini.

24. Mheshimiwa Spika, Msingi wa pendekezo hili ultokana na ukweli kwamba kabla ya 1992 nchi ilikuwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa ambapo wananchi wote walikuwa ni wanachama wa chama hicho hicho na walitoa michango yao ya fedha na nguvukazi katika kununua na kutunza mali za chama. Kwa kutumia utashi mdogo tu ni kwamba mali zote za CCM zilizochumwa wakati wa chama kimoja zinapaswa kuwa mali za umma kwa kuwa zina mchango wa wananchi wote. Lakini kwa zile zilizochumwa

baada ya 1992 ni halali kuwa mali ya CCM. Hadi kufikia muda huu, Serikali imegoma kutekeleza pendekezo hilo.

iii. Kushindwa Kuratibu Ajira katika Sekta ya Michezo

25. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni mara kadhaa ilipendekeza kwamba Serikali iweke utaratibu wa kisheria wa kusimamia ajira za sekta ya michezo ikiwemo mikataba ya wachezaji, maslahi yao na mafao yao. Lengo la pendekezo hilo lilikuwa ni kuhakikisha kuwa wachezaji wote wanaopata nafasi ya kuchezea ngazi za ligi za kitaifa au kimataifa na wanapata malipo ya ajira na mafao kama watumishi wengine wa umma. Serikali hii imekataa kufanya hivyo!

iv. Kushindwa Kuanzisha Shule Maalum za Michezo za Taifa

26. Mheshimiwa Spika, Serikali hii imeshindwa kuanzisha Shule Maalum za Michezo za Taifa kwa ajili ya kuibua na kukuza vipaji katika Sekta ya Michezo licha ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kushauri na kupendekeza hivyo. Itakumbukwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kwa Serikali; kuanzisha au kuteua shule moja ya msingi na moja ya sekondari katika kila Mkoa na kuzifanya kuwa shule maalumu za michezo za Taifa (National Sports Academies).

27. Mheshimiwa Spika, Mantiki ya pendekezo hili ilikuwa ni kwamba watoto ambao wangejiunga na shule hizi wangefundishwa elimu ya kawaida sawa na wenzao wa shule nyiningine isipokuwa wangewekewa mkazo zaidi kwenye michezo mbalimbali. Mpaka Serikali hii inamaliza mhula wake wa uongozi jambo hilo halijafanyika!

v. Kushindwa Kuratibu Uanzishwaji wa Umoja wa Wasanii Nchini

28. Mheshimiwa Spika, Serikali hii imeshindwa kuratibu uanzishwaji wa umoja wa wasanii kwa lengo la kukuza tasnia ya usanii hapa nchini. Itakumbukwa kwamba Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni ilipendekeza uanzishwe umoja wa wasanii nchini; ili waungane na kuwa na sauti moja yenye nguvu kudai haki na maslahi yao. Msingi wa pendekezo hili ulitokana na tabia na njama za Serikali hii ya CCM ya kuwagawa wasanii ili wawatumie vizuri kwa maslahi ya kisiasa.

29. Mheshimiwa Spika, wakati Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa pendekezo hili, ilieleza kwamba kitendo cha Waziri wa Wizara hii na Rais kuwaita wasanii fulani fulani na kufanya nao mazungumzo na kuwabagua wasanii wengine, kunawagawa wasanii na kunajenga matabaka mionganoni mwao. Kundi la wasanii walioonana na Rais au Waziri wanajiona kuwa '*superior*' kuliko wengine. Tulieleza kwamba hali kama hiyo haina afya hata kidogo katika ukuaji wa tasnia ya usanii. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni illitoa rai kwa wasanii kujunga na vyama kulingana na aina ya usanii wanaofanya ili kama kuna jambo ambalo Serikali inataka kuwashirikisha wasanii basi iwaalike wawakilishi wa vyama hivyo kuliko kukutana na msanii mmoja mmoja au baadhi yao.

30. Mheshimiwa Spika, sambamba na uanzishwaji wa Umoja wa Wasanii; tulipendekeza pia kwamba Serikali iweke utaratibu wa kisheria ili kabla msanii hajasajiliwa na BASATA kama sheria inavyotaka, basi msanii huyo awe mwanachama hai wa vyama vya wasanii kama vile vyama vya muziki mfano TUMA, CHAMUDATA, Chama cha Taarabu na hata Chama cha Muziki wa Injili ambavyo vipo ila vinalegalega.

31. Mheshimiwa Spika, ninasikitika kusema kwamba Serikali hii inaondoka madarakani ikiwa haijatekeleza ushauri huo.

vi. Kushindwa Kulinda Soko la Bidhaa za Wasanii wa Ndani

32. Mheshimiwa Spika, Serikali hii inamaliza mhula wake wa kuwa madarakani ikiwa imeshindwa kuweka utaratibu wa kisheria wa kulinda soko la bidhaa za wasanii wa ndani. Itakumbukwa kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kwa Serikali kuweka utaratibu wa kisheria

utakaowezesha vituo vyote vya redio na televisheni nchini kupiga asilimia 80 ya muziki wa wasanii wa nyumbani ili kulinda sanaa zetu na kukuza soko la bidhaa za wasanii wa ndani. Tulieleza kuwa nchi nyingi duniani zina sheria za kuwalinda wasanii wao wa ndani hivyo inabidi nasi kwenda na kasi ya dunia. Hata hivyo, Serikali hii haijaona mantiki ya kuwalinda wasanii wake kiuchumi.

D. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAENDELEO KATIKA WIZARA

33. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii si wa kuridhisha! Pamoja na kwamba Serikali imekuwa ikitumia Wizara hii kama fimbo ya kuudhibiti upinzani hapa nchini kwa kuhakikisha kwamba hakuna uhuru wa mawazo wala wa kupata na kusambaza habari; lakini Serikali hiyo hiyo imeshindwa kuipatia Wizara hii fedha za maendeleo ili iweze kutekeleza matakwa yake dhidi ya upinzani.

34. Mheshimiwa Spika, tukichukulia mwaka wa fedha 2018/2019 mathalani; Wizara hii ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini hadi kufikia Februari, 2019 kiasi kilichopelekwa ni shilingi bilioni 5.2 sawa na asilimia 59 ya fedha iliyoidhinishwa. Hii maana yake ni kwamba bajeti hiyo haikutekelezwa kwa asilimia 41 na kwamba asilimia 41 ya miradi au shughuli za kimaendeleo katika Wizara hazikutekelezwa kabisa!

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka huo huo wa fedha, ukirejea Randama ya Wizara kwa mwaka huo (uk.42) utaona kwamba kiasi cha shilingi milioni 150 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya; lakini fedha hizo hazikutumika kufanya ujenzi huo na mpaka leo hakuna majibu fedha hizo zilitumika kufanya nini na kwa idhini ya nani. Matokeo ya matumizi hayo mabaya ya fedha ni kuendelea kusinyaa kwa tasnia ya michezo nchini.

36. Mheshimiwa Spika, tofauti na mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ilitekelezwa angalau kwa asilimia 59; hali ni mbaya zaidi kwa mwaka wa

fedha 2019/2020. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Fedha kwenye Kamati ya Bajeti ya tarehe 30 Machi, 2020; fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa TBC kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni shilingi bilioni 5. Hata hivyo, hadi kufikika mwezi Machi, 2020 hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyokuwa imetolewa kwa fungu hili. Majibu ya Serikali kwenye hoja hii ni mepesi na dhaifu sana! Eti Serikali inasema utoaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo; uwepo wa bajeti, upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa shughuli zilizopokea fedha awali na kukamilisha taratibu za manunuzi. Aidha, Serikali inaendelea kusema kuwa kwa upande wa miradi ya ujenzi/ukarabati, mafungu yanapaswa kuwasilisha mikataba ya kazi kwa miradi mipya, hati za madai kwa miradi inayoendelea na vielelezo vya utayari wa kutekeleza miradi.

37. Mheshimiwa Spika, majibu hayo yanaashiria kwamba hakuna uongozi (leadership) wala uwajibikaji kwenye Wizara hii. Haiwezekani tuko kwenye robo ya tatu ya mzunguko wa bajeti eti Wizara hajatekeleza kigezo hata kimoja katika hivyo wanavyosema ili fedha itoke; halafu Katibu Mkuu wa Wizara bado yuko ofisini! Anafanya nini?

38. Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua kwamba hakuna seriousness yoyote katika Wizara hii; maelezo ya Wizara kwenye Kamati ya Bajeti ni kwamba inatarajia kuwa fedha hizo shilingi bilioni 5 zitatolewa katika kipindi kilichobaki cha utekelezaji wa bajeti ya 2019/2020 kwa kuzingatia vigezo vilivyoolezwa. Serikali ikumbuke kwamba imebaki takriban miezi miili mwaka wa fedha 2019/2020 umalizike! Ni mambo gani yenye thamani ya shilingi bilioni 5 itakayoyafanya ndani ya kipindi cha miezi miili? Na kama kwa kipindi cha miezi kumi tangu bajeti iidhinishwe na Bunge, Wizara imeshindwa kutekeleza vile vigezo inavyosema ni lazima vitekelezwe ndipo fedha itoke, je, wanaweza kuvitekeleza ndani ya miezi miili?

39. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwatendea haki walipa kodi wa Tanzania!

kutotekeleza miradi ya maendeleo inayolipiwa na kodi za wananchi kwa maelezo dhaifu kama hayo ni dhihaka kwa walipa kodi. Haiwezekani fedha itengwe, ipitishwe na Bunge halafu Wizara ishindwe kutekeleza halafu inaanza kujitetea kwamba vigezo havikutimizwa! Kwa nini iliomba fedha hiyo kama inajua haina uwezo wa kuitumia?

E. HITIMISHO

40. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa wananchi watambue kuwa hakuna mtu duniani anayependa kuteswa, kunyanyaswa au kudhalilishwa! Njia ngumu na chungu tunayoipitia sisi Wabunge wa Upinzani hatuitamani na pengine tungeweza kumwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na kikombe hicho cha mateso. Lakini kufanya hivyo, ni kukimbia jukumu allotukabidhi Mwenyezi Mungu la kuwaongoza watu wake kuelekea kwenye uhuru wa kweli. Kwa sababu hiyo, hatuna budi kukinywa kikombe hicho cha mateso kwa ajili ya ukombozi wa Watanzania walio kutoka katika vifungo mbalimbali vikiwemo vya uchumi, elimu, ajira, haki za binadamu, uhuru wa mawazo, uhuru wa habari, uhuru wa kukusanyika na kadhalika.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

42. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Joseph Osmund Mbilinyi (Mb)
**WAZIRI KIVULI NA MSEMADI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KATIKA WIZARA YA
HABARI, MICHEZO, UTAMADUNI NA SANAA**

22 Aprili, 2020

SPIKA: Baada ya hotuba hiyo, sasa ni wachangiaji. Tutaanza na Mwanahabari mbobevu, Mheshimiwa Amina Saleh Mollel atakuwa mchangiaji wa kwanza, halafu tutahamia kule Msekwa ambapo Mheshimiwa Mwamoto na

Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa watachangia kutokea huko.

Mheshimiwa Amina Mollel una dakika 10.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na kusimama mbele yako.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe kwa jitihada mnazozichukua kwa ajili ya usalama wetu katika Bunge hili na viongozi wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pole kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) kwa msiba mkubwa waliopata. Vilevile niwatie moyo wafanyakazi wa Shirika la Utangazaji Tanzania kwa yote yale yaliyotokea. Kipekee kabisa nampongeze Ayoub Rioba ambaye ni Mkurugenzi wa *TBC* kwa jinsi ambavyo ameonyesha moyo wa upendo na amekuwa kama Baba kwa wafanyakazi ambao kwa kweli walipata hofu kubwa kutokana na janga liliowapata.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na vilevile Makatibu Wakuu wote, Dkt. Abbasi ambaye ni *classmate* wangu katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini na vilevile Naibu wake na Watumishi wote wa Wizara ya Habari.

Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Serikali hasa katika kuliboresha Shirika la Utangazaji Tanzania. Hiki ndicho chombo cha Serikali na tunafahamu; na kwa mimi ambaye nimepitia kwenye *media* hata nchi inapovamiwa, wengi wao wanakimbilia kwenye chombo cha Taifa. *TBC* hongereni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumeona jinsi ambavyo hivi sasa kunafanya mabadiliko makubwa katika Shirika hili la Utangazaji *TBC* na vilevile, tumeona mabadiliko haya ambayo kwa kweli mbali ya ubunifu wenye aliopo ndani ya shirika hili la kipekee kabisa kwa Marin Hassan Marin

ambaye daima tutamkumbuka kupitia kipindi cha Aridhio kwa kweli haya mabadiliko ndiyo tunayoyataka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari nimepitia kwa ufupi katika bajeti yake hii kwa kweli napongeza kwasababu naona kabisa kuna fedha zinakwenda kuongezwa na hii itasaidia kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika Wizara ya Habari. Kwa huyu ambaye namfahamu pia Dkt. Abbas ninaamini kabisa weledi wake atakwenda kumshauri vizuri Waziri na weledi alionao Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa pamoja na Naibu wao utasaidia kwa kiasi kikubwa kututoa hapa tulipo na kwenda tunapotaka. Nimeona kwamba kumeongezwa bilioni tatu lakini vilevile mishahara kwa ajili ya *TSN* ambayo ni 4.8 ambayo itakuwa jumla ya shilingi bilioni saba, haya kwa kweli ni jitihada kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kwamba katika nchi yetu ya Tanzania na niseme kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka. Hata nyumba popote pale uhuru upo lakini hakuna uhuru usiokuwa na mipaka. Tumeona ndani ya miaka mitano pamoja na kwamba Kambi ya Upinzani wanasema wao wataikumbuka kwa mabaya lakini sisi ndani ya Awamu hii ya Tano tutakumbuka kwa mengi yaliyofanyika kupitia Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambayo tangu tumepata uhuru haya ni mabadiliko makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndani pia ya vyombo vyahabari tumeona kwamba katika sheria ambayo tuliletu hapa na tukaipitisha sheria ile, itakwenda kusaidia pia waandishi wa habari. Kwasababu waandishi wa habari watakaoajiriwa na vyombo vyahabari hapa nchini watawalipa ipasavyo kulingana na miongozo iliyopo kupitia sheria hiyo ambayo ilipitishwa ndani ya bunge hili.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba wengi wetu wanasema katika nchi hii uhuru wa vyombo vyahabari hakuna na kwamba wana taaluma wengi wamekuwa wakinyanyaswa. Mwanataaluma yejote anayezingatia weledi na maadili ya kazi wote wamekuwa mahali salama

wakifanya kazi. Endapo unakiuka uhuru ambaao utakiuka mpaka na mipaka hiyo ni dhahiri kabisa wewe utakwenda kuvunja sheria zilizopo ambazo kwa namna moja au nyingine sheria hizo zimewekwa kwa ajili ya wananchi na zimewekwa kwa ajili pia ya wanahabari wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tumeona uhuru uliopo hivi sasa ambapo hata watu wamekuwa wakitumia mitandao na kwenda mbali zaidi, lakini nilijaribu kupitia kwa kuangalia kwamba; Je, katika nchi nyingine mambo yakoje na hasa katika uhuru ambaao hivi sasa tunaona kwamba katika Televisheni mbalimbali tumekuwa pia na *online tv* ambazo zimekuwa zikifanya kazi nzuri na nipongeze kwa kweli wizara, kwasababu hivi sasa habari tunazipata kupitia kwenye simu zetu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu Tanzania ina jumla ya Televisheni 44, Radio 186, magazeti 233, *online Tv* 264, idadi ambayo ni kubwa sana kuliko nchi nyingine za Afrika na hata kuzidi baadhi ya nchi duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika miaka mitano kazi au nyimbo mbalimbali zimehaririwa na BASATA, lakini vilevile vibali vimekuwa vikitolewa kwa wasanii mbaalimbali na kufanya kazi. Tumeona kupitia pia sheria hizo hizo kwa wale ambaao wamekiuka maadili tumeona kwamba sheria hizo zimefanya kazi. Niendelee kwa kusema kwamba, zipo sababu ambazo wanasema kwamba nchi yetu ina ukomo wake kutokana na hasa na mambo ambayo yamekuwa yakikiukwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia katika mojawapo ya habari inasema kwamba wadau wengine kwasababu ya uhuru wa habari wa kujieleza kwamba kwanini una ukomo. Kwa mujibu wa makala iliyoitwa *here are the one sixty four songs that were burned from American Radio after September 11th*. Radio mbaalimbali nchini Marekani kwa kwa maelekezo ya wasimamizi wa sheria na uamuzi wao zilipigwa marufuku kucheza nyimbo mbaalimbali zinazoelezea ugaidi

au kupotosha kuhusu tukio la kigaidi la *September, 11th.*
(Makofî)

Mheshimiwa Spika, makala nyingine ambayo inasema *15 movies that were burned in the USA*, makala hii inaeleza kwamba historia ya filamu Marekani na kutaja filamu maarufu 15 ambazo ziliwahi kupigwa marufuku nchini humu kwasababu mbalimbali ikiwemo uchochezi wa ubaguzi wa jamii za wazungu na weusi au kukiuka misingi ya usalama wa Taifa na maadili ya umma. Kwa hiyo, ni kwamba wale ambao wamekuwa wakikiuka...

SPIKA: Mheshimiwa Amina malizia sentensi moja.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, wale ambao wamekuwa wakikiuka sheria imefanya kazi na sheria hiyo tulipitisha hapa, na wale ambao wamekuwa wakienda vizuri kazi zao zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga hoja mkono lakini vilevile niseme tu kwamba ninaomba kwa wizara waweze kukaa na *RITA* walimalize suala hilo kwa sababu *RITA* ana mchango mkubwa sana kwenye jamii.
(Makofî)

SPIKA: Ahsante sana sana Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mtangazaji Mwandamizi kwa mchango wako na kutuanzishia mjadala wa jioni ya leo. Mheshimiwa Venance Mwamoto nilishakutaja na Mheshimiwa Jasmine Tisekwa Bunga atafuatia wote wako Msekwa, Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kuchukuwa nafasi hii nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili kuongea jioni ya leo kwenye Wizara hii ya Habari Michezo Utamaduni na Sanaa. Kwanza nianze kutoa pole kwa familia na Wabunge wote kwa Mheshimiwa Marehemu Dkt. Getrude mchungaji mwenzangu Rwakatare, kwa yaliyomkuta pole sana na watanzania wataendelea kumlilia kwa busara zake na pia nitoe pole

nyingi kwa wafanyakazi wa *TBC* ambao pia nao wametutoka kwa muda tofauti mwenyezi Mungu yupo pamoja nao.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kukushukuru wewe na kukupongeza kwa jinsi ambavyo umekuwa ukitulinda sisi wabunge wako hasa wana michezo na kutupelekea kushiriki kwenye michezo kule Uganda na sehemu nyingine kwa kweli umetangaza vizuri Bunge letu, kupitia michezo na sisi kama wabunge hatukukuangusha.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli nimpongeze sana Naibu Spika kwa jinsi ambavyo alikuwa akishiriki na kutuletea medali nyingi Mungu ambariki sana na nafikiri hata mzungumzaji wa upande wa upinzani Mbunge Waziri Kivuli amesikia na anaelewa hilo nilishangaa kumpongeze, nimpongeze pia papa Ngeleja Mwenyekiti wetu wa kamati ya michezo ya Bunge amekuwa ni mtu ambaye kiunganishi kizuri kati yetu sisi na wewe Spika.

Mheshimiwa Spika, lakini nichukuwe nafasi hii niwapongeze sana sana wanamichezo wote wa bunge letu la Tanzania pamoja na kazi kubwa walioifanya kule Uganda miaka mingine ya nyuma wamefanya kazi nzuri niseme hatujakuangusha bahati nzuri nilikuwa kocha wa mpira wa miguu tulifanya vizuri nategemea tutakapo rudi mwakanani Inshallah tukiongozwa na wewe basi tutafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwanza nichukuwe nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Habari kaka yangu Mheshimiwa Mwakyembe kwa kweli hotuba yako ya leo imenifanya nisiwe mchangiaji wa sana kwa ukali bali niwe mshauri tena kutohana na nafasi yangu ya kuwa mchungaji mtarajiwu nitowe zaidi ushauri badala ya kukemea zaidi na mengi ambayo nilikuwa nategemea marekebisho yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wizara yako Mheshimiwa wewe na Naibu wako mmejitahidi sana kufanya kazi na wizara kubwa ambayo kwa kweli ukiangalia tu utamaduni iko kwa upana, ukiangalia sanaa iko kwa upana habari kwa upana

michezo ni wizara karibu nne katika wizara moja lakini wewe umejitahidi na tukichukulia kwamba wizara hii bajeti yake miaka yote imekuwa ndogo imekuwa tegemezi zaidi, kwa hiyo niseme umejitahidi. Nikupongeze tu kwa lile ambalo umelisema kwamba umeunga mkono Mheshimiwa Rais kwamba nchi yetu ni nchi ya viwanda na kiwanda kimoja wapo ni michezo sasa kitu ambacho tunajidanganya ni kwamba sisi tunaagiza malighafi kutoka nje tunauwa viwanda vyetu kwa maana idadi ya wachezaji waliokuwa wanatoka nje ni wengi mno timu moja inakuwa na wachezaji zaidi ya kumi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, sasa si rahisi ukawa na timu nzuri ya Taifa kwa hiyo, si mbaya nitoe tu mawazo yangu kwamba kama utakapokaa nao umesema utakaa nao ili wapunguze idadi ya wachezaji kutoka nje wanaweza kuwa na wachezaji wengi lakini watakao ruhusiwa kwenye kucheza kwenye mechii moja wasizidi wanne ili na wachezaji wetu nao wapate nafasi ya kucheza. Kwasababu kilichokuwa kinatokea sasa tulikuwa tunaendelea kuuwa wachezaji wetu na matokeo yake kama vile ambavyo iko wenzetu wa uingereza, ligi yao ni nzuri lakini timu yao Taifa si nzuri kwa sababu wachezaji wengi ni wakigeni kwa hiyo nikupongeze sana Mheshimiwa kwa hiyo nafasi.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze watu wa TFF, ndugu yangu Rais wetu wa TFF pamoja na Katibu wake Kidau wamejitahidi sana kitu ambacho nataka niwashauri bado hawajatushirikisha wabunge wanamichezo kwa sababu nilitegemea hata siku moja tu wangeweza kufika wakaongea wakamuona mwenyekiti wetu papa Ngeleja wakaomba wakaongea na wanamichezo na sisi tungeweza kuwapa maoni.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri mmeona Mheshimiwa Rais alichokifanya baada ya kukutana na watu wa madini alipata mambo mengi ambayo mpaka leo yanaisaidia nchi na ninyi pia mngeweza kupata mambo mengi badala ya kukaa tu wenyewe lakini pia ilikuwa nafasi yenu ya ninyi kukutana na sisi ili kuona kiasi gani tusaidie

kuongeza michezo. Sasa niwaombe tu bado mnanafasi kutaneni na wanamichezo siyo wabunge hata ikiwezekana mzunguke nchi nzima, mzunguke nao watoe mawazo mbalimbali kwasababu hii michezo ni ajira na watu ambao wako kwenye ajira hiyo ni vijana ambao ni wengi kwa kweli tusiogope kukutana nao kwa sababu tukiogopa hatutawatendea haki.

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiangalia hatuna tena riadha, hatuna ngumi hatuna mpira wenyewe ndiyo hiyo tena na michezo mingine imekwenda wapi tuijulize kwa hiyo, tukae pamoja bila gharama yoyote tumetoka wapi? Tuko wapi? Na tuna kwenda wapi? Kwa ajili ya nchi yetu sisi wote tutaondoka lakini tuache kitu ambacho tutaacha miguu yetu *step* zetu watu wakaziona kwamba tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, ukienda mbele zaidi kuna jambo ambalo inhabidi tulizungumze kwa kina, jambo ambalo la uendelezaji wa michezo tulikuwa na michezo Mheshimiwa amesema pale kulikuwa kuna michezo ya *UMISHUTA*, kuna michezo ya *UMISETA*, kuna *SHIMIWI*, na michezo mingine lakini ningeshauri tu kwamba tufufue *Taifa cup*, *Taifa cup* inashirikisha wachezaji wale ambao hawana nafasi za kucheza kwenye hizo sehemu nyingine na nafikiri nina dakika tano bado.

Mheshimiwa Spika, corona, niseme corona lazima tuliseme siku zote na maneno matakatifu ukisoma zaburi ya 62:9 yanasema hivi enyi watu mtumaini siku zote ifunueni mioyo yenu mbele zake Mungu ndiyo kimbilio letu, kwa hiyo, msiogope pamoja na masharti yale ambayo tunatakiwa tunawe tufanye nini lakini tusimsahau Mungu na ndiyo maana leo Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko kule kwenye maombi tuendelee kuionbea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho niseme tu Serikali itakayoondoka kwa mujibu wa katiba ya mwezi wa kumi itaondoka kweli, lakini itarudi siku hiyo hiyo na kuendelea kuongoza nchi hii, kwa hiyo niwaombe tu ndugu zangu tusikatishwe moja na maneno ambayo yakuondoa Serikali

yetu, Serikali yetu ni mahiri mambo yamefanyika tuko kifua mbele, ningemuomba tu ndugu kwamba ajachelewa aombe usajili bado upo wazi na kocha yupo anahitaji wachezaji aende tumuone kama anafaa tutamsajili na kumpa nafasi baada ya kusema hayo kwa kweli naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Venance Mwamoto, ye ye mwenyewe amesema ni mchungaji mpya tunakupongeza sana kwa kada hiyo tunasubiri siku ambayo nayo Mheshimiwa Joseph Mbilinyi atakuwa mchungaji na ye ye maana naona anaelekea elekea huko nadhani siku si nydingi. (*Kicheko*)

Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga na atafuatiwa huko huko Msekwa na Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika wizara hii muhimu na nyeti katika maendeleo yetu ya watanzania. Kabla sijatoa mchango wangu napenda niungane nawe pamoja na Waheshimiwa wote kama mwana Morogoro Mbunge wa Viti Maalum kwa kifo cha Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Rwakatare Mwenyezi Mungu amrehemu, ampumzishe kwa amani tumepokea kwa mshtuko sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kutoa pole sana kwa wenzetu wa Shirika la Utangazaji *TBC* kwa misiba iliyotokea mfululizo ya watangazaji wetu mahiri, Mwenyezi Mungu pia awarehemu pamoja na marehemu wote ambao wametangulia mbele za haki hasa katika janga hili ambalo linatupata sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, hii ni Wizara ya Utamaduni, Habari na Michezo, napenda nijikite zaidi katika kipengele cha utamaduni ambacho kipengele hiki ndiyo kinalinda, kinahifadhi na kuendeleza mila na desturi za Taifa letu. Kwanza kabisa napenda nitoe pongezi za dhati kabisa kwa

Mheshimiwa Rais kwa hatua aliyoichukua ya kuiweka nchi yetu ya Tanzania kwa siku tatu mfululizo katika maombi ya kuombea Taifa letu hili katika janga hili la ungonjwa. Nilikuwa napitia baadhi ya mitandao ya kijamii wakisema kwamba, baadhi wanasema hii siyo *spiritual thing* ni *scientific thing* huu ugonjwa. Lakini ninavyofahamu katika mila na desturi za kiafrika siku zote mababu zetu asili yetu, inapotokea iwe janga iwe furaha walikuwa wanamtanguliza Mungu kwanza.

Mheshimiwa Spika, nimeyaona hayo nikiwa kijijini, nimeona kabisa mtoto akizaliwa wanamshukuru Mungu, kukiwa na sherehe wanamtanguliza Mungu lakini inapotokea janga la aina yoyote Wazee katika koo mbalimbali waliungana. Hata watoto wakizaliwa yaani wale vichaa vichaa vya ajabu ajabu walikuwa wanamtanguliza Mungu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amefanya jambo muhimu sana katika kumtanguliza Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanini nasema kuna uhusiano kati ya Mungu na hii sayansi ambayo wenzetu wanatuambia. Kuna *theory* mbalimbali, nadharia wanasema kwamba huu ugonjwa unawezekana umetengenezwa na binadamu. Kwa hiyo, kwa kumuomba Mwenyezi Mungu tunamlilia, Mwenyezi Mungu huyu ndiyo atakayewaongoza watu. Kuna watu wanaambukiza wenao makusudi, kwa hiyo Mwenyezi Mungu huyu tukimuomba atatoa zile roho chafu zinazowaongoza watu waweze kuwaambukiza wengine au waweze kutengeneza magonjwa mengine kama sasa yalivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ameona mbali na ninampongeza sana kwa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la bajeti ya Wizara hii, kweli naona imeongezwa kutoka shilingi bilioni 30 kuja shilingi bilioni 40. Hata hivyo, natajikita zaidi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 30 kipengele cha 52 katika suala la maendeleo ya Idara ya Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukiangalia hali ilivyo sasa hivi, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake wanafanya kazi

nzuri, sitaki kuyarudia mambo mazuri ambayo wameyaeleza katika kuboresha vipindi, kuweka vipindi vipyta kama Aridhio tunaiona, usikivu na kadhalika pamoja na tafiti mbalimbali. Hata hivyo, ili idara hii iweze kuendelea ni vizuri pia tukatoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaona dunia inavyokwenda kwa mfano tunaona janga la *Corona*, hivi sasa tunasubiri tuletewe dawa za kisayansi wanazosema lakini mimi bado namshauri Mheshimiwa Waziri waendelee kufanya tafiti. Kwa mfano, juzi kwenye maombi yale, mimi niliangalia ile ya kwanza labda sikuona au nilipitisha, sijaona wazee wetu wa jadi wakipewa kipaumbele kwa sababu tayari tumeshakuwa *brainwashed* na wenzetu na sera zao, dini za kisasa na kadhalika lakini wana nafasi kubwa. Mbona kiongozi anapoteuliwa, Mheshimiwa Rais au Waziri, wote hapa tumekuwa Wabunge tumefanyiwa pengine pongezi mbalimbali na wazee wetu wa jadi lakini sikuona kwenye TV hawa wazee wakapewa na wenyewe *priority*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, walitoa fursa ya kujitokeza lakini kwa nini hawakujitokeza? Ni kwa sababu sisi Waafrika tumetawaliwa kifikra hatuwezi kujitambua kutafuta ukweli maisha ni nini, Mungu ni nini, kujua falsafa yetu, sasa tumeshanyanyapaa mpaka mila na desturi zetu. Leo hii mzee akitoka akashika ungo au usinga akatambika watu tayari wanamwita mshirikina au kwamba ni ushetani. Mwanaharakati ye yeyote akitaka kuharibu kitu kizuri lazima atatumia maneno mabovu na mabaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi bado naungana na Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge huko majimboni tunakokwenda tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu. Mimi ninayesema hapa ni Mtanzania, Mwfrika lakini ni msomi, nina shahada tatu, naelewa ninachokiongea kuhusu umuhimu wa mila na desturi za Afrika, pengine wengine hawakuyasomea lakini mimi nimeyasoma. Ukiniambia nianze kudadavua naweza kukuambia bora niende nikatambike kwa mababu zangu kuliko kwenda sehemu nyingine, *that is the reality*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu wametu-*brainwash* sana, kwa mfano, katika *exposure* yangu katika nchi nyiningi nimeona bado watu wana-*combine* mila na desturi zao pamoja na mambo ya kisasa yapi mazuri, yapi mabaya, nenda China, India, Korea au Afrika ya Kusini. Ndiyo maana hata China kuna watu bilioni 1.3 limetokea janga hili la *Corona* lakini waliokufa ni wachache, *why?* Wame-base kwenye utamaduni wa tiba.

Mheshimiwa Spika, sisi Waafrika tuna kila kitu. Siku moja Mheshimiwa Prof. Tibaijuka alisema hapa kwamba kule Uhayani kuna dawa watu wanafukiza lakini hata sisi kwetu kule Uluguru kuna dawa sijui mavumbasi na kadhalika. Nilishuhudia mtoto akitoka surua walikuwa wanampondea majani wanampa na kijiko kidogo anakunywa wanampaka mwili mzima baada ya hapo joto hakuna mtoto anaendelea. Hata hivyo, kwa sababu ya *conflict of interest*, mambo ya soko na kadhalika sasa wenzetu wametuzidi hata tunashindwa kujitambua, hatutafuti ukweli ni nini, hatutafuti maisha ni nini, tunasubiri tupewe majibu, hatutafika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na tafiti hizi anazofanya turudi sasa, ifikapo 2050 kizazi kile kinachojuwa mambo kinaweza kikawa kimepotea kabisa, hatutakuwa na *trace ye yeyote*, hatuandiki vitabu wala hatufanyi juhudhi zozote kuhifadhi asili yetu, naona hapo umesema kuna kitabu kinaandikwa lakini Tanzania tuna makabila zaidi ya 120 hatuwezi tukaweka kila kitu.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunasema vijana hawana maadili, maadili wayapate wapi wakati mila na desturi zilizokuwa zinawajenga vijana hawa kwa maadili zinanyanyapaliwa, wanakatazwa. Watu wanaambiwa wasifanye jando na unyago kule ndiyo walikokuwa wanapata *indigenous education*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Iringa kule, yule *queen* jina limenitoka kidogo alikuwa kila mwaka anachukua mabinti kuwafundisha, wazee hivyo hivyo, ukija kwetu kwa

Waluguru tunafanya hivyo, zile ndiyo zilijenga maadili. Sasa leo unamwambia Diamond kaepuka maadili ya Mtanzania kayapata wapi? Yeye amezaliwa anaangalia TV anachokiona ni kile cha kwenye TV lakini mambo ya mila na desturi hamna.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wazee wamejikunyata mtoto wa miaka 25 mwanaharakati anaenda kumfundisha mzee eti namna ya kuishi. Nafikiri Taifa linapotea turudi, tuangalie upya kwani hatujachelewa, tutumie hawa wazee wetu. Kwa mfano, hapa Bungeni huwa namsikia Mheshimiwa Waziri wa Nishati watu wakisema kwamba anajua mambo ya mifupa. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameridhisha watu wangapi? Tunaye kwa mfano Mtemi Chenge mpaka kaitwa Mtemi ana mambo mengi amerithisha watu wangapi? Kwa hiyo, tutumie hii *asset* sasa hivi kuanza ku-document.

Mheshimiwa Spika, leo hii siku dunia itaanza kupata janga tumeona kila mtu yuko kivyake tutafanyaje lakini hii sayansi yetu ya Afrika itatusaidia. Tumeona huyo mama ambaye mmemweka kwenye ripoti ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Tilsekwa nakushukuru sana.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa ni Mheshimiwa Devotha Mathew Minja kutoka huko huko Msekwa na baada ya hapo tatarudi hapa kwa Khadija Hassan Aboud.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa salamu za pole kwa familia ya Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge mwenzetu wa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia suala la *Corona* kama ilivyo ada kwa Wabunge wengine. Tuko kwenye *public panic* ya ugonjwa wa *Corona*. Ni haki ya Watanzania wote kupata taarifa sahihi ya ugonjwa huu *frequently*.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanategemea taarifa sahihi kama ilivyo elekezwa na Serikali waipate kutoka kwa Waziri wa Afya, Waziri Mkuu au Rais mwenyewe. Tukiangalia taarifa tulizonazo mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri alitoa taarifa juzi kushinda jana lakini ukiangalia siku chache zilizopita alitoa taarifa siku ya Ijumaa. Kwa nini tunasema haya? Tunasema haya kwa sababu taarifa ya Waziri ndiyo ambayo ina *public trust*. Sisi kama nchi kwenye janga kubwa kama hili inapita siku moja, siku mbili wananchi hawajui nini kinaendelea, hawajui kama kuna ongezeko, hata kama hakuna ongezeko wana haki ya kujua hali ya *Corona* ikoje kwa sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu watu wanaanza kutafuta *unreliable source*, sasa kama Waziri alitoa juzi ameshinda jana, jana ni kimya leo hatujui kama itakuwa kimya vilevile. Tukiangalia taarifa ya habari, mimi niipongeze *ITV* ina *reporters* wengi kutoka nchi za Afrika Mashariki, tukiangalia taarifa ya habari ya saa mbili unasilia Waziri wa Kenya anasema nini, wa Uganda anasema nini, nchi zote Burundi, Rwanda wanasesma nini lakini ukija kwetu unasilia maombi. Sasa wananchi wanataka kujua hali ikoje ili waweze kuchukua tahadhari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba ili kuzuia wananchi wasianze kuangalia Kigogo leo ame-*post* nini, mambo ya *hearsay*, mambo ya mitandao, Waziri atumie *media* kuhakikisha kwamba *information* zinakuwepo *day to day*. Hivi kuna shida gani kama Waziri akitengeneza *calendar* kama wenzetu wa nchi za jirani wanavyofanya, kila siku lazima wazungumze kuhusu hali ya *Corona* ilivyo nchini; hata kama kuna ongezeko au hakuna wananchi wajue. Kama ni saa saba kamili wananchi wajue wanamsubiri Waziri

anasema nini kuhusu *Corona*. Watu wanataka kujua hali ikoje kwa sababu janga hili lina *public panics*.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala lingine la *press conference* zinazoendelea hivi sasa nchini kwenye maeneo mbalimbali. Labda Waziri atuambie kama Wizara ya Habari wanachukua hatua gani kuwasaidia waandishi ambao...

TAARIFA

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Ally Saleh, endelea.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mbunge kwamba taarifa ya leo imetolewa na Tanzania wagonjwa wote ni 284. Hii ni kwa mgao kwamba Zanzibar wameongezeka sasa ni 83 na Tanzania Bara ni 201, kwa hivyo, wote ni 284 na vifo 10.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ally Saleh maana inaelekea Mheshimiwa Devotha hafuatilii taarifa, kwa hiyo, analaumu Serikali na Waziri, taarifa hiyo Mheshimiwa Devotha.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nimemsikia lakini nachosema sisi tuna haki kama Watanzania, kama ilivyo mataifa mengine, tunaona jamani ambavyo wenzenetu wanavyotumia *media* kuhabarisha wananchi hata kila baada ya saa mbili au tatu Waziri akitoa taarifa hizi kuna shida gani? Hii itaondoa sana wananchi kwenda kwenye hizi *unreliable sources* za kupata *information*. Mimi msisitizo wangu ulikuwa ni huo. Kwa mfano, kama jana hakukuwa na taarifa yoyote zaidi ya ile ya juzi lakini kama imetoka leo tunashukuru.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia *issues* za *press conference* zinazoendelea hivi sasa wakati wa *Corona*. Naomba Waziri atuambie, tunamwona Waziri wa Afya

anasema atachukua *initiative* kuhakikisha wahudumu wa afya, madaktari, manesi, wanakingwa na *Corona* hii. Sasa Waziri wa Habari ambapo tunasema Wizara ya Habari na Waandishi wa Habari ni mhimili wa nne, Waandishi wetu hawa wa Habari wengi wanatumia *camera* ambazo ni *unprofessional*, ukiangalia wengi wengi hawana *boomyaani* kumu-*interview* mtu inataka *centimeter* mbili tu ya kuweka *microphone* ili iweze ku-*pick* na sauti iweze kupatikana. Mwandishi huyo huyo anamhoji huyu, anatoka anakwenda kwa mwingine, anatoka anaenda kwa Waziri mwishoni anamalizia kwa kufanya *standup* lakini *microphone* ni ile ile. Sijui sasa ni mbinu gani ambazo kama Wizara ingekuwa inaangalia wakati wa utoaji wa taarifa hizi isije ikawa pia ni chanzo kingine cha kusambaza magonjwa.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hayo tuna mambo ya *e-Government*, hivi ni kwa nini Serikali sasa hivi isilinge kwenye mfumo wa kufanya *press release* badala ya kuwakusanya Waandishi wa Habari ambapo unamkuta Mwandishi anamhoji mtu hata barakoa hana. Sasa akutane na watu ambaao wanazungumza kwa kutumia *body muscles* akizungumza *mate* yanafika pale, unamwona Mwandishi huku anarekodi, huku anajikinga na mkono. Kwa hiyo, ifike mahali tuwaonee huruma hawa watu ambaao wanafanya kazi kubwa ya kulielimisha Taifa hili nao wasiingie kwenye shida hii.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kuhusu suala la ukandamizaji wa vyombo vyaa habari. Ninayo barua hapa Mwandishi wa Habari Talib Ussi Hamad wa Tanzania Daima kule Zanzibar amesimamishwa kazi miezi sita eti kwa sababu emeripoti habari za *Corona*. Tunajua Wizara hii sio ya Muungano lakini kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Tanzania lazima tuseme kwa sababu yalianzia hapa sasa yamehamia Zanzibar. Hivi kwa wakati huu ambaao tuko kwenye *public panic* nguvu zinaelekezwa kuminya Waandishi wanakuwa waoga. Umefungia huyu, tunasikia kuna barakoa zinafuliwa zinatumwiwa mara mbili au tatu Waandishi wakienda kwa wataalamu wanawaambia sisi sio wasemaji, msemaji yupo ni Waziri. Sasa hii inaleta hofu, ni lazima tuangalie ni namna

gani wakati huu badala ya kuelekeza nguvu kupambana na vyombo nya habari tuelekeze nguvu kusaidia umma kwa hali tuliyano hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala la ukandamizaji wa vyombo nya habari na waandishi wa habari Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe sijamsikia akitetea waandishi wa habari. Ni bahati mbaya sana kwa miaka mitano namsikia akisema tutahakikisha *this time* tunaiandikia F/FA, tunataka tusajili wachezaji watano wa nje ili wengine wawe ni wazawa lakini sijasikia akizungumza waandishi wa habari kuna kitu kinaitwa *retrenchment* kwenye vyombo nya habari. Mwandishi akiandikia kitu chochote cha kukosoa Serikali anaachishwa kazi. Mwandishi ye yote akikosoa hata kwenye mitandao anaafatiliwa anaachishwa kazi. Sasa sielewi ni kwa nini Waziri hayupo kusaidia Wizara hii na inaitwa ni Wizara ya Habari...

TAARIFA

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Devotha, pokea taarifa. Yuko hapa au Msekwa?

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, Msekwa.

SPIKA: Haya endelea Mheshimiwa Mwakasaka.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba huyo mwandishi wa Zanzibar anayemtaja hakusimamishwa kwa sababu ya kuripoti *Corona* ila yeye alitaja jina la mgonjwa kinyume na maadili yanavyozungumzia kuhusu mtu anapougua.

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwakasaka. Pia nimwambie Mheshimiwa Devotha unajua matumizi ya takwimu yana shida kwa watu kadhaa. Kwa mfano,

unaposema mwandishi yeote akiandika hivi anapata hili maana yake ume-*generalize*, umefanya *the whole population* inahusika badala ya wewe ku-specify kule unapotaka kuelekea ni nani aliandika nini. Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Devotha?

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, taarifa nimeisikia lakini kwa mfano Mwana FA aliamua ku-expose hali yake na waandishi waliandika, ni kama hivyo mgonjwa akiamua ku-expose hali yake mwandishi akaandika halafu anawajibishwa. Ndiyo hayo ninayoyazungumza kwamba ifike mahali tuangalie namna ya kufanya haya mambo pasipo kuumiza watu.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kuhusu habari ya Waziri kushindwa kuwasaidia waandishi wa habari. Katika kipindi cha miaka mitano, nasema kwa mlaka mitano au mitatu ijayo hii tasnia ya habari inakwenda kufa kwa sababu kila kukicha waandishi wanafukuzwa kazi kwenye vyombo vyao vya habari ukifua tilia ni nini, haelezwi sababu ya kufukuzwa kazi ni nini, baadaye anabaki tu haelewi wananyong'onyeshwa, wanabaki waandishi *juniors*, kwa kweli lazima kama taifa tuangalie suala hili. Hatuhitaji kusikia mambo mazuri tu lazima tusikie mambo mengine pia na *analysis* za waandishi. Kwa mfano, sasa hivi barakoa zimekuwa shida moja ni Sh.4,000, mwandishi anasema nimekuta *Selander Bridge* kule ujenzi wake wa billioni 300 unaendelea. Mwandishi akajaribu kuangalia *priority* ni nini anaonekana ni mchochezi. Haya ndiyo mambo ambayo tunasema tunahitaji hawa watu wasaidiwe na Waziri amekuwa kimya.

Mheshimiwa Spika, leo wapo wakosoaji ambao wanatumia kabisa sheria na haki yao ya kujieleza akina Tito Magoti wako ndani, kina Ben Saanane waliokuwa wana mitandao hawaonekani, kina Azori Mwandishi wa Gazeti la Mwananchi mpaka leo haonekani lakini Waziri yupo kimya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Devotha, muda wako umeisha.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani.

SPIKA: Ahsante sana. Ingawa baadhi ya mambo ambayo tunaishauri Serikali aah basi ndiyo ushauri wenyewe lakini, kwa sababu tunapolazimisha Serikali iwe inatuambia kila baada ya saa mbili, huku Lindi kuna mmoja, baada ya nusu saa Kagera ameongezeka, baada ya saa moja Kongwa, baada ya nusu saa Tarime, mwisho siku inasaidia nini? Takwimu zozote zikishakuwa *monotonous it is useless*.

Tazama taarifa za habari za saa mbili usiku na kadhalika mwanzo mwisho zinazungumzia *Corona*. Kwa hiyo, mtu akisema eti taarifa katika nchi yetu hazipo, taarifa ya habari nzima fungua TV hii na ile, tulio wengi tumechoka sasa hivi tunaangalia na kwinge nako kidogo angalau kupata mambo mengine. Siku hizi Watanzania wengi wanaangalia ile Sultan ili angalau kupata *anything different* maana yake ni *Corona*, *Corona which is good* lakini *is already too much actually*. Kwa hiyo, kuilaumu Serikali katika eneo hilo kwa kweli sidhani kama ni sawa.

Halafu hizo nchi ambazo zinasifiwa kwa wale ambao ni waangalifu katika takwimu ziangalieni takwimu za Burundi, Rwanda, Uganda, za Uganda zipo pale pale wiki ya pili, zile zile, hazina badiliko lolote hata za nchi jirani hapo. *Actually* wanaotoa takwimu angalau naweza nikasema zinaonyesha ukweli ni sisi Watanzania, kabisa, ni kwa sababu tumezoea tu kusifia wenzetu ndiyo maana tunasema za wapi na wapi lakini angalia hizo za kwao utaona, sitaki kusema mimi ni Spika lakini ukiwa ni mtu wa takwimu unaona hapa katika nchi jirani *there*

is a problem. Takwimu ni zile zile, hazina badiliko lolote na bado tunazisifu, tunaponda za kwetu. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, yupo Msekwa.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuiendeleza Wizara hii na kubua vipaji vya wanamichezo, wasanii, wanamuziki na hatimaye vipaji hivyo vimepelekea nchi yetu kuitangaza na kuipatia sifa duniani.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wasanii na wanamichezo wote wanaotumia vipaji vyao kuitangaza nchi yetu. Pia nawapongeza wanahabari, wanatumia muda wao mwingi kutuhabarisha vitu mbalimbali na kutupa elimu mbalimbali wakiwemo na hao hao wasanii wanatumia vipaji vyao pia kutuelimisha kupitia sanaa zao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais kwa juhudini kubwa anayochukua katika kuhakikisha Wizara hii na sekta zake inafanya kazi zake kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, utamaduni unaanzia tangu mtoto akiwa tumboni. Mtoto akiwa tumboni ule ujauzito tayari mama yumo ndani ya utamaduni kutokana na mila na desturi anapotoka yule mama. Mpaka kuzaliwa na kukua kwake, mpaka harusi zetu tumo ndani ya mila na utamaduni, lakini mpaka kwenye mazishi basi pia tumo ndani ya mila na utamaduni kwa sababu kuna mambo yanakuwa yanatendeka. Kwa maana hiyo nchi yetu lazima tuulinde na kuudumisha utamaduni wetu. Tuuendeleze na ubakie kama ni historia ya nchi yetu ambayo haitafutika kwa kurithiwa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nikija kwa wasanii; wanatumia muda mwingi kutunga, kubuni na kutia nyimbo muziki mbalimbali. Naomba sana Wizara iendelee kwa nguvu kubwa kuhakikisha wasanii wetu wanapata hatimiliki zao kwa sababu wanapokosa hatimiliki zao inauma sana. Msanii anatumia muda mwingi na hasa kwenye kutunga kama nyimbo au kutia muziki, lakini baadaye utakuta muziki ule au wimbo ule unaimbwaa eneo lingine. Nimeshakuta sehemu nchi fulani wanapiga nyimbo zetu, nikawaambia wimbo huu umetungwa Zanzibar na unatoka Zanzibar. Wakapinga kabisa wakasema huu wimbo hautoki Zanzibar wala hauna asili ya Zanzibar na wanaupiga na wanapata pesa nyingi sana kupitia wimbo ule. Walichofanya wametoa kwenye lugha ya Kiswahili wamepeleka kwenye lugha ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba hii hatimiliki kwa wasanii isimamiwe vizuri, kwa sababu mimi najua machungu ya kutunga halafu mtu anapokuibia haki yako. Nilishafanya kazi kwa muda wa miaka mitano na wasanii kama Naibu Mkurugenzi Idara ya Tamasha, Mila na Sanaa na nilikuwa nao muda wote na nilikuwa naona yale machungu wanayoyapata katika kutunga na kubuni vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo kwenye hatimiliki nashauri Wizara, nilizungumza kwenye Wizara ya Muungano, iongezewe fedha kwenye Kitengo cha Utafiti kwa sababu kuna mambo yanapotoshwa na kuna mambo yatapotoshwa baada ya wanayoyajua kufariki dunia. Mfano, kuna changamoto inajitokeza mara kwa mara, Vita vya Majimaji wengine wanasema Songea, wengine wanasema Mafia, wengine wanasema Kilwa, kuna siku tutaambiwa vilianzia Sengerema. Kwa hiyo zikikaa kumbukumbu vizuri zikarithiwa kwa vizazi vijavyo itadumisha utamaduni wetu na historia ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea hapo hapo kwenye hizo kumbukumbu, kuna vitu vya kitamaduni, mila, vya ukombozi, lakini pia na vitu vya Taifa letu; harakati zetu za ukombozi zilianzaje, viwekwe vizuri. Nilisema kipindi kilichopita mfano aliyetunga jina la Tanzania watu wengi hawamjui,

lakini mimi nimefuatilia historia nimeambiwa kulikuwa na mashindano mwanafunzi wa Dar es Salaam mmoja wa sekondari alishinda akapata tuzo na jina lake likachaguliwa kuwa jina la Tanzania, lakini nani anayejua?

Mheshimiwa Spika, baadaye anaweza huyu mtu akapotea akajitokeza mtu mwingine akachukua hii haki. Kwa hiyo haki miliki ni jambo la muhimu na kuweka kumbukumbu muhimu za Taifa hili ambazo zitarithiwa kwa vizazi vijavyo miaka na baada ya miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watu hawa, wanatumia vipaji vyao kubuni vitu mbalimbali na naipongeza Serikali kwa kuwatambua na kuwathamnini mashujaa pamoja na kuwatambua wabunifu wetu. Naomba kazi hii iendelee.

Mheshimiwa Spika, nami kwa sababu Bunge langu hili kwa kipindi hiki awamu hii ya mwisho, nampongeza sana Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kunitunuku Nishani ya Heshima ya juu sana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Namshukuru kwa dhati sana kwa kuona mchango wangu na nguvu zangu katika Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea baada ya mambo hayo, nizungumzie Kiswahili. Kiswahili ni ajira, lakini kama ni ajira ni vyema sasa hiki Kiswahili tukakitumia kilivyo, kisipotoshwe, kwa sababu kuna baadhi ya maneno sasa hivi yanaanza kupotosha. Mwanafunzi akisoma anakuwa Mwalimu huyu kamwambia hiki, Mwalimu yule kamwambia vile, mtaani kaambiwa kingine. Ni vyema sasa Kiswahili chetu tukifanye kama kweli ni ajira na kitatutangaza Tanzania kama nchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa juhudii aliyoifanya kuhakikisha Kiswahili kinatambulika duniani kote na kukijengea heshima Kiswahili kama lugha yetu ya Taifa. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwenye Sekta hii ya Utamaduni; utamaduni ni ngao, ni vyema sasa wasanii wetu watumie maadili mema kuhakikisha wanatumia nyimbo, michezo, tungo mbalimbali kwa kufuata maadili yetu ya Mtanzania. Kwa kuwa hii ni Wizara ya Utamaduni mimi nazipongeza Serikali zote mbili; Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kule Serikali ya Zanzibar Rais wa Zanzibar amemteua mtu maalum kwamba ni Mshauri wa Rais wa Mambo ya Utamaduni. Hii ni kuonesha kwamba viongozi wetu wanajali na kuthamini jitihada zote zinazofanywa na wasanii wetu na utamaduni wetu kuhakikisha unakua. Naipongeza sana Serikali, inathamini bwana, inathamini wasanii, inathamini watu wote wa utamaduni, inawaheshimu na tunaona vipaji vinakua na kuongezeka. Bila juhudzi za Serikali kuhakikisha wasanii wetu wanafanya kazi zao kwa ubunifu zaidi vipaji vyao vingedidimizwa, lakini tunaona Wizara inafanya kazi ya kuhakikisha wanaibua vipaji mbalimbali kwa mujibu wa kuitangaza nchi, lakini kuwatafutia ajira hao wanamichezo na wasanii wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana, kwa kumalizia kwa kuwa hii ni Wizara ya Utamaduni na mimi ni mdau wa sanaa, mimi ni msanii wa utunzi lakini pia ni msanii wa kazi za mikono *Zanzibar Wood Carving*, mimi ni mtaalam na ni mwanimke wa mwanzo kufanya kazi ile na nilipewa tuzo.

Mheshimiwa Spika, nasema *Rabbi* utubarikie, ibariki nchi yetu na neema tuzidishie katika Taifa letu, maradhi tuondoshee ya *corona* nchini mwetu, maisha yaendelee tuzifanye kazi zetu. *Yaa Rabbi* utulindie wote viogozi wetu, amani tuzidishie ngao ya Taifa letu, Magufuli tulindie, Shein na Spika wetu, mazuri watufanyie zifurahi nyoyo zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

Waheshimiwa Wabunge wengi hamumfahamu vizuri Khadija. Khadija ni mghani, ni mtu ana kipaji kikubwa kabisa katika masuala ya sanaa. Upande wa Chama chetu cha Mapinduzi ni mtu mwenye historia kubwa sana. Alianza tangu chipukizi, taratibu amepanda mpaka kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi na amekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM kwa miaka mingi kabisa. Kwa hiyo ndio maana kapewa nishani na Mheshimiwa Rais Shein kwa ajili hiyo. (*Makofii*)

Tuko na watu hapa, watu hamfahamiani tu, lakini tuna watu ambao wana mchango mkubwa sana katika nchi yeu, mmoja wapo ni Khadija. Tunakushukuru sana kwa mchango wako. (*Makofii*)

Sasa turudi hapa ndani tuanze na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ajiandae baada ya Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na nimefurahi kwamba baada yangu atafuatia Mheshimiwa Mbilinyi, Sugu, nilishawahi kuwa promota wake. Haya nitakayoyasema nitayasema kutokana na uzoefu nilionao katika *music and entertainment industry*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijayasema hayo, napenda kwanza kushukuru na kupongeza Wizara na watendaji wote. Kipekee napenda kumpongeza bwana Gerson Msigwa na Dkt. Abbasi, watu hawa kwa kweli wamekuwa mstari wa mbele katika kuuhabarisha umma wa Watanzania kile kinachoendelea ndani ya Serikali, miradi inavyofanyika na kwa kweli wamekuwa ni wasemaji wa Ikulu na wasemaji wa Serikali. Mimi binafsi kama mtu ambaye nimetokea *newsroom* najivunia watu hawa kwa uchapakazi wao mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kupongeza *TBC* na hasa *Channel* yao ya Safari. Hapa hapa napenda kutoa

ushauri; pamoja na kwamba inapatikana katika King'amuza cha Zuku, nashauri kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii waone uwezekano wa *channel* ile kuonekana katika baadhi ya nchi ambapo watalii wanakuja kwa wingi ili tuweze kutangaza soko letu la utalii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hivyo napenda kupongeza Shirika la Habari na Magazeti ya Serikali, *TSN*, kwa kazi nzuri, kwa kuingia katika *digital* na tena kwa lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza na hivyo hata jumuiya ya kidiplomasia nayo inapata kuhabarika nini kinaendelea katika Taifa letu, miradi mbalimbali ya maendeleo na kadhalika, lakini pia na *TCRA* kwa usimamizi bora wa kimaudhui.

Mheshimiwa Spika, leo pamoja na kuwa ni mwanamichezo napenda kuzungumza sana kuhusu *entertainment industry*. Hapa kidogo nina takwimu ya mchango wa *entertainment industry* katika uchumi wa nchi mbalimbali kutokana na taarifa ya *PWC* yenye kichwa cha habari *Entertainment and Media Outlook 2018-2020*, yaani wanaangalia matazamio na *projection*.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya na natoa hizi takiimu kwa nini? Nasema hivi kwa sababu takiimu hizi zinasema, kwa mfano, imefanyika hii tafiti katika nchi tano za Afrika na nyingine pengine unaweza kusema nchi kama *South Afrika* wenzetu wako mbele zaidi, lakini nchi kama Kenya tunafanana nao kwa namna nyingi tofauti. Katika Kenya wana-project kwamba mapato katika *entertainment industry* kutoka bilioni 1.7 mwaka 2017 mpaka bilioni 2.9 2020; hapa kwetu Tanzania yatatoka katika milioni 496 *USD* mpaka bilioni 1.1 by 2020. Nchi kama Ghana kutoka milioni 552 mwaka 2017 mpaka bilioni 1.5 mwaka 2002, hiyo ikiwa ni *USD*.

Mheshimiwa Spika, pia mchango wa filamu katika mapato au kuingiza mapato, hapa kwetu mwaka 2017 ilikuwa ni dola 710,000 lakini kufikia 2022 itakuwa dola 1,500,000. Ghana ilikuwa dola 1,600,000 itafika dola 2,100,000 za Kimarekani na Kenya ambao ni majirani zetu kutoka dola

4.5 mpaka dola 5.9 by 2020, lakini Nigeria ambao wenzetu katika *film industry* wako mbali zaidi itatoka dola milioni 12 mpaka dola milioni 18.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini nayasema haya? Nayasema haya kwa sababu tunayo kila sababu ya kutengeneza mazingita bora ili *entertainment industry* iweze kuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa letu, lakini pia kama chanzo cha ajira kwa vijana wetu. Dunia sasa hivi inavyokwenda ki-*digital* wanasema kutoka na matumizi ya *internet*, mambo mengi na makusanyo mengi kupitia mitandao kama *You Tube* na *social media* hizi zinaleta mamilioni mengi, lakini sasa je, mazingira ya ufanyakaji kazi ya hawa vijana wetu yakoje? Hapo ndipo ninapotaka nijikite na niishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano; siku ya Machi 31 mwaka huu kijana mmoja alinitumia *message* akinieleza changamoto anayokutana nayo katika kupata *certificate* pale Ofisi za *COSOTA*, Ubungo. Ananiambia kwamba tumejazana hapo Ubungo mikoa yote inategemea ofisi moja. Anasema mimi nimeleta filamu sita ili ziweze kupata hizo *certification*. Mwenzake mmoja alikuwa na filamu 100 na wale wanamwambia hivi eti hawana 120,000 ili kuweza kupata karatasi ya kuweza kuwachapishia zile *certificates*.

Mheshimiwa Spika, ninaposema filamu 100 maana yake ni nini? Nchi kama Nigeria kwa mwaka wanatengeneza filamu zaidi ya 2,000. Sasa mtu anapokwenda pale, kwanza ofisi ipo tu Dar es Salaam, haiko mikoani, hiyo ni *COSOTA*, lakini bado kuna Bodi ya Filamu ambako lazima ukienda filamu yako kwa dakia moja wanakuchaji Sh.1,000, kama filamu ina dakika 60 maana yake ni Sh.60,000, hilo sio tatizo. Tatizo liliopo, ningeshauri Serikali wange-*decentralize* hizi huduma kama ambavyo tumefanya katika maeneo mengine ili msanii anapokuja apate hapohapo *certificate* ya Bodi ya Filamu baada ya kukagua filamu yake, lakini pia apate masuala mazima ya *COSOTA*, lakini ikiwezekana kama bado hajapata usajili basi BASATA na yenyewe iwe maeneo hayo ili mtu huyu aweze kupata huduma sehemu moja.

Mheshimiwa Spika, maana ya hii, yale mamilioni nilyokuwa nayataja kama watu hawa tutawatengenezea mazingira bora maana yake ni kwamba tutaongeza mazingira bora ya ufanyaji wao kazi na hivyo kuongeza *revenue* katika mapato ya Serikali. Kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba na hili jambo nimeshawahi kulisema, nilishauri Serikali wangeweza wange-*decentralize* hata Maafisa Utamaduni katika wilaya, wangeweza kufanya hii kazi. Kama hiyo haiwezekani basi tuanze na *zones*; tuwe na *Zone* labda ya Nyanda za Juu Kusini, *Zone* ya Kusini, *Zone* ya Kaskazini na kadhalika, lakini nia mwisho wa siku ni kuwezesha vijana ambaao kwa mamia na maelfu wanajajiri katika *industry*, kuweza kufanya kazi katika mazingira ambayo ni bora, yenye mvuto, lakini mwisho kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni mwanamichezo, leo asubuhi nilikuwa na swalii; je, lini Serikali inaona utayari wa kuwa na shule za vipaji maalum kwa ajili ya michezo na utamaduni? Naomba pia kushauri Serikali, kama ambavyo tuna shule za kitaaluma, vipaji maalum katika taaluma, tuwe na shule kwa ajili ya masuala ya michezo na utamaduni. Sambamba na kuwa na shule hizi ambazo tunaweza tukaanza kwa *zones* pia tuviangalie vyuo vyetu vya mambo ya michezo kwa maana ya Chuo cha Malya, kwa maana ya Chuo cha Butimba, lakini pia na Taasisi ya Sanaa pale Bagamoyo ambayo mpaka Wazungu kutoka Norway, kutoka *Finland* huwa wanakuja pale kupata mafunzo.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo maana yake ni kwamba tutaweza ku-*compete* katika *media and entertainment industry* katika dunia, lakini mwisho wa siku ajira kutoka kwa vijana wetu ambaao wamejajiri kwa wingi kwenye hizi sekta za mambo ya burudani na michezo, wanaweza wakapata ufanisi, lakini pia hata katika michezo yenywewe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa kumalizia katika michezo wa soka; napenda kupongeza *TFF*, inajitahidi sana, timu za vijana, timu za wanawake, timu ya wakubwa inashiriki katika michezo mbalimbali ya kimataifa. Rai yangu

kwao moja; tuangalie suala la waamuzi, kumekuwa na malalamiko kwamba hawalipwi kwa wakati. Kwa hiyo niwaombe *TF* watafute hata wadhamini ambao mdhamini huyo yecheza atajilengesha katika kuhakikisha kwamba analipa mishahara na posho kwa ajili ya waamuzi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu bila kuwa na waamuzi bora, bila kuwa na waamuzi wenye kuchezesha kwa weledi maana yake hatutakuwa na mchezo wenye kuvutia na usipokuwa na mchezo wenye kuvutia maana yake huwezi kupata wadhamini. Kwa hiyo tuwe na michezo inayovutia, yenye ushindani, tupate wadhamini na tuwe na uwazi na uwajibikaji katika kusimamia kile ambacho wadhamini watakuwa wamekitoa katika michezo yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napongeza na naendelea kumpa pole Mheshimiwa Kapteni Mkuchika hapa kwa kushangilia ushindi na sare badala ya *ku-focus* kwenye ubingwa. Mungu awabariki sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi na hasa ulivymalizia, nilitamani nikuongeze dakika mbili, lakini muda hauko upande wako. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami nichangie, lakini kabla ya kuchangia pia na mimi naomba nitangulie kutoa pole kwa familia na Kanisa zima la Mlima wa Moto Mikocheni kwa msiba wa mama Mchungaji Dkt. Getrude Rwakatare ambaye mimi nilikuwa naye kwenye Kamati na kwa kweli alikuwa mama yetu pale. Pia watoto wake ni marafiki zangu, nilikaa nao Dallas, Texas miaka ya nyuma. Pia nawapa pole familia zingine zote zilizopoteza wapendwa wao kwa janga la *corona*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza nifafanue kidogo kuhusiana na kauli ya aliyetoka kuchangia, Mheshimiwa Chumi. Ndiyo tatizo la vijana wa chama chako, Chama cha

Mapinduzi. Mheshimiwa Chumi wakipewa nafasi wanaanza kujitanua na kujimwambafai. Kwa sababu Mheshimiwa Chumi hakuwa *promoter* wangu. Wakati anasoma nilikuwa namchukua kwenye show zangu akae mlangoni, akatishe tiketi achukue kiingilio ili apate ada ya kwenda kulipa alikokuwa anasoma. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni *initiative* yangu toka zamani kusaidia vijana wasiokuwa na ajira kama alivyokuwa ye ye wakati ule; lakini hapa anakuja anasema sasa ooh, alikuwa promota, alikuwa nini, wakati nilichokuwa nafanya ni msaada tu. Kwa sababu, 1994 mimi ni *National Star*, Mheshimiwa Chumi alikuwa wapi awe *promoter* wangu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, miaka hiyo mimi nilikuwa nafanya kazi za *promotion* na matajiri, akina Mutta... (*Kicheko*)

SPIKA: Basi Mheshimiwa Mbilinyi inatosha. Sasa endelea kuchangia hoja. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, vijana wa CCM ndiyo hivyo, ukipewa uwaziri kidogo unaanza kurusha watu vichura, yaani ndiyo silika ya vijana wa CCM wa sasa. Akina Mheshimiwa Lukuvi hawa wamekuwa Mawaziri wakiwa vijana sana. Sasa kama wewe ulikuwa *promoter* wangu, unajua kwamba Mheshimiwa Lukuvi ndio alikuwa Mgeni Rasmi wa kwanza kwenye uzinduzi wa albamu yangu ya kwanza akiwa Naibu Waziri wa Vijana? Unafahamu hilo? Ulikuwa wapi? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, niendelee na hii kazi ya Wizara. Wizara hii ya Habari nimeitumikia katika muda wote kama Waziri Kivuli toka nikiwa chini ya Mheshimiwa Rais Kikwete akiwa Rais, mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Wamepita Mawaziri wengi; amepita Mheshimiwa Nchimbi, amepita Mheshimiwa Mama Fenella na sasa hivi niko na *my Minister Brother* Mheshimiwa Harrison ambaye, kwa mimi ninavyoijua kabisa, hii Wizara nilikotokanayo mpaka leo imesaidia, ime-

disturb sana hata credibility ya my Minister Brother Mheshimiwa Harrison Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimia Mwakyembe ni mtu ambaye ana *potential* zake kutokana na elimu yake, lakini mmempeleka kwenye hii Wizara hamumpi hela. Mnamwambia mtampa bilioni tano aboreshe *TBC*, mpaka leo hamjampa hata senti tano. Sasa uwezo wake utaonekana vipi? Matokeo yake *brotherwangu* anaonekana tu tapeli. Kwa sababu anakuja na *plan*, anawaleta *plan*, hela hamumpi hata ndururu. Eeh, hata ndururu hamumpi Waziri Mwakyembe, mnatarajia afanye nini katika kuendesha hii Wizara? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi mmempa Wizara ambayo ina habari, utamaduni, michezo na sanaa, lakini habari mmeichukua mkaipeleka kwa Dkt. Abbas, kaka yangu mmemwacha na mpira, matamasha ya wasafi, *concert* za Koffi Olomide basi, ndiyo mlizomwacha nazo. Habari amebakinayo Mheshimiwa Dkt. Abbas ili kuendeleza *spinning* na *propaganda*.

Mheshimiwa Spika, pia kutumia ofisi kama Msemaji wa Serikali na sasa Katibu wa Wizara kupindisha na kudanganya wananchi kuhusiana na masuala mbalimbali ya Taifa hili. Hicho ndiyo kitu mnachokifanya. Sasa hii siyo sawasawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo lilloathirika na ubabe wa Awamu ya Tano ni Sekta ya Habari. Ni miaka mitano ya kufungwa midomo. *Media* imefungwa midomo, Wabunge tumefungwa midomo, Viongozi wa Dini wamefungwa midomo, *NGOs* zimefungwa midomo, wanaharakati wamefungwa midomo, na kadhalika. Hata pale ambapo kuna jambo lillonyooka na la kweli kabisa watu wanakwepa kulzungumzia.

SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi kwagine kote nitakuvumilia, lakini ukisema Wabunge wamefungwa midomo; au kwa sababu tumevaa barakoa? Hapana, hii siyo kufungwa midomo. (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, hapana. Kiongozi wetu sisi...

SPIKA: Kwenye Bunge langu mnazungumza na ndiyo maana nakupa muda hata wewe mwenyewe Mheshimiwa, hujafungwa mdomo, ongea.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, sijazungumza kwamba wewe ndio umetufunga mdomo. Nitakupa mfano; leo kiongozi wetu sisi *KUB* alikuwa na *Press Conference* Ofisi za Kanda pale, ofisi za chama chake anachokiongoza za kanda. Ilikuwa tufanye *Press Conference* saa 4.00 pale.

Mheshimiwa Spika, tumekukwenda pale saa 4.00 tumekutana na *battalionya* Polisi wakiwa na bunduki, *pistols, grunet* za kutupa kwa mkono, mabomu ya machozi na silaha nyingine zinazoonekana na zisizoonekana. Vilikosekana vifaru tu pale, lakini silaha zote za kivita za kijeshi zilikuwepo pale kuzuia Kiongozi wa Upinzani Bungeni, asifanye *press*. Huko siyo kuwazuia Wabunge uhuru wao wa habari?

SPIKA: Labda nifafanue kwanza ili kwa anayetusikiliza ajue kwamba hayo mambo kwanza hayajatokea katika eneo la Bunge, ili isije ikahushwa Bunge na hilo.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, mimi nazungumzia masuala ya Taifa, sizungumzii ndani ya Bunge...

SPIKA: Subiri kidogo Mheshimiwa Mbilinyi, muda wako nakutunzia.

La pili, nichukue ushauri wa Mbunge wa CHADEMA Mheshimiwa Devotha Minja kwamba katika nyakati na mazingira kama haya toeni *press*; habari ya kuita Waandishi wa Habari Serikali imesema habari ya mikusanyiko hapana. Kwa hiyo, hayo ni mambo yanayoendana na *Corona* na nini na nje ya hayo, lakini siyo eneo la Bunge. Endelea tu kuchangia.

Niliona mtu amesimama, au ilikuwa ni...

Endelea Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, humu ndani mimi, wewe na hawa wote ni Wabunge na kazi yetu ni kuisimamia Serikali. Haya ninayoyasema ya ukandamizaji wa uhuru wa habari yanafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano siyo na Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja yangu hapa sijasema kwamba Kiti kinazuia kusema. Kama mimi siku mbili hizi hujanizuia. Hata juzi umenizuia japokuwa katika huko huko kuzuia habari, *clips* zetu sisi Wabunge wa Upinzani, Bunge linazizuia zisitoke. Kwa hiyo, huo nao ni uminyaji wa uhuru wa watu kupata habari za Wabunge wao kupitia Ofisi yako.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama sio wewe, basi ni Katibu wako Ndugu Kagaigai ndio anafanya hiyo kazi. Hata juzi nimemwambia. Nimekutana naye nje anasema, mnanilaumu bure mimi sina kosa lolote, *innocent*. Nikamwambia *innocent* kwa suti nzuri, tai nzuri, lakini kuna vitu ambavyo havifai unavifanya. Akauliza nafanya nini? Nikamwambia unazuia *clips* zetu, *video* zetu, tunachokisema Bungeni unazuia tusipewe wala kisitoke. Akasema mimi sihusiki. Nikamwambia wewe ndio *incharge*, wewe ndio *CEO* hapa, huwezi kuruka kitu chochote kinachofanyika mahali hapa. Kwa hiyo, hayo mazingira kama hayo... (*Makofii*)

SPIKA: Ukiiniuliza mimi, kwenye *You Tube* naona *clips* zenu zaidi na sioni hata ya Mbunge mmoja wa CCM. Tena zako zote unazopiga humu ndani zinatoka safi kabisa. Endelea Mheshimiwa, muda.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, ukinithibitishia kwamba *clip* yangu iliyopita na iliyopita na iliyopita, tatu tu za nyuma zilizopita kwamba ziko *available*

au ukinipa, basi nitashawishi hata yule mgombea wa CHADEMA anayekusumbua kule jimboni a-withdraw ili usimame peke yako. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya mambo tunaingiza *humor* ili kupunguza *tension* ili yopo katika miaka mitano, lakini *in reality* haya mambo yanatumiza na tunayaongea kutoka moyoni. Tunachofanya ni kulainisha tu lugha ili kwamba labda mta-*relax* na yawaingie, myasikie na myafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kiukweli ni kwamba, sasa hivi mimi sija-*concentrate* sana kwenye kushauri, sasa hivi na-*concentrate* kuelezea upungufu wenu wa miaka mitano kwa sababu, muda umekwisha. Hamna muda, hamna tena maarifa, hamna tena fedha za kufanya mabadiliko yoyote katika kipindi kilichobaki kuelekea uchaguzi ndugu zangu. (*Makof*)

(Hapa, kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya mambo yapo na yapo hasa. Mateso ya wanahabari ndiyo usiseme, kufungiwa magazeti...

SPIKA: Katibu Mezani ananiambia ni ya pili, kwa hiyo, malizia sentensi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Aah, ni ya kwanza.

SPIKA: Ananiambia ya pili.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, hata hivyo hata muda wangu hukuutunza.

SPIKA: Ananiambia ya pili na kwa kweli ametunza muda wako. Nakupa dakika mbili umalizie, haya.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, kufungiwa magazeti, kushitakiwa kwa kesi za kubambikiwa mfano kama Maxence Melo wa *Jamii Forum*, Erick

Kabendera kafungwa mpaka mama yake kafariki kwa kesi za kubambikiwa; yote hii ni mateso kwa wanahabari. Kupotezwa kwa Azori Gwanda mpaka leo kimya hatujui yuko wapi; na kufukuzwa kazi kwa waandishi.

Mheshimiwa Spika, juzi gazeti la Mwananchi limetoa habari picha ya Mheshimiwa Rais yuko kwenye soko la samaki; sijui nani akawapigia simu, sijui ikawaje, wakatoka na kanusho wakaandika kumradhi. Kuandika kumradhi, kama nimeandika Lukuvi ameonekana *Anglican* wakati kumbe alikuwa yuko Katoliki, nikiandika kumradhi (*sorry*), hakuwa *Anglican* alikuwa Katoliki kwenye tasnia ya habari hiyo inatosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hofu iliyokuwepo kwenye vyombo vya habari, Mwananchi wakatoka na kujiadhibu zaidi, wanasema kumradhi, lakini pia tutawafukuza kazi, tutawachukulia hatua kali waandishi waliohusika...

SPIKA: Muda hauko upande wako Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: ...na wamewafukuza kazi wale vijana wako nyumbani saa hizi wako nyumbani hawana ajira, wakati tayari

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Kama siyo kubana uhuru wa habari... (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, lakini pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhanah-Wataala*, ametuweka hai hadi hii leo.

Mheshimiwa Spika, nami nianze tu moja kwa moja, kwanza naipongeza sana Serikali kwa juhudini zinazofanyika kukabiliana na ugonjwa huu wa *Corona*. Pili, nawapa pole sana waandishi na watangazaji wenzangu kote nchini hasa pale *TBC* ambako Marin Hassan na Haonga wamepoteza maisha yao. Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, pia uniruhusu tu niwape pole familia ya Mheshimiwa Mchungaji Mama Lwakatare. Mimi ni mtu ambaye nimekuwanaye karibu sana mama yule, Mwenyezi Mungu amweke mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza nimesikiliza michango mingi humu ndani, lakini nami kwa nafasi yangu nimeona nishauri mambo machache. Nchi zote duniani hakuna uhuru usiokuwa na kikomo. Hapa nyuma tullegalega sana sisi hapa kama Taifa, watu wakawa wanafanya mambo wanavyotaka tu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kujenga nidhamu katika Taifa letu, lakini nidhamu hii inakwenda sambamba pia na vyombo vyahabari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo kubwa sana; kuna habari na umbea. Hapa nyuma tumekuwa na umbea mwangi badala ya habari. Nami nampongeze sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwa kusimamia hili. Vyombo vyahabari ni hatari sana; vina faida na hasara. Jifunzeni hapo chini tu hapo Rwanda mwaka 1994 *what happened?* Kuna uhuru, lakini pia uhuru una ukomo. Tusifike hatua tukawa tunalaumu tu Serikali inaminyia vyombo vyahabari, hapana!

Mheshimiwa Spika, hata hii *clip* ameisema rafiki yangu pale Mheshimiwa Mbilinyi kwamba Mheshimiwa Rais alipigwa picha akiwa sokoni, sijui na nini; ni picha ya zamani. Sasa watu wakichukuliwa hatua kwa hilo ni kosa? Hilo nalo ni kosa? Ni dhambi? Wewe uchukue picha ya zamani wakati hakuna ugonjwa wa *Corona* ukaiweke kwenye *clip* kumdhalilisha Rais kwamba hajali kinachoendelea, halafu uachwe! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tena nashukuru, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe mpole kidogo, ingekuwa ni watu wa hatari kama mimi hivi, hata hilo gazeti lisingekuwepo. Lazima tufike wakati tuheshimu sisi kama Taifa letu. Nami naiomba Serikali, kwenye *online television* lazima muwe *serious*, huko ndiyo kuna madudu mengi yanafanyika na hakuna *control*. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hili ni eneo ambalo Serikali inatakiwa iangalie sana. Tusipokuwa makini tutakuja kuingia pabaya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, la tatu, nimesikia hapa pia, Dkt. Abbas ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari na ndio Msemaji wa Serikali. *In context*, Wizara ya Habari ndio Msemaji wa Serikali. Sasa leo mkisema tumemtoa Dkt. Abbas huku sijui mmempeleka huku, bado ana kazi yake ile ile ya Msemaji wa Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nitoe elimu kidogo kwa jambo moja tu. Nchi hii ina magazeti mengi sana na inawezekana ndiyo *leading country* katika Afrika pengine, ukitoa Nigeria labda. Nchi hii ina *televisions* nyingi sana na ina *radio* nyngi sana, sasa ni uhuru upi wa habari tunaouzungumza unaminywa katika Tanzania?

Mheshimiwa Spika, uhuru wa habari katika Tanzania ni mkubwa pengine kuliko hata Marekani, lakini leo tunalalmika kwamba hakuna uhuru wa vyombo vyya habari katika Taifa letu, kitu ambacho siyo sahihi. Mwandishi anapofanya kazi *as an individual*, anatakiwa kuwajibishwa kama yeye. Hawezi kuachwa mtu amefanya makosa eti kwa sababu tunaogopa kwamba, huyu tutaonekana hakuna uhuru wa vyombo vyya habari, *it is wrong!* Ni makosa.

Mheshimiwa Spika, nasi kama Wabunge tukifikia hatua tukaanza kushabikia mambo ya ovyo ovyo kama hayo pia sisi tutakuwa tunapotoka. Kwa sababu, tunaotunga sheria ni sisi; zinapokwenda kusimamiwa hizo sheria huko nje, tunaona kwamba kuna makosa yanafanyika. Kama kweli tunaona kuna makosa yanfanyika, tulete mabadiliko ya sheria hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kusimamia hiyo nidhamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilikuwa nataka nizungumzie ni suala la usikivu wa *TBC*. Tuna matatizo makubwa sana ya usikivu wa *TBC* hata katika Dodoma hii. Ukitoka hapa ukiwa unakwenda Babati, ukifika Haneti, pale mlimani, *TBC* inaishia pale pale. Mheshimiwa Kakoso ananiambia huko Mpanda ndiyo kabisa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Serikali ione sasa umuhimu angalau wanunue mitambo ya *Kv 5* kwa sababu, kuna *problem* kubwa ya hii mitambo ya *FM*, watafute mitambo ya *Kv 5* waifunge katika maeneo hayo ambayo hayasikiki; naamini usukivu utakuwa mkubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo Mundemu pale, kuna mtambo mkubwa, lakini ni *white elephant*, haufanyi kazi, umefungwa muda mrefu. Tunafanya? Tuna eneo kubwa pale Mundemu ambalo ni pori; tutafute fedha za kuweka mtambo wa *Kv 5* ambao nina hakika kwa *radius* ya kilometra 50 *uta-cover* karibu Singida. Kwa hiyo, Serikali iangalieni sana *TBC*. Huko mipakani lazima tuweke kwa sababu *TBC* ndiyo sauti ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *TBC* wanafanya kazi nzuri sana na kuna mabadiliko makubwa tunayaona. Kwa kweli, nami nampongeza sana Mwalimu wangu Rioba kuna kazi kubwa inafanya, lakini ipo haja sasa ya Serikali *ku-inject funds* huko ili tupate mitambo *Kv 5* tu; hata kama siyo tano, hata tatu tu zikifungwa kwenye baadhi ya maeneo nina hakika tutafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwenye michezo. Nami kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mbwana Ally Samata kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza *English Premier League* katika *Club* ya Aston Villa kule Birmingham, ametupa heshima kubwa sana kama Taifa. Naamini vijana wetu wengi wataiga mfano huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo tuna tatizo la ugonjwa wa *Corona* ligi karibu zote duniani zimesimama na hapa kwetu pia ligi imesimama. Kwa kuwa, Serikali iko hapa na wana nafasi nzuri sana ya kutusaidia, ipo haja pengine, tukiona hii hali inazidi kuwa mbaya, mwezi wa Nane zinaanza *Club Championship* za Afrika kama hali itatulia.

Mheshimiwa Spika, ligi ilipofikia ni pagumu. Ikiwezekana, timu inayongoza ligi ipewe ubingwa, halafu timu inayoshika nafasi ya pili ikashiriki FA. Najua wengi mtakasirika, lakini ndiyo ukweli kwamba Azam wale wanashika nafasi ya pili kwenye ligi, wakashiriki Kombe la Shirikisho halafu Simba akashiriki Klabu Bingwa Afrika, halafu hizi nyngine zitasubiri mwakani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa nakupongeza sana wewe binafsi, kuna mabadiliko makubwa sana katika masuala ya habari za Bunge. Na mimi nafarijika sana kuona kwamba, mambo ambayo tuliwahi kushauri miaka karibu saba iliopita yanafanyika leo ya Bunge kuwa na *TVyake*.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh kutoka Msekwa.

TAARIFA

MHE. DKT. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa msemaji kwamba wazo analolitoa ni zuri sana la ligi ilipofikia kuachwa lakini kwa kuwa mechi zilikuwa bado zipo, nimpe ushauri kwamba tutumie tu ile mechi iliokuwa kubwa ambayo Rais alishuhudia. Yule alireshinda ndiyo apewe kuwakilisha nchi kwa sababu hata Rais wa CAF alishuhudia bingwa wa Tanzania ni nani. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia unapokea Taarifa hiyo?

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, taarifa siipokei ila nimeisikia na najua rafiki yangu Mwigulu anazungumza hivyo kwa sababu timu anayoimiliki ya Singida *United* inashuka daraja. Kwa hiyo, pengine anaunga mkono kwa sababu anajua na yeye atapona kwenye timu yake ya Singida. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nilichokuwa nasema sasa kazi yenu ninyi hapa Bunge ni kuhakikisha kwmaba mnakuwa na *TV* yenu, mnakuwa na masafa ambayo itasaidia zaidi badala ya mtu kuja kulalamika humu ndani nataka *clip* yangu ataipata moja kwa moja kupitia Bunge *television*, ikiwa na masafa yake. Ana *tune* huko huko tu alipo. Hii habari ya kulalamika Bunge sio *live*, sio nini na kadhalika itakuwa imeisha na nafarijika sana kuona kwamba yale ambayo tuliwahi kushauri huko nyuma umeyafanya kazi. Nikupongeze sana wewe binafsi. Nimpongeze Naibu Spika, na nakuombea Mungu kule Kongwa wasikuguse guse. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja wa Wizara hii na nimpongeze sana Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Alhaj Juma Nkamia. Mheshimiwa William Mganga Ngeleja halafu tutarudi Msekwa kwa Mheshimiwa Tuhida Casian Gallos.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa fursa hii. Nianze kwa kusema wazi kabisa kwamba naunga mkono hoja na pia naipongeza sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwakayembe mwalimu wetu, Naibu Waziri Mheshimiwa Shonza, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Taasisi zilizoko kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Dkt. Abbas kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu katika Wizara hii. Hongera sana. Umahiri wa kazi zake tunaufahamu, wote tunashuhudia akiwa Msemaji Mkuu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kwa niaba ya wana Jimbo la Sengerema, tunazungumza tukiwa katikati ya majonzi, kuna misiba inaendelea kutokana na gonywa hili kubwa janga hili la corona, lakini pia kuna vifo vyta kawaida kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Sasa naungana na wenzangu kupeana pole na kufarrijiana na kuombea wenzetu waliotangulia mbele ya haki waendelee kulala mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, juu ya hiyo naongea hapa nikiwa Mbunge mwakilishi wa Jimbo la Sengerema lakini pia nikiwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*. Naomba nitumie dakika moja kuwashukuru Wabunge wenzangu wote pamoja na watumishi tukiongozwa na wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge letu tukufu kwa namna ambavyo ninyi kama viongozi wetu wakuu mmesimamia chombo chetu, Taasisi yetu. Mhimili wetu wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kutekeleza kwa vitendo kuhusu sekta ya michezo. Tunakupongeza sana kwa kipindi chako ushiriki wetu umekuwa ni *live* sana na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akujaalie tena tukirudi mwezi wa 11 kasi na *speed* iendelee ile ile kwa namna ambapo umeshiriki kwa vitendo kuonesha njia katika ushiriki na umuhimu wa michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ukisoma kwenye aya 100 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba; kwa sasa Wizara inaendelea kupokea maoni ya wadau kuhusu rasimu ya mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya michezo na kabla haujakamilishwa na kuzinduliwa rasmi basi mambo mengi wanatarajia watakuwa wameyapokea.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii nikiwa sehemu ya wadau wa michezo na ndiyo eneo ambalo nitajielekeza kwa sababu yapo mambo mengi na hatuwezi kuyazungumza yote kwa pamoja kuipongeza sana Serikali na hasa Mheshimiwa Waziri na Timu yake. Kwa kuja na hili na tunafahamu kwamba mkakati huu anaouzungumza unakuja kutatua changamoto nyingi ama unakuja kutoa suluhu za matatizo/changamoto nyingi ambazo zimejitokeza katika eneo hili la michezo hapa Tanzania. Sasa kwenye Taarifa yake Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yake na pia Taarifa ya Kamati na Kamati zote mbili natumaini yako baadhi ya maeneo ambayo wameyabainisha kama maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, moja tu niseme ni la kisera, kwa kadri ambayo itawezekana, Sera na Sheria zetu ziboreshwe ili kujiweka sawa kukabiliana na changamoto za wakati huu wa sasa kwasababu kama tulivyosema michezo sio tu suala la kuimarisha afya, lakini michezo ni ajira, michezo ni viwanda, michezo ni fursa ya uchumi wa mtu mmoja mmoja na kwa Taifa. Kwa hiyo, kimsingi michezo ni eneo pana sana ambalo linahitaji kuangaliwa kwa macho yote kama ambavyo tumekuwa tukiangalia maeneo mengine ya msingi.

Mheshimiwa Spika, uhitaji wa rasilimali fedha ni kubwa sana katika eneo hili. Kwa uchache tu kwa kutegemea bajeti ya Serikali, si rahisi sana kuzimaliza hizi changamoto zilizoko ndani. Hapa nina ushauri nikiendeleza hili ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumza katika aya ya 100 ya hotuba yake ya kupokea ushauri.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kwa sababu mahitaji ya rasilimali fedha ni makubwa, naomba tuifufue bahati nasibu ya Taifa. Bahati nasibu ya taifa ilikuwa inachezwa miaka ya nyuma na ninafahamu kama kumbukumbu zangu ziko sahihi na Mheshimiwa Waziri anaweza kunisahihisha baadaye, kwa mujibu wa sheria ile iliyoanzisha chombo kile cha bahati nasibu ya Taifa, Baraza la Michezo lina asilimia 50 pale kwa ajili ya uendelezaji wa michezo.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachokushauri hapo ni kwamba tufufue hiyo bahati nasibu ya Taifa, *National Lottery* lakini pia tusimamie kwa ukaribu sana yale mapato yatakayopatikana. Na katika kuifufua tunaweza kushirikiana na sekta Binafsi ambazo zimefanikiwa sana katika hii michezo ya kubashiri, tusijifungie sisi wenyewe tu kwa sababu uzoefu unatofautiana, hapa tunajenga nyumba moja hatuna sababu ya kugombania fito. Kwa hivyo nashauri kwamba tuifufue bahati nasibu ya Taifa lakini pia ikiwezekana tushirikiane na Sekta Binafsi, tuchukue uzoefu wao unaweza kutusaidia kutufikisha mahali pia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hii michezo ya kubashiri. Nafahamu, kama sio mwaka jana, mwaka juzi tuliboresha sheria tukasema hii michezo ya kubashiri sasa ichangie katika maendeleo ya michezo Tanzania. Lakini nafahamu kwamba kulikuwa na kanuni na ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, tumeshazungumza mara kadhaa na serikali, tukashauri mambo ya kufanya kuhusu maboresho ya Kanuni ili hilo likatengenezeke vizuri, namna ambavyo michezo ya kubashiri, hao wanaoendesha michezo ya kubashiri, *sports betting* wanaweza kuchangia pia katika uendelezaji wa shughuli za michezo nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu wa maboresho ya Kanuni ninafahamu kwamba sasa hivi Serikali inawasilisha magazeti ya Serikali hapa, sina hakika inawezekana katika haya ninayozungumza inawezekana mawasilisho ya Serikali yanayowasilishwa mezani hapa kwenye Bunge hili, hizi kanuni zipo lakini sina hakika kama tutapata dirisha kuzipitisha kwa Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kama itakupendeza, Kamati yetu ya Sheria Ndogo ipo, kwa magazeti ya Serikali yaliyowasilishwa ikiwemo Sheria Ndogo zilizotungwa na mamlaka mbalimbali za Serikali basi tuzipitie halafu wakati Bunge hili linahitimisha uhai wake, tuwe tumeshapitia tusiwe na vipro kwa sababu yapo mambo mengine yanaweza kuwa yanahitaji maboresha yakafanyika ili wananchi

wasiathirike. Hilo lilikuwa ni jambo moja, ambalo nadhani kwamba ni jambo la msingi kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, kwenye soka tumefanya kazi kubwa sana, pongezi kubwa sana kwa Serikali tukiongozwa na Rais mwenyewe Dkt. Magufuli, tumefanya kazi kubwa sana kuwa mstari wa mbele na tumeona mafanikio yake, nikichukulia mfano wa soka wote tunafahamu, mwaka jana tulifanikiwa kushiriki mashindano ya *AFCON*, michezo ya fainali za nchi za Afrika, lakini pia mwaka huu tulikuwa nadhani tutakwenda *Cameroon* hali ikitulia, ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, pia, timu ya soka ya wanawake, kubwa ninalotaka kusema pia katika ngazi ya vilabu, tunafahamu Simba *Sports Club* kwa kipindi cha miaka miwili, mitatu walichokifanya na hili linastahili pongezi. Ninafahamu kwenye majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atakuja rasmi hapa kusema neno kuhusu mafanikio yaliyosababishwa na Simba *Sports Club*, kutunyanya hadhi ya Taifa letu kwenye kigezo cha ubora na kiwango cha mpira kinachochezwa Tanzania. Leo *Simba Sports Club* ni mionganoni mwa timu 20 Afika kwa ubora lakini hata ukifuatilia kwa wanaofutilia michezo Simba *Sports Club* ni mionganoni mwa timu bora Afrika zenyenye washabiki wengi sana, sasa hili ni jambo la kujisifia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu sasa tunakwendaje kwenye ligi hii? Naungana na wenzangu, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Chumi na wengine akina Mheshimiwa Mwamoto, kusema kwa hali tuliyofikia katika mazingira ambayo tunayo, ni vyema tu kwamba bingwa akatangazwa Simba *Sports Club* kwa sababu tofauti ya *point* ni kubwa sana. Utopolo tuwaache waendelee na shughuli zao, mwaka kesho watakuja wajipange vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine katika hili, tunafahamu kuna wawakilishi katika mashindano ya Shirikisho na ndiyo alikuwa anaongelea Mheshimiwa Juma Nkamia. Nashauri kwa sababu mashindano haya kwenye ngazi ya robo fainali, naomba dakika moja nimalizie. Hizi ni timu nane

zinazoshiriki katika hatua hii na Simba wanaweza kuitoa tu ili kurahisishia kwa sababu imeshachukua ubingwa huku. Wanaweza kucheza *in isolation*, wakajifungia, wakawa *quarantined* ama yule mshindi wa pili kama alivyosema Mheshimiwa Juma Nkamia na Waheshimiwa wengine, Azam atuwakilishe lakini tutakuwa tumeshatimiza lengo kwamba tumekuwa nafasi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo nataka nizungumze ni maendeleo ya sanaa Tanzania. Tuko vizuri sana, tunaona muziki wetu, wasanii wetu wanaiwakilisha vizuri sana nchi yetu lakini ninachotaka kusema ni kujenga mazingira kwa sasa ya kutumia hii nguvu na ushawishi wa wasanii wetu katika kueneza fursa zingine za uchumi wa nchi yetu. Tunapita katika kipindi kigumu ambacho pia uchumi unakwenda kuathirika kwa vyovypote vile kwa sababu namba ni lazima ziathirike. Lakini Sekta moja inayooana sana na wasanii ni pamoja na Sekta ya Utalii kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa sababu tunafahamu Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikishirikiana na wasanii wenyewe ushawishi mkubwa, tuimarishe huo mkakati wa kuwatumia nguvu ya *digital platform*, hii mitandao ya Kijamii ni muhimu sana kuitumia kwa sababu wasanii wanafikika na wanafuatiliwa na watu wengi. Fursa moja tukiitangaza kupitia wao manufaa yake ni makubwa sana. Chukulia nyimbo zinazochezwa hapa na wasanii wa Tanzania ambazo zinasikika katika nchi zetu za Afrika, zinasikika katia nchi za mabara makubwa ikiwemo Amerika, utakuta kwamba wananchi ama watu wanaozifua tilia hizi nyimbo ni wa Mataifa mbalimbali. Msanii mmoja, kwa mfano Diamond, ukiangalia *instagram* hapa ana *followers* milioni tisa na wimbo wake alioimba na Mkongoman yule Inoss B umeshaangaliwa sasa hivi na watu zaidi ya milioni 82. Sasa unaweza kuona tu *impact* ya mtu mmoja tu. Tunao wangapi wa namba hiyo? Akina Ali Kiba, akina Nandy.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana na kwa hatua hii naomba kuendelea kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, sasa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Tauhida, kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kutoka kule kule Msekwa. Baadaye Mheshimiwa Musukuma atafunga shughuli zetu za uchangiaji jioni ya leo.

Mheshimiwa Tauhida tafadhalii.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niendelee kumpongeza Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo anafanya ndani ya nchi yetu. Pia kwa namna ya kipekee nikupongeze wewe mwenyewe binafsi pamoja na Naibu wako kwa kazi kubwa ambayo mnatufanyia.

Mheshimiwa Spika, hatuna neno la kusema juu yako, hukuwa Spika tu kwetu bali kwa watu wenyewe umri kama wangu na kushuka chini umekuwa baba na mlezi mwema na haya wanaweza kuthibisha. Dada yangu devote anaweza kuthibitisha na akina Salome wapo wanaweza kuthibitisha, Sugu pia anaweza kuthibitisha. Wewe si Spika tu kwetu, bali umekuwa ni mlezi na baba ambaye unajali maisha yetu. Ndani ya miaka minne na nusu yote umekuwa nasi kama baba.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache niweze kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa waliyoifanya ndani ya Wizara hii. Wizara hii imepiga hatua na imepata mabadiliko makubwa tumeona wakifanya kazi, wakijituma na si hayo tu, wamekuwa wako karibu na wasanii, wamekuwa msaada wa kutosha kwa wasanii, wamekuwa msaada wa karibu kwa vijana wa Tanzania. Niwapongeze kwa kazi kubwa waliyoifanya ndani ya wakati wao wa utumishi.

Kwa namna ya kipekee kabisa nivishukuru vyombo vilivyokuweko Tanzania. Nivishukuru vyombo vya habari, niipongeze *TBC*, *Star Tv*, *ITV*, *Azam*, *Wasafi*, *Radio One* bila kuisahau *ZBC* na vyombo vingine vyote vilivyopo nchini kwa kazi kubwa waliyofanya. Waliyyoshirikiana na Rais wetu na viongozi wetu kuhamasisha na kutoa maangalizo kwenye suala la Corona, wameitendea haki Tanzania. Yaani nizungumze walichokifanya ni Utanzania halisi, kwenye hili vyombo vya habari vimewajibika Kitanzania zaidi.

Mheshimiwa Spika, sio wao tu, wapo wasanii waliofanya kazi kubwa, waimbaji, wachekeshaji, kwenye suala la corona nchini wametendea haki nchi yao. Huo ndiyo Utanzania, kwenye suala la pamoja, lazima nchi tuwe pamoja. Hakuna anayerudi nyuma kwenye suala la corona, sote tuko kwenye killio kimoja na tukiomba usiku na mchana Mwenyezi Mungu atuondolee maradhi haya, tukiungana na Marais wetu wanavyotuongoza kwenye sala.

Mheshimiwa Spika, leo nina mambo mawili ambayo ninataka niyazungumzie. Jambo la kwanza nniombe sana Wizara, Serikali imehamia Dodoma na sehemu kubwa sasa ya nchi yetu ni Dodoma, Watanzania wanaiangalia Dodoma. Kati ya mambo ambayo ningetamani au Watanzania tungetamani kuona pamoja na kuona kwamba Mheshimiwa Waziri unakuja na suala la kujenga nyumba ya kumbukumbu ndani ya Dodoma, itasaidia jumba la kumbukumbu likijengwa Dodoma lijengwe kwa ufanisi na likijengwa ikionesha ni sehemu ambayo pia vijana wanaweza kwenda kutembelea.

Mheshimiwa Spika, kuna nyumba za kumbukumbu, Zanzibar zipo, Dar es Salaam zipo na ninaamini kuna sehemu nyingine za ndani ya Tanzania zipo nyumba za kumbukumbu. Kuna nyumba za kumbukumbu tunaweza kuziongelea kama magofu ya kihistoria, ninazungumza nyumba za kumbukumbu ambazo tunaweza tukaweka jengo kama Watanzania likawepo Dodoma na tukachukua baadhi ya kumbukumbu zetu maana kuweka kumbukumbu zetu ni moja ya

utamaduni ambao tunaweza kuweka historia ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia muda wote tukiweko Bungeni kuna makundi ya vijana wanafunzi wa shule wanakuja ndani ya Bunge kwa ajili ya kujifunza. Wanapokuja kujifunza basi wapate fursa nyingine ya kipekee kwamba wanaweza kwenda kutembelea jengo la kumbukumbu ya Tanzania. Bila ya kuacha kwamba ndani ya kumbukumbu hizo si vibaya kukakuweko na historia mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kuonesha utamaduni wa Mtanzania, kuonesha kwamba ndani ya utamaduni ule, ndani ya nchi yetu kutoka ndani ya makabila tofauti tofauti. Naweza kusema unaweza ukachukua Wagogo, utamaduni wa Kingoni, utamaduni wa Kizaramo, kila tamaduni au kila kabilo zina asili yake. Ukija kwenye mavazi, ukija kwenye makaazi, walikuwa na asili yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, utakapoweka nyumba hii, faida tutakayoipata ni kubwa, faida ya kwanza, wananchi au vijana wa Tanzania wanaweza wakasoma historia ya nchi yao isiyopotea. Wanaweza kusoma historia ya nchi yao endelevu, pia ukiacha hilo Mheshimiwa Waziri, tunaweza kutengeneza utalii ndani ya Dodoma kwa maana historia kubwa na historia ambayo inajitegemea ambayo tunataka kuiweka ndani ya jengo hilo hata kwa njia ya picha kwamba kuna picha zinaweza zikapigwa zikawekwa, kuna vitu ambavyo vinaweza vikatengenezwa kuonesha humu ndani kuna kumbukumbu ya watanzania. Ukiacha maeneo mengine ambayo kuna kumbukumbu hizo.

Mheshimiwa Spika, ninategemea kwamba licha ya watalii kuja kwenye kumbukumbu hizo pia kutakuwa na suala la ajira ndani yake, kuna ajira ambazo zitajizalisha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la utamaduni kwa vijana ambao kwao litakuwa endelevu kujua historia ya nchi yao. Hata tukiweka nusu ya historia ya Mapinduzi, tukiweka

nusu ya historia ya Muungano, tukiweka vitu ambavyo vitafanya nchi yetu kuendelea zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia hili litajenga uzalendo kwa vijana Watanzania, unapomchukua kijana wa Tanzania, ukampeleka kwenda kusoma historia ya nchi yake maana yake umepandikiza uzalendo ndani yake. Ninatamani jengo hilo liwe katika usimamizi wa Wizara ya Habari kwasababu utakuwa umetunza utamaduni wa Mtanzania. Utakuwa umetunza mila za Kitanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, tutaweza kupata mapato mengi. Kuna muda tunaweza tukapata mapato kupitia watalii lakini lile jengo tunaweza tukaweka kiasi cha fedha kidogo ili wanafunzi na walimu waweze kuendelea kupata huduma ndani ya jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, nijielekeze pia kwenye suala la wasanii. Serikali yetu imefanya mambo mengi, Waziri amesimamia mambo mengi makubwa ndani ya nchi yetu. Niombe kwa jinsi ya kipekee Wizara yako inaweza ikaangalia namna gani tunaweza kuwaongezea nguvu wasanii wa Tanzania, kwa kusema wasanii maana yake tunawatambua. Leo tukisema msanii mkubwa Tanzania harakaharaka tutawataja Diamond, Ally Kiba, Ommy, wapo wengi hao nimewatolea mfano lakini kwa upande wa Waziri hebu jaribu kutengeneza kitu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakuja na kama maoni kwako tunaweza tukaangalia, je, katika hizi *passsport* tunazozitumia nchini, hatuwezi kuwapa *passport* ya kiutumishi kumuonesha kwamba huyu ni msanii mkubwa ndani ya Tanzania na tunamtegemea kuiwakilisha Tanzania. Kama litakupendeza na litakuwa jema ndani ya Serikali yetu, tuone eneo hilo tunaliwakaje vizuri. Leo tunasema Diamond au Ally Kiba au kina Ommy wanakwenda kutuwakilisha kama Watanzania walau kuwe na kitu kitakachowapa moyo na nguvu kuonesha kwamba mimi ni msanii ninayetoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini faida yake si kumpa moyo tu lakini jambo lingine tutatunza nidhamu na heshima ya wasanii. Endapo msanii atakayepatiwa *passport* hiyo ya kiutumishi labda anakwenda kinyume na maadili ya Watanzania, anakuwa hana nidhamu za Kitanzania lazima msanii yule anyang'anywe *passport* ile au awajibishwe.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Tauhida, muda wako umeisha.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, hii italeta ari na muamko kila msanii atataka walau afikike lile lengo la kupata nguvu zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Tauhida muda haupo upande wako, ahsante

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, kwa hayo maneno machache, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida Cassian Galos kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na bado wachangiaji wawili ili tumuite Mheshimiwa Waziri. Naona watu wengi mnamtolea macho sana Mheshimiwa Waziri Mpina, yuko vizuri, ni kwamba huo ndiyo utaratibu unavyotakiwa uwe. Sasa nashangaa mnashangaashangaa hivi, Mheshimiwa nakupongeza sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ambaye yupo kule Msekwa.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema kiongozi wetu Mtume Muhammad (*Sallallahu Alaihi Wasallam*).

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Habari kwa kweli ni nyeti, inatuhabarisha habari nyingi za nchi yetu na za nje ya nchi yetu, kwa hiyo mnastahili sifa. Ni lazima tuwapongeze Waziri, Naibu Waziri pamoja na watu wote wa habari kwa kazi nzuri wanayoifanya kutuhabarisha Watanzania na wengineo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nchi yetu au dunia imeelemewa na *Corona*, hili ni janga la kitaifa na dunia na kwa kweli nchi na dunia imetikisika na uchumi umetikisika, nchi imeingia hofu, *wallah* hii ni bakora ya Mwenyezi Mungu. Maradhi haya hayana tiba ila ni maelekezo na kufuata taratibu tunazopewa na wataalam wetu wa afya. Kwa kweli ni mtihani mkubwa, hii ni bakora Mwenyezi Mungu haleti jambo ila tukiwa tumemkasirisha. Yawezekana tumefanya makosa, kuna nchi zimehalalisha hata ndoa ya jinsia moja, hili ni kosa ambalo hata kwenye kitabu chochote hamna. Kuna dhuluma zimeenea katika dunia na kuna mambo makubwa makubwa, kwa hivyo, lilitobakia ni kumlilia Mwenyezi Mungu ili atuondolee janga hili. Hili ni janga la dunia ambalo halina dawa.

Mheshimiwa Spika, tukiacha hilo, tumekumbwa na mafuriko, nchi nzima inatikisika. Kila mkoa watu wanakufa, vyakula vinasombwa na maji, yote hii ni bakora ya Mwenyezi Mungu. Nasema turudi kwa Mwenyezi Mungu kumlilia ili atuondolee janga na maafa haya yaliyotufika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari ni nyeti na kila siku tunaililia sisi inapewa bajeti ndogo, si hapa safari hii imeongezwa lakini pamoja na kuongezwa bado haitokamilisha mipango yake. Kuna viwanja chungu nzima ambavyo havijaendelezwa kwa kukosa fedha, tunategemea za wafadhili lakini si haba pengine mara hii tutaanza kuvijenga viwanja vyetu ili kuboresha tuliyoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, chombo cha *TBC* ni cha Taifa, alizungumzia mwenzangu hapa. Ni chombo ambacho

tunakitegemea na kinalipiwa na wananchi lakini bado hakisikiki katika mikoa mingi sana hata Zanzibar, Pemba kule hakisikiki na mikoa mingine amesema Mheshimiwa Nkamia ambaye ni Makamu Mwenyekiti wangu, kwa kweli hiki chombo kinatakiwa kiboreshweli ili kisikike nchi nzima hasa kipindi hiki kinachokuja cha uchaguzi keshokutwa kila mtu atakuwa ana hamu kusikia yaliyopita na kitende haki kwa vyama vyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Dodoma ni kitovu au Makao Makuu ya nchi, inasikitisha kuwa mpaka leo magazeti yanatoka Dar es Salaam asubuhi yaletwe hapa na ndege. Kwa nini Serikali inashindwa kutoa fedha ili kufunga mtambo hapa Dodoma magazeti yakatoka hapahaha Dodoma na machapisho mbalimbali ili Serikali iweze kupata mapato mbalimbali, ni kwa nini hawafanyi hivyo? Kwa hiyo, tunaomba Serikali isogeze kila kilichokuwa kinahitajika Dodoma maana ndege pengine ikiharibika magazeti hayafiki, wakati mwingine yanachelewa. Kwa hivyo, nawaomba Serikali hili lifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara ya Habari ni nyeti na *TBC* walisema kuwa wana upungufu wa wafanyakazi. Kwa hivyo, wajitahidi ili wanapopata fedha za bajeti hii waongeze wafanyakazi ili iweze kufanya kazi zake vizuri na mikoa yote iweze kusikika.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi sina mengi, nimechangia machache tu, ahsanteni. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika. Sasa mchangiajai wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, karibu sana Mheshimiwa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, nimpongeze Msemaji Mkuu wa Serikali Dkt. Abbas ambaye pia ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Watanzania tunafahamu kazi ambayo ameifanyia nchi yake na katika kipindi cha Awamu ya Tano amekuwa msemajii mzuri wa Serikali katika mema lakini katika hata mishale kwa

kuwa amekuwa msemaji wakati Tanzania nayo imeshakuwa kwenye digitali, vijana wameelimika.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nikumbushe mchango wangu wa mwaka 2018/2019 wakati wa bajeti nilzungumza humu ndani nikasema katika sehemu ambayo Wizara imefeli ni Wizara ya Michezo hususani kwenye kitengo/upande wa filamu. Nikasema wasanii wetu waliokuwa maarufu sasa wamegeuka kuuza madanguro na wengine kujiza kwa wanaume wa jinsia moja lakini nilionekana muongo hapa na nakumbuka Mheshimiwa Shonza, Naibu Waziri alisimama akasema nithibitishe, ilikuwa tarehe 22.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 niliwaleta wasanii na mashirikisho yote na Mheshimiwa Waziri Mkuu akatusikiliza na Mheshimiwa Juliana akiwemo bahati mbaya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe hakuwepo. Moja ya mambo yaliyozungumziwa, yeye aliulizwa swalii na Waziri Mkuu ungekuwa wewe ungefanyaje? Tasnia hii *totallywasanii* wote walimlalamikia aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Mama Fissoo, hakuna hata mmoja aliyemtetea. Waziri Mkuu akamuuliza Naibu Waziri kwamba ungekuwa weve ungetoa jibu gani. Akasema kwa kweli huyu haiwezekani Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilikuwepo ilikuwa mchana na Waziri Mkuu akatoa maagizo atolewe kwenye nafasi ile.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha baada ya kuagizwa kumtoa kwenye nafasi ile kwa sababu ameua hii *industry*, baada ya muda mchache sasa ndiyo Mkurugenzi wa Utamaduni. Maana yake agizo la Waziri Mkuu lilipuuzwa na badala yake akapewa zawadi. Maana mashirikisho yote, hauwezi kupitisha sera yoyote, kwa sababu hawa walioteuliwa kuchukua nafasi yake sasa yeye amewekwa mkubwa wao lazima *document* zote zipite kwao halafu ndiyo ziende kwa Katibu Mkuu. Hii kitu haiwezekani, kwanza, ni kumdhaililisha Mheshimiwa Waziri Mkuu. Cha pili labda watueleze walikaa kikao gani na waliona mbinu gani mpya zilizowafurahisha kama Wizara wakaamua kumpandisha cheo badala ya kumshusha kama alivyoelekeza Mheshimiwa Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, ungekuwa unaweza kupita huko mtaani bila ving'ora wasanii wa Tanzania ulikuwa unawajua wanang'aa, wale ulikuwa unaona picha za zamani, wana ukurutu hata Musukuma anang'aa leo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe akisimama hapa, hili nipo *serious*, atuambie ni kanuni gani alizotumia kum-*promote* Mama Fissoo? Wasanii wanamsikia Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe akiwa unajibu, tutachukua *Hansard* au hata sauti ili na wao wasikie, ni kitu gani kilichomfanya kumuona yeche ana mbinu mpya akaamua kumpandisha cheo ilhali mashirikisho yote kule *UDOM* yalimkataa Mama Fissoo na Waziri Mkuu akamuondoa kwenye nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mama Fissoo huyu huyu ndiye ameshiriki kutengeneza Kanuni za mwaka 2012, zikaua kabisa tasnia ya *Bongo Movie*. Hata tungepiga debe namna gani kama hatujabadilisha kanuni, hatuwezi kwenda popote. Mheshimiwa Waziri anafahamu, Waziri Mkuu alitoa maelekezo 21 lakini moja ya elekezo la muhimu ilikuwa ni kwamba wabadirilishe kanuni mpaka leo toka mwezi Aprili, 2019 ameshapelekewa sijui hasaini kwa sababu gani, labda kama atakuwa na sababu.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutusikiliza, wafanyabiashara tulienda kwenye kikao na Mheshimiwa Rais kule Ikulu. Moja ya mambo ambayo tulimuomba, ni wasanii wenyewe waliomba kwa Waziri Mkuu kwamba kuna mtu ambaye alikuwa tayari anawa-*promote* wasanii anaitwa Kampuni ya *Steps*, alikuwa na kiwanda cha kutengeneza vitu vyote kama huko china. Kwa sababu ya kamisheni za akina Mama Fissoo wakazunguka huko wakam-*disturb* mpaka akafungiwa na *TRA*. Mheshimiwa Rais alitoa msamaha pale wa shilingi bilioni 3 kiwanda kifunguliwe na *TANESCO* wakaenda wakatoa msamaha wa shilingi milioni 10, wewe mpaka leo unalazimisha mtu afungue kwa kanuni mbovu.

Mheshimiwa Spika, pengine Mheshimiwa Waziri hamkupitia kwenye biashara, mmetoka vyuoni na kupata

veyo, hebu jivishe wewe leo ungekuwa unaendesha hiyo biashara labda ya bilioni 10, Mheshimiwa Rais kafuta kodi, *TANESCO* wamefuta deni la milioni 10, wewe kusaini tu *document* watu waingie mtamboni mpaka leo mwaka mmoja, siyo sahihi. Mambo mengine yanauma najua Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ni rafiki yangu lakini leo utanisamehe nishughulike kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma kwenye ukurasa wa 29 unasema mnafanya jithada ya kuyaunganisha mashirikisho *COSOTA*, *BASATA* sijui na Bodi ya Filamu halafu unayaunganisha ili yakamsaidie nani watu wote wameshafilisika? Hii kitu inauma sana na ninamuomba Msomi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe aliangalie suala hili ili kuwasaidia wasanii.

Mheshimiwa Spika, wasanii tulivyoalikwa na Mheshimiwa Rais pale Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Rais kwa kuguswa na wasanii alitoa shilingi milioni 100 mpaka leo kuzitengenezea utaratibu hajawezekana. Unawaambia wasanii na mashirikisho ya filamu eti leteni mpango kazi, watu hawana ofisi, hawana hata mia moja mfukoni wala katiba wanakaa wapi kujadili na kuandika mpango kazi?

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kiukweli kama heshima yako inataka kushuka ni kuacha hili Taifa limeua hii *industry* ya sanaa hasa *Bongo Movie*. Ninyi Wabunge wenzangu mnafahamu kabisa kwamba tasnia hii ilikuwa inachukua watu wa rika zote wenye vipaji hata wa darasa la saba, ilikuwa imeajiri watu kibao. Leo tunaiua mikononi mwako msomi mkubwa wa chuo kikuu. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe lazima ukisimama hapa usimame na vitu vizuri ambavyo vitatushawishi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu waganga wa kienyeji...

TAARIFA

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma unapewa taarifa na Mheshimiwa Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu taarifa Mheshimiwa Joseph (wajina) kwamba kwa utaratibu Rais akiahidi kama vile akisema nawapa wasanii shilingi milioni 100 ili utekelezaji wa fedha hizo ufanyike ni lazima Katibu Mkuu Kiongozi aandike dokezo, vinginevyo tutawalaamu watu wa chini tu.

Mheshimiwa Spika, hii nimeijuaje? Nimeijua kule Mbeya, kule Mheshimiwa Rais aliahidi barabara kilometra 10 lakini mpaka leo zile barabara hazjajengwa. Nikamfuata Waziri wa Ujenzi nikamwambia kwa nini Rais ameahidi barabara kwa wananchi halafu ninyi hamtekelezi mnataka ashindwe kuja kuomba kura 2020? Akanipa huo utaratibu kwamba kwa utaratibu Rais akiahidi ni lazima Katibu Mkuu Kiongozi aandike dokezo, asipoandika dokezo hiyo hela haitoki na mtawaonea hao wa chini. (*Makofii*)

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa yake siipokei kwa sababu yeye alishatoka kwenye usanii sasa hivi ana-*deal* na Ubunge. Tayari pesa hiyo ilishatoka na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe yupo hapa kama shahidi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumza kuhusu waganga wa kienyeji, naungana na juhudini zote za Serikali. Leo nimeshangaa sana kuna mama mmoja, dokta yule amezungumza akiwa Msekwa, cheupe yule Mheshimiwa Tisekwa. Unajua kupuuza hivi vitu mkaamini sana sayansi wakati mwagine ni matatizo. Katika janga hili la *Corona* tunashukuru Serikali imeelekeza watu waende kwenye ibada lakini tutafute na jitihada binasfi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dunia nzima haijagundua dawa ya Corona na mfano mzuri huwa tunautolea kwa Mheshimiwa Dkt. Kalemani kwamba ana dawa ya kutibu mifupa, mtu aliyevunjika anamtibu ndani ya

wiki moja, sijui kama mnanielewa? Hii teknolojia ya Mheshimiwa Dkt. Kalemani ingekuwa iko Marekani huyu mtu asingekuwa na sisi hapa, hakuna mtu anataka kufungwa muhogo. Hata Mheshimiwa Mdee namshangaa, toka nenda kwa Mheshimiwa Dkt. Kalemani utupe hogo lako hilo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ndiyo unalea hawa waganga wa kienyeji, kwa sababu dunia haijagundua dawa lakini sisi watu wa imani tunaamini viro vitu ambavyo vimewakuza hata ninyi tujaribu hivyo. Naona mnaanza kunielewa kwa sababu leo nimeona Mheshimiwa Dkt. Tiise kwa msomi mzima amefanunua kidogo, hajaingia ndani amesema anayaelewa na mkinipingapinda hapa si tunaenda uchaguzi wanawasikiliza waganga wa kienyeji.

Mheshimiwa Spika, nakuomba tutafute *modality* yoyote nzuri kwa sababu wapo wataalam wanaoweza siyo watabiri. Tuangalie matabibu wanaoweza kujaribu, kwa sababu sasa hivi tunajaribu mara maji ya betri, mara hiki; hata wasomi wenyewe mmechanganyikiwa. Kwa hiyo, tujaribu na hawa watu watabibu hawa tuwape angalau wagonjwa wawili/watatu tuone majoribio. Kama Tanzania tunaweza kugundua hii dawa ya kutibu *Corona ni deal*.

Mimi naona kama mnawabana waganga hamuamini kama kuna dawa wakati waganga hawa wa kienyeji wana uwezo wa kumlaza hata Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kaka yangu Lukuvi hapa asiweze kusimama mpaka uchaguzi unaisha, kwa nini msiwape nafasi kwenye hilli tatizo la kidunia? Kama kuna uwezekano, tunajaribu, maana hata huko hospitali naona watu wanabambanya tu mara *chloroquine*, mara nini, naomba tuweze kuwapatia nafasi watu hawa nao wajaribu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makof*)

Sasa naona kama mnawabana waganga hamuamini kama kuna dawa, wakati waganga hawa wa kienyeji wanauwezo wa kumlaza hata Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kaka yangu Mheshimiwa Lukvi hapa akalala, miguu hawezi hata kusimama mpaka uchaguzi unakwisha. Kwanini msiwape nafasi kwenye hili tatizo la kidunia?Kama kuna uwezekano tunajaribu, maana hata huko hospitali naona watu wanabambanya tu mara *chloroquine* mara nini. Naomba tuweze kuwapatia nafasi hawa watu na wao waweze kuona.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma kwa ushauri wako hasa huu wa mwisho, ni kweli Mheshimiwa Musukuma *mentality* za elimu ya Magharibi imetuhabusana. Nilishakutana na msomi mmoja kwa mfano ameshafanya utafiti *deeply* na kutoa dawa fulani ambayo anashawishi kabisa kwamba hii inaweza kuua *virus* wa aina hii ambayo katika *group* hii ya *viruses* hata huyu *Covid* sifa zake nyingi zinakuwa hapo na anasema mimi sizungumzi hili ili nipate *patent* niweze kufaidikana kutokana na hivi *no nitaitoa* kama *contribution* kwa nchi, Serikali yenyelewe itajua nini cha kufanya mradi itibu *humanity*.

Tukasaidiana naye kidogo na nini tukajaribu *NIMR* na wapi, sitaki kusema sana hapa, lakini kila mkubwa anayehusika na mambo haya yuko *busy*, kila mmoja yuko *busy*, kila mmoja yuko *busy*, lakini ni *scientific research* tena *ame-publish* siyo kwa maana ya *Covid 19* amesha-*public scientifically* na *papers* *naziona*, *papers* ambazo watu wengi wanajiita wasomi hapa, lakini ukiitazama ile kuelewa ukurasa wa kwanza, wa pili, watatu ujikunje, vinginevyo kama hukufanya *chemistry* angalau hata ya *form six* huwezi kuona chochote pale ndani. Watanzania na Waafrika sisi sote tume-*resign*, tunasubiri mzungu ndiyo afanye haya mambo atuletee dawa.

Kwa hiyo unachokisema ni kweli yaani waganga wa kienyeji au tiba ya kienyeji sisi *indigenous knowledge* hii hatuipi uzito na umuhimu unaotakiwa, lakini tusikate tamaa tuendelee kuishauri Serikali katika eneo hilo. Ni eneo ambalo Waafrika tunalo na tunafaida nalo kubwa sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nashUkuru sana kwa nafisi hii na nianze kwa kumpongeza mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matuamini katika Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, nianze na usimamizi wa soka katika na nchi yetu, Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*) limekuwa na usimamizi wa ligi kuu na ligi nydingine za daraja ya chini. Ligi imekuwa inabadili kanuni bila ushirikishwaji mzuri wa wadau, kwa kwa mfano kuongeza timu katika 16 mpaka 20 bila ya kufanya utafiti wa kutosha na ushirikishwaji wa wadhamini na kupelekeea ligi kutokuwa na wadhamini kwa miaka kadhaa. Mfano mwengine in kanuni ya ruhusa ya wachezaji wa kigeni ambayo imekuwa ikibadilishwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye hili Mheshimiwa Waziri ukae na kuwashauri *TFF* wawe na kitengo cha utafiti.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ligi ya wanawake. Eneo hili tumeonesha kuwa na mafanikio makubwa sana na hamasa ni kubwa. Ushauri wangu *TFF* iimarishe ligi ya wanawake kwenye ngazi za chini na mashulenii, nchi yetu ina vipaji vingi sana, hili ni eneo la kuweka mkazo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kuboresha *TBC* zaidi ili waweze kutoa huduma bora. Aidha, waone namna ya kutoa habari za Wizara zetu kwa kina zaidi ili wananchi waweze kufahamu mafanikio ya kisera kwa kina.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ione namna ya waandishi wetu wa habari na hasa vyombo vyetu vya Serikali wawe na ubobezi wa kuandika na kuripoti masuala kuhusu sekta mbalimbali, mfano kuwe na wabobezi katika uwekezaji, sekta binafsi na sekta nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwenye mafanikio katika sekta ya habari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, nianze na *TBC*; Shirika hili linaendeshwa kwa kodi za wananchi na kimsingi ni mali ya Watanzania lakini kwa kipindi kirefu sasa Shirika hili linatoa huduma kwa upendeleo wa wazi na hata kutumia muda mwingi kutangaza habari za Chama Tawala, hii inaleta mgawanyo kwa walaji na kupelekea wengi wetu kuangalia televisheni nyingine.

Mheshimiwa Spika, kusikika kwa redio na televisheni sehemu nyingi hasa Wilaya ya Rungwe maeneo ya Ilia, Bujela, Itagata na Swaya kumekuwa na shida kidogo, tunaomba Wizara hii iongeze mitambo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matangazo ya televisheni na redio, kunapokuwa na maafa au majanga unaona wao wanaendelea na matangazo ya kawaida, tunaomba watumie muda huo kuelezea umma wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wasanii, binafsi naomba sana Wizara isimamie maadili ya wasanii wetu kuheshimu tamaduni zetu na si kila msanii lazima avae uchi au aige watu wa nje ya nchi nadhani tuwe na mfumo na muongozo kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchezo wa ngumi, naishukuru Wizara kuunda Kamisheni ya Ngumi ili isimamie haki za mabondia. Naomba Wizara iongeze kitengo kitakachowatetea mabondia wa kike na haki zao za kimsingi hasa kupata chao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja vyatya michezo Wilayani; Wilaya ya Rungwe hatuna viwanja vizuri vyatya michezo hivyo kutoweza kupata vipaji vyatya watoto hasa kwenye soka na *netball*.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa fursa ya kuchangia na naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, licha ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri Harrison Mwakyembe na timu yake yote kwa kazi nzuri sana wanazofanya, nikuombe upokee malalamiko ya wananchi wa Namtumbo kuhusu Wizara hii. Wanalalamikia kutowaleta mawasiliano ya sauti (TBC Taifa) na wala mawasiliano ya video (*TBC One*) hususan maeneo yote ya Taraifa za Sasawala na sehemu kubwa za Taraifa za Undendeule na Kata chache za Taraifa ya Mkongo. Wananchi hao hawapendezewi kabisa wanavyolazimika kusikiliza midundo ya muziki kwenye redio za nchini Msumbiji na ama Malawi. Ingawa midundo hiyo ni ya kufurahisha na inaamsha hisia nzuri, lakini watu hao hawapati fursa ya kuungana na Watanzania wenzao na kujenga utamaduni mmoja wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumuomba Waziri Mwakyembe, shemeji yangu atusaidie Wananaamtumbo katika kuwawezesha kusikiliza babari na burudani za vyombo vyatya habari vyatya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na nawasilisha.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba suala la michezo inayofanyika katika uwanja, mapato yanayopatikana faida kuwe na gawio kwa Halmashauri ya Temeke au Serikali ili iboreshe huduma za afya kama vile Kituo cha Afya cha *DUCE*, ambacho kinapokea wagonjwa wa dharura wanaokuja kuangalia michezo na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na hotuba ya bajeti nzuri. Nawapongeza kwa jinsi mnavyoendelea kuhakikisha watu wanaendelea kupata maudhui bila malipo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri bado kuna tatizo la usikivu wa *TBC*. Ni haki ya msingi kwa Watanzania wote waweze kupata habari kuititia kwenye Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*). Pamoja na kuwa usikivu kwa *TBC* umefikia 54%, bado yapo maeneo mengi kama Ngara, Kyerwa kule Kagera ambapo *TBC* haisikiki. Ni vema Serikali iwapatie Wizara ya Habari fedha za kutosha ili waweze kufanikisha mawasiliano na kufikisha habari nchi nzima kuititia *TBC*.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili Tanzania wana jukumu kubwa la kukuza Kiswahili ambacho kwa sasa ni bidhaa adimu. Kwa vile watu wengi sasa hapa duniani wameamua kutumia Kiswahili, ni lazima BAKITA wapewe fedha za kutosha ili waandae wabobezi kwenye Kiswahili na tuwe na wakalimani, watafsiri na walimu wa Kiswahili wengi zaidi. Mwisho naendelea kuwapongeza kwa jinsi mnavyoendelea kuboresha na kurusha maudhui yenye kutangaza vivutio vya utalii nchini kuititia *Safari Channel*.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yangu itoe bajeti ya kutosha kwa Wizara hii ili waweze kuandaa wanamichezo wazuri na wengi katika nyanja mbalimbali, kwani wote

tunatambua kuwa michezo, sanaa ni ajira. Pili wakipewa bajeti ya kutosha wanaweza kuboresha viwanja vyta michezo Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa na mimi niweze kushiriki na kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya mwaka 2020/2021 iliyopo mbele yetu. Hotuba hii inakwenda sambamba kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 kama ilivyoelekeza katika sekta ya michezo, utamaduni, sanaa na habari. Aidha nitumie pia nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa upatikanaji wa habari zilizo sahihi kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, kuhakikisha uhuru wa habari unaendelea kustawi, aidha naipongeza Serikali kwa usimamizi ulio sahihi kwa vyombo vyote vyta habari nchi nzima kwa kufuata taratibu na sheria hasa katika utoaji wa habari na uendeshaji wa vyombo hivyo. Sisi sote ni mashahidi hasa pale baadhi ya vyombo vyta habari vinapokiuka baadhi ya masharti tumeona mamlaka husika zikichukua hatua mbalimbali ili kuwakumbusha kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kuishauri Serikali kuendelea kuwakumbusha baadhi ya vyombo vyta habari kutoa habari zilizo sahihi, uandishi wenye tija na faida kwa nchi, kuwakumbusha waandishi wa habari kuwa wazalendo kwa nchi yao pindi wanapoandaa habari na kuitoa kwa wananchi. Waandishi ni watu muhimu sana kwani huweza kubomo au kujenga hasa wasipokuwa makini katika utoaji wa habari basi wanaweza kuipeleka nchi katika majanga, lakini wakiwa na weledi na uzalendo katika utoaji wa habari hakika watalipeleka Taifa lao mbele na kulipa sifa.

Aidha Serikali iangalie namna ya kuvikumbusha vyombo vyetu nya habari nchi nzima namna ya kutenga muda kwa ajili ya kuitangaza nchi yetu hasa katika rasilimali nzuri tulizonazo, hii itatusaidia sana hasa katika nyanja mbalimbali za kiuwekezaji hapa nchini kujulikana na vivutio vizuri tulivyokuwa navyo.

Mheshimiwa Spika, michezo sasa ni ajira, imesaidia sana vijana wetu hasa wenyе vipaji kutumia michezo na kujipatia kipato, ni wajibu wetu sote kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu hasa katika jitihada mbalimbali inazochukua katika kuendeleza shughuli za michezo hapa nchini. Naishauri Serikali kuendelea kusaidia wanamichezo wetu pindi wanapokuwa katika maandalizi ya kujandaa na mashindano ya kimataifa ili kuwapa moyo na hali. Hata hivyo kuna haja sasa Serikali kuweka mkazo hasa katika kukuza vipaji kwa vijana wetu ili kupata wanamichezo bora watakaokuja kuliletea Taifa letu sifa hapo baadae.

Mheshimiwa Spika, sanaa ni kitu kikubwa sana na kina wigo mpana, sanaa zimekuwa zikitumika kama kitambulisho kwa baadhi ya nchi, sisi kama Taifa tumebarikiwa kuwa na wasanii mbalimbali hasa katika tasnia ya uchoraji, uchongaji na kadhalika, lakini baadhi ya wasanii hawa wamekuwa wakikabiliana na changamoto mbalimbali hasa kutokutumika vizuri kwa Taifa lao katika baadhi ya kazi zao wanazozitengeneza.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa kuangalia namna ya kuzidisha ukaribu na wasanii wetu hasa kwa kuwatumia katika kazi mbalimbali, kuzitumia kazi zao ili waweze kufaidika na vipaji vyao, pia waweze kuitangaza nchi yetu hasa kupitia sanaa zao. Tuna wasanii wanaoimba aina tofauti ya miziki, hawa pia ni sehemu ya watu ambao ni wajibu wetu kama Serikali kuwatumia katika kuitangaza nchi yetu duniani.

Mheshimiwa Spika, kila Taifa hapa duniani lina tamaduni yake, hakika Tanzania yetu tumebarikiwa kuwa na tamaduni mbalimbali za kuvutia sana, naishauri Serikali

kupitia Wizara kuhakikisha tunaendelea kudumisha tamaduni zetu na kuzitangaza.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuendelea kudumisha tamaduni zetu kwani zimekuwa na tija kubwa kufuatana na historia ya nchi yetu na watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuchangia kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Bunge Iako kufuatia msiba wa Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare na mwanahabari nguli Marin Hassan Marin na watangazaji na wafanyakazi wengine wa *TBC* ambaao wametangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na kuwaweka mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza viongozi wote wa Wizara chini ya uongozi wa Waziri Dky. Mwakyembe, Naibu Waziri Mheshimiwa Shonza na Katibu Mkuu Dkt. Abbas kwa kuwa makini na kusimamia Wizara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa mabadiliko ambayo yanaendelea pale *TBC* chini ya uongozi wake Mkurugenzi Ayoub Ryoba.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa umakini na kusaidia kuweka mambo sawa pale panapoonekana pana hitilifu.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara kupitia *TBC* na vyombo vingine vya habari kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kutoa elimu ya Corona na pia kazi kubwa inavyofanywa na Serikali katika kutimiza ahadi zake chini ya llani ya CCM na juhudhi za Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kila eneo ambalo nimefika.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inahitaji kuangalia kwa umakini sana eneo la Shirika lake la *TBC* ambalo linakabiliwa na uhafifu wa mitambo na pia bado kuna maeneo usikivu wake ni hafifu au haupo kabisa. Mara nyingi nimekuwa nikiuliza maswali juu ya hilo na kupata majibu kwamba linashughulikiwa lakini bado hali haiko sawa kwa mfano baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani, mbali ya usikivu hafifu pia kuangalia maslahi ya wanahabari ambaao wanafanya kazi kwa kujituma na kwa uadilifu nina imani kama maslahi yataboreshwa watafanya ubunifu wa hali ya juu zaidi, kwa mfano, mbali ya hao wa *TBC* pia wale wa kwenye magazeti nao wako katika kundi hilo hilo na hasa kwa kipindi hiki cha virusi vya Corona wanafanya katika hali hatarishi. Nashauri ili kuwapa motisha zaidi wanahabari wetu nina imani kutakuwa na mabadiliko zaidi kwenye vyombo vyetu vya habari.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magazeti ya Serikali linafanya kazi katika mazingira ya ushindani mkubwa, lakini linakabiliwa na uhaba wa fedha, ni vyema Wizara ikasaidia kufuatilia madeni ya matangazo wenyewe taasisi za Serikali ili kuweza kuwapatia fedha zao na kuwawezesha kufanya kazi vizuri, madeni ni chanzo cha kurudisha nyuma maendeleo ya shirika.

Mheshimiwa Spika, ni mkakati gani ambaao Wizara umeuweka kwa wanahabari wa vyombo mbalimbali katika kulinda maadili ya utangazaji na uandishi wa habari, tatizo hili linaondoa uzalendo, ulinzi wa amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa kupata na kutoa habari unahitajika pande zote mbili na hili Wizara imeweza kulisimamia vizuri ila ni vyema kukaa na mkakati wa kuangalia wale ambaao wanaharibu au kupotosha na kuvunja maadili inabidi sheria ichukue nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naipongeza Wizara kwa kuona uwiano wa uongozi baina

ya wanawake na wanaume katika sehemu za kazi chini ya taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa kwa muda muafaka.

Pia naishauri Serikali ikarabati viwanja na kujenga viwanja vipyta vyta michezo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ikiwezekana kila Wilaya iwe na uwanja mzuri na wa kisasa ili uweze kutumika na Wilaya husika kuliko ilivyo sasa viwanja hakuna na vilivyopo havina hadhi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo ili kuboresha miundombinu ya chuo hivyo. Pia naishauri Serikali iajiri wakufunzi wa kutosha wa fani ya tasnia ya sanaa, habari na michezo katika vyuo vinavyofundisha fani hizo ili kuweza kupata na kuibua vipaji vyta wananchi na kupata ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa yale maeneo ambayo hakuna usikivu wa kutosha ya redio mfano maeneo ya Bumbuli na Mlalo kutokana na jiografia ya maeneo hayo *TBC* Chaisikiki, hivyo ushauri kwa Serikali iboreshe mitambo yake ili kuweza kupata usikivu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuchukua hatua kwa vijana amba ni waimbaji wa muziki wa kizazi kipyta pia wanenguaji hususan wa kizazi kipyta takribani wote nguo wanazovaa hazina stara na sio maadili ya Mtanzania, maana wanavaa mavazi nusu uchi na wanaoneshwa katika *television* zetu na huku wahusika wanatazama na hawakemei. Naishauri Serikali ichukue hatua.

Mwisho naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha mara kwa mara kuhusu janga hili la maradhi ya Corona kwa kutumia radio, magazeti na *television*.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha leo kutoa mchango wangu katika Wizara hii kwa njia ya maandishi. Lakini pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kipekee kwa namna unavyoendelea kusimamia mhimili huu kwa busara, hekima na weledi mkubwa.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kusimamia Wizara hii hasa katika kuimarisha na kuendeleza michezo nchini. Bila ya kuwasahau Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa utendaji wao mzuri na kufanya kazi kwa uaminifu mkubwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha pongezi zangu kwa kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa John Pombe J. Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya katika kusimamia maendeleo ya nchi yetu na ustawi wa watu wetu. Katika kudumisha mila na utamaduni wa Mtanzania na kuendeleza michezo nchini na kuongeza wigo wa ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za hapo juu sasa naomba kuishauri Serikali kuititia Wizara hii kwa mambo yafuatayo; kwanza ni usikivu wa *TBC Fm*.

Mheshimiwa Spika, *TBC Fm* ni redio ya Taifa, hivyo basi ni matumaini ya Watanzania wengi kuwa ingesikika nchi mzima. Lakini kutokana na changamoto mbalimbali kama zilivyoainishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ikiwa ni pamoja na bajeti ndogo inayotengwa, kwa mfano katika Mkoa wa Lindi katika Wilaya ya Liwale *TBC FM* haijawahi kusikika katika Wilaya hii tangu ilipobadilishwa jina toka *RTD*. Hivyo basi naishauri Serikali kuhakikisha wananchi hawa

wanapata haki yao ya Kikatiba ya kupata habari kutoka kwenye chombo wanachokiamini cha Ukweli Na Uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyama vya michezo; kumekuwako na vyama vingi vya michezo lakini wingi wa vyama hivi bado haviakisi au kukidhi matakwa na mahitaji ya michezo husika. Maandalizi ya wachezaji wengi nchini ni wa kustukiza, walio wengi hutambuliwa wanapoliwakilisha vyema Taifa letu bila ya kutambua kuwa waliandaliwaje. Kwa utaratibu huu tumekuwa tukipoteza vipaji mbalimbali nchini kwa vyama vingi kushindwa kulea vipaji. Ukiondoa mchezo wa mpira wa miguu michezo ilio baki usimamizi wake sio mzuri wa kuridhisha. Hivyo basi naishauri Wizara kuongeza nguvu katika kuvisimamia vyama hivyo kama vile Chama cha Mchezo wa Riadha, Ngumi, Kuogelea, Mpira wa Pete na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kumekuwepo na usimamizi usioridhisha kwa timu zetu za Taifa hasa zinapokwenda nje kuwakilisha Taifa, hapa maandalizi yamekuwa ni ya kukurupuka kama vile hakuna kalenda inayofahamika ya mchezo husika ikiwa ni pamoja na ukosefu au ucheleweshaji wa fedha za kambi kwa mchezo husika. Jambo hili limekuwa likituletea aibu sana na nchi yetu kuwa kama kichwa cha mwendawazimu cha kujifunzia kunyoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba sasa niungane na Mheshimiwa Rais katika mapambano haya ya janga hili la Corona. Niendelee kuwashimiza Watanzania wenzangu kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wetu wa afya. Tupunguze safari, mikusanyiko isiyo ya lazima. Vilevile tuache au tupunguze kusambaza habari zisizo hakikiwa au kutoka kwenye vyanzo sahihi. Upotoshwaji huongeza taharuki na *pressure* kuliko athari za ungonjwa wenyewe.

Mungu Ibariki Tanzania Mungu Ibariki Afrika.
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu naomba nishauri kama ifuatavyo; *TBC*, *TSN* ni visemeo vya Serikali lakini upelekwaji wa pesa za *development* haziendi kama inavyotakiwa wakati inajulikana kuwa vyombo hivyo ndivyo sauti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashauri kutokana umuhimu wa vyombo hivi ni vizuri Serikali ione umuhimu wa kuboresha mazingira ya utendaji kazi. Kwa mfano, Ofisi za *TBC* Dodoma haifanani na Makao Makuu ya Serikali. Ili kupnguza gharama za uendeshaji katika magazeti ya Serikali hasa magazeti ya *Daily News* na *Sunday News* tuangalie uwezekano wa kutoka kwenye *tabloids* na kwenda kwenye *broadsheets* kama yalivyo *Habari Leo*. Hii itasadia kupnguza gharama kubwa za uchapaji lakini usomaji rafiki kwa msomaji. Siyo vibaya kuiga kwa majirani zetu Kenya na Uganda ambao magazeti yao ya Serikali yanachapishwa kwa mfumo wa *broadsheet*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Michezo cha Malya nishukuru Serikali kwa kukijali sana chuo hiki lakini tatizo ni kutopelekewa pesa za maendeleo na za *OC*, naishauri Serikali chuo hiki kitazamwe kwa jicho la tofauti kwani chuo hicho ni kiwanda cha kuzalisha watalaan wa kufundisha michezo nchini.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa matayarisho mazuri ya hotuba yao na kuweza kuwasilisha kwa umakini kabisa. Mungu awape afya njema na mashirikiano mazuri ili waweze kusukuma huduma za Wizara kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na usikivu hafifu katika visiwa vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudini inayochukua ya kuboresha usikivu katika nchi yetu. Nchi yetu ni kubwa sana na inatofautiana kijiografia. Usikivu katika maeneo mengi umeboreka lakini bado katika baadhi ya maeneo ya visiwa vidogo vidogo si mazuri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suala hili naomba Serikali yetu iboreshe usikivu katika maeneo hayo ili kuwaweka wananchi wa maeneo kupata usikivu hasa katika wakati huu wa maradhi kuweza kujua nini kinaendelea, kinatokeza katika ulmwengu. Naunga mkono hoja.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, pongezi nyngi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, Waziri wa Habari kwa kazi nzuri. Pamoja naye ni Naibu Waziri, Katibu Mkuu na kikosi kizima cha Wizara.

Mheshimiwa Spika, Tanzania iko katika nafasi nzuri sana kwenye mizania ya kimataifa katika ushiriki wake na kuwa sehemu ya historia ya ukombozi wa Bara la Afrika. Ni vema kama Taifa tukatumia fursa hiyo kukuza utalii na kwa hiyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika yaani *The African Liberation Heritage Program*.

Mheshimiwa Spika, kambi zote za wapigania uhuru nchi nzima zina mabaki ya miundombinu na vivutio vingine ambavyo ni urithi muhimu wa Tanzania na Watanzania. Ni vema Serikali ikaanza kutenga fedha za kutosha ili kuwekeza katika eneo hili. Hivyo kiundwe kikosi kazi mahsusini cha kuorodhesha na kuvitangaza maeneo haya na vivutio vilivymo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Masonya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni cha pekee kwa kuwa haikuwa kambi tu ya *FRELIMO* bali pia kambi pekee iliyohifadhi wanawake na watoto, muhimu zaidi wanawake wa kituo hiki ndio waliosababisha kwa sehemu kubwa upatikanaji wa uhuru wa Msumbiji. Ahsante.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake yote kwa Taifa letu. Nawaomba Watanzania wote kuliombea Taifa letu na dunia nzima Mwenyezi Mungu atuondoshee balaa hili la ugonjwa wa Corona, kwa kweli Corona ni ugonjwa hatari sana. Hivyo hatuna budi kushirikiana, kupendana, kuweka nia yetu pamoja katika vita hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini naipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa jinsi ilivyotekeleza llani ya CCM ya mwaka 2015-2020 hususan Jimbo la Mbulu Mjini kuanzia kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, kwa kweli CCM imeng'ara sana kwa miaka hii mitano. Kwa niaba ya Wanambulu Mji tunawaombea mafanikio mema na majaliwa ya kuongoza Taifa letu kwa miaka mitano tena.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu kwa Wizara hii, kwanza naishauri Serikali yetu itoe kalenda (ratiba) ya mashindano ya Kombe la Taifa kuanzia ngazi za Wilaya, Mikoa, Kanda na Taifa ili kupata mchujo mzuri wa kupata vijana wenye vipaji vizuri kwa manufaa mazuri ya Taifa letu na fursa za ajira. Pili, Serikali ijithidi kuajiri/kuendeleza walimu wa michezo katika shule zote za msingi na sekondari katika Halmashauri zote nchini. Pia bajeti ya Kitengo cha Michezo katika Halmashauri zetu zipewe uzito unaostahili kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati za Michezo chini ya ma-*DC* na *RC* zisimamiwe kutekeleza majukumu yao katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta binafsi na wadau mbalimbali zishirkishwe katika mipango ya maendeleo kwenye ngazi za Wilaya, Mikoa kwa kila mwaka chini ya Kamati za ngazi hizo ili kuchangia kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakupongeza sana kwa jinsi ulivyoliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100% na naomba kuwasilisha.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kutoa mchango kwenye hoja hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Wizara na Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Naibu waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri inayoonesha dira ya Serikali kuleta maendeleo kwenye tasnia hii ya habari na michezo pamoja na utendaji mzuri wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mpango wa kujenga Kituo Kikuu cha Uwekezaji wa kujenga kituo kikubwa cha kazi mbalimbali cha sanaa ambacho kitakuwa kituo cha kuonesha kazi za sanaa za wasanii wetu na kukuza sanaa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali uwekezaji kwa kujenga kituo vya michezo ya kukuza vipaji vya wanamichezo kibashara pamoja na shule za michezo ili kutengeneza ajira na kukuza uchumi.

Pili, kuendelea kuvumbua vipaji kwenye michezo ya UMISHUMTA na UMISETA katika shule zetu ili kuwakuza vijana na kuiendeleza vipaji hivyo kwa manufaa ya wanamichezo wenyewe na Taifa kwa ujumla. Tatu, naomba kushauri michezo ya Taifa ili kupata msisimko na mashindano wachezaji wake wawe kama wa timu za Taifa kila mchezajiachezee timu ya asili ya mkoa anaotoka badala ya kuchezea mkoa anaoishi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara dakika 10. Baada ya hapo Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe jitahidi dakika 25, nafikiri unaweza kujitahidi kupitiapitia baadhi ya hizi hoja. Mheshimiwa Waziri dakika tafadhali 10.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hii bajeti muhimu ya Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mwakyembe na Naibu Waziri, Mheshimiwa Shonza; Katibu Mkuu, Dkt Abbas; Naibu Katibu Mkuu, Dkt Possi; pamoja na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kipekee nimongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara hii. Pia niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Dkt. Abbas kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteullwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitajikita sana sana kwenye suala la Taasisi ya *COSOTA* na nianze kwa kutambua mchango wa Mheshimiwa Chumi pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia na kupendelekeza namna bora ya kufanya mapitio na maboresho ya *COSOTA* ili iweze kuwasaidia wasanii wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa maagizo aliyoyatuo kwamba vyombo vinavyohusu haki, maslahi na upatikanaji huduma kwa wasanii ni vyema vikaenda kwenye Wizara yenyeye dhamana ya moja kwa moja na wadau husika. Akaagiza pia Wizara yangu ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, tukae tuangalie namna bora ya kuhakikisha *COSOTA*, *BASATA* pamoja na Bodi ya Filamu tunakuwa na utaratibu au mfumo ambao utasaidia wasanii nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hili nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe tumeshirikiana vizuri mwezi

Agosti mwaka jana tulikaa na kuwa na mukutano wa wadau kujadili namna bora ya kufanya maboresho katika hizi taasisi. Kama ilivyoonyesha kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, hivi sasa maoni ya wadau tunaandaa andiko kwa ajili ya kupeleka kwenye kikao cha maamuzi ili tuweze kuwa na *COSOTA*, *BASATA* na Bodi ya Filamu ambayo imejikita katika kuhudumia wasanii wetu nchini.

Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu amefanya hivyo kwa kutambua kwamba wasanii na sekta ya sanaa nchini ni sanaa inayokua kwa kasi sana na inaajiri takribani vijana milioni tisa. Kwahiylo Serikali kwa kutambua mchango mkubwa wa wasanii tunapitia taasisi hizi ili kuweza kuzifanya maboresho na kuhakikisha ajira za vijana hawa milioni tisa nchini pamoja na wengine wanakuwa na ajira za uhakika lakini wanatumia sekta hii kujipatia kipato na kuchangia kwenye uchumi wa nchi kwasababu tunahitaji kuwa na uchumi ambao uko *diversified*.

Kwa hiyo Serikali inatambua umuhimu wa sekta hii na mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara ambapo *COSOTA* ipo kwenye Wizara hii, tayari andiko ambalo tumeliandaa na kufanya uchambuzi tumeona *COSOTA* ikienda kwenye Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, itaweza kuwahudumia wasanii vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwahiylo niungane na Mheshimiwa Chumi Serikali imesikia na Mheshimiwa Mwakyembe amekuwa kiongozi mzuri katika hili na namhakikishia Mheshimiwa Waziri tutashirikiana mpaka mwisho ili taasisi hizi ziweze kuwasaidia wasanii wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi Mheshimiwa Mwakyembe ameya-cover katika hotuba yake, lakini napenda nichangie upande waTaasisi ya *COSOTA* kwasababu Waheshimiwa Wabunge walipenda kuona ni namna gani Serikali tumejipanga kuhakikisha *COSOTA* pamoja na taasisi nyingine zinaboreshwala ili ziweze kusikia kilio cha wasanii. Serikali imeshasikia kilio cha wasanii na sasa tunaboresha taasisi hizi ili ziweze kuwa na manufaa kwao.

Mheshimiwa Spika, baada na kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.(*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Waziri Bashungwa kwa mchango wako.

Kabla sijamwita Mheshimiwa Mwakyembe nimalizie kwa kusema, yule *scientist* niliyekuwa nasema ambaye ni *professional scientist* siyo mtu wa mtaani ambaye anahitaji ili kuelekea kwenye hii mambo ya *COVID 19* aungane na *professional by chemistry*, apate *microbiologist* aliyebolea katika masuala ya *viruses* na kadhalika na mtaalamu wa maabara *NIMR* kwasababu ndiyo maabara kubwa katika nchi yetu nakadhalika; tayari *already amekwisha-develop* dawa ya vidonda vya tumbo. *Actually* akimwona mtu anahangaika na vidonda anacheka tu, anashangaa na ni katika dawa zetu za kiasili hizi, amesha-*purify*kila kitu anacho.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge yejote ambaye unasumbuliwa na vidonda vya tumbo, nione tu kabisa unapata unafuu katika muda mfupi ujao tu wala hamna shida, yaani ndani ya wiki moja *you are just okay*. Hii yote tunazungumzia habari ya utegemezi kwa watu weupe peke yao kwamba ndiyo wakati na sisi tunabaraka za Mwenyezi Mungu hapa hapa Afrika.

Mheshimiwa Waziri Dkt Mwakyembe, tafadhali sasa ni muda, najua hoja ni nyingi sana, lakini jitahidi kwa 25 minutes kujaribu kupitia pitia hoja zilizo mbele yako. Mheshimiwa Waziri karibu sana.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya Waheshimiwa Wabunge 20 wamechangia hotuba hii. Wabunge 20 wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge na naona kwenye mtandao Wabunge wanaendelea wengine kuchangia na hao watakuwepo kwenye taarifa yetu ya maandishi kwa masuala yote yaliyoelezwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikiri kwamba tumepokea maoni mazuri sana ambayo yanalenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ujumla. Maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni wenye tija na tunaahidi kuufanyia kazi kwa ajili ya maboresho na kama niliyyosema nitapata nafasi tu pengine kuzitolea ufanuzi hoja chache tu,lakini hoja zote zilizotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge tutazijibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayonihusu, Mheshimiwa Peter Serukamba; ametaka Serikali iongeze bajeti ya taasisi yetu ya Sanaa na Utamaduni ya Bagamoyo. Nataka tu kujibu tu kwamba katika mwaka 2020/2021,TASUBA inaombewa bajeti ya shilingi milioni 250 na ninauhakika Bunge lako Tukufu litapitisha hili kwa ajili ya kuimarisha miundombinu yake na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ya Kudumu inataka Wizara ishirikishe sekta binafsi katika kujenga miundombinu ya michezo hapa nchini na kwa hadhi ya kimataifa. Kwa kweli ushauri huu sisi tunaupokeana nimeeleza kwenye hotuba yangu kwamba tumeshaanza hilo, kwanza kwa kushirikiana na Idara ya PPP, chini ya Wizara ya Fedha katika ujenzi wa *Sports and Arts Arena* ambayo sisi tunaijenga, tumedhamiria lakini kwa kushirikisha kwa karibu sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Kamati ya Kudumu ya Bunge inataka ni *TSN*iwezeshwe kifedha kununua mtambo wa kisasa wa kuweka hapa Mkoani Dodoma ni suala ambalo hata Mheshimiwa Mbene nafikiri ameliongelea ili kuongeza nguvu ya usambazaji wa magazeti nchini. Naomba niseme tu kwamba tayari tathmini ya mtambo

unaohitajika hapa Dodoma imekwishafanyika na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi na maelekezo zaidi ya utekelezaji. Vile vile lazima itambuliwe na Bunge lako tukufu kwamba kwa kweli *TSN* imenunua mtambo mkubwa kwa gharama ya shilingi milioni 3.3 ambao tayari umeshaanza kazi Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tumejata maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alikuwa anahojii Serikali imejienda vipi kibajeti kukabiliana na mtikisiko wa uchumi katika tasnia ya michezo na sanaa kutokana na ugonjwa wa *corona* ili kuzuia tasnia hii isianguke akawa anataka tuige mfano wa Serikali ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza wasanii, wanahabari na wanamichezo katika kutoa elimu ya kujikinga na virusi vya *corona* (*COVID 19*). Kazi waliyoifanya ni kubwa, lakini Waheshimiwa Wabunge wote mnajua kwamba Serikali yetu si ya kukurupuka na kila mwananchi anajua hilo. Serikali kwa sasa inachokifanya inakamilisha tathmini ya athari za ugonjwa huu wa *corona* kwa sekta zote nchini ikiwemo pia Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Tathmini hiyo inalenga kuweka mikakati ya kunusuru sekta husika kutokana na athari zinazobainika kutokana na tathmini.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali yetu inashirikiana na *International Confederation of Societies of Authors and Composers* na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) katika kampeni ya kuwawezesha kiuchumi wakati huu wa janga la *corona*. Mkakati wa taasisi hizi umewekwa kwaajili ya kuwapa wabunifu kote duniani nafuu ya kiuchumi. Tunaendelea kufuatilia kwa karibu. Lakini vile vile hatujabweteka tu tukaangalia hilo, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *COSOTA* tunakamilisha ukusanyaji wa fedha toka watumiaji mbalimbali wa kazi za sanaa, tunafuatilia hata senti tano, hata senti 10 ili tuweze ndani ya miezi miwili hii kuweza kuwalipa wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda tu hili Waheshimiwa Wabunge waelewe natembea na dude kubwa namna hii, ni orodha ya wasanii wa Tanzania, tumefikisha majina 1,934 na wote hawa tunahakikisha kila sehemu ambako kuna kazi ya sanaa tunafuatilia ni kiasi gani cha pesa ambacho msanii alitakiwa alipwe na tuko katika kazi hiyo na ninauhakika wa kushirikiana na mwenzangu wa Wizara ya Viwanda tutalimaliza. Siyo tu wasanii jumla tu hata Waheshimiwa Wabunge ambao ni wasanii hapa kwenye jina la 227 tuna Victoria Pascal Kamata na yeze namwona na sitataja kiasi gani ambacho tumekipata huko, namwona pia 886 Martha Mosses Mlatha, naye yumo humu.

Kwa hiyo hatujakaa, namwona Profesa J 1351 nakadhalika nakadhalika. Kwahiyo kazi inafanyika nani ngumu kwasababu tumetoka kwenye mazingira ya utamaduni unaoamini kabisa kwamba kazi za sanaa ni mali ya jamii, hailipiwi. Sasa hatuwezi kutumia polisi kukamata watu, tunakwenda kwa kuelimisha, lakini kwa kipindi hiki tutakwenda kwa kasi zaidi ili Waheshimiwa Wabunge muone Serikali yenu inavyoweza kuangalia wasanii.

Mheshimiwa Spika, halafu Mheshimiwa Mbilinyi ameituhumu Wizara kuzima urushwaji wa matangazo ya moja kwa moja ya mijadala ya Bunge. Nashukuru sana Mheshimiwa Mkamia ametoa elimu kwenye hili na nilidhani Mheshimiwa Mbilinyi kwamba anaelewa sasa baada ya kukaa muda mrefu Bungeni kuwa, sisi kama Wizara hatuna ubavu kuweza kufanya maamuzi kama hayo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huu ni mhimili una maamuzi yake. Bunge limeanzisha utaratibu wake wa kurusha matangazo ya shughuli zake ni kama mabunge mengine duniani yanavyofanya na sisi *TBC* kazi yetu tu ni kuendelea kutangaza, kuchukua matangazo kuyarusha, lakini yatakwenda kwa maelekezo ya Bunge. Bunge ni mhimili hauendeshwi na Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara. Nashangaa kulisikia hilo kutoka kwa mdogo wangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vile vile *TBC* kwa kweli nawatetea tumeendelea kurusha kipindi cha maswali/ve na vile vile

tunaendelea na vipindi kwa mfano kuanzia sita mpaka saba na 11 mpaka 12 kupitia *TBC2* na katika *TBC* Taifa matangazo ya Bunge hurushwa katika redio kupitia kipindi cha leo katika Bunge, hata hivyo kwa sasa Bunge *TV* inamiliikiwa na Bunge na inaendeshwa kwa taratibu zilizowekwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbilinyi vile vile anadai kuwa Sheria ya Makosa ya Kimtandao (*Cyber Crime Act*)ni ya ukandamizaji. Nataka tu niwape taarifa kwamba nchi zote duniani zina maudhui hayo hayo, unaweza ukaenda Uingereza ukakuta haiiti hivyo, inaitwa pengine *Protection of Children Act*, siyo lazima iitwe *Cyber Crime Act*, maudhui ni yale yale. Hakuna nchi duniani imeacha tu milango wazi, uhuru wa ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Nkamia kusisitiza kwamba jamani hakuna uhuru usio na mipaka. Hakuna! Nitolee mfano wa nchi hapa duniani ambapo uhuru unatoka tu hapa; maana unajua tunavyongea sisi Wabunge, tunatoa picha kwa wananchi kwamba unafika nchi kama Marekani, jioni tu unatoka pale unaingia pale Ikulu ili unywe chai na Mheshimiwa Rais, ni uhuru tu. Tusitoe picha za namna hiyo duniani, hakuna kitu kama hicho. Kila nchi ina tararibu zake na hizo taratibu zinauma ukizivunja.

Mimi tu niulize, kuna ndugu yetu mmoja anaitwa Mwaikambo, hivi Mheshimiwa Mbilinyi anadhani alipelekwa Mahakamani Uingereza na kuchuliwa hatua kwa kutumia sheria gani? Sheria ya Kusalimiana? Ni *Cyber Crime Art*; unarusha picha za watu wamekufa, hairuhusiwi kwa wenzetu, ila kwa Tanzania ni ukandamizaji. Hapana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mollel ametuomba Wizara tukae na Madam Ritta tuyamalize kwa maneno yake. Mimi sioni kama Wizara ina tatizo lolote na Madam Ritta. Naomba niwasitisizie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara inatambua mchango mkubwa huyu mama katika kuendeleza sanaa, tunaelewa. Hii haina maana asitekeleze wajibu wake kimkataba. Hili ni suala ni la kimkataba.

Mheshimiwa Spika, huyu Mtanzania mwingine aliyalalamika ni Mtanzania, ana haki. Kilichofanyika ni kwamba, timizeni wajibu wenu kimikataba. Yeye mwenyewe ametuandikia barua kwamba atalimaliza hilo ndani ya muda wa mwezi mmoja. Hatuna shida! Kwa kweli sisi tunampongeza Madam Ritta kwa kazi kubwa anayoifanya, lakini atekelze wajibu wake kimkataba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwamoto, suala la ukomo wa wachezaji wa nje, wengine wanafikiria kwamba tunaongelea soka. Nitoe mfano mdogo; mwaka 2019 tulikuwa na mashindano ya *Netball* Arusha; kuna timu moja hapa ya *Netball* nchini, ilipata ubingwa wa Taifa ilingiza wachezaji wote kutoka Uganda. Wote! Sasa tukaanza kuuliza, hivi tukoje?

Mheshimiwa Spika, nikaja kugundua kila mtu kwenye mchezo wake ana ka-*pocket* kake ka mamlaka. Haiwezekani! *We are sovereign state*. Tuna malengo ya sasa, ya kesho, kesho kutwa na ya Taifa hili. Ndiyo maana tunambana Waziri wa Fedha na viongozi kwenye Serikali watoe fedha kila mwaka kwa ajili ya fedha za UMITASHUMTA, UMISETA ya nini? Kuibua vipaji ili viweze kutumika kitaifa, ili viweze kuonekana duniani na viweze kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kama hatuwezi kuvitengenezea vipaji njia vikaonekana, vikatumiwa nchini, tunafanya makosa makubwa sana. Nchi kubwa kama Marekani leo inatoa maelekezo kwamba tunazuia watu wasiingie, tunalinda ajira kwa ajili ya Wamarekani. Sembuse sisi! Tusijadiliane Watanzania kwa sababu tu kwamba tuna vifaa sijui kutoka Sudan, kifaa gani?

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania leo hii tumekuwa gumzo duniani kwa kuweza kufanya vitu vikubwa ambavyo miaka michache iliyopita tulikuwa hatuwezi. Tunafanya uperesheni za ajabu Muhibibili sasa hivi. Zamani ilikuwa lazima twende Ulaya. Leo kupiga dude lina hewa ndani, tunahitaji kweli *expertise* tukajaribu kuvutana shati hapa! Kama

hatuwezi hayo, tuwaachie watoto wa kike ambao wameonyesha kung'ara Kimataifa na Kitaifa kwa soka bila hata kutafuta watu wengine pembedi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sijatoa uamuzi wowote hapa, nilichosema, nimeigiza *BMT*, iendeshe mjadala shirikishi na wadau wa michezo, hebu tujiangalie kama Taifa, tunakwenda wapi? Tukiweka tu milango wazi yejote anaweza kuja. Tumefika mahali hata wale wanaowatafuta wachezaji wa nje hawatumii uangalifu wowote, ni dili tu. Kati 10; watatu, wanne watakuwa wazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa timu zote hapa, naweza mimi nikawa-*challenge* viongozi wote na wadau wote wapenda michezo hapa katika timu zote; Yanga, Simba zote zinazochukua wachezaji toka nje. Sijaona zaidi ya wachezaji wanne wazuri kabisa wakiwango cha juu. Wengine wanakaa benchi. Wewe umetolewa nje unakuja kukaa benchi! Ni kutumia vibaya haya mamlaka tunayopewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, badala yake, badala ya kukazania kuangalia vipaji gani vinaibuka kwa UMITASHUMTA na UMISETA, kwa mfano mwaka 2019 nimeona ile fainali ya Songwe na Ruvuma, mpira wa hali ya juu! Aaah, hamna umuhimu; tuko *busy* kuangalia sijui Burundi anatokea nani! Haiwezekani! Hebu tukae chini; na ninaomba *BMT* wahakikishe wanawapa fursa Wabunge kuweza kuchangia katika mada hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Devotha Ninja ameongelea sana kuhusu ukandamizaji wa vyombo vya habari. Nimefurahi sana, ametoka kuongelea sasa hivi kuhusu mwandishi kwamba ameonewa huko Zanzibar; akajibiwa hapa na Mheshimiwa Mwakasaka kwamba hapana, mbona alikuwa ana makosa! Sasa ndiyo vitu kama hivi, Wabunge tukitetea bila kuangalia maudhui, kwa kweli tunazidi kupotosha hii jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli siongezi zaidi ya yale aliyosema Mheshimiwa Nkamia hapa. Hakuna

ukandamizaji wowote ambao leo hii tunaweza kama Taifa tukaanza kulijadili. Mimi nashangaa *is really paradox*. Leo kama kuna ukandamizaji wa ajabu hapa wa vyombo vyahabari, kwa nini vinaumuka kwa uyoga? Nimewatajia hapa, kwa nini itoke hivyo? Tatizo ni sisi au tatizo ni vyombo vyahabari! Sielewi; ni sisi au ni desturi yetu wenyewe!

Mheshimiwa Spika, haiwezeikani duniani hapa kwamba kuna ukandamizaji lakini vyombo viko 200, 300 tena ni *private sector*. Siyo sisi. Ananisema Mheshimiwa kwamba "sijakuona siku moja ukitetea Waandishi wa Habari." Niwatetee wepi? Mimi sio mganga wa kienyeji kuanza kufikiria eti, yule wa Tanzania Daima leo amenuna, atakuwa lazima ameonewa nianze eti...; nina kazi nydingi za maana za kufanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kama wanahabari wenyewe hawana nafasi kuja kumuona Waziri wao, mimi ni Mwanahabari mwenzao, njooni, nitasikiliza. Sijawahi kumfukuza Mwanahabari ye yote ofisi kwangu ambaye ana hoja ya msingi. Sitawaja wawili ambao walikuja na wote niliwasaidia kwa sababu nina mamlaka chini ya Sheria ya Huduma ya Habari. Kama hawaji, nianze kuwatafuta, nina shida gani? Mimi mwenyewe nina kazi nydingi za kufanya.

Mheshimiwa Spika, nimalizie swalí lingine hapa la Mheshimiwa Chumi, samahani. Nafurahi mawazo yake yote ni mazuri sana, anataka *Safari Channel* ionekane nje ya Bara la Afrika sasa. Ukitosha vizuri hotuba yangu, kwa kweli tunakua kwa pole pole. Tusimuumize sana Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa, atashindwa hata kufanya vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunakwenda kwa pole pole, tumeshaanza, sasa hivi tuna-cover Afrika nzima na mwezi wa Sita nimesema tunaanzisha *Programu Tumizi App* ili tuwezeshe *Safari Channel* irushwe kwa lugha zaidi ya sita za Kimataifa. Tunaanza na baadaye tutaingia sasa katika ile anga kubwa zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, yalikuwepo malalamiko kidogo kuhusu *COSOTA* aliyasema. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda amelieleza vizuri sana. Niже niongeze kwa upande wa Bodi ya Filamu, tuna Bodi za Mikoa na Wilaya za Filamu ambazo Makatibu wake ni Maafisa Utamaduni wa Wilaya na Mikoa. Nashangaa huyu jamaa aliyetokea huko mikoani anakuja Dar es Salaam kujipanga hapa kwa ajili ya Bodi ya Filamu, ni kukosa uelewa tu.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ambalo nimesisiza kuhusu *BMT*ni kwamba waangalie vilevile ili tuweze kufaidika zaidi. Timu zetu wanapowapa kazi makocha kutoka nje, wasije na wasaidizi wao, tuweke hayo masharti. Unajua sisi ni Taifa, wasaidizi wao watafutwe hapa hapa nchini ili wanapoondoka wawe wameacha weledi hapa. Sasa anakuja mtu na wasidizi wanne, watu wengine wamekaa tu, unaona kama huyu jamaa wa nini? Ni kuongeza gharama. Unamwambia aah, *condition* ni kwamba kama anatafuta kazi bwana, kwa hiyo, wasaidizi wawili atawakuta Tanzania. Lazima tufikie hapo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nafikiri itabidi sasa hivi tufanye kazi kwa karibu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hawa watu wengine kwa kweli inabidi sasa hivi tuanze kuwaminya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbilinyi anasema Serikali imeninyima fedha za maendeleo, tumepata asilimia 50 tu. Nataka kusema kwamba asilimia 50 iliyobakia ni kwa ajili ya *procurement*. Tuna kazi ya kununua sana vifaa. Katibu Mkuu wa Fedha na Mipango yuko, hata kesho asubuhi nikimpekelea nyaraka zile, hiyo fedha italipwa, ni suala la *procurement*.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimsahihishe Mheshimiwa Mbilinyi. Nimesikitishwa sana akisema kwamba Wizara yangu imegawanyika na kwamba sasa kuna Abbas anaendesha habari, mimi naendesha vitu vingine. Mimi ndiye Waziri, *I am a Minister*, Abbas ni Katibu Mkuu wangu. Kwa hiyo, akifanya kazi kwenye habari vizuri, ni heshima kwangu. Sasa ukianza

kutugawa namna hii mimi nakushanga. Katibu Mkuu, *he is doing a wonderfull job! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie haraka haraka kusema kwamba hapa kuna suala hapa la kesi ya Mwananchi *Online*. Naomba Watanzania tuelewane, tumechukua hatua hiyo kali ya kufungia hiyo *Online TV* kwa sababu ni makusudi ya kumfedhehesha Mkuu wa Nchi. Tukiingia huko Watanzania kumchezea mtu ambaye ndiye anabeba sura, *sprit* ya Taifa, aah, tumeshindwa kazi. Haiwezekani! Kipindi hiki cha *Corona*, unatafuata picha ya nyuma; Rais ni mtu *sociable* sana. Amekwenda huko ametembelea kivukoni, anaongea na watu wake. Picha ya siku nyingi, kashika samaki; unasema, jana akiwa Chato! *(Makofi)*

Mhesimiwa Spika, hatuwezi kukubali upuuzi wa namna hiyo, kutoa pilcha kwa wananchi kwamba nchi ina matatizo ya *Corona*, unamwona Rais wenu anazunguka zunguka. Ni uongo kabisa! Mna bahati, ni kwa sababu tu nayo ina usajili wake ile *TV*; isingekuwa na usajili wake, kwa kweli tungefungia na vitu vingine hapa ili kutoa fundisho kwa wengine wasifanye mzaha namna hiyo. *(Makofi)*

(Hapa kengele imelia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele imegonga, nashukuru tu kwa mchango wa Mheshimiwa Ngeleja, anasema michezo inahitaji rasilimali kubwa. Ni kweli, niko kwenye maongezi, nimeshamwandikia barua Waziri wa Fedha kuhusu suala la Bahati Nasibu ya Taifa. Tuliisimamisha kwa nia njema, kwani kulikuwepo na matumizi ya ovyo, ilikuwa haileweki inaendaje. Nina uhakika, chini ya Mheshimiwa Dkt. Mpango na Katibu na Doto, likikaa vizuri lile dude litachangi vizuri kabisa katika michezo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la ligi kuu liliwyongelewa hapa, naomba niwaachie watalaam siyo suala la kisera, ni suala kiufundi, nina uhakika *TFF* watalimaliza vizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nyingi na sipendi nipigiwe kengele ya pili, ni utovu wa nidhamu, ila kama nilivyosema nitazijilbu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, naomba sasa Bunge likubali na kuridhia kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ya jumla shilingi 40,140,641,000/=. Kati fedha hizo mishahara ni shilingi 20,679,231,000/=. Matumizi mengineyo ni shilingi 11,446,410,000/= na miradi ya maendeleo ni shilingi 7,715,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nina hakika muda hautoshi kupitia kila hoja, lakini umejitalihidi zile zilizo muhimu umezi-cover.

HOJA ZA KISERA

SPIKA: Sasa tunaingia utaratibu ule Waheshimiwa Wabunge ambao wanaomba ufanuzi zaidi kwa Mheshimiwa Waziri katika mambo mbalimbali. Utaratibu wetu ni kwamba tutaendeleza sana; utauliza, tutapata majibu; na mwingine atapata nafasi.

Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, tafadhali.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kupata ufanuzi kutoka Serikalini. Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa kwa kipindi kifupi na inaendelea kufanya kazi nzuri katika kipindi hiki. Na sisi wananchi wa Dodoma tunaishukuru sana Serikali ya

Awamu ya Tano kwamba imeshahamia na inafanya kazi nzuri katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kipindi kilichopita Serikali ya Morocco ilikubali kuungana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujenga uwanja mzuri wa Kimataifa hapa Dodoma. Nilipoangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sikuona kama Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza maandalizi ya awali na hata kuungana na Serikali ya Morocco kule kwa ajili ya kujenga uwanja huo wa Kimataifa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Dodoma na Watanzania wangojea kwa hamu sana kuona kwamba uwanja huo wa Kimataifa unajengwa hapa Dodoma. Naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa au kwenye bajeti yake, mimi sijaona, lakini kama ipo, naomba tu ufanuzi kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Swali hili ni muhimu sana, sana, sana. Kila tukipita hapo Mheshimiwa Waziri Mwakyembe tunajiuliza swali hilo hilo. Ufanuzi tafadhalii Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Bura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wote mtakubaliana nami kwamba ujenzi wa *Sport Complex*, ni mchakato mrefu ambao una awamu zake katika utekelezaji. Awamu ya kwanza kubwa kabisa ilikuwa ni kupata kiwanja kikubwa kabisa ambacho kitatosheleza mahitaji ya jiji hili kwa miaka zaidi ya 50 ijayo. Ndiyo maana tukapata eneo la zaidi ya ekari 320 na mahitaji yetu ya sasa hivi kwa kila kitu ni ekari 150 tu, lakini tumepata yote hiyo kwa mahitaji ya baadaye vilevile. Hiyo ni pesa.

Mheshimiwa Spika, la pili, Dodoma ina tetemeko na ina udongo ambao unatofautiana hapa na pale. Kulikuwa

na kazi kubwa sana ya kufanya kuhusu utafiti wa udongo. Siyo hivyo tu, hata *seismic survey* kwa ajili ya tetemeko; hatuwezi kuwa na uwanja tumeujnga halafu kesho umepasuka. Hata *cross za akina Ajibu* sijui zitapigwaje pale uwanja umepasuka katikati. Kwa hiyo, kazi ya kitaalam imekuwa kubwa, *topographical* na kadhalika, *feasibility studies* zimekamilika zote, nyingine tumezirudia. Uwanja huu uko tayari kwa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nisisitize kitu kimoja, unapoongea na kiongozi mwenzako wa nje, akasema mimi nitajenga. Watanzania naomba sisi Wabunge tusiwe mbele sana kuanza sasa kuuliza, unajenga lini sasa? Aah, aliyeomba hatukuwa sisi; aliomba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni ahadi yake yeye. Nami ndiyo maana nimemaliza hapa, yote nimekabidhi kwamba Mheshimiwa sasa saluti, nimemaliza, kila kitu kimeisha, akakwambie sawa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimweleweshe Mheshimiwa Bura kwamba tupo tayari kwa ujenzi, lakini asjiali sana kuhusu bajeti inasemaje, kwa sababu hata mwanzoni halikuwa suala la bajeti. Tulimwomba rafiki ambaye alisema mimi nitajenga; na huyo rafiki siyo kwamba alikuwa na kitu kimoja cha kujenga, alikuwa na vitu kadhaa. Ameshakamisha vizuri sana mradi wa ujenzi wa Msikiti Dar es Salaam ambao ni wa Kimataifa na sasa hivi ni suala tu la muda kuweza kuelewa kuhusu hatma ya uwanja huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, nimetetee kidogo Mheshimiwa Bura, anawahi hili ulilojibu wewe kwa sababu mwaka huu ni wa uchaguzi na nina hakika kwa mkoa wa Dodoma hoja kubwa itakuwa ni hiyo. Kwa hiyo, ni lazima kuanza kupata majibu na kuwandaa ili mtusaidie. Maana mwishoni mwa mwaka huu sisi ndiyo tutakuwa tunafafanua kwa wananchi. Nina hakika *issue* yao itakua ni hiyo moja tu kwa Dodoma. Mengine yote safi kabisa, hakuna swali hata moja.

Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, janga la Corona ni janga la kitaifa na Serikali kwa ujumla wake inapaswa kupambana nalo. Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo ina nafasi kubwa sana kwenye kipengele cha kutoa elimu dhidi ya raia wetu kujikinga na janga la Corona. Sasa nataka kujua, wizara ina makakati gani wa kuwatumia wasanii kutoa elimu dhidi ya kujikinga na janga hili kwa kuwa wasanii hawa wana mashabiki wengi sana hasa kwenye mitandao ya kijamii. Mfano mtandao mmoja tu wa Instagram Msanii Diamond ana mashabiki milioni tisa, Wema Sepetu milioni sita, Ally Kiba milioni tano, Harmonize milioni tano na wengine wengi. Sasa nataka kujua mkakati wa wizara kuwatumia wasanii kutoa elimu dhidi ya kujikinga na janga hili, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe ufanuzi tafadhali.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kutoa ufanuzi kwa Mheshimiwa Goodluck Mlinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu nimewapongeza sana wanahabari na wasanii kwa mchango wao mkubwa katika kuleta *awareness*, kuleta elimu kwa wananchi kuhusu hili gonjwa linalotukabili. Sasa hivi nina takwimu hapa, kuna makala zaidi ya 800 katika magazeti, tuna vipindi zaidi ya 2,000 katika *Tv* na radio vikiongelea suala la Corona, huu ni mchango mkubwa sana. Vilevile, nilitaka nimsisitizie tu Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwamba sasa hivi tuna zaidi ya wasanii au vikundi zaidi ya 80 ambavyo vina nyimbo baadhi zimeshaonekana, zimerushwa katika radio zetu na katika luninga zetu yote ni kampeni dhidi ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi upande wetu wa wizara tulishawatia moyo wasanii wetu wachangie kwenye hilo suala na wasanii wakubwa nao tumewatia moyo

waweze kuchangia kwenye hilo. Jana tu nilikuwa na ujumbe wa watu wanenamuziki wa siku nyingi wakiongozwa na Hamza Kalala na wawakilishi wa bendi mbalimbali *DDC Mlimani Park Orchestra*. Wao wameamua sasa kuja na wimbo ambao unasema ni Funga Kazi na walikuja kuomba kuwezeshehwa wizara inalifanya kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tupo kila siku sisi na leo hii jioni nina kundi la wasanii nalo likiomba kusaidiwa hapa na pale kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wasanii wote nchini kwamba hii vita bado haijaisha tuendelee tusirudi nyuma, tusikate tamaa kuhabarisha umma na kusisitizia kwamba kuna vitu vya msingi ambavyo lazima wote tuzingatie ili tuweze kushinda katika vita hii.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, ahsante sana kwa majibu mazuri, Nadhani Mheshimiwa Devotha atakuwa Msekwa, kama yupo kule Mheshimiwa Devotha Minja unaweza kuuliza swali lako la ufanuzi.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kwa miaka mitano mfululizo waandishi wa habari, wanaharakati, raia wa kawaida ambao wamekuwa wakitumia uhuru wao kutoa mawazo hasa wale ambao wamekuwa wakiikosoa Serikali hii ya Awamu ya Tano wamekuwa wakijikuta katika matatizo makubwa. Wengine wamepoteza maisha, wengine wamejikuta waandishi wa habari wanakosa ajira. Mfano mzuri kabisa tunazungumza hivi sasa kina Roma Mkatoliki, kina Tito Magoti, kina Azori Gwanda mpaka sasa hawajulikani walipo na hata hivi karibuni kuna waandishi wa habari waliripoti tatizo la barabara kule Ngorongoro matokeo yake waandishi wale Mkuu wa Mkoa akasema wanatakiwa wapewe case ya uhujumu uchumi ilihali walikuwa wakitimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini Serikali hii itaacha matendo haya ambayo yanasingina katiba kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe, majibu ya swali hilo la uchokozi.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, nashukuru naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Devotha Ninja na nimuombe tu kwanza asipende sana kushabikia porojo. Naomba tu nimkumbushe aliyoyasema hapa, anaongelea waandishi wa habari, yeye ni mwandishi wa habari sahihi. Wanaharakati na raia wa kawaida, nikimwambia tu anipe majina matatu atarudiarudia tu hizi hadithi ambazo zinasemwa kila siku ambazo hazina hata msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, anamtaja Roma Mkatoliki, Roma Mkatoliki amepata tatizo gani, ningependa nisikie kutoka kwa Roma Mkatoliki mwenyewe. Tusiwijaze hawa vijana maneno mdomoni ambayo wao hawajatamka, amefanya nini au amefukuzwa kwenda Marekeani! Ameenda kwa hiyari yake, anataka kurudi kama huna uwezo kwamba Corona sasa kwa upande wake iahirishwe aje yeye na ndege Panama peke yake sjui *whatever* Emirates aletwe hapa Dar es Salaam fanya hivyo. Hebu acheni jamani kuweka chumvi kwenye vitu ambavyo havipo, namdai dada yangu wala sihitaji sjui kusema hapa mbele ya bunge. Mimi namtaka yeye aniletee ushahidi Roma anasema nimeonewa niko huku Marekani kwasababu Serikali kandamizi, hayo ni yako Mheshimiwa Devotha Ninja mpaka utakaponithibitisha. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Roma Mkatoliki naongea naye, sasa hayo unayapata wapi, leo unakuja na hoja ambazo wazungu wanatuletea hapa na nyie ndiyo mnawapa. Azori Gwanda kapotea naomba niseme mbele yako, hakuna kitu kinachonisikitisha kuhusu sisi watanzania kupoteza utaifa, eneo ambalo Azori Gwanda anazungumziwa kupotea ni eneo ambalo watanzania wengi sana wamepoteza maisha, na maisha ya kila mtanzania yana thamani kama maisha ya mwandishi yoyote wa habari. (Makof)

Mheshimiwa Spika, wale wengine wote mamia waliopotea hakuna shida kwasababu ilikuwa ni sehemu yenye matatizo ila huyu mmoja kapotezwa na Serikali. Tusifike mahali ambapo unapigwa na mumeo unasema ni mpango wa Serikali, unapigwa na mkeo unasema ni mpango wa Serikali. Hebu tuache hizi vitu vidogo vidogo vinaturudisha nyuma sana, hii nchi ina makubwa imefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo wengine tunaenda kwenye mikutano nje ukikaribishwa tu, Waziri kutoka Tanzania *take the floor* ukumbi wote unakuangalia, kwanini! Unaanza kusema ooh, pengine sijui nimevaa vibaya, hapana! Umeweka suti nzuri tu kama ya kwangu hapa lakini ukienda nje maswali tu ni kwamba, bwana eeh, hivi huyu Dkt. Magufuli yukoje! Mnaendaendaje nyie, mmefanikiwaje hiki na kile! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba jamani turudishe uzalendo, hebu tuache hizi porojo ambazo wazungu na *amnesty International* au sijui nini, kwanza kuja tu kuchafua chafua hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo lao kubwa nalijua toka sisi tumeweka msimamo kwenye suala la ndoa za jinsia moja tutambue kwamba ni haki ya binadumu, ushoga haki ya binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi ni Taifa, sisi tunamuogopa Mungu, hatuwezi kukubali vitu ambavyo vinaenda kinyume cha *Quran*, kinyume cha Biblia. Wenzetu subirini mje kukubali hayo na majitu yenye sharibu mnaoana shauri yenu mtachomwa moto kama Sodoma na Gomora. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya uhakika. Nilikuwa namsikiliza siku moja mtaalam mmoja katika wataalam waliobobea wa uchumi duniani pia akawa anazungumzia kwamba kuna uwezekano mkubwa Wachina kuwa Taifa lenye uchumi mkubwa zaidi duniani ndani ya miaka 20 ijayo au chini ya hapo na akatoa sababu kadhaa. Moja ya sababu alioitoa

ni kwamba China wana Serikali ambayo inaheshimika mionganoni mwa Wachina na Wachina wenyewe wana mila na desturi ya *ku-act* pamoja kwa nidhamu na Taifa lao. (*Makofii*)

Huko Marekani kila huyu akisema hivi huyu anapinga hivi; huyu akisema hivi huyu anapinga hivi, sasa utamaduni huo ndiyo unatuletea sisi hapa, Serikali ikisema jamani twendeni hivi kuna wanaopinga hapo hapo liwe zuri liweliweje yaani kupingana tu. Mkishakuwa na utamaduni wa kupingana kupingana kwa kila jambo kwa vyovoyote vile hamuwezi kusogea. Si mbaya kupingana katika yale ambayo yanafaa kupingana lakini kupingana kwa kila jambo sasa hii tena, mnatuletea utamaduni ambao hauwezi kutusogezza hata kidogo, mkisema kushoto geuka wengine wanageuka kulia haiwezekani.

Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili i niombe suala la ufanuzi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ametupatia sasa hivi. Pia nipongeze Serikali kwa mambo ambayo yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi dunia nzima tunalia na hili gonjwa la Corona na niwapongeze sana vyombo vya habari, nipongeze wanahabari kwa kazi kubwa sana ambayo wamekuwa wakituhabarisha katika vyombo mbalimbali, na nitoe pole kwa wanahabari ambao wamepoteza pia uhai kwa ajili ya gonjwa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iseme ni mkakati gani unao au sera gani kuhakikisha kwamba wanahabari ambao wanafanya hii kazi ya kupambana na hili gonjwa. Kwanza wanapewa elimu ili waweze kuelimisha maana yake nimezunguka katika mkoa wangu nimeona wanahabari wakipita kuhabarisha hizi habari lakini hawana elimu ya kutosha. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba

wanawapatia elimu lakini pia wanawapa vifaa vya kujikinga wanapoenda kutoa hizo habari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu utakuta wanapita huko hawana hizi barakoa na vilevile wanaowahoji pia hawana barakoa kwa hiyo wanahatarisha sana maisha yao. Sasa nilikuwa naomba tu nini mkakati kuhakikisha kwamba hawa wanahabari hasa wanaenda kuhabarisha huko vijjini, hawa wa mijini ni afadhali hata wanaweza lakini wanaokwenda huko vijjini bado athari ni kubwa sana za kupata huu ugonjwa wa Corona, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mwakyembe ufanuzi tafadhalii.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ufanuzi kwa Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumelisema nafikiri nadhani sasa hivi itabidi nitamuomba ruhusa Mheshimiwa Waziri Mkuu nitoke kidogo kuzunguka tena kwenye *Media Houses* mbalimbali kusitisitiza tu ambayo tumeyasisitiza sana. Kwanza ni wajibu wa wawamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha kwamba mwanahabari anapotoka nje ya chumba cha habari kwenda nje kufanya kazi kule, lazima awe amenunuliwa/amepewa barakoa na *gloves* na vilevile *sanitizer*. Mmiliki wa chombo cha habari ambaye hafanyi hivyo anatahadharisha maisha ya hawa vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, chini ya Sheria yetu ya Huduma ya Habari ya mwaka 2006 kila mwanahabari lazima awekewe bima, ndio inakuja hiyo sababu kubwa. Kwa hiyo, sisi hatujaanza kuwakamata kwa hilo kufukuzana lakini tunataka waoneshe ule moyo tu wa kwamba unawajali hawa vijana. Lakini pili tunesisitiza suala la vyumba vya habari, vyumba vya habari mara nyengi ni sehemu ni mkusanyiko mkubwa wa wanahabari hata wale ambao wamekuja tu hana kazi ya kufanya anapiga porojo. Sasa hivi lazima ibadilike kila chumba cha habari wawepo wanahabari wale tu ambao

wanakazi wakati huo ili kupunguza msongamano kwenye vyumba vy'a habari. Nimeshaona katika baadhi ya *Media Houses* hilo linatekelezwa pengine hizi ndogo ndogo ndiyo shida hii kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nimeshauriwa hapahapa nafikiri lazima kulichukua kwa nguvu sasa, vyombo vy'a habari vyenye nguvu sana sasa hivi ni hizi *Television* na Radio za mtandaoni ambazo ndiyo lukuki na ndiyo ambao hata ukiona kuna kiongozi wanaongea basi wana vi-microphone vyao vimejaa pale kama msitu ni hao. Nadhani kuna humuhimu sasa tutakaa chini na wenzangu nafikiri leo hii tuangalie hatua ya kuchukuwa sasa ingawa najuwa haohao wanao lalamika leo kwamba wenzetu kwamba mnapunguza uhuru watakuwa wa kwanza kusema. Unaona sasa wanakandamiza sasa hivi *online TV* na *online radio*. Lakini nina uhakika kwa Mheshimiwa Ritta Kabati anania njema tu mimi nazungumzia tu wale wenzetu ambao wanapinga kila kitu lakini kwa kweli hili tumelichukua ngoja tulifanyie kazi zaidi na zaidi kwa sababu hii vita tunayo na lazima tupigane kisayansi. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata uwe wa mwisho.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri yeye na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote. Ulikuwepo mwaka 2005 wakati tumeingia hapa bungeni aliyekuwa anazungumzia sanaa ni Martha Mlata na akaitwa jina Mama COSOTA. Sasa wasemaji wamekuwa wengi na wasanii wamepata heshima kubwa sana Tanzania, heshima kubwa waliyoipata ni Mheshimiwa Rais kuwaweza kwenye wizara rasmi na kwa kweli hiyo ni heshima na kazi kubwa imefanyika na ndiyo maana wasanii sasa hivi wanawenza kuzungumza na mambo yao yanakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuunganisha COSOTA, BASATA pamoja na filam amelisema vizuri sana Waziri wa Viwanda, lakini kuna suala la maafisa utamaduni

walioko kwenye wilaya zetu na mikoani wale wako chini ya TAMISEMI kwa hiyo na hakuna elimu yoyote inayotolewa kwa wasanii kwamba wale watu wanafanya shughuli zippi. Mimi nilikuwa naomba pamoja na kuunganisha hayo, Mheshimiwa Waziri unipe tu ufanuzi vizuri kwamba muunganisho huo utafanyaje kazi kwasababu watu ni wale wale. Ukienda COSOTA kama unavyosema hizo fedha umetusoma hapo mimi mwenyewe nawadai hawalipi zile fedha wanakusanya fedha. Sasa hivi wasanii wamefungiwa matamasha *at least* wangewalipa hata zile fedha hao wazee wa *band* waliokuja wangeweza kupata fedha zao wenyewe lakini hawalipi ile mirabaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanuzi, mtawezaje kuunganisha na maafisa utamaduni wale wataingiaje pale ili waweze kufanya kazi vizuri kwa ajili ya wasanii na falida ya Taifa kwa ujumla, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata, ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe majibu tafadhali.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa hii fursa kufafanua hili suala aliloleta Mheshimiwa Martha Mlata na kweli mchango wake tunautambua sana katika eneo hilo. Nilitaka nisitisize tu kitu kimoja tu kwamba katika kujibu hili swalii la Mheshimiwa Mlata nikumbushie tu hata suala la wengine ambao amelileta hapa Mheshimiwa Msukuma kuhusu agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu isije ikaleta picha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni mkuu wetu wa kazi anatoa maelekezo halafu sisi hatuyazingatii. Kichekesho ni kwamba sasa anayejua hatuyazingatii ni Mheshimiwa Msukuma nje ya Serikali sijui inawezekanaje.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya mabadiliko katika Bodi ya Filam, Bodi ya Filam *is the legal entity*. Kiongozi Mkuu wa bodi ya filam ana maamuzi yake yote, ana bodi yake ya wakurugenzi haendeshwi na Mkurugenzi wa Idara na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba huyu

mama hatumpi adhabu, hawa tu hawamtaki apelekwe kwenye *equivalent position* wizarani sasa tumfanye nani mpishi!

Mheshimiwa Spika, *she is the only women*, katika nchi hii mwenye *qualification* ya *cyno photography* hapa ni mtaalamu ni bingwa. Tumempeleka pale lakini vilevile busara ya Katibu Mkuu wangu ni kwamba yanapokuja masuala yanayohusu Bodi ya Filam ashungulikie mkurugenzi msaidizi hakuna shida hatujaliona hilo. Na sisi tukiona kama anakuwa kikwazo tutamuondoa lakini utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi tunayapata kwa maandishi siyo yale mnayoongea kwenye mukutano pale lakini tunayapata kwa maandishi. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunamueshimu sana akisema kushoto geuka tunageuka na hilo nalo nilitaka nilisisitize. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili la kiunganisha Bodi ya Filam, *COSOTA* pamoja na *BASATA* linatokana na ushauri na vilevile maelekezo ya Mkuu wa Nchi. Hataki vijana wake wahangaike huku na kule kutafuta huduma ambayo unaweza kuingia kwenye *one stop center* ukamaliza kila kitu hapo. Na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara tumefika mbali na hilo tunalimaliza haya mengine, Mheshimiwa Mlata ya kwamba sasa maafisa utamaduni huko itakuwaje. Hebu ngoja tuanze tukisha nyoosha pale juu huku chini si ni gwaride tu kushoto geuka, kulia geuka watafuata tu, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, ahsante sana kwa ufanuzi wa masuala mbalimbali ambao Waheshimiwa Wabunge walikuwa wameuliza. Hapa tulipofika sasa ni hatua ya kuweza kuamua kuhusiana na hoja ambayo Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo aliiweka mbele yetu Waheshimiwa Wabunge na mbele ya Bunge hili kwamba muweze kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kura mmekwishazipiga ziko hapa, ninazo zote nani kapiga vipi,

kila kitu ninacho, hakika waliosema ndiyo wameshinda.
(Makofî)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Wizara ya Habari, Utamaduni,
Sanaa na Michezo.....Sh. 32,425,641,000

MIPANGO YA MAENDELEO

Wizara ya Habari, Utamaduni,
Sanaa na Michezo.....Sh. 7,715,000,000

SPIKA: Nichukue nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe; Mheshimiwa Naibu Waziri Shonza; Katibu Mkuu Dkt. Abbas; Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii ya Habari kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya, kwa kweli Watanzania tunahabarika sana labda kama wewe ni mvivu wa kutafuta habari, lakini ziko nyingi rasmi na hata zile za kizushi kwenye mitandao mbalimbali ziko zimejaa, ili mradi uwe na muda tu wa kupitia maeneo mbalimbali. Uwezekano wa Mtanzania kupata habari leo ni mkubwa kuliko wakati wowote tangu tupate uhuru na hii ni matokeo ya kazi nzuri ambayo mnafanya Mheshimiwa Waziri. Tunajua fungu ambalo tunawapa kama Wizara, sisi kama Wabunge haturidhiki, mnastahili kuwa na fungu kubwa zaidi lakini kupanga ni kuchagua, taratibu tunaamini kadri tunavyoenda na hali yetu ya makusanyo inavyoboreka tutafika mahali ambapo tutakuwa na fungu bora zaidi.

Kuhusu *TBC* Waheshimiwa Wabunge wamesema sana, *TBC* ni mtoto wetu tunampenda sana tunge-*support* sana na tunaendelea kuku-*support* sana Mheshimiwa Waziri kwamba *TBC* ipate fedha ambazo zinakuwa katika bajeti yake ili iweze kuboresha kazi zake. Mimi nichukue nafasi hii

kama Spika, kuwapa pole *TBC* kwa kupotelewa na waandishi watatu mahiri kabisa akiwemo ndugu yetu Marin Hassan ambaye tulikuwa naye viwanja vya Bunge kwa muda mrefu, Ndugu Joseph Kambanga pamoja na Ndugu Lutengano Haonga. Ni pigo kubwa mno kwenye *institution* hii ya *TBC*, ukisha-*train* watu kama hawa wamefika mahali pa kubobea sana katika uandishi wa habari ukawapoteza kwa mpigo, kwa kweli ni pigo kubwa sana. Tunampa pole sana Mkurugenzi wa *TBC* lakini pia kwako mwenyewe Mheshimiwa Waziri na tulikuona kule Zanzibar ukizika, kwa kweli tunawaombea ndugu hawa Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi.

Mwaka jana sisi kama Wabunge tulipata nafasi ya kwenda Cairo kwenye mashindano ya *CAF*, tulienda Wabunge karibu 70, ni mara ya kwanza Bunge limewahi kunyanyuka kwa wingi kiasi hicho kwenda kuipa moyo Timu yetu ya Taifa. Ni jambo ambalo linaliingiza Bunge la Kumi na Moja katika historia ya kipekee kabisa. Tulifika na tuliona na tunajua Mheshimiwa Waziri una kazi kubwa kwenye eneo la mpira wa miguu, una kazi kubwa sana na peke yako huwezi. Kwa hiyo, unahitaji pia *support* yetu na sisi tunahakikisha tutakupa *support* huko tuendako, yako maeneo ya kurekebisha, kwa pamoja tunaweza. (*Makof!*)

Kwenye Kiswahili, ushauri wangu ni ushirikishi katika kupatikana kwa maneno mapya ya Kiswahili. Naona kama hao wanaotohoa au sijui Kiswahili kipi kizuri zaidi, wanaokuja na maneno mapya, kwa sababu siku hizi kuna mitandao na kadhalika, hebu washirikishe watu kidogo, kama kuna maneno yanataka kuja basi washirikishe kidogo hivi, watafute utaratibu wa Watanzania kushiriki kwamba neno gani liwe vipi. Maana mwisho wa siku Kiswahili kitakuwa kigumu sana kwa Mswahili. Mtu wa Kongwa kule barakoa mpaka sasa hivi nina hakika asilimia 70, 80 ya watu wangu ukiwaambia barakoa atakuambia ndiyo dudu gani, hawajui. Hata ukiangalia neno lenyewe sijui limetoka wapi, sijui wanatohoatohoaa vipi, tusingepata neno fupi? Kwa lugha ya wenzetu *mask* kaneno kafupi, sisi kwa nini iwe barakoa, labda

wana sababu, lakini wangekuwa wanashirikisha hivi kidogo ingekeeua inasaidia.

Maneno kama kishikwambi, limekaa kama lakihunihuni hivi kidogo, kishikwambi kama kishtobe, yaani limekaakaaje sijui. Wangekuwa wanashirikisha kidogo ingeweza kuwa vizuri zaidi. Haya ni maoni yangu tu jamani ukishazeeka basi unakuwa tu hivyo. Kama neno kuzizima wao wamesema ni kuchangamka, kitu kuwa *positive*. Sijui nitoe mfano gani, yaani wanasema Jiji lilizizima maana yake kulichangamka sana, palikuwa na furaha kubwa lakini kibantu ninachokijua mimi kuzizima ni kupoa, ni kuzima. Kwa mfano, sisi Wagogo sisi hatuna 'z', tunasema 'tzi', sijui Lusinde yuko wapi hapa na wengine, '*kutzitzima*' ni kupoa. Ukipikia baridi namna hii mtu anakuuliza eeh '*kutzitzima*', *kutzitzima*' kawaida ni kurudi chini, unazimazima, wao wanakuja wanasema kuzizima ni kuchangamka zaidi. Sasa mimi siwezi kulitumia neno hilo na wengi hawawezi kulitumia kwa sababu hawa wanaotohoa hawashirikishi yaani wataharibu hii lugha wakiwa wanafanya peke yao. Tukipata mtohoaji ni Mgogo peke yake anaweka ya Kigogo, tukipata Mmakonde peke yake anabandika maneno mwisho wa siku mtu ataweka herufi zake mwenyewe za jina lake, la shangazi na la mjomba anatupatia neno, kumbe ni ufupi wa maneno au vinginevyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunashauri hawa watu kwa sababu ya mitandao na kadhalika sasa waanze kushirikisha kwa maneno mapya, vinginevyo Kiswahili ni kigumu, chukueni maneno ya kisayansi hayo wanayotohoa ni magumu. Ukipewa mtihani wa hesabu ninyi wa zamani huwezi kwanza kulielewa linauliza nini kwa Kiswahili ni vigumu kwa sababu maneno yake ni magumu, washirikishe kidogo.

Mwisho, kama tulivyotangaza jana kwamba kesho itakuwa mazishi ya ndugu yetu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Rwakatare. Kama tulivyosema itakuwa ni mazishi yanayoongozwa Kiserikali, tunawaomba wahusika wote waendelee kukubali ushauri huo wa Serikali na tuzingatatie, tusijazane huko, kutakuwa na watu wasiozidi kumi au utaratibu mwingine wowote ambayo Serikali

itauweka tuzingatie. Sisi kama Bunge tumepeleka ubani wetu kama kawaida mwenzetu akitutoka, huwa tuna utaratibu wetu kama Bunge tumeshatekeleza ambapo hata jeneza pia huwa tunagharamia. Pia tumepeleka fedha ili kama wanahitaji jeneza ambalo ni la kiwango cha kuzidi hapo basi *contribution* yetu tumepeleka kwenye akaunti ya familia.

Niseme tu kama nilivyosema hapo kabla tunao watu ndani ya Bunge ambao *contribution* zao katika maisha ya Watazania ni kubwa sana lakini hazijulikani vizuri, wengi tu. Wengi wao kwa sababu ya mitandao ya sasa *information* wanazopata ni zile za kuwabomoa, kuwadhalilisha, kuonesha si watu wema *that includes myself*. Ukitafuta huko sana utakuta Ndugai ni mtu wa hivi na hivi kitu ambacho *completely* siyo kabisa.

Sijui tunaweza kufanyaje kama taifa lakini mtu kama Mchungaji Dkt. Rwakatare ukiangalia binti aliyezaliwa huko Ifakara, nadhani sijui Mlimba anakotoka Susan anakoeleza kila wakati hata barabara za kupita hamna huko ndiyo leo Awamu ya Tano imepeleka barabara huko na madaraja maana kule mito ni mingi. Anatoka kule, anasoma katika mazingira aliyosoma katika umaskini mkubwa, anafika mjini na kadhalika anakua, anafikia mahali pa kuwa na mchangano katika elimu ya Tanzania kwa kiwango alichowenza kuchangia kwa kujenga shule nzuri katika mikoa kadhaa ya nchi yetu. Si jambo rahisi ndugu zangu na ni mfano mzuri unaoweza *ku-inspire* wasichana wengi wakawenza kuiga na wenyewe wakafanya kama hayo na makubwa kuliko hayo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, uko umuhimu wa kufahamu maisha ya watu hawa, kujua *biographies* zao, namna gani amefika mahali pa kuwa Mchungaji tena wa Kanisa, Mikocheni B, *Assemblies of God*, Mlima wa Moto na wafuasi wengi, akawa anashughulikia kazi ya Mungu. Imefika mahali pa kuwa Dokta, ni shahada ya heshima kwa mtu aliyetoka katika mazingira hayo.

Tunao wasomi lakini wengine wamesomasoma tu kirahisirahisi hivi mpaka wamefika huko walikofika. Profesa

sawa, lakini umepita kwenye shushi lakini tuna watu yaani akikuambia historia yake na hapo alipofika hata kama ana *degree* moja, lakini hiyo *degree* moja alivyopita na namna alivyopitia ni *inspiration* kubwa sana kwa vijana wetu wengi sana katika nchi yetu kuweza kufanya mabadiiiko makubwa. Mheshimiwa Dkt. Rwakatare amefika mahali pa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa historia hiyo hiyo, ni mafanikio makubwa.

Kwa hiyo, nilichokuwa nasema ni kwamba ni vizuri historia za watu kama hawa zikafahamika zinaweza zika-*inspire* vijana wengi sana lakini kipekee vijana wa kike wa nchi hii. Kwa hiyo, kila mmoja mahali pake tuisahau kumwombea mwenzetu ili Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi na tuzidi kuombeana na sisi.

Niwahakikishie kwenye ukumbi huu tunajitahidi kwa hali kuhakikisha kwamba tuko *safe*. Kwa hiyo, kwa Mbunge yeote ambaye ana zamu ya kuingia humu ndani muingie tu wala msiwe na wasiwasi tunafanya kila kinachowezekana, siyo ukumbi huu tu Msekwa pia na kumbi nyingine zote ambazo tunafanya kazi. Kila wakati tuna *innovate*, tukitoka tu hapa vijana wanaingia kufanya usafi wa hali ya juu kila dawati, kila mahali tulipokaa, *microphone* tunazozitumia na kadhalika, tunajitahidi sana.

Tunachoendelea kusisitiza ni kwamba na wenzetu mnapoondoka hapa basi m jitahidi huko mliko. Bila kusahau kwamba ukijisikia kidogo hali yako si nzuri, Mbunge yeote Yule, tafadhalii chukua hatua za kufika kwenye huduma za afya ukianzia na kituo chetu hapa ili tuweze kujua kinachoendelea.

Pia kama kawaida unaweza ukapumzika nyumbani ukatujulisha, ukishatujulisha sisi masuala mengine kuhusiana na utaratibu tunajua wenyewe jinsi ya kuzingatia wala hakuna mashaka katika hilo. Usjilazimishe kuja hapa kwa sababu zetu zile za Waheshimiwa Wabunge wakati hali yako ni ya homahoma, hapana, katika nyakati hizi lazima kuchukua *precaution*.

Waheshimiwa Wabunge hapa wamesema kwamba hata zile *tradition practices* ²²⁹ basi huko nyumbani tuanze kujifukiza na kadhalika. Kama unajisikia kidogo siyo vizuri usidharau zile njia zetu za kiasili, muanze kuchukua *measures*.